HUDUMA YA USTAWI

1952 Compilation

Waandishi, Waombezi, Washauri, Teknolojia, Wahariri, Wasanii

Aimo Abayo-Morogoro, Tanzania

Daniel Nyangaresi Masaka- Kisii, Kenya,

David Jabez Masaka -Pennsylvania, Marekani

Paul Momadi Masaka - New Jersey, Marekani

Obadiah Murimi - Githurai, Kenya

Sandra Barron- Kentucky, Marekani

Gerard Saakumi Nyafanga - Shirati, Tanzania

Faustin Momadi Mkama - Dar-Es-Salaam, Tanzania

Dr and Mrs Wilson Trickett- Michigan, Marekani

Damas Kivunge- Arusha, Tanzania

Jemimah Kivunge Nyafanga-Arusha, Tanzania

Milinje Bariki Momadi-Masasi, Tanzania

Stefano Kasiri-Kibaha, Tanzania

Gibson Wilson Mujuni-Kagera, Tanzania

Mbusi Mpagalushu -Bariadi, Tanzania

Grace Masaka-Momadi-New Jersey, Marekani

Taarifa Kuhusu Kitabu Hiki

Muhtasari

Chapisho hili la ePub limetolewa kama huduma ya Ellen G. White Estate. Ni sehemu ya mkusanyiko mkubwa zaidi. Tafadhali tembelea tovuti ya Ellen G. White Estate kwa orodha kamili ya machapisho yanayopatikana.

Kuhusu Mwandishi

Ellen G. White (1827-1915) anachukuliwa kuwa mwandishi wa

Kimarekani ambaye vitabu vyake vimetafsiriwa zaidi, kazi zake zikiwa zimechapishwa katika lugha zaidi ya 160. Aliandika zaidi ya kurasa 100,000 kuhusu mada anuwai za kiroho na za kiutendaji. Akiongozwa na Roho Mtakatifu, alimwinua Yesu akiwaelekeza watu katika Maandiko kama msingi wa imani ya mtu.

Viungo Zaidi

A Brief Biography of Ellen G. White

About the Ellen G. White Estate

Mkataba wa Leseni ya Mtumiaji

Kutazama, kuchapisha au kupakua kitabu hiki hukupatia uhuru wenye ukomo, usiojumuishi na usiohamishika wa kukitumia wewe peke yako kwa matumizi binafsi. Leseni hii hairuhusu kuchapishwa upya, usambazaji, ugawaji, leseni ndogo, uuzaji, utayarishaji wa kazi za mkataba, au matumizi mengine. Matumizi yoyote yasiyoruhusiwa ya kitabu hiki huweka ukomo wa leseni iliyotolewa hapa.

© Hakimiliki 2010 na Ellen G. White Estate, Inc.

Kwa habari zaidi kuhusu mwandishi, wachapishaji, au jinsi unavyoweza kusaidia huduma hii, tafadhali wasiliana na Ellen G. White Estate: (anwani ya barua pepe). Tunashukuru kwa shauku

na maoni yako na tunakutakia baraka za Mungu unapokisoma.

Yaliyomo

Habari kuhusu Kitabu hiki..... 1

Overview 1

Kuhusu Mwandishi 1

Viungo Zaidi. 1

Mkataba wa Leseni ya Mtumiaji..... 1

Dibaji 9

Sehemu ya I Falsafa ya Kiungu ya Mateso na Umaskini 13

Wazo la Thamani 14

Sura ya Kwanza-Kwa Nini Umaskini na Dhiki? 15

Sura ya Pili - Huruma ya Kristo kwa Binadamu Wanaoteseka..... 23

Sehemu ya II Mpango wa Mungu kwa Ajili ya Kanisa Lake 27

Wazo la Thamani 28

Sura ya Tatu-Isaya 58- Maagizo ya Mungu..... 29

Sura ya Nne - Hii Ndio Dini Safi..... 35

Sura ya Tano - Mfano wa Msamaria Mwema 42

Sehemu ya III Mfano wa Agano Jipya 51

Wazo la Thamani 52

Sura ya Sita - Mfano Wetu katika Huduma ya Ustawi..... 53

Sura ya Saba - Kutembelea - Mpango wa Agano Jipya..... 59

Sura ya Nane-Dorkasi-Huduma na Mvuto wa Huduma Yake..... 66

Sehemu ya IV Uinjilisti wa Ujirani 69

Wazo la Thamani .....
70

Sura ya Tisa - Aina za Kazi katika Uinjilisti wa Ujirani..... 71

Sura ya Kumi –Wema Ufunguo wa Mioyo 81

Sura ya Kumi na Moja-Jinsi ya Kutembelea na Nini cha Kufanya 87

Sura ya Kumi na Mbili - Ufanisi wa Uinjilisti wa Kutembelea..... 97

Sura ya Kumi na Tatu - Kulipanga Kanisa kwa Ajili ya Huduma ya Ustawi..... 105

Sehemu ya V Kumfariji Binadamu Anayeteseka 115

Wazo la Thamani 116

Sura ya Kumi na Nne -Katika Nyayo za Mwalimu 117

Sura ya Kumi na Tano - Huduma ya Tiba katika Makazi ya Watu 125

Sura ya Kumi na Sita-Kujiandaa kwa Ajili ya Hatari na Majanga ya Siku za Mwisho..... 134

Sehemu ya VI Vuguvugu la Dorkasi Kanisani 141

Wazo la Thamani 142

Sura ya Kumi na Saba-Wanawake Wameitwa Kazini 143

Sura ya Kumi na Nane - Sifa za Wanawake kwa Ajili ya Utumishi 149

Sura ya Kumi na Tisa - Mvuto wa Wanawake Wakristo..... 157

Sehemu ya VII Maskini 167

Wazo la Thamani 168

Sura ya Ishirini - Huduma kwa Maskini 169

Sura ya Ishirini na Moja - Maskini Waliomo Kanisani 178

Sura ya Ishirini na Mbili - Maskini wa Duniani 188

Sura ya Ishirini na Tatu - Kuwasaidia Maskini Kujimudu Wenyewe..... 194

Sura ya Ishirini na Nne - Maskini Kutenda kwa Ukarimu..... 203

Sehemu ya VIII Wasiojiweza 207

Wazo la Thamani 208

Sura ya Ishirini na Tano - Wajibu wetu kwa Wasiojiweza 209

Sura ya Ishirini na Tisa - Msaada na Faraja kwa Wajane 214

Sura ya Ishirini na Saba - Kuwahudumia Yatima 220

Sura ya Ishirini na Nane - Kuwalea Watoto na Kuwafanya Wana 232

Sura ya Ishirini na Tisa - Utunzaji wa Wazee 237

Sura ya Thelathini - Wajibu Wetu kwa Vipofu 239

Sehemu ya IX Waliotengwa na Jamii 243

Wazo la Thamani 244

Sura ya Thelathini na Moja - Kufanya Kazi kwa Ajili ya Waliotengwa na Jamii 245

Sura ya Thelathini na Mbili - Maonyo Yaliyotamkwa 253

Sura ya Thelathini na Tatu - Wito kwa Ajili ya Kazi Yenye Usawa.....

Sehemu X Rasilimali Fedha kwa Ajili ya Kazi ya Ustawi 261

Wazo la Thamani 262

Sura ya Thelathini na Nne - Wajibu Wetu Binafsi..... 263

Sura ya Thelathini na Tano - Kuiachia Mito ya Ukarimu..... 268

Sura ya Thelathini na Sita – Fedha Mahususi kwa Ajili ya Kazi ya Ustawi 272

Sura ya Thelathini na Saba - Utajiri wa Mataifa 277

Sura ya Thelathini na Nane - Mauzo ya Chakula..... 284

Sura ya Thelathini na Tisa – Njia Zilizokatazwa za Kuchangisha Fedha..... 289

Sehemu ya XI Faida ya Huduma ya Ustawi 293

Wazo la Thamani 294

Sura ya Arubaini - Mvuto wa Huduma ya Ujirani..... 295

Sura ya Arubaini na Moja - Reflex Baraka 301

Sura ya Arubaini na Mbili - Thawabu za Sasa na za Milele..... 311

Kiambatisho 321

Uzoefu Binafsi wa Ellen G. White kama Mfanyakazi wa Ustawi..... 321

Ellen G. White katika Kazi ya Kiutendaji ya Dorkasi..... 322

Huduma ya Ustawi wa Jamii katika Miaka Mingi 325

Utangulizi katika Australia 327

Bi White Alihifadhi Huruma Pana Katika Maisha Yote..... 338

Barua kwa Watoto Wasio na Baba..... 340

Dibaji

Huduma ya Ustawi inatoa maagizo ya roho ya unabii katika kazi nyeti ya kufikia mioyo na kuongoa roho kupitia wema wa ujirani (au ujirani mwema?). Hii ni aina ya huduma ya kuongoa roho

ambayo Waadventista wa Sabato wengi wanaifahamu kikawaida tu – lakini bado ni kazi iliyowekwa na Mungu kama njia sahihi kabisa ya kumleta Kristo na Ukristo katika usikivu wa watu wa ulimwengu. Ni kazi yenye ahadi za thawabu nyingi.

Si tu kwa maagizo mafupi, yenye maneno mazuri mwandishi ameweka mbele yetu aina hii ya huduma, bali kwa miaka mingi, ingawa anashughulishwa na majukumu yake ya nyumbani na majukumu yake kama mjumbe wa Bwana, mara nyingi bila kujua aliweka mfano kadiri moyo wake ulivyovutwa kwa wahitaji waliomzunguka. Rekodi ya tawasifu (habari za maisha ya mtu zilizoandikwa na yeye mwenyewe) ya huduma isiyo ya ubinafsi ya Ellen G. White kama mfanyakazi wa ustawi, zilizochukuliwa kutoka kwenye shajara

na barua zake, kama inavyopatikana katika kiambatisho cha kitabu hiki, zitatumiwa kwa shauku kubwa na inaweza kuwa vyema kuzisoma kabla ya kujifunza mashauri yanayopatikana katika jamii ya maneno halisi ya mwandishi. Vyovyote iwavyo, msomaji punde atagundua kwamba huduma ya ustawi ambao kwa huo kanisa linaitwa si tu huduma ya jamii bali ni aina fulani ya huduma ya upendo na juhudi ya uongoaji wa roho - aina ya juu kabisa ya uinjilisti wa ustawi.

Katika kukusanya mashauri ya Roho ya Unabii yanayohusiana na uwanja huu muhimu wa kazi, dondoo zimechukuliwa kutoka kwenye hazina kubwa ya mafundisho ya thamani yaliyoandikwa katika kipindi cha miongo saba. Yamekusanywa si tu kutoka katika vitabu vilivyochapishwa

vilivyopo kwa sasa bali pia kutoka katika maelfu ya makala za E. G. White ambazo zilitayarishwa kwa ajili ya majarida ya kanisa, shuhuda maalum zilizotolewa kwa namna ya kijitabu, na faili za miswada ya E. G. White. Yakiwa yamechaguliwa kama yalivyo kutoka katika vyanzo hivi mbalimbali vilivyoandikwa kwa nyakati tofauti, kwa kutarajia kuwa yanamleta msomaji katika njia ile ile ambayo amekwishaipita kabla, ili kusisitiza baadhi ya mambo muhimu yaliyo ya kiini kwa ajili ya ukuzaji kamili wa mada. Marudio kama hayo, ingawa yamepunguzwa kufikia kiwango cha chini, hayawezi kuepukwa kabisa katika mkusanyiko kama huu, kwa kuwa wakusanyaji wana mipaka katika kazi zao kwa ajili ya uchaguzi wa mada na

upangaji wake katika mtiririko wa kimantiki, kutoa vichwa tu.

Imekuwa ni vigumu na karibu kutokuwezekana kabisa kuleta ndani ya majalada ya kitabu kimoja kiasi kikubwa cha mafundisho ambayo Ellen G. White ameyatoa kuhusu aina hii ya kazi, na ambayo kwa usahihi yangeweza kuonekana katika kitabu kinachobeba kichwa cha Huduma ya Ustawi. Si jambo rahisi kuchagua taarifa na kuchora mstari kati ya kutembelea jirani na wito wa umisionari, wala kutenganisha kazi ya wanawake mashuhuri Waadventista wa Sabato katika sura zake pana kutoka kwa kazi iliyobainishwa vyema zaidi inayofanywa kwa malengo ya umisionari peke yake. Kwa mtoto wa Mungu hizi huchanganyika pamoja katika shughuli mbalimbali za maisha ya kila siku.

Usikivu hapa unaelekezwa kwa maneno fulani yanayotokea mara kwa mara katika kitabu hiki kama vile "kazi ya umisionari wa tiba" na "kazi ya msaada wa Kikristo." Ikumbukwe kwamba uchunguzi wa kina wa maandishi ya Ellen G. White unaonesha kwamba kirai "kazi ya umisionari wa tiba" kinatumiwa na mwandishi kujumuisha huduma za kitaalamu za madaktari na wauguzi waliojiweka wakfu, na kwamba umuhimu wake pia unafikia mbali, na ng'ambo ya mipaka hii na kujumuisha matendo yote ya huruma na fadhila zisizotafuta faida. "Kazi ya msaada wa Kikristo" pia ni neno lililotumiwa sana na Waadventista wa Sabato katika miaka yao ya awali kuliko sasa na linarejelea aina ya kazi iliyoelezewa katika kitabu hiki.

Akiandika kama alivyofanya katika mabara mbalimbali, mwandishi katika kurejelea fedha wakati mwingine anazungumzia dola na wakati mwingine paundi na shilingi.

Inasisitizwa kwamba msomaji ajifunze maagizo haya katika mazingira yake sahihi, ili kugundua kanuni za msingi zinazohusika katika kila hali. Kwa mfano, uchunguzi wa mashauri yanayohusu "chakula cha Kanisa" utadhihirisha kwamba ingawa tunaonywa dhidi ya kutumia tamanisho la hamu ya chakula na kupenda raha kama njia ya kupata fedha za kanisa, lakini ni fursa ya vikundi vya Kanisa kushiriki katika kuandaa na kuuza chakula chenye afya ikiwa kazi hiyo itafanywa vizuri na kufanywa mahali panapofaa.

Isipokuwa katika mifano michache sana ambapo sentensi moja au mbili zinaweza kutamka wazi kanuni fulani, wakusanyaji wamejitahidi kujumuisha miktadha ya kutosha ya kila dondoo ili kumhakikishia msomaji matumizi sahihi ya taarifa iliyochaguliwa. Katika kila mfano tarehe ya kuandikwa au ya kuchapishwa kwa mara ya kwanza imeoneshwa kwa mintarafu ya mwandiko wa chanzo ambacho kauli hiyo imetolewa.

Hati hii imeandaliwa katika ofisi ya machapisho ya Ellen G. White na Wadhamini, ambao hubeba jukumu la utunzaji na uchapishaji wa maandishi ya E. G. White. Kazi hii imefanywa kwa upatanifu kamili wa maagizo ya Bi White kwa Wadhamini hawa katika kutoa "kwa ajili ya uchapishaji wa

makusanyo kutoka katika maandishi yangu," kwani alisema, "maagizo ambayo Bwana amenipa kwa ajili ya watu Wake."

Kwamba kitabu hiki cha mafundisho kinachoelekezwa kwa Waadventista wa Sabato - walei na wachungaji sawa - kiweze kulitia moyo kanisa kutumia vizuri fursa katika huduma ya ujirani; kwamba maagizo yake yapate kuongoza katika huduma ya akili, ya uangalifu na ya upendo; na kwamba kupitia mwongozo wake kunaweza kuwa na mavuno mengi ya roho katika ufalme wa Mungu ni matakwa ya dhati ya Wachapishaji na Wadhamini wa Machapisho ya Ellen G. White.

SW, Washington, D.C.

Septemba 10, 1951

Sehemu ya I Falsafa ya Kiungu ya Mateso na Umaskini

Wazo la Thamani

Dhambi imezima upendo ambao Mungu aliuweka ndani ya moyo wa mwanadamu. Kazi ya kanisa ni kuuamsha tena upendo huu. Kanisa linabidi lishirikiane na Mungu katika kung'oa ubinafsi kutoka katika moyo wa mwanadamu, kuweka badala yake ukarimu uliokuwa katika moyo wa

mwanadamu katika hali yake ya awali ya ukamilifu.-*Letter* 134, 1902.

Sura ya Kwanza-Kwa Nini Umaskini na Dhiki?

Heri Wenye Rehema. Bwana Yesu alisema, "Heri wenye rehema; kwa maana watapata rehema." Hakukuwahi kuwa na wakati ambapo kulikuwa na hitaji kubwa la matumizi ya rehema kuliko leo. Maskini wako kila mahali kutuzunguka, wenye dhiki, wanaoteseka, wenye huzuni, na wale ambao wako karibu kuangamia. **{WM 15.2}**

Wale ambao wamepata mali wameichuma kupitia kwa matumizi ya

zile talanta walizopewa na Mungu, lakini talanta hizi za kuchuma mali walikabidhiwa kwa ajili ya kuzitumia kwa ajili ya kuwapa afueni na kuwasaidia wale wanaoishi katika umaskini. Zawadi hizi zilitolewa kwa wanadamu na Yeye ambaye hufanya jua Lake liangaze na mvua Yake iwanyeshee wenye haki na wasio haki, ili kwa dunia kuzaa matunda wanadamu wapate ruzuku nyingi kwa ajili ya mahitaji yao yote. Mashamba yamebarikiwa na Mungu, na "kutokana na wema Wake Yeye amewaandalia maskini."—*The Signs of the Times*, Juni 13, 1892. **{WM 15.3}**

Mateso na Taabu Hazikukusudiwa na Mungu.- Kuna wengi ambao wanamlalamikia Mungu kwa sababu ulimwengu umejaa dhiki na

mateso, lakini Mungu kamwe hakumaanisha kwamba dhiki hii ipate kuwepo. Hakuwahi kumaanisha kwamba mtu mmoja apate kuwa na starehe tele za maisha wakati watoto wa wengine wanalalamika kwa ajili ya mkate. Bwana ni Mungu wa wema.- *Testimonies for the Church* 6:273.**{WM 15.3}**

Mungu amewafanya watu kuwa mawakili Wake, na hapaswi kushtakiwa kwa sababu ya mateso, taabu, uchi, na uhitaji wa wanadamu. Bwana amefanya riziki ya kutosha kwa wote. Amewapa maelfu ya watu ruzuku kubwa ambazo kwazo wangepunguza ukali wa uhitaji wa wenzao; lakini wale ambao Mungu amewaweka kuwa mawakili hawajalishinda jaribio hilo, kwani

wameshindwa kutuliza mateso na wahitaji. **{WM 16.1}**

Wakati watu ambao wamebarikiwa sana na Mbingu kwa utajiri mkubwa wanaposhindwa kutekeleza mpango wa Mungu, na hawawasaidii maskini na waliolemewa, Bwana anachukizwa, Naye hakika atawapatiliza. Hawana udhuru wa kuzuia majirani zao kupata msaada ambao Mungu ameuweka katika uwezo wao kutoa; na Mungu anatiwa fedheha, tabia yake inatafsiriwa vibaya na Shetani, na anawakilishwa kama hakimu mkali ambaye husababisha mateso kuja juu ya viumbe alivyoviumba. Uwakilishaji huu usio sahihi wa tabia ya Mungu unafanywa kuonekana kama ukweli, na hivyo kupitia majaribu ya adui mioyo ya wanadamu inakuwa migumu dhidi ya Mungu. Shetani

anaweka juu ya Mungu uovu ule hasa ambao yeye mwenyewe amesababisha watu wautende kwa kuzuilia mali zao kuwasaidia wanaoteseka. Anamwekea Mungu sifa zake yeye mwenyewe. -*The Review and Herald*, Juni 26, 1894. **{WM 16.2}**

Hakuna Haja ya Kuwa na Mateso, Hakuna haja ya kuwa na Ufukara. - Ikiwa watu wangetimiza wajibu wao kama mawakili waaminifu wa mali za Bwana wao, hakungekuwa na kilio kwa ajili ya mkate/chakula, hakuna hata mmoja anayeteseka katika ufukara, hakuna aliye uchi na mwenye uhitaji. Ni ukosefu wa uaminifu wa wanadamu ambao huleta hali ya mateso ambayo ubinadamu umetumbukia. Iwapo wale ambao Mungu amewafanya kuwa mawakili wangeliweka kando mali ya

Bwana wao kwa ajili ya sababu ile iliyomfanya awape, hali hii ya mateso na vilio, isingelikuwapo. Bwana anawapa watu mtihani/jaribio kwa kuwapa vitu vingi vizuri, kama vile alivyomjaribu tajiri kijana katika mfano. Ikiwa tunajidhihirisha kuwa sisi si waaminifu katika utajiri wa haki, ni nani basi atakayetukabidhi mali ile ya Kweli? Itakuwa ni wale ambao watashinda katika jaribio duniani, ndio ambao wameonekana kuwa waaminifu, wale ambao wameyatii Maneno ya Bwana kwa kuwa na huruma, kwa kutumia mali zao kwa ajili ya maendeleo ya ufalme Wake, ndio ambao watasikia kutoka katika midomo ya Bwana, "Vema, mtumishi mwema na mwaminifu."— *Kitabu hicho hicho*. **{WM 16.3}**

Baadhi Matajiri-Baadhi Maskini. - Sababu kwa nini Mungu ameruhusu baadhi ya familia za wanadamu kuwa matajiri sana na wengine kuwa maskini sana itabaki kuwa siri kwa wanadamu hadi milele, isipokuwa wameingia katika uhusiano sahihi na Mungu na kutekeleza mipango Yake badala ya kutenda kwa mawazo yao ya ubinafsi. - *Testimonies to Ministers and Gospel Workers*, 280. **{WM 17.1}**

Kuhimiza Upendo na Rehema.- Katika majaliwa ya Mungu matukio yamepangwa kiasi kwamba maskini daima wako pamoja nasi, ili kuwe na utendaji kila wakati katika moyo wa mwanadamu wa sifa za rehema na upendo. Mwanadamu anapaswa kukuza tabia iliyo nyororo na yenye huruma ya

Kristo; yeye hapaswi kujitenga na wenye huzuni, wanaoteseka, wahitaji, na wenye dhiki. -*The Signs of the Times*, Juni 13, 1892.**{WM 17.2}**

Ili Kukuza Tabia Kama ya Mungu Ndani ya Mwanadamu. - Wakati ambapo ulimwengu unahitaji huruma, wakati ambapo unahitaji maombi na msaada wa watu wa Mungu, wakati ambapo unahitaji kumwona Kristo katika maisha ya wafuasi Wake, watu wa Mungu vile vile wanahitaji fursa ambazo huvuta huruma zao, kutoa ufanisi kwa maombi yao, na kukuza ndani yao tabia kama ile ya mfano wao wa Bwana. **{WM 17.3}**

Ni kwa ajili ya kutoa fursa hizi Mungu amewaweka kati yetu maskini, wale waliopatwa majanga, wasiojiweza,

wagonjwa, na wanaoteseka. Wao ni urithi wa Kristo kwa kanisa Lake, na wanapaswa kutunzwa kama ambavyo Yeye angewajali. Kwa jinsi hii Mungu huondoa uchafu na kuitakasa dhahabu, akitupa utamaduni/elimu ya moyo na tabia ambayo tunahitaji.**{WM 17.4}**

Bwana angeweza kuendeleza mbele kazi yake bila ushirikiano wetu. Yeye hatutegemei sisi kwa ajili ya fedha zetu, wakati wetu, au kazi yetu. Bali kanisa ni la thamani sana machoni Pake. Ni sanduku ambalo linabeba vito Vyake vya thamani, zizi ambalo linawazungushia boma kundi Lake, na anatamani kuliona likiwa bila doa au waa au kitu chochote kama hicho. Yeye ana matamanio na kanisa Lake, kwa upendo usioelezeka. Hii ndiyo sababu Yeye ametupa fursa za kufanya kazi kwa ajili Yake, Naye

anazikubali kazi zetu kama ishara za upendo na uaminifu wetu. - *Testimonies for the Church* 6:261.**{WM 18.1}**

Ili Tupate Kuielewa Rehema ya Mungu. - Maskini pamoja na tajiri ni mboni/lengo la utunzaji maalum wa Mungu na uangalifu. Ondoa umaskini, na hatutakuwa na njia yoyote ya kuelewa rehema na upendo wa Mungu, hakuna njia nyingine ya kumjua Baba wa mbinguni Mwenye huruma na sikitiko Lake kwa wale waliopatwa na shida. -*Letter* 83, 1902.**{WM 18.2}**

Mungu Anatupa ili Tuwape Wengine. -Mungu anatugawia baraka Zake ili tupate kuwagawia wengine. Tunapomwomba mkate wetu wa kila siku, Yeye anaangalia ndani ya mioyo yetu kuona kama tutaushiriki na wale

walio na uhitaji zaidi kuliko sisi wenyewe. Tunapoomba "Mungu nihurumie mimi mwenye dhambi," Yeye anaangalia kuona kama tutadhihirisha huruma kwa wale tunaohusiana/tunaoshirikiana nao. Huu ni ushahidi wa muungano/uhusiano wetu na Mungu, kwamba sisi tu wenye rehema kama vile Baba yetu aliye mbinguni alivyo na rehema. - *Testimonies for the Church* 6:283, 284. **{WM 18.3}**

Kuzuia Ukuaji wa Kiroho wa Kimbilikimo. - Hakuna kitu kinachopunguza hali ya kiroho kutoka rohoni haraka kuliko kuifunga [hiyo roho] katika ubinafsi na kujijali. Wale ambao wanaendekeza nafsi na kupuuza kujali roho na miili ya wale ambao Kristo ametoa maisha yYke kwa ajili yao,

hawali mkate wa uzima au kunywa maji kutoka katika kisima cha wokovu. Wao ni wakavukavu na wasio na nguvu, kama mti usiozaa matunda. Ni kibete/mbilikimo wa kiroho, ambao hutumia mali zao juu ya nafsi zao; lakini "Chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna."—*The Review and Herald,* Januari 15, 1895. **{WM 18.4}**

Ni kwa sababu matajiri wanapuuza kufanya kazi kwa ajili ya maskini ambayo Mungu alipanga wapate kuifanya, ndio maana wanazidi kuwa wenye kiburi (pembe zinazidi kuota), wenye kujitosheleza, wenye kuendekeza nafsi, na wenye mioyo migumu. Wanawatenga maskini mbali na wao kwa sababu tu ni masikini, na kwa hiyo wanapata nafasi ya kuwa na husuda na wivu. Wengi wanakuwa na uchungu, na

wanajawa na chuki kwa wale ambao wana kila kitu wakati wao hawana chochote. **{WM 19.1}**

Mungu hupima matendo, na kila mtu ambaye amekuwa si mwaminifu katika uwakili wake, ambaye ameshindwa kurekebisha maovu ambayo yalikuwa katika uwezo wake wa kurekebisha, hatakuwa na heshima katika nyua za mbinguni. Wale ambao hawajali mahitaji ya maskini watahesabiwa kuwa mawakili wasio waaminifu, nao watasajiliwa kama maadui wa Mungu na wanadamu. Wale ambao hutumia vibaya mali ambazo Mungu amewakabidhi kwa ajili ya kuwasaidia wale ambao hasa wanahitaji msaada wao, wanathibitisha kwamba hawana uhusiano na Kristo, kwa sababu wanashindwa kudhihirisha wema wa Kristo kwa wale ambao

hawana bahati kama wao wenyewe. – The Review *and Herald*, Desemba 10, 1895.**{WM 19.2}**

Ikiwa Matajiri Watatembea katika Nyayo za Kristo. - Mtu tajiri ni wakili wa Mungu, na ikiwa anatembea katika nyayo za Kristo, akidumisha maisha ya unyenyekevu, yale ya kumcha Mungu, anakuwa, kupitia mabadiliko ya tabia, mpole na mnyenyekevu wa moyo. Anatambua kuwa mali zake ni hazina zilizokopeshwa tu, na anahisi kuwa dhamana takatifu imekabidhiwa kwake kwa ajili ya kusaidia wahitaji na wanaoteseka, badala ya Kristo. Kazi hii italeta thawabu yake katika talanta na hazina zilizowekwa juu kando ya kiti cha enzi cha Mungu. Hivyo mtu tajiri anaweza kuwa na maisha ya kiroho yenye mafanikio, kama wakili

mwaminifu wa bidhaa *za* Bwana wake. - *Manuscript* 22, 1898.**{WM 19.3}**

Mateso - Njia Mojawapo ya Kukamilisha Tabia. - Maneno ya Mwokozi pia yana ujumbe wa faraja kwa wale ambao wanateseka au kufiwa. Huzuni zetu hazichipuki kutoka ardhini. Mungu "hapendi kuwatesa wanadamu. Wala kuwahuzunisha." Pale anaporuhusu majaribio na mateso, huwa ni "kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu Wake." Ikiwa litapokelewa kwa imani, jaribio lile ambalo linaonekana kuwa chungu na gumu kubeba litathibitika kuwa baraka. Pigo la kikatili linaloharibu furaha za dunia litakuwa njia ya kugeuza macho yetu kuelekea Mbinguni. Ni wangapi ambao wasingeweza kumjua Yesu kama huzuni

isingeliwaongoza kutafuta faraja ndani Yake! **{WM 20.1}**

Majaribio ya maisha ni watenda kazi wa Mungu, ili kuondoa uchafu na mikwaruzo kutoka katika tabia yetu. Kuchongwa kwake, kusawazishwa kwake, uumbaji wake katika ile shepu ifaayo, kukwatua kwake na msuguo wake, ni mchakato wa kuumiza; ni hali ngumu kwa mtu kubanwa kwenye gurudumu la kusaga. Ila jiwe linaletwa kutoka pale likiwa tayari kujaza nafasi yake katika hekalu la mbinguni. Juu ya nyenzo yoyote isiyo na maana Bwana hatoi kazi kama hiyo iliyo makini, na kamilifu. Ni vito Vyake vya thamani peke yake, ndivyo vinavyosuguliwa kama jumba la kifalme. **{WM 20.2}**

Bwana atafanya kazi kwa wote wanaoweka tumaini lao Kwake. Ushindi wa thamani utapatikana kwa waaminifu. Masomo ya thamani yatafundishwa/yatafunzwa. Uzoefu wa thamani utapatikana. - *Mount of Blessing*, uk. 23, 24.**{WM 20.3}**

Mateso na Maafa si Dalili ya Chuki ya Mungu.—"Hata alipokuwa akipita alimwona mtu, kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi Wake wakamwuliza wakisema, Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu? Yesu akajibu, Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake." ...**{WM 21.1}**

Kwa ujumla iliaminiwa na Wayahudi kwamba dhambi inaadhibiwa katika maisha haya. Kila shida ilichukuliwa kuwa ni adhabu ya tendo fulani ovu, ama anayeteseka mwenyewe au wazazi wake. Ni kweli kwamba mateso yote hutokana na uvunjaji wa sheria ya Mungu, lakini ukweli huu ulikuwa umepotoshwa. Shetani, mwanzilishi wa dhambi na matokeo yake yote, alikuwa amewaongoza wanadamu kutazama magonjwa na kifo kama vile yanatoka kwa Mungu - kama adhabu inayotolewa kidikteta kwa sababu ya dhambi. Kwa hiyo mtu yule ambaye shida au msiba mkubwa ulikuwa umeanguka juu yake, alikuwa na mzigo wa ziada wa kuonekana kama mwenye dhambi mkubwa....**{WM 21.2}**

Mungu alitoa somo lililokusudiwa kulizuia hili. Kisa cha Ayubu kilionesha kwamba mateso yanasababishwa na Shetani, na yanabatilishwa na Mungu kwa makusudi ya rehema. Lakini Israeli hawakulielewa somo hili. Kosa lile lile ambalo kwalo Mungu alikuwa amewakemea marafiki wa Ayubu lilirudiwa na Wayahudi katika kumkataa Kristo. **{WM 21.3}**

Imani ya Wayahudi kuhusu uhusiano wa dhambi na mateso ilishikiliwa na wanafunzi wa Kristo. Yesu aliposahihisha kosa lao. Hakuelezea sababu ya mateso ya mtu huyo, bali aliwaambia kitu gani kingelitokea. Kwa sababu ya hicho kazi za Mungu zingewekwa wazi. "Muda nilipo ulimwenguni," Alisema, "Mimi ni nuru ya ulimwengu." Ndipo baada ya

kumpaka yule kipofu machoni, akamtuma kwenda kunawa katika bwawa la Siloamu, na macho ya huyo mtu yakaponywa. Hivyo Yesu alilijibu swali la wanafunzi kwa njia ya vitendo, kama ambavyo kwa kawaida alijibu maswali yaliyoulizwa Kwake kutokana na udadisi. Wanafunzi hawakuitwa kujadili swali juu ya nani alikuwa ametenda dhambi au hakutenda dhambi, bali kuelewa uweza wa rehema ya Mungu katika kutoa kuona kwa kipofu. -*The Desire of Ages*, 470, 471. **{WM 21.4}**

Kristo Anapaswa Kuonekana na Kusikilizwa Kupitia Kwetu. - Mungu anapanga kwamba wale walio wagonjwa, wale wasiojiweza, wale wenye pepo wabaya, wataisikia sauti Yake kupitia kwetu. Kupitia kwa mawakala

Wake wa kibinadamu, Yeye Anatamani kuwa mfariji Yule, ambaye ulimwengu haujawahi kumwona hapo awali. Maneno Yake yanapaswa kutamkwa na wafuasi Wake: "Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na Mimi pia." **{WM 22.1}**

Bwana atafanya kazi kupitia kila roho ambayo itajitoa ili ifanyiwe kazi, si tu katika kuhubiri lakini pia katika kuwahudumia wale waliokata tamaa na kutia msukumo wa tumaini katika mioyo ya wasio na tumaini. Tunapaswa kutenda sehemu yetu katika kutuliza na kulainisha shida za maisha haya. Shida, mafumbo na siri za maisha haya ni nyeusi na yenye mawingu kama yalivyokuwa maelfu ya miaka iliyopita. Kuna kitu kwetu cha kufanya: "Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja,

Na utukufu wa Bwana umekuzukia." Kuna wahitaji walio karibu na sisi; mateso yako katika mipaka yetu hasa. Lazima tujaribu kuwasaidia. Kwa neema ya Kristo, chemchemi zilizozibwa za kazi ya dhati na bidii, kama ya Kristo inabidi zizibuliwe. Kwa nguvu Zake Yeye ambaye ana nguvu zote tunapaswa kufanya kazi kama vile ambavyo hatujawahi kufanya hapo awali. - *Manuscript* 65b, 1898. **{WM 22.2}**

.

Sura ya Pili - Huruma ya Kristo kwa Binadamu Wanaoteseka

Kristo Mwenyewe Anateseka Pamoja na Wanadamu Wanaoteseka. - Kristo anatambulisha shauku Yake na ile ya wanadamu ***wanaoteseka***. Alilikemea taifa Lake Mwenyewe kwa kuwatendea vibaya wanadamu wenzao. Kupuuzwa au kudhulumiwa/kuonewa kwa walio dhaifu kabisa, waumini waliokosea kabisa Yeye anazungumza juu yao kama waliomkosea Yeye Mwenyewe binafsi. Fadhila au upendeleo uliooonyeshwa kwao zinatambuliwa rasmi kama zimetolewa Kwake Mwenyewe. Yeye hajatuacha gizani kuhusu wajibu wetu, lakini mara nyingi anarudia masomo yale yale kupitia maumbo tofauti na katika nuru tofauti. Anawapeleka watendaji mbele kufikia siku ile kuu ya

mwisho (siku ya hukumu), na kutangaza kwamba jinsi alivyotendewa mmojawapo wa ndugu Zake walio wadogo, ndivyo hupongezwa au kulaumiwa kana kwamba ilitendwa Kwake Yeye Mwenyewe. Anasema, "Mlinitendea Mimi," au, "Hamkunitendea Mimi." **{WM 23.1}**

Yeye Ndiye mbadala na mdhamini wetu; Anasimama badala ya binadamu, kiasi kwamba Yeye Mwenyewe anaathirika kama vile mfuasi wake dhaifu anavyoathirika. Hivyo ndivyo ilivyo huruma ya Kristo, ambayo haimruhusu kamwe kuwa mtazamaji asiyejali, wa mateso yoyote yanayosababishwa kwa watoto Wake. Hakuna jeraha dogo kabisa hata moja linaweza kutolewa na neno, roho, au tendo, ambalo haligusi moyo wa Yeye

aliyetoa maisha Yake kwa ajili ya binadamu walioanguka. Tukumbuke kwamba Kristo Ndiye moyo mkubwa ambao kutoka Kwake damu ya uhai hutiririka kwenda kwa kila kiungo mwilini. Yeye Ndiye kichwa, ambacho kutoka Kwake huenea kila mshipa wa fahamu hadi kiungo kidogo na cha mbali zaidi cha mwili. Wakati kiungo kimoja cha mwili ambao Kristo ameunganishwa nao kwa jinsi ya ajabu kiasi kile, kinateseka, pigo hilo la maumivu linahisiwa na Mwokozi wetu. **{WM 23.2}**

Je, kanisa litaamka/litazinduka? Je! Washiriki wake watamuunga mkono Kristo, na hivyo watakuwa na huruma Yake kwa kondoo na wana-kondoo wote wa zizi Lake? Kwa ajili yao Mkuu wa mbinguni alijifanya kuwa hana sifa

yoyote; kwa ajili yao alikuja katika ulimwengu uliokaangwa kabisa na moto mkali na kuharibiwa na laana, alijitahidi mchana na usiku kuwafundisha, kuwainua, na kuleta furaha ya milele kwa watu wasio na shukrani, wasio na utii. Kwa ajili yao alikuwa maskini, ili kupitia umaskini Wake wapate kuwa matajiri. Kwa ajili yao alijikana Mwenyewe; kwa ajili yao alivumilia ufukara, dhihaka, masimango, dharau, mateso, na kifo. Kwa ajili yao alichukua mfano wa mtumwa. Huu ndio Mfano wetu; je, sisi tutauiga? Je!Sisi Tutakuwa na utunzaji wa urithi wa Mungu? Je! Tutathamini huruma nyororo/laini kwa wakosaji, wanaojaribiwa, na waliojaribiwa?—*Letter* 45, 1894. **{WM 24.1}**

Yeye Anaguswa na Hisia za Udhaifu Wetu. - Kristo, mbadala wetu na mdhamini, alikuwa Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko. Maisha Yake ya kibinadamu yalikuwa ni ya kazi ngumu kwa niaba ya urithi ambao alipaswa kuununua kwa gharama isiyo na kipimo. Aliguswa na hisia za udhaifu wetu. Kwa kuzingatia thamani anayoiweka juu ya kile kinachonunuliwa na damu Yake, Anawapanga/anawaasili kuwa watoto Wake, anawafanya kuwa lengo la utunzaji Wake laini/mwororo, na ili waweze kupatiwa mahitaji yao ya maisha na ya kiroho, huwapa kanisa Lake, akisema, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi.” - *Manuscript* 40, 1899.**{WM 24.2}**

Kristo Alikuja Kutuliza Mateso.

- Ulimwengu huu ni nyumba kubwa ya kuuguza maskini wenye ukoma na magonjwa ya kuambukiza, lakini Kristo alikuja kuwaponya wagonjwa, kutangaza ukombozi kwa mateka wa Shetani. Alikuwa ndani Yake Mwenyewe afya na nguvu. Alitoa maisha Yake kwa wagonjwa, walio matesoni, wale waliopagawa na pepo. Yeye hakumfukuza hata mmoja aliyekuja kuupokea uweza Wake wa uponyaji. Alijua fika kwamba wale waliomwomba msaada walikuwa wamejiletea ugonjwa; lakini Yeye hakukataa kuwaponya. Na wakati wema kutoka kwa Kristo ulipoingia ndani ya roho hizi maskini, walisadikishwa kuhusu dhambi, na wengi waliponywa magonjwa yao ya kiroho, na pia magonjwa yao ya kimwili.

Injili bado ina uwezo ule ule, na kwa nini basi, sisi leo tusishuhudie matokeo yale yale? **{WM 24.3}**

Kristo anahisi shida za kila anayeteseka. Wakati roho chafu wanapolirarua umbo la kibinadamu, Kristo anahisi laana hiyo. Wakati homa inapounguza mkondo wa maisha yetu, Yeye anahisi uchungu mkali. Naye Yu tayari kuponya wagonjwa sasa kama vile alivyokuwa hapa duniani. Watumishi wa Kristo ni wawakilishi Wake, njia ambayo kwayo anafanya kazi. Anataka sana kupitia kwao kutumia nguvu Zake za uponyaji. - *The Desire of Ages*, 823, 824. **{WM 25.1}**

Kristo peke yake alikuwa na uzoefu katika huzuni na majaribu yote ambayo huwapata wanadamu. Kamwe hakuna

mtoto mwingine yeyote aliyezaliwa na mwanamke ambaye alisumbuliwa vikali na majaribu kama Yeye; kamwe hakuna mwingine aliyebeba mzigo mzito wa dhambi na maumivu ya ulimwengu. Kamwe hakukuwa na mwingine yeyote ambaye huruma Zake zilikuwa pana au laini sana kiasi hicho. Mshiriki katika uzoefu wote wa binadamu Aliweza kuhisi si tu kwa ajili ya, bali pamoja, na kila aliyelemewa na kujaribiwa na anayepambana.—*Education*, 78. **{WM 25.2}**

Kristo Aliwafikia Matajiri na Maskini Sawa. - Kristo alichukua nafasi ambayo ilikuwa katika usawa na maskini, ili kupitia katika umaskini Wake tuweze kuwa matajiri katika uzuri wa tabia, na kuwa, kama alivyokuwa, harufu ya uzima iletayo uzima. Kwa

Yeye kuwa maskini Aliweza kuwahurumia maskini. Ubinadamu Wake ungeweza kuugusa ubinadamu wao na kuwasaidia kupata ukamilifu wa mienendo, mazoea sahihi na tabia nzuri. Angeweza kuwafundisha jinsi ya kujiwekea hazina zisizoharibika mbinguni. Akiwa ni Amiri Jeshi katika nyua za mbinguni, alikuwa mmoja wa wanadamu, mshirika wa mateso na huzuni zao, ili kupitia uwakilishi wa tabia Yake katika usafi Wake usio na uchafu, watu wapate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, wakiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. Na Kristo alikuwa ni furaha kwa matajiri, kwani angeweza kuwafundisha jinsi ya kutoa mali zao za kidunia, ili kuwa dhabihu kusaidia kuokoa roho

zinazoangamia katika giza la makosa. -*Letter* 150, 1899. **{WM 25.3}**

Kuza Huruma na Upole Kama wa Kristo. - Huruma laini za Mwokozi wetu ziliamshwa kwa ajili ya wanadamu walioanguka na wanaoteseka. Kama wewe ungetaka kuwa mfuasi Wake, basi ni lazima ukuze huruma na sikitiko kwa wale wanaoteseka. Kutokujali shida za wanadamu lazima kutoe nafasi kwa shauku hai katika mateso ya wengine. Mjane, yatima, mgonjwa na wale walio karibu kufa, daima watahitaji msaada. Hapa kuna fursa ya kuitangaza injili - kumwinua Yesu, tumaini na faraja ya watu wote. Wakati mwili unaoteseka umefarijiwa, na umeonesha shauku hai kwa mwenye shida, moyo unafunguliwa, nawe unaweza kumwaga tiba/zeri ya mbinguni. Ikiwa unamwangalia Yesu, na

unapata kutoka Kwake maarifa na nguvu na neema, wewe unaweza kutoa faraja Yake kwa wengine, kwa sababu Mfariji Yuko pamoja nawe.—*The Medical Missionary*, Januari, 1891. **{WM 26.1}**

Sehemu ya II Mpango wa Mungu kwa Kanisa Lake

Wazo la Thamani

Soma Isaya 58 ninyi mnaodai kuwa wana wa nuru. Je hasa, mnaisoma tena na tena ninyi ambao mmehisi kusita sana kujiletea usumbufu kwa kuwafadhili maskini. Ninyi ambao mioyo, pamoja na nyumba zenu ni finyu sana kuweza kufanya maskani kwa ajili ya wasio na makazi, isomeni; ninyi ambao mnaweza kuona yatima na wajane wakionewa na mkono wa chuma wa umaskini na kuinamishwa na walimwengu wenye mioyo migumu, isomeni. Je! Unaogopa kwamba mvuto utaletwa katika familia yako ambao

utakugharimu kazi zaidi? Isome! Hofu zako zinaweza kukosa kuwa na msingi, na baraka inaweza kuja, inayojulikana na kutambuliwa na wewe kila siku. Lakini ikiwa vinginevyo, ikiwa kazi ya ziada itatakiwa, wewe unaweza kumsogelea Yule aliyeahidi: "Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara” **{WM 28.1}**

Sababu ya ‘kwa nini watu wa Mungu hawana nia ya kiroho zaidi, na hawana imani zaidi’, nimeoneshwa, ni kwa vile wanafanywa kuwa finyu na ubinafsi. Nabii anawahutubia watunza Sabato, na sio wale wenye dhambi, si wale wasioamini, bali wale wanaofanya mfano mkubwa wa utauwa (wanaojifanya kuwa wacha Mungu). Si wingi wa mikutano yenu, ndiyo ambayo

Mungu huikubali. Na si maombi yaliyosheheni, bali ni kutenda wema, kutenda lililo jema na kwa wakati ulio sahihi. Ni kujiangalia nafsi yako kidogo na kuwa mkarimu zaidi. Roho zetu lazima zipanuke. Ndipo Mungu atakapozifanya kuwa kama bustani inayonyweshewa, ambayo maji yake hayapungui. - *Testimonies for the Church* 2:35, 36. **{WM 28.2}**

Dini iliyo safi na isiyo na hitilafu mbele ya Mungu Baba ni hii: Kuwasaidia yatima na wajane katika shida zao, na kujilinda mwenyewe usichafuliwa na ulimwengu huu. Yakobo 1:27

Sura ya Tatu-Isaya 58 - Maagizo ya Mungu

Sura Inayofafanua Kazi Yetu. - Sura yote ya hamsini na nane ya Isaya inapaswa kuchukuliwa kama **ujumbe** kwa wakati huu, ambao unapaswa kutolewa tena na tena. - *Special Testimonies, series B, no. 2, uk. 5.* **{WM 29.1}**

Bwana anasema nini katika sura ya hamsini na nane ya Isaya? Sura nzima ni ya umuhimu wa juu mno. - *Testimonies for the Church 8:159.* **{WM 29.2}**

Nimeagizwa kuwaelekeza watu wetu katika sura ya hamsini na nane ya Isaya. Soma sura hii kwa makini na uelewe aina ya huduma ambayo italeta uzima katika makanisa. Kazi ya injili inapaswa

kufanywa kwa njia ya ukarimu wetu na pia kwa kazi zetu. Unapokutana na roho zinazoteseka ambazo zinahitaji msaada, wape msaada huo. Na mtakapowakuta wale walio na njaa walisheni. Kwa kufanya hivi utakuwa unafanya kazi katika mielekeo ya huduma ya Kristo. Kazi takatifu ya Bwana ilikuwa ni kazi ya ukarimu na wema. Hebu watu wetu kila mahali wahimizwe kushiriki katika kazi hii. - *Manuscript* 7, 1908. **{WM 29.3}**

Kazi Iliyoainishwa.-Tafadhali soma Isaya 58: “Je! Kufunga namna hii ni saumu niliyoichagua Mimi? Je! Ni siku ya mtu kujitaabisha nafsi yake? Ni kuinama kichwa kama unyasi, na kutanda nguo za magunia na majivu chini yake? Je! Utasema ni siku ya kufunga, na ya kukubaliwa na Bwana? Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna

hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe? Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde. Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, Naye atasema, Mimi hapa. Kama ukiiondoa nira; isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu; na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka

gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui. **{WM 29.4}**

Hii ndiyo kazi maalum sasa iliyoko mbele yetu. Kuomba kwetu kote na kujizuia kula chakula hakutakuwa na faida yoyote isipokuwa tumeishikilia kazi hii kwa kudhamiria na uthabiti. Wajibu mtakatifu uko juu yetu. Kazi yetu imetajwa waziwazi. Bwana amesema nasi kupitia kwa nabii Wake. Mawazo ya Bwana na njia Zake si kama yale ya wanadamu vipofu, wenye ubinafsi wanayoamini kuwa ndivyo yalivyo au kama vile ambavyo

wangetamani yawe. Bwana huangalia moyo. Kama ubinafsi unaishi humo, Yeye anaujua. Tunaweza kujitahidi kuficha tabia yetu ya kweli kwa ndugu na dada zetu, lakini Mungu anajua. Hakuna kitu kinachoweza kufichwa Kwake. **{WM 30.1}**

Saumu ambayo Mungu anaweza kuikubali imeelezwa. Ni kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliofukuzwa nyumbani kwako. Usingojee waje kwako. Si juu yao kujitahidi au kuhenyeka kukutafuta wewe ulipo na kukusihi kuhusu kupata maskani kwa ajili yao wenyewe. Wewe unapaswa kuwatafuta na kuwaleta nyumbani kwako. Unapaswa kuitoa roho yako kwa ajili yao. Kwa mkono mmoja unatakiwa kuunyosha na kwa imani uushike mkono *Ule* wenye nguvu

ambao unaleta wokovu, wakati kwa mkono mwingine wa upendo unawafikia wale walioonewa na kuwafariji. Haiwezekani kwako kujifunga katika mkono wa Mungu kwa mkono mmoja wakati mkono mwingine unatumika kuhudumia furaha au anasa zako mwenyewe. **{WM 30.2}**

Ikiwa utashiriki katika kazi hii ya rehema na upendo, je kazi hiyo itathibitika kuwa ngumu sana kwako? Je! Utashindwa, na kupondwapondwa na kulemewa na mzigo huo, na familia yako kunyimwa msaada na mvuto wako? La, hasha; Mungu kwa uangalifu ameondoa mashaka yote juu ya swali hili, kwa kutoa ahadi kwako kwa sharti la utii wako. Ahadi hii inajumuisha yote ambayo yule ambaye ni bahili mno, ambaye anasita mno, angeweza

kutamani. "Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara." Amini tu kwamba Yeye ni Mwaminifu ambaye ameahidi. Mungu anaweza kufanya upya nguvu ya kimwili. Na zaidi, anasema kuwa atafanya hivyo. Na ahadi hii haiishii hapa. "Haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma." Mungu atajenga ngome kukuzunguka wewe. Ahadi hii haiishii hata hapa. “Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, Naye atasema, Mimi hapa.” Ikiwa utanyamazisha uonevu na kuondoa kunena kwa ubatili, ikiwa utasogeza roho yako karibu na wenye njaa, "basi nuru yako itainuka katika giza, na giza lako litakuwa kama adhuhuri; na Bwana atakuongoza daima, na kuishibisha nafsi yako wakati wa ukame [njaa], na

kunenepesha mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ya maji, ambayo maji yake hayapungui."— *Testimonies for the Church* 2:33-35. **{WM 31.1}**

Marekebisho ya Mara Mbili ya Isaya 58. - Kazi iliyoelezwa bayana katika Maneno haya [Isaya 58] ni kazi ambayo Mungu anataka watu Wake waifanye. Ni kazi iliyoagizwa na Mungu Mwenyewe. Pamoja na kazi ya kutetea amri za Mungu na kurekebisha ufa ambao umefanywa katika sheria ya Mungu, sisi tunapaswa kuchanganya huruma kwa wanadamu wanaoteseka. Tunapaswa kuonesha upendo mkuu kabisa kwa Mungu; tunapaswa kuitukuza kumbukizi Yake, ambayo imekanyagwa na miguu isiyo mitakatifu; na pamoja na hili tunapaswa

kudhihirisha rehema, wema, ukarimu, na huruma nyororo/laini kabisa kwa jamii iliyoanguka. "Mpende jirani yako kama nafsi yako." Kama kanisa ni lazima tuishike kazi hii. Upendo uliodhihirishwa kwa wanadamu wanaoteseka hutoa umuhimu na nguvu kwa ile Kweli.- *Special Testimonies, series* A, no. 10, uk. 3, 4. **{WM 32.1}**

Tafsiri ya Kweli ya Injili. - Ni kwa shauku isiyo na ubinafsi peke yake kwa wale wanaohitaji msaada ndipo tunapoweza kutoa uthibitisho wa busara juu ya Ukweli wa injili. “Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi, na kupungukiwa na riziki, na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba; lakini asiwape mahitaji ya mwili; yafaa nini? Vivyo hivyo na imani, isipokuwa

ina matendo, imekufa nafsini mwake. “Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo.” **{WM 32.2}**

Mambo mengi zaidi ya kuhubiri peke yake yamejumuishwa pamoja na kuhubiri injili. Wasiojua wanapaswa kuelimishwa; waliokata tamaa wanapaswa kuinuliwa; wagonjwa wanapaswa kuponywa. Sauti ya mwanadamu inapaswa kutenda sehemu yake katika kazi ya Mungu. Maneno ya upole, laini, huruma, na upendo yanapaswa kuushuhudia Ukweli. Maombi yenye bidii na ya dhati yanapaswa kuwaleta malaika karibu....

Bwana atakupa mafanikio katika kazi hii; ... imesokotwa pamoja na maisha ya kiutendaji, pale mtu anapoiishi na

kuitekeleza. Muunganiko wa kazi kama ya Kristo kwa mwili na kazi kama ya Kristo kwa roho ndiyo tafsiri ya kweli ya injili. - *The Review and Herald*, Machi 4, 1902. **{WM 32.4}**

Shauri Liko Wazi. - Sina hofu kwa wafanyakazi ambao wanahusika katika kazi inayowakilishwa katika sura ya hamsini na nane ya Isaya. Sura hii iko wazi, na inatosha kumwelimisha mtu yeyote anayetaka kufanya mapenzi ya Mungu. Kuna fursa tele kwa kila mtu kuweza kuwa baraka kwa binadamu. Ujumbe wa malaika wa tatu haupaswi kupewa nafasi ya pili katika kazi hii, bali inapaswa kuwa umoja pamoja nayo. Kunaweza kuwapo, na ipo, hatari ya kuzika kanuni kuu za Ukweli wakati wa kufanya kazi ambayo ni sahihi kuifanya. Kazi hii inapaswa kuwa kwa ujumbe kile

ambacho mkono unakuwa kwa mwili. Mahitaji ya kiroho ya nafsi yanapaswa kuwekwa wazi siku zote. - *Letter* 24, 1898. **{WM 33.1}**

Kazi Yetu Iliyopangwa na Mungu. - Siwezi kuwahimiza washiriki wetu wote wa kanisa kwa nguvu zaidi ya hivi navyofanya, wote ambao ni wamisionari wa kweli, wote wanaouamini ujumbe wa malaika wa tatu, wote wanaogeuza miguu yao mbali na Sabato, kuzingatia ujumbe huu wa sura ya hamsini na nane ya Isaya. Kazi ya ukarimu iliyoagizwa katika sura hii ni kazi ambayo Mungu anawahitaji watu Wake wapate kuifanya kwa wakati huu. Ni kazi aliyoipanga Yeye Mwenyewe. Hatujaachwa katika mashaka juu ya mahali gani ujumbe huu unahusika, na wakati wa utimilifu wake dhahiri, kwani

tunasoma: "Na watu wako watapajenga mahali palipokuwa ukiwa; utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, mwenye kurejeza njia za kukalia." Aya ya 12. Kumbukizi ya Mungu, Sabato ya siku ya saba, ishara ya kazi Yake ya kuuumba ulimwengu, imehamishwa na mtu wa dhambi. Watu wa Mungu wana kazi maalum ya kufanya katika kuurekebisha ufa ambao umefanywa katika sheria Yake; na kadiri tunavyokaribia mwisho, ndivyo kazi hii inavyozidi kuwa muhimu. Wote wanaompenda Mungu wataonesha kwamba wanabeba ishara Yake kwa kuzishika amri Zake....**{WM 33.2}**

Kanisa linapokubali kazi yake iliyopewa/iliyopangwa na Mungu, ahadi ni hii: “Ndipo nuru yako

itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde”— *Testimonies for the Church* 6: 265-267. **{WM 34.1}**

Sura ya Nne - Hii Ndio Dini Safi

Dini Safi Inafafanuliwa. - Dini iliyo safi ni ipi? Kristo ametuambia kwamba dini safi ni zoezi la huruma, kusikitika na wale walio shidani, wema, na upendo nyumbani, kanisani, na ulimwenguni. Hii ndio aina ya dini ambayo watoto wanapaswa kufundishwa, nayo ni makala ya kweli/halisi. Wafundishe kwamba

hawapaswi kuweka mawazo yao juu ya wao wenyewe, bali kwamba popote penye hitaji la kibinadamu na mateso, hapo pana uwanja wa kazi ya umisionari.-*The Review and Herald*, Novemba 12, 1895. **{WM 35.1}**

Dini iliyo safi na isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii: “Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.” Matendo mema ndio matunda ambayo Kristo anahitaji tupate kuyazaa: maneno mazuri, matendo ya ukarimu na wema, yale y a kuwajali maskini, wahitaji, wenye dhiki. Pale mioyo inapoihurumia mioyo iliyolemewa na kukata tamaa na huzuni, pale mkono unapotoa msaada kwa wahitaji, pale walio uchi wanapovalishwa, mgeni au mtu baki usiyemjua, anapokaribishwa

kwenye kiti katika sebule yako na mahali katika moyo wako, malaika watakuja karibu sana hapo, na wimbo wa kujibu unaitikiwa mbinguni. - *Testimonies for the Church* 22:25. **{WM 35.2}**

Mtihani wa Mungu kwa Dini Yetu. - Nimeoneshwa mambo kadhaa kuhusiana na wajibu wetu kwa wasiojiweza ambayo ninahisi ni wajibu wangu kuyaandika kwa wakati huu. **{WM 35.3}**

Niliona kwamba ni katika majaliwa ya Mungu kwamba wajane na yatima, vipofu, viziwi, vilema, na watu wanaoteseka kwa namna mbalimbali wamewekwa katika uhusiano wa karibu wa Kikristo na kanisa Lake; ni kwa ajili ya kuwathibitisha watu Wake na kukuza tabia yao ya kweli. Malaika wa Mungu

wanatazama kuona jinsi tunavyowatendea watu hawa ambao wanahitaji huruma, upendo, na fadhili zetu zisizo na upendeleo. Huu ndio mtihani wa Mungu kwa tabia zetu. Ikiwa tuna dini ya kweli ya Biblia, tutahisi kuwa deni la upendo, fadhili, na shauku ni haki ya Kristo kwa niaba ya ndugu zake; na hatuwezi kufanya chochote pungufu ya kuonesha shukrani zetu kwa upendo wake usiopimika kwetu wakati tulipokuwa wenye dhambi wasiostahili neema yake, kwa kuwa na shauku ya kina na upendo usio na ubinafsi kwa wale ambao ni ndugu zetu na ambao hawana bahati kama sisi wenyewe. – *Testimonies for the Church*3:511. **{WM 35.4}**

Nuru Yako Inang'aaje? - Wale ambao wangepaswa kuwa nuru ya

ulimwengu wameangaza miale iliyo hafifu na dhaifu/gonjwa. Nuru ni nini? Ni uchaji Mungu, wema, Ukweli, rehema, upendo; ni kudhihirisha ile Kweli katika tabia na maisha. Injili inategemea uchaji Mungu wa mtu binafsi wa waumini wake kwa ajili ya nguvu yake ya kutaka maendeleo, na Mungu ametoa riziki kupitia kifo cha Mwanawe mpendwa, ili kila roho iweze kuandaliwa kwa ajili ya kila kazi nzuri. - *The Review and Herald*, Machi 24, 1891. **{WM 36.1}**

Ishara Inayotofautisha Dini ya Kweli na ya Uongo. - Huruma ya kweli kati ya mwanadamu na mwanadamu mwenzake inapaswa kuwa ishara ya kutofautisha wale

wanaompenda na kumcha Mungu kutoka kwa wale ambao hawazingatii sheria Yake. Ni huruma kubwa kiasi gani ambayo Kristo alionyesha kwa kuja katika ulimwengu huu ili kutoa maisha Yake kama dhabihu kwa ajili ya ulimwengu unaangamia! Dini Yake iliongoza katika kufanya kazi halisi ya umisionari wa tiba. [Msomaji anapaswa kukumbuka kwamba neno "kazi ya umisionari wa tiba" kama linavyotumiwa mara nyingi na Bi White ilipanuka ng'ambo ya mipaka ya huduma ya matibabu ya kitaalamu ili kujumuisha matendo yote ya rehema na ukarimu usio na ubinafsi (fadhili isiyo na upendeleo)-Wakusanyaji.] Yeye alikuwa ni uweza uponyao. "Nataka rehema, wala si sadaka," Alisema. Hili ndilo jaribio ambalo Mwanzilishi Mkuu

wa Ukweli alitumia kutofautisha kati ya dini ya Kweli na ya uwongo. - *Manuscript* 117, 1903.**{WM 36.2}**

Huruma kwa Vitendo ni Jaribio la Utakaso. - Shetani anacheza mchezo wa maisha kwa kila nafsi. Anajua kwamba huruma kwa vitendo ni jaribio la usafi na kutokuwa na ubinafsi kwa moyo, na atafanya kila juhudi iwezekanayo kufunga mioyo yetu kwa mahitaji ya wengine, ili hatimaye tusiweze kusukumwa kwa kuona mateso. Ataleta mambo mengi kuzuia onesho la upendo na huruma. Hivyo ndivyo alivyomharibu Yuda. Yuda daima alikuwa akipanga kujinufaisha mwenyewe. Katika hili yeye anawakilisha tabaka kubwa la wanaokiri kuwa Wakristo leo. Kwa hivyo tunahitajika kujifunza mfano wake.

Tuko karibu na Kristo kama alivyokuwa. Hata hivyo bado, kama ilivyokuwa kwa Yuda, ushirika na Kristo hautufanyi tuwe wamoja Naye, ikiwa haukuzi ndani ya mioyo yetu huruma ya dhati kwa ajili ya wale ambao Kristo alitoa maisha Yake kwao, tuko katika hatari sawa na ilivyokuwa kwa Yuda ya kuwa nje ya Kristo, windo la majaribu ya Shetani. **{WM 37.1}**

Tunahitajika kujilinda dhidi ya mkengeuko wa kwanza kutoka katika haki; kwa kuwa kosa moja, kupuuza mara moja kudhihirisha roho ya Kristo, hufungua njia kwa nyingine na nyingine tena, mpaka akili itakapotawaliwa na kanuni za adui. Ikiwa italelewa na kukuzwa, roho ya ubinafsi itakuwa shauku ya kuteketeza ambayo hakuna kitu isipokuwa nguvu ya Kristo peke

yake inaweza kuitiisha. - *Testimonies for the Church* 6:264, 265. **{WM 37.2}**

Dini Safi ni Kufanya Matendo ya Rehema na Upendo. - Ucha Mungu wa kweli hupimwa kwa kazi iliyofanywa. Taaluma au kukiri tu peke yake si kitu (maneno matupu toka mdomoni si kitu); cheo si kitu; tabia kama tabia ya Kristo ndio ushahidi kwamba Mungu amemtuma Mwanawe ulimwenguni. Wale wanaokiri kuwa Wakristo, na bado hawatendi kama ambavyo Kristo angetenda, iwapo angekuwa katika nafasi yao, hakika wanalidhuru sana kusudi la Mungu. Wanamwakilisha Mwokozi wao vibaya, na wamesimama chini ya bendera isiyo halali-wanajifanya

kuwa tofauti na jinsi walivyo....**{WM 37.3}**

Dini iliyo safi na isiyo na taka si hisia, bali ni kutenda kazi za huruma na upendo. Dini hii ni muhimu kwa ajili ya afya na furaha. Huingia katika hekalu la roho lililochafuliwa, na kwa mjeledi huwafukuza waingiaji wenye dhambi wasiotakiwa. Ikichukua kiti cha enzi, huweka wakfu yote kwa uwepo wake, ikiumulika moyo kwa miale inayong'aa ya Jua la Haki. Inayafungua madirisha ya roho kuelekea mbinguni, ikiruhusu mwangaza wa upendo wa Mungu kuingia ndani. Pamoja nayo huja utulivu na umakini. Nguvu za kimwili, kiakili, na kimaadili huongezeka, kwa sababu angahewa ya mbinguni kama wakala aliye hai, mwenye bidii huijaza roho. Kristo anaumbwa ndani, tumaini la

utukufu. - *The Review and Herald*, Oktoba 15, 1901.**{WM 38.1}**

Kuwa mvuja jasho, kuendelea kwa uvumilivu katika kutenda mema ambako huhitaji kazi ya kujikana nafsi, ni kazi tukufu, ambayo Mbingu inatabasamu kwa ajili yake. Kazi ya uaminifu inakubalika zaidi kwa Mungu kuliko ibada inayofanywa kwa moyo na kudhaniwa kuwa takatifu kabisa. Ni katika kufanya kazi pamoja na Kristo, ndiko ambako ni ibada ya Kweli. Sala, kusihi, na mazungumzo ni matunda ya bei hafifu (yasiyo na gharama), ambayo mara nyingi huhusishwa pamoja; lakini matunda ambayo hudhihirishwa katika matendo mema, katika kuwatunza wahitaji, yatima, na wajane, ni matunda ya Kweli, na hukua kwa kawaida kwenye

mti mzuri. - *Testimonies for the Church* 2:24.**{WM 38.2}**

Je, Sisi ni Watoto wa Mungu? - Si huduma inayofaa ambayo Mungu anaikubali; si mipasuko ya kimhemko ya uchaji Mungu ambayo inatufanya kuwa watoto wa Mungu. Yeye Anatuita sisi kufanya kazi kwa kanuni zilizo za Kweli, thabiti, na za kudumu. Ikiwa Kristo ataumbwa ndani, tumaini la utukufu, Yeye atafunuliwa katika tabia, itafanana na ya Kristo. Tunapaswa kumwakilisha Kristo kwa ulimwengu, kama Kristo alivyomwakilisha Baba. - *The Review and Herald*, Januari 11, 1898.**{WM 38.3}**

Tunatakiwa kuonesha wema wa Kikristo na ukunjufu wa moyo wa kweli, si kana kwamba tunafanya kitu fulani

cha ajabu, bali kile tu ambacho tungemtarajia Mkristo yeyote wa Kweli afanye kwa upande wetu wenyewe kama tungeliwekwa katika hali kama hiyo. - *Letter* 68, 1898.**{WM 39.1}**

Tusichoke katika Kutenda Mema. - Mara nyingi juhudi zetu kwa ajili ya wengine zinaweza kupuuzwa, au zisionekane au hata kuonekana kupotea kabisa. Lakini hii haipaswi kuwa udhuru kwetu kuchoka katika kutenda mema. Ni mara ngapi Yesu amekuja kutafuta matunda katika mimea iliyo chini ya utunzaji Wake, na hakupata chochote isipokuwa majani! Tunaweza kukatishwa tamaa na matokeo ya juhudi zetu bora, lakini hii haipaswi kutuongoza katika kutokujali shida za wengine na kutokufanya chochote. “Ulaani Merozi, alisema malaika wa

Bwana, Walaanini kwa uchungu wenyeji wake; Kwa maana hawakuja kumsaidia Bwana, Kumsaidia Bwana juu ya hao wenye nguvu.” Waamuzi 5:26 — *Testimonies for the Church* 3:525.**{WM 39.2}**

Katika Kuwatendea Wengine Tunamtendea Kristo. - Kutokana na kile kilichooneshwa kwangu, watunza Sabato wanazidi kuwa wabinafsi kadiri wanavyozidi kuongezeka utajiri. Upendo wao kwa Kristo na watu Wake unapungua. Hawaoni mahitaji ya wahitaji, wala hawahisi mateso na huzuni zao. Hawatambui kwamba katika kuwapuuza maskini na wanaoteseka wanamsahau Kristo, na kwamba katika kutuliza mahitaji na mateso ya maskini kadiri inavyowezekana, wanamhudumia Yesu....

“Kisha atawaambia na wale walioko mkono Wake wa kushoto, Ondokeni Kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake; kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula; nalikuwa na kiu, msininyweshe; nalikuwa mgeni, msinikaribishe; nalikuwa uchi, msinivike; nalikuwa mgonjwa, na kifungoni, msije kunitazama. Ndipo hao pia watajibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona Wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au U uchi, au U mgonjwa, au U kifungoni, tusikuhudumie? Naye atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea Mimi. Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki

watakwenda katika uzima wa milele" Mathayo 25:41-46. **{WM 39.4}**

Yesu hapa anajitambulisha pamoja na watu Wake wanaoteseka. Ni Mimi niliyekuwa na njaa na kiu. Ni Mimi niliyekuwa mgeni. Ni Mimi niliyekuwa uchi. Ni Mimi niliyekuwa mgonjwa. Ni Mimi niliyekuwa gerezani. Pale ulipokuwa unafurahia chakula kutoka katika meza yako iliyotandazwa na kusheheni vyakula, Mimi nilikuwa ninataabika na njaa katika kibanda kibovu au katika mtaa ambao haukuwa mbali na wewe. Ulipofunga milango yako dhidi Yangu, huku vyumba vyako vilivyopambwa vizuri vilikuwa havina wakaaji, mimi sikuwa na mahali pa kuweka kichwa Changu. Kabati lako la nguo lilikuwa limejazwa na wingi wa masuti ya nguo za kubadilisha, ambazo

kwa ajili yake fedha zilitapanywa, ambazo ungeweza kuwapa wahitaji. Mimi nilikuwa mhitaji wa nguo ya kuridhisha. Ulipokuwa ukifurahia afya, mimi nilikuwa mgonjwa. Majanga na bahati mbaya zilinitupa mimi gerezani na kunifunga kwa pingu, ikiinamisha roho yangu, ikininyima uhuru na tumaini, huku wewe ukitangatanga kwa kuwa na uhuru. Ni umoja ulioje ambao Yesu hapa anauelezea kuwa upo kati Yake na wanafunzi Wake wanaoteseka! Yeye anafanya hali yao kuwa Yake Mwenyewe. Yeye Anajitambulisha Mwenyewe kama kwa nafsi Yake Yeye Mwenyewe Ndiye mtu yule hasa anayeteseka. Zingatia, wewe Mkristo mbinafsi: kila kumpuuza maskini mhitaji, yatima, wasio na baba, ni

kumpuuza Yesu Mwenyewe katika nafsi zao. **{WM 40.1}**

Ninawafahamu watu ambao hufanya madai ya hali ya juu, ambao mioyo yao imefungiwa sana katika kujipenda nafsi na ubinafsi kiasi kwamba hawawezi kufahamu kile ninachoandika. Katika maisha yao yote wamefikiri na kuishi kwa ajili ya nafsi tu. Kujitoa mhanga kwa ajili ya kuwatendea wengine mema, kwa kupata hasara wao wenyewe ili wengine wapate faida, ni jambo lisilowezekana kwao. Hawana wazo hata kidogo kwamba Mungu anahitaji hili kutoka kwao. Nafsi ndio sanamu yao. Majuma ya thamani, miezi, na miaka inapita kuwa umilele, lakini hawana rekodi mbinguni ya matendo ya fadhila, ya kujitoa mhanga kwa ajili ya mema ya wengine, ya kuwalisha wenye njaa,

kuwavisha walio uchi, au kumkaribisha mgeni. Huku kuwakaribisha/kuwakirimu wageni kwa kubahatisha hakupendezi. Na lau kama wangelijua kuwa wale ambao walitaka kushiriki ukarimu wao ni watu waliostahili, ndipo huenda wangelivutwa kufanya jambo fulani katika mwelekeo huu. Lakini kuna fadhila katika kujaribu kufanya jambo fulani. Huenda kwa bahati tu, sisi tunaweza kuwakaribisha malaika. - *Testimonies for the Church* 2:24.**{WM 40.2}**

Sura ya Tano - Mfano wa Msamaria Mwema

Asili ya Dini ya Kweli Inaelezwa.-Katika kisa cha Msamaria mwema, Kristo anaeleza kwa mfano asili ya dini ya Kweli. Yeye Anaonyesha kwamba haitegemei mifumo, kanuni za imani, au kaida za ibada, bali hutegemea utendaji wa matendo ya upendo, ya kuleta mambo makubwa kabisa ya kufaa kwa wengine, katika wema wa Kweli.... Somo hili halihitajiki kwa upungufu katika ulimwenguni wa leo kuliko wakati lilipoanguka kutoka katika midomo ya Yesu. Ubinafsi na urasimu baridi zimezima kabisa moto wa upendo na kuondoa neema zile ambazo zilipaswa kufanya tabia kuwa na harufu nzuri.

Wengi wanaolikiri Jina Lake wamepoteza kuona ule Ukweli kwamba Wakristo wanapaswa kumwakilisha Kristo. Isipokuwa kuna kujitoa kiutendaji kwa ajili ya manufaa ya wengine, katika duru ya familia, katika ujirani, kanisani, na popote tulipo, basi hata tukikiri jinsi gani sisi si Wakristo. -*The Desire of Ages*, 497, 504. **{WM 42.1}**

Jirani Yangu ni Nani? — Miongoni mwa Wayahudi swali, "Jirani yangu ni nani?" lilisababisha mabishano yasiyoisha. Hawakuwa na shaka juu ya wapagani na Wasamaria. Hawa walikuwa wageni na maadui. Lakini tofauti inapaswa kuwa wapi kati ya watu wa taifa lao wenyewe, na kati ya

matabaka tofauti ya jamii? Kuhani, rabi, na mzee, wanapaswa kumchukulia nani kama jirani? Walitumia maisha yao katika mzunguko wa maadhimisho ili kujifanya safi. Kugusana na umati wa wasiojua na wazembe, walifundisha kuwa, kungeleta unajisi ambao ungelihitaji juhudi za kuchosha kuweza kuuondoa. Je, walipaswa kuwachukulia "wasio safi" kama majirani? **{WM 42.2}**

Swali hili Kristo alilijibu katika mfano wa Msamaria mwema. Alionesha kwamba jirani yetu hamaanishi mtu fulani tu ambaye ni mmojawapo katika kanisa letu au imani ambayo sisi tunayo. Hairejelei tofauti ya jamii, rangi, au tabaka. Jirani yetu ni kila mtu anayehitaji msaada wetu. Jirani yetu ni kila nafsi iliyojeruhiwa na kuchubuliwa

na adui. Jirani yetu ni kila mtu ambaye ni mali ya Mungu. -*Christ's Object Lessons*, 376. **{WM 43.1}**

Imeelezwa kwa Kielelezo na Mfano. - Kristo alikuwa akizungumza na kusanyiko kubwa. Mafarisayo, wakitumaini kupata kitu kutoka kwa midomo Yake ambacho wangeweza kukitumia kumhukumu (kumnasa), walimtuma mwanasheria mmoja Kwake akiwa na swali, "Nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" Kristo alisoma mioyo ya Mafarisayo kama kitabu cha wazi, na jibu Lake kwa muuliza swali lilikuwa, “Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje? Akajibu, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa nguvu zako zote na kwa akili zako zote; na, jirani yako kama nafsi yako."**{WM 43.2}**

"Umejibu vema," Kristo alisema; "Fanya hivi, nawe utaishi." Mwana-sheria alijua kwamba kwa jibu lake mwenyewe alikuwa amejihukumu mwenyewe. Alijua kwamba hakumpenda jirani yake kama nafsi yake. Lakini akitaka kujidai kuwa mwenye haki, aliuliza, "Jirani yangu ni nani?"**{WM 43.3}**

Kristo alijibu swali hili kwa kusimulia tukio, ambalo kumbukumbu yake ilikuwa mpya katika akili za wasikilizaji Wake. — *Manuscript* 117, 1903. **{WM 43.4}**

"Mtu mmoja," alisema, "alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi; wakamvua nguo, wakamtia jeraha,

wakaenda zao, wakimwacha karibu ya kufa" **{WM 43.5}**

Katika kusafiri kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko, msafiri alilazimika kupita katika sehemu ya jangwa la Yudea. Barabara iliongoza chini ya bonde lisilokaliwa, lenye miamba, ambalo lilisheheni wanyang'anyi na mara nyingi lilikuwa ni eneo la vurugu zenye ukatili. Ilikuwa ni hapa ambapo msafiri alishambuliwa, akavuliwa kila kitu kilichokuwa cha thamani, na kuachwa kando ya njia akiwa hoi au (nusu mfu). Akiwa amelala hivyo, kuhani alipita njia hiyo; akamwona yule mtu amelala akiwa amejeruhiwa na kuchubuliwa, ametota katika damu yake mwenyewe; lakini alimwacha bila msaada wowote. "Alipita kando." Ndipo Mlawi mmoja akatokea. Akiwa na hamu

ya kujua ni nini kilichotokea, alisimama na kumtazama yule mgonjwa anayeteseka. Alisadikishwa kuhusu kile alichopaswa kufanya, lakini haikuwa jukumu linalokubalika. Alitamani kwamba asingeipita njia hiyo, ili asimwone yule mtu aliyejeruhiwa. Alijishawishi mwenyewe kwamba suala hilo halikuwa ni jukumu lake, na yeye pia "akapita kando." **{WM 44.1}**

Bali Msamaria, akisafiri kwenye barabara hiyo hiyo, alimwona yule majeruhi, na alifanya kazi ambayo wengine walikuwa wamekataa kuifanya. Kwa upole na huruma alimhudumia mtu aliyejeruhiwa. "Alipomwona alimhurumia, akakaribia, akamfunga jeraha zake, akizitia mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni,

akamtunza. Hata siku ya pili akatoa dinari mbili, akampa mwenye nyumba ya wageni, akisema, Mtunze huyu, na cho chote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa.” Kuhani na Mlawi wote wawili walikiri uchaji Mungu, lakini Msamaria alionesha kwamba alikuwa ameongoka kweli kweli. Haikuwa inakubalika zaidi kwake kufanya kazi hiyo kuliko kwa kuhani na Mlawi, bali katika roho na matendo alijidhihirisha kuwa katika upatanifu na Mungu. **{WM 44.2}**

Katika kutoa somo hili Kristo aliwasilisha kanuni za sheria kwa njia ya moja kwa moja, yenye nguvu, akiwaonesha wasikilizaji Wake kwamba walikuwa wamepuuza kutekeleza kanuni hizi. Maneno Yake yalikuwa wazi na yaliyoelekezwa kiasi kwamba wasikilizaji

hawakuweza kupata fursa ya kuyalalamikia. Mwana-sheria hakuona chochote katika somo ambacho angeweza kukosoa. Hisia zake za ubaguzi na chuki kuhusu Kristo ziliondolewa. Lakini hakuwa ameishinda chuki yake ya kitaifa vya kutosha kiasi cha kuweza kutoa sifa kwa Msamaria kwa jina. Kristo alipouliza, "Waonaje wewe, katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi?" akajibu, "Ni huyo aliyemwonea huruma." **{WM 44.3}**

"Yesu akamwambia, Enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo." Onesha wema kama huo kwa wale wanaouhitaji. Ndivyo utatoa ushahidi kwamba unaishika sheria yote. -*Christ Object Lessons*, 379, 380. **{WM 45.1}**

Mtu Yeyote Mwenye Hitaji Ni Jirani Yetu. - Mtu yeyote ambaye anahitaji huruma yetu na huduma yetu ya wema ni jirani yetu. Wanaoteseka na mafukara wa matabaka yote ni majirani zetu; na pale mahitaji yao yanapoletwa kwetu, ni wajibu wetu kuyatuliza kwa kadiri iwezekanavyo. - *Testimonies for the Church* 4:226, 227.**{WM 45.2}**

Kwa mfano huu wajibu wa mwanadamu kwa mwanadamu mwenzake umeamuliwa milele. Tunapaswa kujali kila hali ya mateso na kujiangalia sisi wenyewe kama mawakala wa Mungu kwa ajili ya kuwapa afueni na kuwasaidia wahitaji kwa uwezo wetu wote. Tunapaswa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Kuna wengine ambao wanaonesha upendo mkubwa kwa jamaa zao, kwa marafiki

na wapenzi wao, ambao bado wanashindwa kuwa wema na wenye kuwafikiria wale wanaohitaji huruma, ambao wanahitaji wema na upendo. Kwa mioyo ya dhati hebu na tuulize, Jirani yangu ni nani? Majirani zetu si tu washirika wetu na marafiki maalum; si tu wale ambao ni wa kanisa letu, au wale ambao wanafikiri kama sisi. Majirani zetu ni familia nzima ya wanadamu. Tunapaswa kuwatendea mema watu wote, na hasa jamaa ya waumini. Tunapaswa kuupa ulimwengu onesho la nini inamaanishwa kuibeba sheria ya Mungu. Tunapaswa kumpenda Mungu zaidi ya vyote na jirani yetu kama nafsi zetu wenyewe. - *The Review and Herald*, Januari 1, 1895. **{WM 45.3}**

Dini ya Kweli Yawakilishwa Isivyo Sahihi.- Kuhani na Mlawi

walikuwa wakienda kwa ajili ya ibada Hekaluni, ambalo utumishi wake ulipangwa na Mungu Mwenyewe. Kushiriki katika huduma hiyo ilikuwa ni fursa kubwa na iliyotukuka, na kuhani na Mlawi waliona kwamba kwa kuheshimiwa hivyo, hawakustahili kumhudumia mgonjwa asiyejulikana kando ya njia. Hivyo walipuuza fursa ya pekee ambayo Mungu alikuwa amewapa kama mawakala Wake kumbariki mwanadamu mwenzao.**{WM 46.1}**

Wengi leo wanafanya kosa kama hilo. Wanatenganisha majukumu yao katika matabaka mawili dhahiri. Tabaka moja linatengenezwa na vitu vikubwa, vinavyopaswa kudhibitiwa na sheria ya Mungu; tabaka lingine linatengenezwa na vitu vinavyoitwa vidogo, ambavyo juu yake amri, "Mpende jirani yako kama

nafsi yako," inapuuzwa. Uwanja huu wa kazi umeachwa kubadilika badilika, kulingana na mwelekeo au msukumo. Hivyo tabia inaharibiwa, na dini ya Kristo inawakilishwa vibaya.**{WM 46.2}**

Wapo wale ambao wangedhani kuwa ni kujishusha hadhi kuwahudumia binadamu wanaoteseka. Wengi huwatazama kwa kutokuwajali na dharau wale ambao wameyalaza mahekalu ya roho katika uharibifu (waraibu nk). Wengine huwapuuza maskini kutokana na sababu tofauti. Wanafanya kazi, wanavyoamini, katika kusudi la Kristo, wakijitahidi kujenga jambo fulani linalostahili heshima. Wanajisikia kwamba wanafanya kazi kubwa, na hawawezi kuiacha ili kuweka maanani mahitaji ya maskini na wenye

dhiki. Katika kuendeleza kazi yao inayodhaniwa kuwa ni kubwa wanaweza hata kuwakandamiza maskini. Wanaweza kuwaweka katika hali ngumu na yenye kujaribu, kuwanyima haki zao, au kupuuza mahitaji yao. Na bado wakahisi kwamba hii yote ni halali kwa sababu, kama wanavyodhani, wanaendeleza kusudi la Kristo. - *Christ Object Lessons*, 382, 383.**{WM 46.3}**

Masharti Yenye Athari Nyingi ya Sheria ya Mungu. - Kumwacha jirani anayeteseka bila kufarijiwa ni uvunjaji wa sheria ya Mungu. Mungu alimfanya kuhani kupita njia hiyo ili kwa macho yake mwenyewe aweze kuona jambo ambalo lilihitaji rehema na msaada; lakini kuhani, ingawa alikuwa na kibarua/ofisi ya huduma takatifu, ambayo kazi yake ilikuwa ni kutoa

rehema na kutenda mema, alipita kando. Tabia yake ilioneshwa katika asili yake halisi mbele ya malaika wa Mungu. Kwa kujifanya angeweza kuomba kwa muda mrefu, lakini hakuweza kushika kanuni za sheria katika kumpenda Mungu kwa moyo wake wote na jirani yake kama nafsi yake. Mlawi alikuwa ni wa kabila moja na yule mgonjwa aliyejeruhiwa, aliyechubuliwa. Mbingu zote zilimtazama Mlawi alipokuwa akipita katika barabara ile, ili kuona kama moyo wake ungeguswa na shida ya mwanadamu. Alipomwona mtu yule alisadikishwa juu ya kile alichopaswa kukifanya; lakini kwa kuwa halikuwa jukumu la kupendeza, alitamani asingeipita njia hiyo, hivyo asingelazimika kumwona mtu aliyejeruhiwa na kuchubuliwa, aliye uchi

na mwenye kuangamia, na mwenye kuhitaji sana msaada kutoka kwa wenzake. Kisha aliendelea na safari yake, akishawishika kwamba haikumhusu kabisa, na kwamba hakuwa na haja ya kujisumbua juu ya hali hiyo. Akidai kuwa mfafanuzi wa sheria, kuwa mhudumu katika vitu vitakatifu, bado alipita kando.**{WM 47.1}**

Akiwa ametunzwa na nguzo ya wingu, Bwana Yesu alitoa agizo maalum kuhusu utendaji wa matendo ya huruma kwa mwanadamu na mnyama. Wakati ambapo sheria ya Mungu inahitaji upendo mkuu kabisa kwa Mungu na upendo usio na upendeleo kwa majirani zetu, masharti yake yenye athari nyingi pia huhusisha viumbe bubu ambavyo haviwezi kuelezea kwa maneno mahitaji au mateso yao. "Umwonapo punda wa

nduguyo au ng'ombe wake ameanguka kando ya njia, usijifiche kama usiyemwona; sharti umsaidie kumwinua tena." Yeye ambaye anampenda Mungu si tu atawapenda wanadamu wenzake bali pia atawajali kwa huruma viumbe ambavyo Mungu ameviumba. Roho wa Mungu anapokuwamo ndani ya mwanadamu, anamwongoza kutuliza badala ya kutengeneza mateso. -*The Review and Herald*, Januari 1, 1895. **{WM 47.2}**

Kanuni za Sheria ya Mungu Zilisahaulika. - Kuhani na Mlawi hawakuwa na udhuru kwa kutokujali kwao bila huruma. Sheria ya rehema na wema ilielezwa wazi katika Maandiko ya Agano la Kale. Ilikuwa ni kazi yao iliyopangwa kuhudumia hali kama hizo hasa ambayo mojawapo walikuwa

wameipita kando bila kuvutiwa nayo. Kama wangeitii sheria waliyodai kuiheshimu, wasingempita mtu huyu bila kumsaidia. Lakini walikuwa wamesahau kanuni za sheria ambazo Kristo, aliyefunikwa katika nguzo ya wingu, alikuwa amewapa baba zao alipowaongoza jangwani....**{WM 48.1}**

Jirani yangu ni nani? Hili ni swali ambalo makanisa yetu yote yanahitaji kulielewa. Ikiwa kuhani na Mlawi wangesoma kwa kuelewa kanuni ya Kiebrania, utendaji wao kwa mtu aliyejeruhiwa ungekuwa tofauti sana. -*Manuscript* 117, 1903.**{WM 48.2}**

Masharti ya Kuurithi Uzima wa Milele. - Masharti ya kuurithi uzima wa milele yameelezwa wazi na Mwokozi wetu kwa njia rahisi kabisa. Mtu yule

aliyejeruhiwa na kunyang'anywa anawawakilisha wale ambao ni wahusika wa shauku yetu, huruma, ukarimu na upendo. Ikiwa tunapuuza mambo ya wahitaji na wasiojiweza ambayo yanaoneshwa kwetu, haijalishi wao ni akina nani, hatuna uhakika wa uzima wa milele; kwani hatujibu madai ambayo Mungu anayo juu yetu. Sisi hatuna huruma na masikitiko kwa binadamu, kwa sababu inawezekana wasiwe jamaa au rafiki kwetu. Umeonekana kuwa mvunjaji wa amri kuu ya pili, ambayo juu yake amri sita za mwisho zinategemea. Yeyote anayekosea katika neno moja ana hatia juu ya yote. Wale ambao hawafungui mioyo yao kwa mahitaji na mateso ya wanadamu hawatafungua mioyo yao kwa madai ya Mungu kama

yalivyoelezwa katika amri nne za kwanza za Amri Kumi. Sanamu zinadai moyo na mapenzi, na Mungu haheshimiwi, Naye hatawali na kuwa kuwa mkuu kuliko wote. – *Testimonies for the church* 3:524.**{WM 48.3}**

Fursa Yako na Yangu. - Leo Mungu anawapa watu fursa ya kuonesha kama wanampenda jirani yao. Yeye ambaye kwa kweli anampenda Mungu na mwanadamu mwenzake ndiye yule anayeonesha rehema kwa maskini, wanaoteseka, waliojeruhiwa, wale ambao wako karibu na kufa. Mungu anatoa wito kwa kila mtu kuanza kufanya kazi yake iliyopuuzwa, kujitahidi kurejesha sura ya kimaadili ya Muumba ndani ya binadamu. - *Letter* 113, 1901.**{WM 49.1}**

Jinsi Tunavyoweza Kuwapenda Majirani Zetu Kama Nafsi Zetu.- Sisi tunaweza kumpenda jirani yetu kama nafsi zetu iwapo tu tutampenda Mungu kuliko vyote. Upendo kwa Mungu utazaa matunda ya upendo kwa majirani zetu. Wengi wanafikiri kwamba haiwezekani kumpenda jirani yetu kama nafsi zetu, lakini hili ndilo tunda pekee la Kweli la Ukristo. Upendo kwa wengine ni kumvaa Bwana Yesu Kristo; ni kutembea na kufanya kazi huku ukiuona ulimwengu ule usioonekana. Kwa jinsi hiyo tunapaswa kuendelea kumtazama Yesu, Mwenye kuanzisha na Mwenye kutimiza imani yetu. -*The Review and Herald*, Juni 26, 1894. **{WM 49.2}**

Sehemu III Mfano wa Agano Jipya

Wazo la Thamani

Wafuasi wa Kristo wamekombolewa kwa ajili ya utumishi. Bwana wetu anafundisha kwamba lengo la kweli la maisha ni huduma. Kristo Mwenyewe alikuwa ni mfanyakazi, na kwa wafuasi Wake wote anatoa sheria ya utumishi – utumishi kwa Mungu na kwa wanadamu wenzao. Hapa Kristo amewasilisha kwa ulimwengu dhana ya juu ya maisha kuliko walivyowahi kujua. Kwa kuishi ili

apate kuwahudumia wengine, mwanadamu analetwa katika uhusiano na Kristo. Sheria ya huduma inakuwa pete (kama mnyororo) ambayo inatuunganisha kwa Mungu na kwa wanadamu wenzetu.**{WM 52.1}**

Kwa watumishi Wake Kristo, Yeye hukabidhi "bidhaa Zake," - kitu cha kutumiwa kwa ajili Yake. Anampa “kila mtu kazi yake.” Kila mmoja ana nafasi yake katika mpango wa milele wa mbingu. Kila mmoja anapaswa kufanya kazi kwa ushirikiano na Kristo kwa ajili ya wokovu wa roho. Si hakika zaidi kwamba mahali pameandaliwa kwa ajili yetu katika makao ya mbinguni kuliko katika mahali pale maalum palipotengwa duniani ambapo tunapaswa kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. –*Christ’s Object Lessons*, 326,

327.**{WM 52.2}**

Sura ya Sita - Mfano Wetu katika Huduma ya Ustawi

Kristo Anasimama Mbele Yetu Kama Mfano Mkuu. - Ifanye kazi ya Kristo kuwa mfano wako. Daima alisonga mbele akifanya mema - akiwalisha wenye njaa na kuwaponya wagonjwa. Hakuna mtu hata mmoja aliyekuja Kwake kwa ajili ya kutaka huruma aliyevunjwa moyo. Amiri jeshi wa nyua za mbinguni, Alifanyika mwili na akakaa kati yetu, na kazi Yake ya maisha ni mfano wa kazi tunayopaswa kuifanya. Upendo Wake, wenye

kuhurumia unakemea uchoyo na ubinafsi wetu na kutokuwa na huruma kwetu. - *Manuscript* 55, 1901.**{WM 53.1}**

Kristo alisimama kichwa cha ubinadamu katika vazi la ubinadamu. Mtazamo Wake ulijawa na huruma na upendo kiasi kwamba walio maskini kabisa hawakuogopa kuja Kwake. Alikuwa mwema kwa wote, rahisi kuendewa na watu wa hali ya chini kabisa. Alikwenda nyumba kwa nyumba, akiwaponya wagonjwa, akiwalisha wenye njaa, akiwafariji waombolezao, akiwatuliza wanaoteseka, akiongea amani kwa wenye dhiki.... Alikuwa tayari kujinyenyekesha, kujikana nafsi. Hakutafuta kujipatia sifa. Alikuwa mtumishi wa wote. Ilikuwa ni chakula na kinywaji Chake kuwa faraja na

kitulizo kwa wengine, kumfurahisha yule aliyehuzunika na mwenye kulemewa ambao alikutana nao kila siku. **{WM 53.2}**

Kristo anasimama mbele yetu kama Mwanadamu aliye kielelezo, Mmisionari Mkuu wa Tiba - mfano kwa wote ambao wanapaswa kuja baadaye. Upendo Wake, safi na mtakatifu, uliwabariki wote waliokuja ndani ya eneo la mamlaka Yake. Tabia Yake ilikuwa kamilifu kabisa, isiyo na doa lolote dogo kabisa la dhambi. Alikuja kama kielelezo cha upendo mkamilifu wa Mungu, si kupondaponda, si kuhukumu na kulaani, bali kuponya kila tabia dhaifu, yenye kasoro, kuwaokoa wanaume na wanawake kutoka katika mamlaka ya Shetani. Yeye Ndiye Muumbaji, Mkombozi, na Mtegemezaji wa jamii ya

wanadamu. Kwa wote anatoa mwaliko, “Njooni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi.”**{WM 53.3}**

Ni mfano gani basi, tunapaswa kuuonesha kwa ulimwengu? Tunapaswa kufanya kazi ile ile ambayo Mmisionari Mkuu wa Tiba alijitoa kuifanya kwa niaba yetu. Tunapaswa kufuata njia ile ya kujitoa kafara iliyopitwa na Kristo. — *Special Testimonies*, series B, no. 8, uk. 31, 32.**{WM 54.1}**

Kristo Alisukumwa na Huruma.

- Kristo alipowaona makutano ya watu uliokusanyika kumzunguka, “Aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.” Kristo aliona ugonjwa, huzuni, hitaji na hali mbaya ya umati ule ambao ulisongamana katika hatua Zake. Kwake mahitaji na shida za wanadamu katika ulimwengu wote ziliwasilishwa. Miongoni mwa walio juu na walio chini, wanaoheshimiwa mno na wadhilifu kabisa, Aliona roho ambazo zilikuwa zikitamani baraka zile hasa ambazo alikuwa amekuja kuleta....

Leo hii mahitaji yayo hayo yapo. Ulimwengu unahitaji wafanyakazi ambao watafanya kazi kama Kristo alivyofanya kwa ajili ya wanaoteseka na wenye dhambi. Hakika kuna makutano ya kufikiwa. Ulimwengu umejaa magonjwa, mateso, huzuni, na dhambi. Imejaa wale wanaohitaji kuhudumiwa - wanyonge, wasiojiweza, wasiojua/wajinga, wadhilifu. - *Testimonies for the Church* 6:254. **{WM 54.1}**

Mfano Tunaopaswa Kuuiga. - Roho ya Kweli ya umisionari ni roho ya Kristo. Mkombozi wa ulimwengu alikuwa mmisionari mkuu wa mfano wa kuigwa. Wengi wa wafuasi Wake wamefanya kazi

kwa bidii na bila ubinafsi katika njia ya wokovu wa mwanadamu; lakini hakuna kazi ya mtu inaweza kulinganishwa na kujikana, kujitoa kafara, na ukarimu, wa Yeye aliye Mfano wetu. **{WM 55.1}**

Upendo ambao Kristo ameutoa kwa ajili yetu hauna kifani. Jinsi alivyofanya kazi kwa bidii! Ni mara nyingi kiasi gani alikuwa peke yake katika maombi ya nguvu, kando ya mlima au katika mahali palipojitenga bustanini, akimimina dua Zake kwa kilio cha nguvu na machozi. Jinsi alivyosisitiza kwa uvumilivu maombi Yake kwa niaba ya wenye dhambi! Hata msalabani alisahau mateso Yake Mwenyewe kwa sababu ya upendo Wake wa kina kwa wale ambao alikuja kuwaokoa. Ni jinsi gani upendo

wetu ni baridi, ni jinsi gani shauku yetu ni dhaifu, ikilinganishwa na upendo na shauku iliyooneshwa na Mwokozi wetu! Yesu alijitoa Mwenyewe kuikomboa jamii yetu, na bado ni kiasi gani tuko tayari kutoa udhuru kwa ajili ya kushindwa kutoa vyote tulivyo navyo kwa ajili ya Yesu. Mwokozi wetu alijisalimisha kwa kazi ya kuchosha, aibu, na mateso. Alikatishwa tamaa, alidhihakiwa, alikejeliwa, wakati alipokuwa akijishughulisha na kazi kubwa ambayo alikuja duniani kuifanya. **{WM 55.2}**

Je, ninyi, ndugu na dada zangu, mnajiuliza: Ni mfano gani tuuige? Siwaelekezi kwa watu wakubwa na walio wema, bali kwa Mkombozi wa ulimwengu. Ikiwa tunataka kuwa na roho ya Kweli ya umisionari, ni lazima

tujazwe na upendo wa Kristo; ni lazima tumtazame Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu, tujifunze tabia Yake, tukuze roho Yake ya upole na unyenyekevu, na kutembea katika nyayo Zake. **{WM 55.3}**

Wengi hudhani kwamba roho ya umisionari, sifa kwa ajili ya kazi ya umisionari, ni zawadi maalum au majaliwa waliyopewa wachungaji na washiriki wachache wa kanisa na kwamba wengine wote wanapaswa kuwa watazamaji tu. Kamwe hakujawahi kuwako kosa kubwa zaidi ya hili. Kila Mkristo wa kweli atakuwa na roho ya umisionari, kwani kuwa Mkristo ni kuwa kama Kristo. ***Hakuna mtu anayeishi kwa ajili yake yeye mwenyewe***, na "mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si

Wake." Kila mtu ambaye ameonja nguvu za ulimwengu ujao, akiwa mdogo au mzee, msomi au hajasoma, atachochewa na roho ambayo ilimsukuma Kristo. Msukumo wa kwanza kabisa wa moyo uliofanywa upya ni kuwaleta wengine pia kwa Mwokozi. Wale ambao hawana matamanio haya, hutoa ushahidi kwamba wamepoteza upendo wao ule wa kwanza; wanapaswa kuichunguza kwa karibu mioyo yao wenyewe katika nuru ya Neno la Mungu, na kutafuta kwa bidii ubatizo mpya wa Roho wa Kristo; wanapaswa kuomba kwa ajili ya ufahamu wa kina zaidi wa upendo huo wa ajabu ambao Yesu aliudhihirisha kwetu katika kuacha ulimwengu wa utukufu na kuja katika ulimwengu ulioanguka ili apate kuwaokoa

wanaoangamia. - *Testimonies for the Church* 5:385, 386. **{WM 55.4}**

Tafsiri ya Kristo ya Injili. – Agizo la Bwana halihitaji marekebisho. Njia ya Kristo ya kuwasilisha Ukweli haiwezi kuboreshwa. Mwokozi aliwapa wanafunzi masomo ya kiutendaji, akiwafundisha jinsi ya kufanya kazi kwa namna ambayo itazifanya roho kufurahia Ukweli. Aliwahurumia waliochoka, waliolemewa, walioonewa. Aliwalisha wenye njaa na kuwaponya wagonjwa. Mara kwa mara Yeye alisonga mbele akifanya mema. Kwa wema alioutimiza, kwa maneno Yake ya upendo na matendo ya fadhili, aliifasiri injili kwa wanadamu. **{WM 56.1}**

Kifupi kama kilivyokuwa kipindi cha huduma Yake ya hadhara, alikamilisha

kazi aliyokuja kuifanya. Kweli alizofundisha zilikuwa ni za kuvutia kiasi gani! Ni kiasi gani kazi Yake ya maisha ilikamilika! Ni chakula cha namna gani cha kiroho alikitoa kila siku pale alipolisha mkate wa uzima kwa maelfu ya roho zenye njaa! Maisha Yake yalikuwa ni huduma hai ya Neno. Hakuahidi chochote ambacho hakukitekeleza.**{WM 56.2}**

Maneno ya maisha yaliwasilishwa kwa usahili kiasi kwamba mtoto aliweza kuyaelewa. Wanaume, wanawake, na watoto walivutiwa sana na namna Yake ya kuelezea Maandiko kiasi kwamba wangeweza kushika lafudhi hasa ya sauti Yake, kuweka msisitizo ule ule katika maneno yao, na kuiga ishara Zake. Vijana walishika roho Yake ya huduma, na kutaka kufuata njia Zake za neema

kwa kujitahidi kuwasaidia wale ambao waliona kuwa wanahitaji msaada.**{WM 57.1}**

Kama vile tunavyofuatilia njia ya mto kwa mstari wa kijani kibichi unaouzalisha, ndivyo Kristo angeweza kuonekana katika matendo ya rehema ambayo yalionesha njia Yake katika kila hatua. Popote alipokwenda afya ilichipuka, na furaha ilifuata popote alipopita. Na vipofu na viziwi walifurahia uwepo Wake. Maneno Yake kwa wasiojua yaliwafungulia chemchemi ya uzima. Alitoa baraka Zake kwa wingi na kwa kuendelea. Zilikuwa ni hazina zilizokusanywa katika umilele, zilizotolewa katika Kristo, thawabu ya gharama kubwa mno ya Bwana kwa mwanadamu.**{WM 57.2}**

Kazi ya Kristo kwa niaba ya mwanadamu haijakwisha. Inaendelea leo. Vivyo hivyo mabalozi Wake wanapaswa kuhubiri injili na kudhihirisha upendo Wake wa huruma kwa roho zilizopotea na zinazoangamia. Kwa shauku isiyo na ubinafsi kwa wale wanaohitaji msaada wanapaswa kutoa onesho la kiutendaji la Ukweli wa injili. Mengi zaidi ya kuhubiri tu hujumuishwa katika kazi hii. Uenezaji wa habari ya injili kwa ulimwengu ndio kazi ambayo Mungu amewapa wale wanaosonga mbele kwa Jina Lake. Wao Wanapaswa kuwa watenda kazi pamoja na Kristo, wakiwafunulia wale walio karibu na kuangamia upendo Wake mwororo, wenye huruma. Mungu anawaita maelfu wapate kumfanyia kazi, si kwa kuwahubiria wale wanaoujua Ukweli wa

wakati huu, bali kwa kuwaonya wale ambao hawajawahi kusikia ujumbe wa mwisho wa rehema. Fanya kazi kwa moyo uliojaa shauku ya dhati kwa ajili ya roho. Fanya kazi ya umisionari wa tiba. Kwa jinsi hiyo utapata namna ya kuifikia mioyo ya watu, na njia itaandaliwa kwa ajili ya utangazaji wa dhati zaidi wa Ukweli.**{WM 57.3}**

Ni nani wanaofanya kazi pamoja na Kristo katika kazi hii iliyobarikiwa ya umisionari wa tiba? Ni akina nani wamejifunza kutoka kwa Mwalimu masomo na wanajua jinsi ya kushughulikia kwa ustadi roho ambazo Kristo amekufa kwa ajili yake? Tunahitaji, ndio, sana, matabibu kwa ajili ya roho ambao wameelimishwa katika shule ya Kristo na ambao wanaweza kufanya kazi katika mielekeo

ya Kristo. - *The Review and Herald*, Desemba 17, 1914.**{WM 58.1}**

Sura ya Saba - Kutembelea - Mpango wa Agano Jipya

Mbinu za Kristo za Kufanya Kazi. - Kutokana na mbinu za Kristo za kufanya kazi tunaweza kujifunza masomo muhimu. Yeye hakufuata mbinu moja tu; kwa njia anuwai/tofauti Yeye Alitafuta kuvuta usikivu wa makutano, ili apate kuwatangazia Ukweli wa injili.**{WM 59.1}**

Kazi kuu ya Kristo ilikuwa ni kuwahudumia maskini, wahitaji, na wasiojua/wajinga. Kwa usahili alifungua mbele yao baraka ile ambayo wangeweza kupokea, na hivyo akaamsha njaa ya

roho kwa ajili ya mkate wa uzima. Maisha ya Kristo ni mfano kwa wafuasi wake wote. Ni wajibu wa wote ambao wamejifunza njia ya maisha kuwafundisha wengine ni nini maana ya kuliamini Neno la Mungu. Kuna wengi ambao kwa sasa wapo katika uvuli wa mauti ambao wanahitaji kufundishwa kweli za injili. Karibu ulimwengu wote unalala katika uovu. Hata hivyo tunayo Maneno ya matumaini kwa wale wanaokaa gizani. -*The Review and Herald*, Mei 9, 1912.**{WM 59.2}**

Mawanda ya Huduma ya Kristo ya Nyumba kwa Nyumba. - Mwokozi wetu alikwenda nyumba kwa nyumba, akiwaponya wagonjwa, akiwafariji waombolezaji, akiwatuliza wanaoteseka, akiongea amani kwa wenye huzuni. Aliwachukua watoto wadogo mikononi

Mwake na kuwabariki na kusema Maneno ya matumaini na faraja kwa akina mama waliochoka. Kwa wema na upole usiokoma Yeye Alikabiliana na kila aina ya shida na mateso ya wanadamu. Si kwa ajili Yake Mwenyewe, bali kwa ajili ya wengine, alifanya kazi. Alikuwa ni mtumishi wa wote. Ilikuwa ni chakula Chake na kinywaji Chake kuleta tumaini na nguvu kwa wote aliokutana nao (japo mtu anaweza kwenda mtandao hadi mtandao kushea injili, bado uso kwa uso ni muhimu). - *Gospel Workers*, 188.**{WM 59.3}**

Mbinu ya Kristo Inaleta Mafanikio ya Kweli. - Mbinu ya Kristo peke Yake itakupa mafanikio ya kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alijichanganya na wanadamu kama mtu yule aliyetamani mema kwa ajili yao.

Alionesha huruma Yake kwao, akahudumia mahitaji yao, na kujipatia imani na ujasiri wao. Kisha akawaambia: “Nifuateni.” — *The Ministry of Healing*, 143.**{WM 60.1}**

Hivi ndivyo Kanisa la Kikristo lilivyoanzishwa. Kristo kwanza alichagua watu wachache na kuwaamuru wamfuate. Kisha wao wakaenda kuwatafuta jamaa zao na marafiki wao, na kuwaleta kwa Kristo. Hii ndio njia ambayo kwayo tunapaswa kufanya kazi. Roho chache zinazoletwa na kuimarishwa kikamilifu katika Ukweli, kama wanafunzi wa kwanza, hao watakuwa watenda kazi kwa ajili ya wengine. - *The Review and Herald*, Desemba 8, 1885.**{WM 60.2}**

Mfano wa Kiungu wa Uinjilisti Binafsi. - Yesu alikutana Mwenyewe binafsi na watu. Hakusimama mbali na kujitenga na wale waliohitaji msaada Wake. Aliingia katika nyumba za wanadamu, Naye akamfariji mwombolezaji, akawaponya wagonjwa, akawaamsha wazembe, na kwenda huku na huko akitenda mema. Na ikiwa tunafuata nyayo za Yesu, ni lazima tutende kama alivyotenda. Lazima tuwape watu aina ile ile ya msaada ambao Yeye aliutoa. - *The Review and Herald*, Aprili 24, 1888.**{WM 60.3}**

Si kuhubiri, ndiko ambako ni muhimu zaidi ya yote; ni katika kazi ya nyumba kwa nyumba, utoaji wa hoja kutokana na Neno, kusemezana pamoja na kulifafanua Neno. Ni wafanyakazi wale ambao wanafuata mbinu ambazo

Kristo alifuata, ndio ambao wataongoa roho kwa kazi yao. - *Gospel Workers*, 468.**{WM 60.4}**

Bwana anataka sana kwamba Neno Lake la neema litafahamishwa vyema/barabara kwa kila nafsi. Kwa kiwango kikubwa hili inabidi litimizwe kwa kazi ya mtu binafsi. Hii ilikuwa ndio mbinu ya Kristo. Kazi Yake kwa kiasi kikubwa ilifanywa kwa mahojiano ya binafsi. Yeye Aliheshimu kwa uaminifu hadhira ya mtu mmoja. Kupitia kwa roho hiyo moja ujumbe mara nyingi ulienezwa kwa ***maelfu***. *Christ's Object Lessons*, 229.**{WM 60.5}**

Kumi na Wawili Watumwa Kusonga Mbele katika Kazi ya Nyumba kwa Nyumba. - Katika safari hii ya kwanza, wanafunzi

walipaswa kwenda mahali pale tu ambapo Yesu alikuwa amekwenda kabla yao na alikuwa amekwisha kutengeneza marafiki.... Hakuna kitu kinachopaswa kuruhusiwa kuchepua akili zao kutoka katika kazi yao kubwa au kwa njia yoyote ile kuchochea upinzani na kufunga mlango kwa ajili ya kuendelea kwa kazi. Hawakupaswa kuchukua mavazi ya walimu wa kidini, wala kutumia mtindo wowote wa mavazi ili kuwatofautisha na wakulima wanyenyekevu. Hawakupaswa kuingia katika masinagogi na kuwaita watu pamoja kwa ajili ya huduma ya umma; juhudi zao zilipaswa kuwekwa katika kazi ya nyumba kwa nyumba.... Walipaswa kuingia katika maskani kwa salamu nzuri, “Amani iwemo nyumbani humu.” Nyumba hiyo ingebarikiwa kwa

maombi yao, nyimbo zao za sifa, na kufunguliwa kwa Maandiko katika familia moja. - *The Desire of Ages*, 351, 352.**{WM 61.1}**

Wale Sabini Pia. - Akiwaita wale kumi na wawili karibu na Yeye, Yesu aliwaambia waende wawili wawili katika miji na vijiji. Hakuna aliyetumwa peke yake, bali ndugu alishirikishwa na ndugu, rafiki na rafiki. Kwa jinsi hiyo wangeweza kusaidiana na kutiana moyo, wakishauriana na kuomba pamoja, nguvu ya kila mmoja ikijaliza udhaifu wa mwenzake. Kwa jinsi hiyo hiyo baadaye, Yeye aliwatuma wale sabini. Lilikuwa ni kusudi la Mwokozi kwamba wajumbe wa injili wangepaswa kushirikishwa kwa jinsi hii. Katika wakati wetu kazi ya uinjilisti ingekuwa yenye mafanikio makubwa zaidi ikiwa

mfano huu ungefuatwa kwa karibu zaidi. — *The Desire of Ages*, 350.**{WM 61.2}**

Paulo Alikwenda Nyumba kwa Nyumba. — Paulo, pamoja na kufanya kazi kwa bidii hadharani, alikwenda nyumba kwa nyumba akihubiri toba kwa Mungu na imani kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Alikutana na watu majumbani mwao na kuwasihi kwa machozi, akiwaambia shauri lote la Mungu. - *The Review and Herald*, Aprili 24, 1888. **{WM 61.3}**

Siri ya Nguvu na Mafanikio ya Paulo. - Wakati mmoja Paulo alisema: "Ninyi wenyewe mnajua tangu siku ya kwanza nilipokanyaga hapa Asia, jinsi nilivyokuwa kwenu wakati wote, nikimtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote, na kwa machozi, na majaribu

yaliyonipata kwa hila za Wayahudi; ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia Neno lolote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba."...**{WM 62.1}**

Maneno haya yanaelezea siri ya nguvu na mafanikio ya Paulo. Yeye hakuzuia chochote ambacho kilikuwa na faida kwa watu. Alimhubiri Kristo hadharani, katika maeneo ya soko na masinagogi. Alifundisha nyumba kwa nyumba, akitumia mahusiano/maingiliano ya kawaida ya nyumbani kwa familia moja. Aliwatembelea wagonjwa na wenye kuhuzunika, akiwafariji wale walioteseka, na kuwainua walioonewa. Na katika yote aliyosema na kufanya alimhubiri Mwokozi aliyesulubiwa na

kufufuka. - *The Youth's Instructor*, Novemba 22, 1900.**{WM 62.2}**

Paulo Pia Alipata Kuwafikia Wengine Kupitia katika Stadi ya Ufundi wake. - Katika kipindi kirefu cha huduma yake huko Efeso, ambapo kwa miaka mitatu aliendesha juhudi za nguvu za kiinjilisti katika eneo hilo lote, Paulo tena alifanya kazi ya stadi ya ufundi wake....**{WM 62.3}**

Kulikuwa na baadhi ambao walipinga juhudi za Paulo kufanya kazi kwa mikono yake, wakitangaza kwamba ilikuwa haipatani na kazi ya mhudumu wa injili. Kwa nini Paulo, mtumishi wa cheo cha juu kabisa, aunganishe kazi za ufundi/mitambo au stadi za mikono na kulihubiri Neno? Je! Mtenda kazi hakustahili ujira wake? Kwa nini basi

atumie muda wake katika kutengeneza mahema muda ambao kwa kadiri ionekanavyo kibinadamu ungeweza kutumika kwa manufaa zaidi?**{WM 62.4}**

Lakini Paulo hakuchukulia kuwa umepotea muda ule uliotumika hivyo. Alipokuwa akifanya kazi na Akila aliendelea kuwasiliana na Mwalimu Mkuu, bila kupoteza fursa yoyote ya kumshuhudia Mwokozi na kuwasaidia wale waliohitaji msaada. Akili yake daima ilikuwa ikifikia maarifa ya kiroho. Alikuwa akiwapa wafanyakazi wenzake mafundisho katika mambo ya kiroho, na pia alionesha mfano wa uchapaji kazi na bidii nyingi. Alikuwa ni mfanyakazi mwepesi, mwenye ustadi, mwenye bidii katika shughuli, "mwenye juhudi katika roho, akimtumikia Bwana." Kadiri

alivyokuwa akifanya kazi katika fani yake ya ufundi, mtume huyu alipata namna ya kulifikia tabaka la watu ambao hangeweza kuwafikia vinginevyo....**{WM 63.1}**

Wakati mwingine Paulo alifanya kazi usiku na mchana, si tu kwa ajili ya kujitegemeza yeye mwenyewe, bali ili aweze kuwasaidia wafanyakazi wenzake. Aligawana mapato yake na Luka, na alimsaidia Timotheo. Hata wakati mwingine alivumilia njaa, ili apate kupunguza mahitaji ya wengine. Maisha yake yalikuwa ni maisha yasiyo na ubinafsi. - *The Acts of the Apostles*, 351, 352.**{WM 63.2}**

Mfano Mzuri wa Kiutendaji wa Paulo kwa Walei Wanaojitegemeza. —Paulo aliweka

mfano dhidi ya mawazo, ambayo kwa wakati ule yalikuwa yakiliathiri kanisa, kwamba injili inaweza tu kutangazwa kwa mafanikio na wale ambao walikuwa wamewekwa huru kabisa kutokana na haja ya kufanya kazi ngumu za kimwili (mitulinga). Alionesha kwa njia ya vitendo kile kinachoweza kufanywa na walei waliojiweka wakfu katika maeneo mengi ambapo watu walikuwa hawajui Ukweli wa injili. Njia yake iliwachochea vibarua wanyenyekevu wengi wenye hamu ya kufanya kile wanachoweza katika kuiendeleza kazi ya Mungu, wakati huo huo wakijitegemeza kwa kazi ya kila siku.**{WM 63.3}**

Akila na Prisila hawakuitwa kutoa muda wao wote katika huduma ya injili, lakini bado watenda kazi hawa wanyenyekevu walitumiwa na Mungu

kumwonesha Apolo njia ya Kweli kwa ukamilifu zaidi. Bwana hutumia mawakala anuwai kwa kutimiza kusudi Lake; na wakati ambapo baadhi walio na talanta maalum wameteuliwa kutoa nguvu zao zote kwa kazi ya kufundisha na kuhubiri injili, wengine wengi, ambao mikono ya wanadamu haijawahi kuwekwa juu yao katika kuwaweka wakfu kwa ajili ya kazi, wao wameitwa kutenda sehemu muhimu katika uokoaji wa roho.**{WM 63.4}**

Kuna uwanja mkubwa ulio wazi mbele ya mfanyakazi wa injili wa kujitegemeza mwenyewe. Wengi wanaweza kupata uzoefu muhimu katika utumishi wakati wakitumia sehemu ya muda kufanya kazi fulani ya mikono, na kwa njia hii wafanyakazi wenye nguvu wanaweza kukuzwa kwa ajili ya huduma

muhimu katika maeneo yenye hitaji. - *The Acts of the Apostles*, 355.**{WM 64.1}**

Nenda kwa Roho Ile Iliyomjalia Paulo. - Nenda kwa majirani zako mmoja baada ya mwingine, na uwakaribie mpaka mioyo yao ichangamshwe moyo na shauku na upendo wako usio na ubinafsi. Wahurumie, onyesha sikitiko lako kwao, omba pamoja nao, tafuta fursa ya kuwatendea mema, na kadiri unavyoweza, kukusanya wachache pamoja na kufungua Neno la Mungu kwa akili zao zilizotiwa giza. Endelea kuangalia kama mtu yule ambaye lazima atatoa hesabu kwa ajili ya roho za wanadamu, na utumie vizuri kabisa fursa zile ambazo Mungu anakupa za

kufanya kazi pamoja Naye katika shamba Lake la mizabibu.**{WM 64.2}**

Usipuuze kuzungumza na majirani zako na kuwatendea wema wote ulio katika uwezo wako kutenda, ili "kwa njia zote" upate kuwaokoa watu. Tunahitajika kutafuta roho ile ambayo ilimbidisha mtume Paulo kwenda nyumba kwa nyumba, akiomba kwa machozi na kufundisha "wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo." — *The Review and Herald*, Machi 13, 1888.**{WM 64.3}**

Kazi za Kwanza za Kanisa la Agano Jipya. - Kazi za kwanza za kanisa zilionekana pale waumini walipowatafuta marafiki, jamaa, na watu waliofahamiana nao, na kwa mioyo iliyofurika upendo, walisimulia kisa cha

kile Yesu alichokuwa kwao. - *Special Testimonies*, series A, no. 2, p. 17.**{WM 64.4}**

Mafanikio ya Mpango wa Agano Jipya. – Kwa kadiri mpango wa Agano Jipya unavyofuatwa kwa makini katika kazi ya umisionari, ndivyo juhudi zinazowekwa zitakavyokuwa na mafanikio. Tunapaswa kufanya kazi kama alivyofanya Mwalimu wetu wa Kiungu/mbinguni, tukipanda mbegu za Ukweli kwa uangalifu, kwa hamu, na kwa kujikana nafsi. Ni lazima tuwe na akili ya Kristo ikiwa hatutaki kuchoka katika kutenda mema. Maisha Yake yalikuwa ni maisha ya kujitoa daima kwa ajili ya manufaa ya wengine. Ni lazima sisi tufuate mfano Wake. — *Testimonies for the Church* 3:210.**{WM 65.1}**

Sura ya Nane - Dorkasi-Huduma na Mvuto wa Huduma Yake

Arejeshewa Uhai Ili Apate Kuendelea na Utumishi Wake. -

Katika kipindi cha huduma yake mtume Petro aliwatembelea waumini huko Lida. Hapa alimponya Ainea, ambaye

kwa miaka minane alikuwa amelala kwenye kitanda chake kwa kupooza. "Ainea, Yesu Kristo akuponya," mtume alisema; "ondoka, ujitandikie ‘kitanda chako’." “Mara akaondoka. Na watu wote waliokaa Lida na Sharoni wakamwona, wakamgeukia Bwana.”**{WM 66.1}**

Huko Yopa, karibu na Lida, aliishi mwanamke mmoja aliyeitwa Dorkasi, ambaye matendo yake mema yalifanya apendwe sana. Alikuwa mwanafunzi mwema wa Yesu, na maisha yake yalijaa matendo ya wema/fadhili. Alijua ni nani alihitaji mavazi mazuri na ni nani alihitaji huruma, na aliwahudumia kwa ukaribu na bure wale waliokuwa maskini na wenye huzuni. Vidole vyake vyenye ustadi vilifanya kazi kuliko ulimi wake.**{WM 66.2}**

"Ikawa siku zile, akaugua, akafa." Kanisa la Yafa lilitambua Walichopungukiwa; na kusikia kwamba Petro alikuwa Lida, waumini walituma wajumbe kwake, "kumsihi na kusema, Usikawie kuja kwetu. Ndipo Petro akaondoka akafuatana nao. Naye alipofika, wakampeleka juu orofani wajane wote wakasimama karibu naye, wakilia na kumwonesha zile kanzu na nguo alizozishona Dorkasi wakati ule alipokuwa pamoja nao." Kwa mtazamo wa maisha ya huduma ambayo Dorkasi alikuwa ameishi, si ajabu kwamba waliomboleza, kwamba machozi ya moto yalianguka juu ya udongo usio na uhai.**{WM 66.3}**

Moyo wa mtume uliguswa na huruma alipoona huzuni yao. Ndipo, akiagiza kwamba marafiki wale wanaolia

waondolewe kutoka chumbani, naye akapiga magoti na kuomba kwa bidii kwa Mungu amrejeshe Dorkasi katika uzima na afya. Akimwelekea yule maiti, akasema, Tabitha, ondoka. Naye akafumbua macho yake, na alipomwona Petro akajiinua, akaketi." Dorkasi alikuwa amelisaidia sana kanisa, na Mungu aliona kuwa ni vyema kumrejesha katika uhai kutoka katika mikono ya adui, ili kwamba ujuzi na nguvu zake zizidi kuwa baraka kwa wengine na pia kwamba kwa onesho hili la uweza Wake kusudi la Kristo lipate kuimarishwa. — *The Acts of the Apostles,* 131, 132.**{WM 66.4}**

Mwanafunzi Mwenye Sifa Njema Ambaye Hakuweza Kuachwa. - Yeye [Dorkasi] alikuwa mwanafunzi mwema wa Yesu Kristo, na

maisha yake yalielezwa na sifa ya matendo ya upendo na huruma kwa maskini na wenye huzuni na bidii katika njia ya Ukweli. Kifo chake kilikuwa ni hasara kubwa; Kanisa changa lisingeweza kuacha juhudi zake bora bila kupata maumivu....**{WM 67.1}**

Kazi hii kubwa ya kufufua wafu ilikuwa njia ya kuwageuza wengi huko Yafa kumwamini Yesu. - *The Spirit of Prophecy* 3:323, 324.**{WM 67.2}**

Sehemu ya IV Uinjilisti wa Ujirani

Wazo la Thamani

Washiriki wa kanisa wanapaswa kufanya kazi ya uinjilisti katika nyumba

za majirani zao ambao bado hawajapokea ushahidi kamili wa Ukweli wa wakati huu. Uwasilishaji wa Ukweli kwa upendo na huruma, kutoka nyumba hadi nyumba nyingine, unapatana na maagizo ambayo Kristo aliwapa wanafunzi Wake wakati alipowatuma katika safari yao ya kwanza ya umisionari. Kwa nyimbo za sifa kwa Mungu, kwa maombi ya dhati ya unyenyekevu, kwa uwasilishaji sahili wa ukweli wa Biblia katika familia, wengi watafikiwa. [Mfanyakazi] wa Bwana/mbingu atakuwepo kupeleka usadikisho mioyoni. "Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote" ndio ahadi Yake. Kwa uhakika wa uwepo wa kudumu wa Msaidizi kama huyo, tunaweza kufanya kazi kwa tumaini na imani na ujasiri.... **{WM 70.1}**

Ndugu na dada zangu, jitoeni kwa Bwana kwa ajili ya huduma. Usiruhusu fursa hata moja ipite bila kutumiwa vyema. Watembelee wale walio karibu nawe, na kwa huruma na wema, jaribu kuifikia mioyo yao. Watembelee wagonjwa na wanaoteseka, na uoneshe shauku ya ukarimu kwao. Ikiwezekana, fanya kitu fulani ili kuwafanya waridhike zaidi (mahitaji yao ya kimwili, kiakili, na kiroho yatimizwe-comfortable). Kupitia njia hii unaweza kufikia mioyo yao, na kuzungumza neno kwa ajili ya Kristo. Ni umilele peke yake ndio utakaodhihirisha ni athari nyingi kiasi gani mwelekeo kama huo wa kazi unaweza kuwa nao. - *The Review and Herald*, Novemba 21, 1907.**{WM 70.2}**

Let your light so shine before men, that they may see your good works, and glorify your Father which is in heaven. Matthew 5:16

Sura ya Tisa - Aina za Kazi katika Uinjilisti wa Ujirani

Kazi Kubwa Mbele ya Makanisa Yetu. - Kuna kazi ya kufanywa na makanisa yetu ambayo wachache tu wana wazo lolote juu yake.... Tutalazimika kutoa mali zetu kuwasaidia watenda kazi katika shamba la mavuno, nasi tutashangilia kwa miganda ya mavuno itakayokusanywa. Lakini wakati hili ni sahihi, kuna kazi, ambayo hadi sasa bado haijaguswa, ambayo ni lazima ifanyike. Utume wa Kristo ulikuwa ni kuwaponya wagonjwa, kuwatia moyo wasio na matumaini, kuwafunga waliovunjika moyo. Kazi hii

ya urejeshaji inapaswa kufanywa miongoni mwa wale wanadamu wahitaji wanaoteseka.**{WM 71.1}**

Mungu hahitaji ukarimu wako peke yake tu, bali hata uso wako mchangamfu, maneno yako ya matumaini, kushika kwa mkono wako. Wafariji baadhi watu wa Mungu wanaoteseka. Wengine ni wagonjwa, na matumaini yameondoka. Warejeshee uchangamfu wa moyo. Kuna roho ambazo zimepoteza ujasiri wao; zungumza nao, waombee. Kuna wale ambao wanauhitaji mkate wa uzima. Wasomee Neno la Mungu. Kuna ugonjwa wa roho ambao hakuna zeri inaweza kuufikia, hakuna dawa inaweza kuuponya. Waombee hawa, na uwalete kwa Yesu Kristo. Na katika kazi yako yote Kristo atakuwepo kwa ajili ya kutoa

mvuto kwa mioyo ya wanadamu. -*Manuscript 105, 1898*.**{WM 71.2}**

Tembelea Kila Familia na Ujue Hali Yao ya Kiroho. - Popote kanisa linapoanzishwa, washiriki wote wanapaswa kushiriki kikamilifu katika kazi ya umisionari. Wanapaswa kutembelea kila familia katika ujirani wao na kujua hali yao ya kiroho. Ikiwa wale wanaokiri kuwa Wakristo wangejishughulisha na kazi hii tangu wakati majina yao yalipowekwa kwenye vitabu vya kanisa kwa mara ya kwanza, sasa kusingekuwapo na kutokuamini kulikoenea kiasi hiki, vina vya jinsi hii vya udhalimu, uovu usio na kifani kiasi hiki, kama inavyoonekana ulimwenguni kwa wakati huu. Ikiwa kila mshiriki wa kanisa angejitahidi kuwaelimisha wengine na nuru aliyonayo, maelfu kwa

maelfu leo wangesimama pamoja na watu wa Mungu wanaoshika amri za Mungu leo.**{WM 71.3}**

Na si tu ulimwenguni tunaona matokeo ya kanisa kupuuza kufanya kazi katika mielekeo ya Kristo. Kwa kupuuza huku hali ya mambo imeletwa katika kanisa ambayo imepoteza nguvu ya mvuto wa juu na mtakatifu wa kazi ya Mungu. Roho ya ukosoaji, uchungu na ukali imeingia kanisani, na utambuzi wa kiroho wa wengi umehafifishwa-umetiwa giza. Kwa sababu hii kusudi la Kristo limepata hasara kubwa. Akili za mbinguni zimekuwa zikisubiri kushirikiana na wakala wa kibinadamu, lakini hatujatambua uwepo wao.**{WM 72.1}**

Wakati sasa umefika tututbu. Watu wote wa Mungu wanapaswa kupata shauku katika kazi ya kutenda mema. Wanapaswa kuungana kabisa katika jitihada ya kuwainua na kuwaelimisha wanadamu wenzao. - *Testimonies for the Church*, 6:296, 297.**{WM 72.2}**

Kuwatafuta Wale Ambao Watasikia. - Miaka mingi iliyopita, wakati wa ziara ya awali ya Kusini, nikiwa katika safari ndefu ndani ya gari, wakati mwingine nilijiuliza ni nani aliyeishi kwenye nyumba tulizozipita, na nilitaarifiwa kuwa katika nyumba nyingi kubwa za Kusini kulikuwa na watu wenye majukumu muhimu katika utunzaji wa mashamba makubwa. Baada ya kuuliza zaidi, nilitaarifiwa kwamba hakuna mtu aliyewahi kujaribu kuleta mbele ya watu hawa Neno la Uzima.

Hakuna mtu hata mmoja aliyekwenda kwao, na Biblia mkononi, na kusema, "Tuna kitu cha thamani sana kwa ajili yenu, na tunatamani kwamba mpate kukisikia." Sasa imewasilishwa mbele yangu mara kwa mara kwamba huu ni mwelekeo wa kazi ambayo lazima ifanyike. Tunapaswa kwenda kwenye barabara kuu na kando kando kwenye maboma kupeleka kwa watu ujumbe wa Ukweli ambao Kristo ametupa. Tunapaswa kuwabidisha wengi wapate kuingia. - *Manuscript* 15, 1909.**{WM 72.3}**

Kufanya Uhusiano Kuna Maana kwa Kristo. - Wapo wengi ambao tumaini limeondoka kwao. Warejeshee uchangamfu mioyoni mwao (jua lizuke mioyoni mwao). Wengi wamepoteza ujasiri wao. Zungumza nao maneno ya

furaha na kuwatia moyo. Waombee. Wapo wale ambao wanahitaji mkate wa uzima. Wasomee kutoka kwenye Neno la Mungu. Juu ya wengi kuna ugonjwa wa roho ambao hakuna zeri ya kidunia inaweza kuufikia au kuponywa tabibu. Omba kwa ajili ya roho hizi. Walete kwa Yesu. Waambie kwamba katika Gileadi kuna zeri na Tabibu. —*Prophets and Kings, 718, 719*.**{WM 73.1}**

Kufanya Kazi kwa Ajili ya Matabaka Yote. - Kila mahali kuna kazi ya kufanywa kwa ajili ya matabaka yote ya jamii. Tunapaswa kuwakaribia maskini na waliopotoka-yaani waisokuwa na maadili mema, au wale walioingia kwenye uovu, wale ambao wameanguka kwa kutokuwa na kiasi (wameshindwa kuzitawala nafsi). Na, wakati huo huo, hatupaswi kuyasahau

matabaka ya juu - mawakili, mawaziri, maseneta, na majaji, ambao wengi wao ni watumwa wa tabia za kutokuwa na kiasi. Hatupaswi kuacha juhudi yoyote bila kujaribiwa katika kuwaonesha kwamba roho zao zinastahili kuokolewa, kwamba inastahili kujitahidi kwa ajili ya maisha ya milele. - *Testimonies for the Church* 7:58.**{WM 73.2}**

Kuitwa katika Mielekeo Mbalimbali ya Huduma. - Bwana anawaita watu Wake kuchukua mielekeo tofauti ya kazi ya umishonari, kupanda mbegu kando ya maji yote. Tunafanya sehemu ndogo sana ya kazi ambayo anataka tuifanye miongoni mwa majirani na marafiki wetu. Kwa huruma kwa maskini, wagonjwa, au wafiwa tunaweza kuwa na mvuto juu yao, kiasi kwamba Ukweli wa Bwana utapata njia

ya kuifikia mioyo yao. Hakuna fursa kama hiyo ya huduma inapaswa kuruhusiwa kupita bila kutumiwa vizuri. Hii ndio kazi ya juu kabisa ya umishonari ambayo tunaweza kuifanya. Uwasilishaji wa Ukweli kwa upendo na huruma, kutoka nyumba hadi nyumba, unapatana na agizo la Kristo kwa wanafunzi Wake alipowatuma katika safari yao ya kwanza ya umishonari. The Review and Herald, June 6, 1912.**{WM 73.3}**

Wasaidie Wanadamu Kama Kristo Alivyofanya. - Alipokuwa [Kristo] akipita katika miji na majiji, alikuwa kama mkondo wa uhai, akisambaza uzima na furaha popote alipoenda. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kufanya kazi kama alivyofanya. Tunapaswa kuwalisha

wenye njaa, kuwavisha walio uchi, na kuwafariji wanaoteseka na wanaoumia. Tunapaswa kuwahudumia wanaokata tamaa na kuamsha tumaini kwa wasio na tumaini — *The Desire of Ages*, 350. **{WM 74.1}**

Kazi Ambayo Kila Kanisa Lilipaswa Kuwa Linaifanya. - Kazi ya kuwakusanya wahitaji, walioonewa, wanaoteseka, mafukara, ni kazi ambayo kila kanisa linaloamini Ukweli wa wakati huu linapaswa kuwa limekuwa likiifanya kwa muda mrefu. Tunapaswa kuonesha huruma laini ya Msamaria katika kutoa mahitaji ya kimwili, kuwalisha wenye njaa, kuwaleta maskini ambao wametupwa nje ya nyumba zetu, tukikusanya kila siku kutoka kwa Mungu neema na nguvu ambayo itatuwezesha kufikia vina hasa vya taabu

za binadamu na kuwasaidia wale ambao hawawezi kujisaidia wenyewe. Katika kufanya kazi hii tuna nafasi nzuri ya kumtangaza Kristo Yeye aliyesulubiwa. - *Testimonies for the Church* 6:276.**{WM 74.2}**

Mahubiri Hayawezi Kuifanya. - Kwa kazi binafsi wafikie watu pale walipo. Zoeana nao. Kazi hii haiwezi kufanywa na wakala au kwa kumtuma mtu mwingine. Fedha zilizokopeshwa au kutolewa haziwezi kuitimiza. Mahubiri kutoka kwenye mimbari hayawezi kuifanya. - *Gospel Workers*, 188.**{WM 74.3}**

Vikosi vya Kuleta Uchangamfu moyoni. - Kuna nguvu katika huduma ya wimbo. Wanafunzi ambao wamejifunza kuimba nyimbo tamu za

injili kwa tuni na kusikika kwa udhahiri wanaweza kufanya mema mengi sawa na wainjilisti waimbaji. Watapata fursa nyingi za kutumia vipaji ambavyo Mungu amewapa katika kubeba sauti tamu ya wimbo na uchangamfu kwenda katika maeneo mengi yenye upweke yaliyogubikwa na huzuni na mateso, wakiimba kwa wale ambao hupata mara chache faida kubwa za kuwa na kanisa. **{WM 75.1}**

Wanafunzi, nendeni nje katika barabara kuu na maboma. Jitahidini kuwafikia watu wa matabaka ya juu na pia matabaka ya chini. Ingia katika nyumba za matajiri na za maskini, na kadiri unavyopata fursa, uliza, "Je, mngependa tuimbe nyimbo za injili?" Kisha pale mioyo inapolainishwa, njia inaweza kukufunguliwa kwa ajili ya

kutoa maneno machache ya maombi kwa ajili ya baraka za Mungu. Si wengi watakaokataa kusikiliza. Huduma kama hiyo ni kazi ya Kweli ya umisionari. - *Counsels to Parents, Teachers, and Students*, 547, 548.**{WM 75.2}**

Uwanja Mpana wa Huduma ya Kiutendaji. - Kuna uwanja mpana wa kutoa huduma kwa ajili ya wanawake na wanaume pia. Mpishi mzuri anayejua kufanya kazi yake kwa ufanisi, mshonaji, muuguzi - msaada wa hawa wote unahitajika. Hebu washiriki wa kaya maskini wafundishwe jinsi ya kupika, jinsi ya kutengeneza na kurekebisha mavazi yao wenyewe, jinsi ya kuwatunza wagonjwa, jinsi ya kutunza nyumba na mali iliyomo humo vizuri. Hata watoto wanapaswa kufundishwa kufanya kazi ndogo ndogo za upendo na rehema kwa

wale wasio na bahati kama wao wenyewe.**{WM 75.3}**

Njia zingine za kutumika kwa ufanisi ili kuleta manufaa zitafunguliwa mbele ya wale ambao wako tayari kufanya kazi iliyo karibu nao. Si wasemaji wenye ufasaha au wasomi wenye lugha ya kushawishi ambao wanahitajika sasa, bali ni wanaume na wanawake wanyenyekevu, walio kama Kristo.**{WM 75.4}**

Fanya kazi bila upendeleo, kwa upendo, kwa uvumilivu, kwa wale wote unaokutanishwa nao. Usioneshe pupa au kukosa subira. Usitamka neno lolote lisilo jema. Hebu upendo wa Kristo uwe mioyoni mwenu, sheria ya wema midomoni mwenu. - *The Review and Herald*, Agosti 7, 1913.**{WM 76.1}**

Kutumia Likizo Zetu Kupeleka Ujumbe wa Bwana. - Kuna njia zingine za kufanya kazi. Wengine wana uwezo wa kusoma Maandiko na kuwasilisha kwa wengine kile tunachokiamini. Hizi zinaweza kuwa njia za nuru na faraja yenye thamani kubwa kwa baadhi ya roho maskini waliovunjika moyo ambao wanaonekana kushindwa kufahamu tumaini na kuizoeza imani yao. Wengine wanapaswa kutafuta na kujifunza jinsi wanavyoweza kupeleka ujumbe kwa ajili ya Bwana. Ikiwa wale ambao ajira zao zinachukua muda wao mwingi, isipokuwa Jumapili au likizo, badala ya kutumia muda huu kwa furaha zao wenyewe, wautumie katika kuwabariki wengine, watakuwa na msaada katika njia ya Mungu. Mfano wako utawasaidia

wengine kufanya jambo fulani lenye nguvu kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Maneno ya mtume aliyevuviwa, "Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu." Hivyo kanuni hai italetwa katika maisha yako ya kila siku ya utendaji, maisha ya kuwa mwema na mwenye kutenda mema....**{WM 76.2}**

Haitawezekana kwa wote kutoa muda wao wote kwa kazi hiyo, kwa sababu ya kazi ambayo ni lazima waifanye ili kupata riziki yao ya kila siku. Lakini bado hawa wana likizo zao na nyakati ambazo wanaweza kujitolea kwa kazi ya Kikristo, na kufanya mema kwa njia hii ikiwa hawawezi kutoa mali zao nyingi. - *Letter* 12, 1892.**{WM 76.3}**

Saa ambazo mara nyingi zinatumiwa katika burudani ambazo haziburudishi mwili wala roho zingepaswa kutumiwa katika kuwatembelea maskini, wagonjwa, na wanaoteseka, au katika kutafuta kumsaidia mtu ambaye ana uhitaji. - *Testimonies for the Church* 6:276.**{WM 76.4}**

Huduma ya Ustawi Katika Siku ya Sabato. - Kulingana na amri ya nne, Sabato iliwekwa wakfu kwa ajili ya mapumziko na ibada ya kidini. Kazi zote za kidunia zilipaswa kuwekwa kando, lakini kazi za rehema na ukarimu zilikubaliana na kusudi la Bwana. Hazikupaswa kuwekewa mipaka ya muda au mahali. Kuwasaidia wenye shida, kuwafariji wenye huzuni, ni kazi ya upendo ambayo inaleta heshima kwa

siku takatifu ya Mungu. - *Redemption: or the Teachings of Christ,* no. 4, uk. 46. **{WM 77.1}**

Mbinu za Kutembelea za Siku za Awali. - Hebu wale wanaohisi kuwa mzigo wa roho uko juu yao watoke na kufanya kazi nyumba kwa nyumba, na kuwafundisha watu amri juu ya amri, huku kidogo, na huku kidogo, wakiwaongoza polepole kwenye nuru kamili ya Ukweli wa Biblia. Hiki ndicho tulichopaswa kukifanya katika siku za awali za ujumbe. Kadiri juhudi za dhati zinapowekwa, Bwana ataruhusu baraka Yake ikae juu ya wafanyakazi na juu ya wale ambao wanatafuta ufahamu wa Ukweli kama ulivyo katika Neno la Mungu.**{WM 77.2}**

Kuna Ukweli wa thamani kubwa, Ukweli tukufu, katika Neno la Mungu, na ni faida kuu kwetu kuleta Ukweli huu mbele ya watu. Katika sehemu zile za mashambani ambapo wengi hawawezi kuhudhuria mikutano mbali na nyumba zao, tunaweza kuwaletea Ukweli moja kwa moja na tunaweza kufanya kazi pamoja nao kwa usahili.**{WM 77.3}**

Kuna nuru gani katika Neno! Katika Isaya tunasoma, "Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu Wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao." Hii ndio kazi tunayopaswa kuifanya. Zingatia maneno: “Watu Wangu” Kwa nini nabii aseme, "Watu Wangu"? Hawakuwa wanatembea kulingana na nuru ya Ukweli, lakini Mungu alitamani kuwaokoa kutoka katika dhambi zao.

Ukweli ulipaswa kuletwa upya kwao katika usahili wake.**{WM 77.4}**

Ujumbe wa malaika wa tatu lazima uende kwa watu wote, na Kristo ametamka kwamba unapaswa kutangazwa katika barabara kuu na ndogo. "Piga kelele, usiache," Anaagiza. Hii inamaanisha kwamba popote watakapowasilisha Ukweli, iwe mbele ya kusanyiko la hadhara au nyumba kwa nyumba, wao wanapaswa kuuwasilisha kama unavyodhihirishwa katika Neno la Mungu. - *Manuscript* 15, 1909.**{WM 77.5}**

Tusisubiri Roho Zije Kwetu. - Hatupaswi kusubiri watu waje kwetu; ni lazima sisi tuwatafute mahali walipo. Neno linapokuwa limehubiriwa katika mimbari, kazi ndipo tu imeanza. Kuna

watu wengi ambao hawatafikiwa na injili isipokuwa imepelekwa kwao. – *Christ's Object Lessons*, 229.**{WM 78.1}**

Fanya kazi kutoka nyumba hadi nyumba, bila kuwapuuza maskini, ambao kwa kawaida hupitwa. Kristo alisema, "Amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema," nasi tunapaswa kwenda kufanya vivyo hivyo. - *The Review and Herald*, Juni 11, 1895. **{WM 78.2}**

"Nimepotea! na Wewe Kamwe Hukunionya!" - Nenda kwenye nyumba hata za watu wale ambao hawaoneshi kuvutiwa. Wakati sauti tamu ya rehema inamwalika mwenye dhambi bado, wewe fanya kazi kwa kila nguvu ya moyo na ubongo, kama vile Paulo, "ambaye hakuacha kumwonya

kila mtu usiku na mchana kwa machozi." Katika siku ile ya Mungu ni wangapi watakaotukabili na kusema, "Nimepotea! Nimepotea! Na kamwe hamkunionya; kamwe hamkunisihi kuja kwa Yesu. Kama ningeamini kama mlivyoamini nyinyi, ningeliifuata kila roho itakayoingia Hukumuni iliyo karibu nami, kwa maombi na machozi na maonyo." — *The Review and Herald*, Juni 24, 1884.**{WM 78.3}**

Uhusiano wa Uinjilisti wa Kutembelea kwa Hali Yetu ya Kiroho Sisi Wenyewe. - Watembelee majirani zako kwa urafiki, na uzoeane nao....Wale ambao hawaifanyi kazi hii, wale ambao wanatenda kwa kutokujali ambako baadhi wameonesha, punde wataupoteza upendo wao wa kwanza na wataanza kuwalaumu, kuwakosoa, na

kuwalaani ndugu zao wenyewe. - *The Review and Herald*, Mei 13, 1902.**{WM 78.4}**

Kazi si ya Kuchosha au Isiyovutia. - Wote wale ambao wanazungumza na Mungu watapata kazi tele za kufanya kwa ajili Yake. Wale wanaosonga mbele katika roho ya Mwalimu, wakitafuta kuzifikia roho na Ukweli, hawataiona kazi ya kuvuta roho kwa Kristo kuwa kazi ngumu, ya kuchosha na isiyovutia/isiyopendeza moyo. Wameagizwa kufanya kazi kama watunza shamba la Mungu, na watazidi kujazwa na nguvu kadiri wanavyojitoa kwa utumishi wa Mungu. Ni kazi ya furaha kufungua Maandiko kwa wengine. - *Testimonies for the Church* 9:118.**{WM 79.1}**

Wafanye Wengine Kuwa na Furaha. - Uwe na furaha katika Mungu. Kristo ni nuru, na ndani Yake hakuna giza lolote. Tazama kuelekea kwenye nuru. Jizoezeni kuzungumzia sifa za Mungu. Wafanye wengine kuwa na furaha. Hii ndio kazi yenu ya kwanza. Nayo itaimarisha sifa bainifu za tabia zilizo bora. Fungueni madirisha ya roho wazi kabisa kuelekea mbinguni, na nuru ya jua la haki ya Kristo ipate kuingia. Asubuhi, adhuhuri, na usiku mioyo yenu inaweza kujazwa na miale inayong'aa ya nuru ya mbinguni. - *The Review and Herald*, Aprili 7, 1904.**{WM 79.2}**

Amsha Tena Roho Ile ya Uinjilisti ya 1844. - [Huu, ujumbe wa mwisho wa Ellen G. White kwa Konferensi Kuu katika kikao cha uchaguzi mwaka wa 1913, ulisomwa kwa

Mkutano na mwenyekiti, A. G. Daniells, Jumanne asubuhi, Mei 27.] – Hivi karibuni katika wakati wa usiku akili yangu ilivutiwa na Roho Mtakatifu na wazo kwamba ikiwa Bwana anakuja karibuni kama tunavyoamini, tunapaswa kuwa hai zaidi kuliko tulivyokuwa katika miaka ya nyuma katika kupeleka Ukweli mbele ya watu. **{WM 79.3}**

Kuhusiana na hili akili yangu ilirejea katika shughuli za waumini wa Marejeo mnamo mwaka 1843 na 1844. Wakati ule kulikuwa na matembezi mengi ya nyumba kwa nyumba, na juhudi zisizokoma zilifanywa ili kuwaonya watu juu ya mambo ambayo yanasemwa katika Neno la Mungu. Tunapaswa kuwa tunaweka juhudi kubwa hata zaidi kuliko ilivyowekwa na wale waliotangaza

ujumbe wa malaika wa kwanza kwa uaminifu kiasi kile. Tunakaribia mwisho wa historia ya dunia hii kwa kasi; na pale tunapotambua kuwa Yesu anakuja hivi karibuni, tutaamshwa kufanya kazi kuliko ambavyo tumewahi kufanya hapo awali. Tunaamrishwa kutoa tangazo la onyo kwa watu. - *The General Conference Bulletin*, Mei 27, 1913, uk. 164.**{WM 79.4}**

Leta Tena Kazi Hii Katika Utendaji. - Kadiri, ambavyo kama wanafunzi, mnakwenda kutoka sehemu moja hadi nyingine, mkisimulia kisa cha upendo wa Mwokozi, mtatengeneza marafiki na mtaona matunda ya kazi yenu. Wafanyakazi wote wa kweli, wanyenyekevu, wenye upendo, waaminifu watategemezwa na kuimarishwa na nguvu kutoka juu.

Watafanikiwa njia yao ya kufikia mioyo ya watu watakapofuata mfano wa Kristo. Wagonjwa watahudumiwa, wenye shida wataombewa. Kutasikika sauti ya kuimba na sauti ya kuomba. Maandiko yatafunguliwa ili kuushuhudia Ukweli. Na kwa ishara zitakazofuata, Bwana atalithibitisha Neno lililonenwa.**{WM 80.1}**

Aina hii ya kazi ni mtindo ulioachwa (haiko kwenye fasheni tena). Hebu na iletwe tena katika utendaji. Mashamba yote ni meupe tayari kwa kuvunwa. Bwana anatamani wengi zaidi waende shambani kwa ajili ya kuvuna. Yeye Atakuwa pamoja na wale wanaojifunza Neno Lake na kutii amri Zake. Yeye Atawapa neema Yake. Enendeni kwa Jina la Kristo, mkikumbuka kwamba Yeye ni mwenzi wenu, kwamba kila sala,

kila neno, kila wimbo, husikilizwa na Yeye. Ujumbe wa ujio wa Bwana hivi karibuni kwa nguvu na utukufu mkubwa utaleta usadikisho kwa mioyo mingi. - *The Review and Herald*, Februari 4, 1904.**{WM 80.2}**

Sura ya Kumi - Wema Ufunguo wa Mioyo

Wengi Walifikiwa kwa Upendo na Wema Peke Yake. - Wale wanaohusika katika kazi ya nyumba kwa nyumba watapata fursa za huduma kwa njia nyingi. Watapaswa kuwaombea wagonjwa na watapaswa kufanya kila

wawezalo kuwaondolea mateso. Watapaswa kufanya kazi kati ya watu wa hali ya chini, maskini, na walioonewa. Tunapaswa kuwaombea na kuomba pamoja pamoja na wale wasiojiweza ambao hawana nguvu ya dhamira ya kudhibiti hamu ya chakula ambayo imeshushwa na hisia kali za uchu/ulafi. Jitihada za dhati na za kudumu lazima zifanyike kwa ajili ya wokovu wa wale ambao katika mioyo yao shauku imeamshwa. Wengi wanaweza kufikiwa kwa njia pekee ya matendo ya wema yasiyo na upendeleo au ubinafsi. Haja zao za kimwili lazima kwanza zitulizwe. Pale wanapoona ushahidi wa upendo wetu usio na ubinafsi, itakuwa rahisi kwao kuuamini upendo wa Kristo.**{WM 81.1}**

Wauguzi wamishonari wana sifa zinzostahili kabisa kwa ajili ya kazi hii, lakini wengine wanapaswa kuungana nao. Hawa, ingawa hawana elimu maalum na mafunzo katika uuguzi, wanaweza kujifunza kutoka kwa wafanyakazi wenzao namna bora ya kufanya kazi.**{WM 81.2}**

Mazungumzo, Ufarisayo, na kujisifu ni kwingi; lakini haya kamwe hayataongoa roho kwa Kristo. Upendo safi, uliotakaswa, kama upendo ule uliooneshwa katika kazi ya maisha ya Kristo, ni kama manukato matakatifu. Kama kichupa cha marhamu cha Mariamu kilichovunjwa, upendo unajaza nyumba nzima kwa harufu nzuri. Lugha ya kushawishi, ufasaha, umbuji, ujuzi wa Ukweli, vipaji adimu, vikichanganywa na upendo, vyote ni

majaliwa ya thamani kubwa. Lakini uwezo peke yake, vipaji bora peke yake, haviwezi kuchukua nafasi ya upendo. - *Testimonies for the Church* 6:83, 84. **{WM 81.3}**

Kwa Upendo Ambao Unatoka Moyoni. - Upendo ndio msingi wa utauwa. Kwa vyovyote vile wanavyokiri, hakuna mtu aliye na upendo safi kwa Mungu isipokuwa ana upendo usio na ubinafsi kwa ndugu yake. Lakini hatuwezi kamwe kuwa na roho hii kwa kujaribu kuwapenda wengine. Kinachohitajika ni upendo wa Kristo moyoni. Wakati nafsi imeunganishwa na Kristo, upendo huchipuka wenyewe. Ukamilifu wa tabia ya Kikristo unapatikana wakati msukumo wa kuwasaidia na kuwabariki wengine daima unatokeza kutoka ndani-wakati

jua la uchangamfu wa mbinguni unaijaza moyo na kudhihirishwa katika uso.**{WM 81.4}**

Haiwezekani kwa moyo ambamo ndani yake Kristo anakaa kutokuwa na upendo. Ikiwa tunampenda Mungu kwa sababu alitupenda sisi kwanza, tutawapenda wote ambao kwa ajili yao Kristo alikufa. Hatuwezi kugusana na Uungu bila kugusana na ubinadamu; kwa kuwa ndani Yake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi cha ulimwengu, Uungu na ubinadamu vimeunganishwa. Tukiunganishwa na Kristo, tumeunganishwa na wanadamu wenzetu kwa viungo vya dhahabu vya mnyororo wa upendo. Ndipo huruma na masikitiko ya Kristo yatadhihirika katika maisha yetu. Hatutasubiri hadi maskini na wasiojiweza wameletwa kwetu.

Hatutahitaji kuombwa kwa kusihi kuhisi shida za wengine. Itakuwa ni kawaida kwetu kuwahudumia wahitaji na wanaoteseka kama ilivyokuwa kwa Kristo kwenda huku na huko akitenda mema. **{WM 82.1}**

Popote ambapo pana msukumo wa upendo na huruma, popote moyo unapofikia kwa ajili ya kubariki na kuwainua wengine, hapo panadhihirishwa utendaji wa Roho Mtakatifu wa Mungu. - *Christ's Object Lessons*, 384, 385.**{WM 82.2}**

Upendo na Huruma ya Kristo Viliwavuta Watu. - Walikuwa ni wale waliotengwa, watoza ushuru na wenye dhambi, waliodharauliwa katika mataifa, ambao Kristo aliwaita waje Kwake. Tabaka moja ambalo kamwe

hangeliangalia lilikuwa ni wale ambao walijitenga kando kwa kujitukuza kwao na kujifikiria ni wa muhimu zaidi, na kuwadharau wengine. -*The Ministry of Healing*, 164.**{WM 82.3}**

Kupenda Kama Kristo Alivyopenda. - Upendo ambao unatiwa msukumo na upendo tulio nao kwa Yesu utaona katika kila nafsi, tajiri na maskini, thamani ambayo haiwezi kupimwa kwa makadirio ya kibinadamu. Ulimwengu unazama katika kutokuwa na maana kwa kulinganishwa na thamani ya roho moja. Upendo wa Mungu uliodhihirishwa kwa mwanadamu ni zaidi ya mkokotoo wowote wa kibinadamu. Ni upendo usio na mwisho. Na wakala wa kibinadamu ambaye ni mshirika wa asili ya Kiungu atapenda kama Kristo anavyopenda,

atafanya kazi kama Kristo alivyofanya kazi. Kutakuwapo na huruma ya asili (kutoka ndani) na utu wema ambavyo havitapungua au kukatishwa tamaa. Hii ndio roho ambayo inapaswa kuhimizwa kuishi katika kila moyo na kudhihirishwa katika kila maisha. Upendo huu unaweza kuwepo na kufanywa kuwa umetakaswa, mtakatifu, safi, na kuinuliwa kupitia upendo uliomo rohoni kwa ajili ya Yesu Kristo peke yake, ukilishwa kwa mazungumzo ya kila siku na Mungu. Ubaridi wote huu kwa upande wa Wakristo ni kuikana imani. Lakini roho hii itayeyuka kabisa mbele ya miale inayong'aa ya upendo wa Kristo ndani ya mfuasi wa Kristo. Kwa hiari, kwa urahisi, atatii amri ile isemayo "Mpendane kama nilivyowapenda

ninyi.” -*Manuscript* 60, 1897.**{WM 83.1}**

Omba kwa Ajili ya Mioyo Yenye Huruma. - Kwa kadiri tunavyomwamini Kristo kwa hakika na kufanya mapenzi Yake, wala si kujiinua, bali kutembea kwa unyenyekevu wote wa akili, ndivyo hakika Bwana atakavyokuwa pamoja nasi.... Omba kwamba atakupa moyo wa nyama, moyo ambao unaweza kuhisi huzuni za wengine, ambao unaweza kuguswa na shida za mwanadamu. Omba kwamba atakupa moyo ambao hautakuruhusu kuwa kiziwi kwa mjane au yatima. Ombeni ili mpate kuwa na hali ya kuwaonea huruma maskini, wenye udhaifu, na walioonewa. Ombeni, kwamba mpate kupenda haki, na kuchukia unyang’anyi, na wala usifanye

tofauti katika utoaji wa fadhila zako, isipokuwa pale unapozingatia hali za maskini na wasiojiweza. Ndipo ahadi zilizoandikwa katika Isaya 58 zitakapotimizwa kwako. - *Letter* 24, 1889.**{WM 83.2}**

Ukiongea Neno la Kutia Moyo. - Kamwe, kamwe usije kuwa katili, baridi, usiye na huruma kwa wengine, na mwenye kulaumu. Kamwe usipoteze fursa hata moja ya kusema neno la kutia moyo na kutia msukumo kuwa na tumaini. — *Testimonies for the Church* 5:613.**{WM 84.1}**

Katika kufanya kazi kwa wahanga wa tabia mbaya, badala ya kuwaelekeza kwenye kukata tamaa na uharibifu ambao wanaharakisha kuuendea, geuza macho yao kwa Yesu. Waelekeze katika

utukufu wa mbinguni. Hii itafanya zaidi katika kuuokoa mwili na roho kuliko itakavyofanya hofu zote za kaburi zinapowekwa mbele ya wasiojiweza na wanaoonekana kutokuwa na tumaini. - *The Ministry of Healing*, 62.**{WM 84.2}**

Hakuna Anayerejeshwa kwa Lawama. - Siku zote ni jambo linalotia fedheha kuweka wazi makosa ya mtu. Asiwepo hata mmoja atakayefanya uzoefu huo kuwa mchungu zaidi kwa lawama zisizo za lazima. Hakuna mtu aliyewahi kurejeshwa kwa lawama; isipokuwa wengi wamefukuzwa kwa kufanya hivyo, na kuongozwa katika kufanya mioyo yao kuwa migumu kama chuma dhidi ya usadikisho. Roho nyororo, laini, yenye upole, na mwenendo wa kuvutia vinaweza

kuwaokoa wenye makosa na kuficha wingi wa dhambi. - *The Ministry of Healing*, 166.**{WM 84.3}**

Himiza Upendo wa Ukarimu. - Kadiri mnavyotazama kwa makini shauku yenu ya milele, amkeni, na anzeni kupanda mbegu njema. Mlichopanda ndicho mtakachovuna. Mavuno yanakuja - wakati wa mavuno mengi, wakati tutakapovuna kile tulichopanda. Hakutakuwa na kushindwa kwa mazao kuzaa vizuri. Mavuno ni ya hakika. Sasa ndio wakati wa kupanda. Sasa fanya juhudi za kuwa tajiri katika kutenda mema, "wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli." Nawasihi, ndugu zangu, katika kila

mahali, mjiondolee huo ubaridi wenu wa barafu. Himiza ndani yenu kuupenda ukarimu, upendo wa kuwasaidia wale wanaohitaji msaada. -*The Review and Herald*, Aprili 20, 1886.**{WM 84.4}**

Fufua Roho ya Msamaria Mwema. - Roho ya Msamaria mwema kwa kiasi kikubwa haijaletwa katika makanisa yetu. Wengi wanaohitaji msaada wamepitwa kando, kama vile kuhani na Mlawi walivyopita kando ya mgeni aliyejeruhiwa na kuchubuliwa ambaye alikuwa ameachwa afe kando ya njia. Wale hasa ambao walihitaji uweza wa Mponyaji wa Bwana kutibu majeraha yao wameachwa bila kujaliwa na bila kutambuliwa. Wengi wametenda kana kwamba inatosha kujua kwamba Shetani alikuwa ameweka mtego wake umetegwa kwa ajili ya roho fulani, na

kwamba wangeweza tu kwenda nyumbani na kutowajali kondoo waliopotea. Ni dhahiri kwamba wale wanaodhihirisha roho kama hiyo hawajawa washiriki wa asili ya Kiungu/mbingu, bali wa sifa bainishi za adui wa Mungu. - *Testimonies for the Church* 6:294, 295.**{WM 85.1}**

Huruma Pia

Fadhila/ukarimu/upendo. - Nimeoneshwa kwamba miongoni mwa wale wanaoukubali Ukweli wa sasa kuna wengi ambao mielekeo na tabia zao zinahitaji kuongolewa. Kila mtu anayedai kuwa ni Mkristo anapaswa kujichunguza mwenyewe, na kuona kama yeye ni mwema na mwenye kuwafikiria wanadamu wenzake kama vile anavyotaka wanadamu wenzake wawe kwake. Wakati hili litakapofanyika

kutakuwa na onesho litakalofanana na mfano wa Bwana/Kiungu.**{WM 85.2}**

Bwana anaheshimiwa kwa matendo yetu ya rehema, kwa utendaji wa kuwafikiria kwa uangalifu wale wasiojiweza na wenye shida. Mjane na yatima wanahitaji zaidi ya fadhila zetu. Wanahitaji huruma na uangalizi na maneno ya huruma na mkono wa msaada kuwaweka mahali ambapo wanaweza kujifunza kumudu maisha wao wenyewe. Matendo yote yanayotendwa kwa wale wanaohitaji msaada ni kana kwamba yametendwa kwa Kristo. Katika kujifunza kwetu kujua jinsi ya kuwasaidia wasiojiweza tunapaswa kujifunza njia ambayo kwayo Kristo alifanya kazi. Hakukataa kufanya kazi kwa wale waliofanya makosa; kazi Zake za rehema zilifanywa kwa kila

tabaka, wenye haki na wasio haki. Kwa wote sawa aliponya ugonjwa na kutoa masomo ya mafundisho ikiwa walimwomba kwa unyenyekevu.**{WM 85.3}**

Wale wanaodai kumwamini Kristo wanapaswa kumwakilisha Kristo katika matendo ya wema na rehema. Watu kama hao hawatajua kamwe hadi siku ya hukumu ni mema gani wametenda katika kujitahidi kufuata mfano wa Mwokozi. - *Letter* 140, 1908. **{WM 86.1}**

Wema ni Ufunguo kwa Uinjilisti Mkubwa. - Kama tungejinyenyekesha mbele za Mungu, na kuwa watu wema na wenye adabu na wapole na wenye huruma, kungekuwapo na waongofu mia moja wa kuufuata Ukweli pale

ambapo kwa sasa yupo mmoja tu. - *Testimonies for the Church* 9:189.**{WM 86.2}**

Sura ya Kumi na Moja - Jinsi ya Kutembelea na Nini cha Kufanya

Njoo Karibu na Majirani Zako-Wakaribie!. - Nenda kwa majirani zako mmoja baada ya mwingine, na uwakaribie mpaka mioyo yao imechangamshwa na shauku na upendo wako usio na ubinafsi. Wahurumie, waombee, angalia fursa za kuwatendea mema, na kadiri uwezavyo, wakusanye

wachache pamoja na kufungua Neno la Mungu kwa akili zao zenye giza. - *The Review and Herald*, Machi 13, 1888. **{WM 87.1}**

Toa Msaada Pale Ambapo Msaada Unahitajika Hasa. - Kuna wale ambao wanakuwazunguka kote, nao wana matatizo, wale ambao wanahitaji maneno ya huruma, upendo, na upole, na maombi yetu ya unyenyekevu na ya huruma. Wengine wanateseka chini ya mkono wa chuma wa umaskini, wengine kwa ugonjwa, na wengine kwa maumivu ya moyo, kukata tamaa, na majonzi. Kama Ayubu, wewe unapaswa kuwa macho kwa vipofu na miguu kwa vilema, na unapaswa kuuliza juu ya kusudi ambalo hulijui na kulichunguza kwa lengo lenye nia ya kupunguza mahitaji yao na kusaidia pale

hasa wanapohitaji msaada. - *Testimonies for the Church* 3:530. **{WM 87.2}**

Kwanza kidhi mahitaji ya maisha ya wahitaji na kupunguza haja na mateso yao ya kimwili, na hapo ndipo utakapopata njia ya wazi ya kuingia moyoni, ambapo utaweza kupanda mbegu nzuri ya wema na dini. - *Testimonies for the Church* 4:226, 227. **{WM 87.3}**

Mbinu ya Kushawishi kwa njia chanya.- Waendee watu kwa namna ya kushawishi, kwa ukarimu, ukiwa umejaa uchangamfu na upendo kwa Kristo.... Hakuna ulimi wa mwanadamu unaoweza kuelezea thamani ya huduma ya Neno na Roho Mtakatifu. Hakuna maneno ya kibinadamu yanayoweza

kuifafanulia akili yenye ukomo thamani ya ufahamu na kwa imani hai kupokea baraka ambayo hutolewa na Yesu wa Nazareti anapopita. - *Letter* 60, 1903. **{WM 87.4}**

Dumisha Mtazamo Sahihi kwa Watu. - Ni jambo nyeti kushughulika na akili za watu. Ni Yeye tu anayesoma moyo Ndiye anayejua jinsi ya kuwaleta watu kwenye toba. Ni hekima Yake tu inayoweza kutupatia mafanikio katika kuwafikia waliopotea. Unaweza kusimama kwa ushupavu, ukihisi, "Mimi ni mtakatifu kuliko wewe," na haijalishi ni jinsi gani kufikiri kwako ni sahihi au jinsi gani maneno yako ni ya kweli; kamwe hayatagusa mioyo. Upendo wa Kristo, unaodhihirishwa katika maneno na matendo, utafanikiwa kupata njia ya kufikia roho, wakati

ambapo kurudiwa rudiwa kwa amri au kuhojiana kusingetimiza chochote. - *The Ministry of Healing*, 163, 164. **{WM 88.1}**

Onesha Huruma ya Dhati. Tunahitaji zaidi huruma kama ya Kristo; si huruma kwa wale tu ambao wanaonekana kwetu kuwa hawana makosa, bali ni huruma kwa roho maskini, wanaoteseka, wanaotaabika, ambao mara nyingi wanapatikana na makosa, wakitenda dhambi na kutubu, wakijaribiwa na kuvunjika moyo. Tunapaswa kwenda kwa wanadamu wenzetu, tukiguswa, kama Kuhani wetu Mkuu Mwenye rehema, na hisia za udhaifu wao. - *The Ministry of Healing*, 164. **{WM 88.2}**

Fanya Kazi kwa Namna Ambayo Itaondoa Chuki. - Ndugu na dada zangu, watembeleeni wale wanaoishi karibu nanyi, na kwa huruma na wema jitahidini kuifikia mioyo yao. Hakikisha unafanya kazi kwa namna ambayo itaondoa chuki badala ya kuitengeneza. Na kumbuka kwamba wale ambao wanaujua Ukweli wa wakati huu na bado wanazuia juhudi zao kwa makanisa yao wenyewe, wakikataa kufanya kazi kwa majirani zao ambao hawajaongoka, wataitwa kutoa hesabu kwa ajili ya wajibu ambao haukukamilishwa. - *Testimonies for the Church* 9:34, 35. **{WM 88.3}**

Ingia Nyumbani Unapoweza. Sogea karibu na watu; ingia katika familia za watu unapoweza; usingoje

watu wamsakesake mchungaji. - *Letter* 8, 1895. **{WM 89.1}**

Hatua Tatu Muhimu katika Huduma ya Nyumba kwa Nyumba. - Mzigo sasa ni kuzisadikisha roho kwa Ukweli. Hii inaweza kufanywa vizuri kabisa kwa juhudi za binafsi, kwa kuleta Ukweli ndani ya nyumba zao, kuomba pamoja nao, na kuwafungulia Maandiko. - *The Review and Herald,* Desemba 8, 1885. **{WM 89.2}**

Umuhimu wa Kupeana Mikono. - Mengi hutegemea jinsi ambavyo unakutana na wale ambao unawatembelea. Unaweza kushika mkono wa mtu katika salamu kwa namna ambayo itakufanya upate ujasiri/imani yake mara moja, au kwa namna ya baridi kiasi kwamba

itamfanya afikiri kwamba huna shauku yoyote naye. - *Gospel Workers*, 189. **{WM 89.3}**

Upole wa Kikristo Unahitajika. - Kuna watu kiasi cha kutosha ambao wanataka kuwa Wakristo, na ikiwa tutaruhusu chachu kuanza kufanya kazi, itashika mmoja na kisha mwingine, kama vile roho ya Mungu itakavyofanya kazi na sisi nasi tutaona kwamba tunaweza kuwafikia watu, si kwa werevu wetu wenyewe, bali kwa Roho wa Mungu. Lakini bado tutahitaji vipaji na uwezo ambavyo Mungu ametupa vitumike. Hatutaki kuwa watu wanaojifunza, au wasiojua kitu milele; tunataka kujua jinsi ya kuenenda ipasavyo sisi wenyewe; tunataka upole wa Kikristo. Na tunataka kuuchukua pamoja nasi katika kazi yetu yote.

Hatutaki pembe yoyote rafu au kali ambayo inaweza kuwa katika tabia yetu kufanywa kuwa maarufu au kushamiri, bali tunataka kufanya kazi kwa unyenyekevu, hivyo tutazisahau hizo pembe rafu, na kisha sifa bainifu zilizo bora zitaingia ndani. Tunataka uchangamfu katika kazi yetu. - *Manuscript* 10, 1888.**{WM 89.4}**

Nguvu ya Uungwana (au kujistahi na kuwa na adabu). Ukuzaji wa uungwana ulio sawa, na nia ya kuwatendea wengine kama ambavyo tungetaka watutendee, vingeangamiza nusu ya shida za maisha. Roho ya kujitwalia zaidi ni roho ya Shetani; lakini moyo ambao ndani yake upendo wa Kristo unahifadhiwa, utakuwa na ukarimu na upendo ule ambao hautafuti

mambo yake mwenyewe. — *Patriarchs and Prophets*, 133.**{WM 90.1}**

Mtazamo Sahihi kwa Maskini. - Hamtakiwi kujichukulia kana kwamba ni kujishusha kukutana na familia maskini. Zungumza kana kwamba ni wanadamu wazuri kama ulivyo. Wana nuru na furaha kidogo, na kwa nini basi tusibebe furaha na nuru ya ziada ipate kuwaangazia na kuijaza mioyo yao. Tunachotaka ni huruma laini ya Yesu Kristo, na ndipo tutaweza kulainisha njia yetu moja kwa moja kuingia ndani ya mioyo yao. Tunataka kuvaa, si kwa fahari au 'majigambo na kujionyesha', bali kwa mavazi sahili kabisa, ili waweze kujisikia kwamba sisi ni sawa na wao na kana kwamba tulichukulia kwamba wao walikuwa na thamani ya kufaa kuokolewa, na tunaweza kulainisha njia

yetu kuingia ndani ya mioyo yao. **{WM 90.2}**

Sasa, ndugu na dada, tunataka chuma kiondolewe kutoka katika roho zetu, na tunataka kiondolewe kutoka katika namna ya kazi yetu. Nasi tunaweza kuwaelimisha wafanyakazi katika kila kanisa. - *Manuscript* 10, 1888. **{WM 90.3}**

Mwenye Busara Kama Alivyokuwa Kristo. -Yeye Alikuwa na busara ya kukutana na akili zilizodhurika, na kuwashangaza kwa vielelezo ambavyo vilivuta usikivu wao. Kwa akili alifikia moyo. — *The Desire of Ages*, 254.**{WM 90.4}**

Zungumza Ujasiri. - Usitoe neno hata moja la kukatisha tamaa, kwa kuwa maneno kama hayo humfurahisha

Shetani. Zungumza juu ya wema wa Kristo na sema juu ya nguvu Zake. Maneno ya matumaini na imani na ujasiri yanazungumzwa kwa urahisi kama maneno ya malalamiko. “Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini.” — *The Review and Herald*, Aprili 7, 1904. **{WM 90.5}**

Uje kwenye Lengo Kuu moja kwa moja, usizungukezunguke. Sasa, tunapoingia ndani ya nyumba hatupaswi kuanza kuzungumza juu ya mambo ya kipuuzi, bali tuje moja kwa moja na kueleza hoja au lengo kuu hasa na kusema, Ninataka wewe upate kumpenda Yesu, kwa maana alikupenda wewe kwanza.... Wapelekee machapisho na uwaombe wayasome. Na watakapoona kuwa wewe ni mnyofu/dhati, hawatadharau yoyote

katika juhudi zako. Kuna njia ya kufikia mioyo migumu kabisa. Karibia kwa usahili, na unyofu, na unyenyekevu ambao utatusaidia kuzifikia roho za wale ambao Kristo alikufa kwa ajili yao. - *Manuscript* 10, 1888. **{WM 91.1}**

Mwasilishe Kristo wakati mnakaa na kuota Moto Wakati wa Baridi. - Kwa wote ambao wanafanya kazi pamoja na Kristo napenda kusema, Popote ambapo unaweza kupata kuwafikia watu kando ya moto, tumia vizuri fursa yako. Chukua Biblia yako, na ufungue mbele yao Kweli Zake kuu. Mafanikio yako hayatategemea sana juu ya maarifa yako na mafanikio yako kama vile juu ya uwezo wako wa kupata njia ya kufikia mioyo. Kwa kuwa mchangamfu na kuwa karibu na watu, unaweza kugeuza mkondo wa mawazo yao kwa

urahisi zaidi kuliko kwa hotuba yenye ustadi mno. Kumwasilisha Kristo katika familia, kando ya tanuru la kuotea moto, na katika mikusanyiko midogo katika nyumba binafsi mara nyingi hufanikiwa zaidi katika kuongoa roho kwa Yesu kuliko mahubiri yanayofanyika nje, kwa umati ulio katika mwendo, au hata katika kumbi au makanisa. — *Gospel Workers*, 193.**{WM 91.2}**

Elezea Jinsi Ulivyompata Yesu. - Watembelee majirani zako na uoneshe shauku ya wokovu wa roho zao. Amsha kila nguvu ya kiroho ipate kutenda kazi. Waambie wale unaowatembelea kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia. Bwana Yesu Kristo atafungua mlango wa mioyo yao na ataweka juu ya akili zao hisia/mawazo ya kudumu. **{WM 91.3}**

Jitahidi kuwaamsha wanaume na wanawake kutoka katika hali yao ya kutokujali mambo ya kiroho. Waambie jinsi ulivyompata Yesu na jinsi ulivyobarikiwa tangu ulipopata uzoefu katika kazi yake. Waambie ni baraka gani inakuja kwako unapoketi miguuni pa Yesu na kujifunza masomo ya thamani kutoka katika Neno Lake. Waambie juu ya uchangamfu na furaha ambayo iko katika maisha ya Kikristo. Maneno yako ya kusisimua na yenye kuhamasisha yatawashawishi kwamba umepata lulu ya thamani kubwa. Hebu maneno yako yenye ari na uchangamfu, maneno yenye kutia moyo yaoneshe kwamba kwa hakika umepata njia ya juu zaidi. Hii ni kazi ya Kweli ya umisionari, na kadiri inavyofanywa, wengi wataamka kama vile kutoka katika

ndoto. - *Testimonies for the Church* 9:38. **{WM 92.1}**

Mwasilishe Kristo na Upendo Wake Mtamu Sana unaoyeyusha moyo. - Kuna roho nyingi zinazotamani isivyoweza kuelezeka kwa ajili ya nuru, kwa ajili ya uhakika na nguvu ng'ambo ya kile ambacho wameweza kukifahamu. Wanahitaji kutafutwa na kufanyiwa kazi kwa subira, kwa uvumilivu. Msihi Bwana kwa maombi ya bidii kwa ajili ya msaada. Mwasilishe Yesu kwa sababu unamjua Yeye kama Mwokozi wako binafsi. Hebu upendo Wake mtamu sana, neema Yake tele, vitiririke kutoka katika midomo ya wanadamu. Hupaswi kuwasilisha hoja za Mafundisho Makuu isipokuwa umeulizwa (doctrines). Lakini chukua Neno, na kwa upendo laini, wenye shauku kwa ajili ya roho,

uwaoneshe haki ya thamani ya Kristo, ambayo ni lazima kwa hiyo wewe na wao mwokolewe. - *Manuscript* 27, 1895. **{WM 92.2}**

Katika kazi yako yote hebu na ionekane kwamba unamjua Yesu. Wasilisha usafi Wake na neema iokoayo, ili wale unaofanya kazi kwa ajili yao, kwa kutazama, wapate kubadilishwa kufanana na sura ya Bwana. Mnyororo ambao umeshushwa kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu ni mrefu kiasi cha kutosha kufikia kina cha chini kabisa cha dhambi. Mshikilie kwa nguvu Mwokozi anayesamehe dhambi mbele ya waliopotea na wapweke, kwani Yesu amefanya maombezi ya Bwana kwa niaba yao. Anaweza kuwainua kutoka kwenye shimo la dhambi, ili waweze kukubaliwa kama watoto wa Mungu,

warithio pamoja na Kristo kwa urithi wa milele. Wanaweza kuwa na maisha yanayolingana na maisha ya Mungu. - *The Review and Herald*, Aprili 11, 1912. **{WM 92.3}**

Uwezo wa Nyimbo Takatifu. - Wale walio na kipawa cha wimbo wanahitajika. Wimbo ni mojawapo ya njia bora kabisa za kuvutia Ukweli wa kiroho katika moyo. Mara nyingi kwa maneno ya wimbo mtakatifu chemchemi za toba na imani zimefunguliwa. Washiriki wa kanisa, vijana na wazee, wanapaswa kuelimishwa kwenda kutangaza ujumbe huu wa mwisho kwa ulimwengu. Ikiwa wataenda kwa unyenyekevu, malaika wa Mungu watakwenda pamoja nao, wakiwafundisha jinsi ya kupaza sauti katika kuomba, jinsi ya kuinua sauti

katika kuimba, na jinsi ya kutangaza ujumbe wa injili kwa wakati huu. - *The Review and Herald*, Juni 6, 1912. **{WM 93.1}**

Mioyo Huguswa na Wimbo Sahili. - Jifunze kuimba nyimbo sahili kabisa. Hizi zitakusaidia katika kazi ya nyumba kwa nyumba, na mioyo itaguswa na mvuto wa Roho Mtakatifu. Kristo mara nyingi alisikika akiimba nyimbo za sifa; na bado nimesikia watu wakisema, "Kristo kamwe hakutabasamu." Ni kiasi gani mawazo yao kuhusu Mwokozi yamekosewa! Kulikuwamo na furaha moyoni Mwake. Tunapata habari kutoka katika Neno kwamba kuna furaha kati ya malaika wa mbinguni kuhusu mwenye dhambi mmoja anayetubu, na kwamba Bwana Mwenyewe analifurahia kanisa Lake

kwa kuimba. - *The Review and Herald,* Novemba 11, 1902. **{WM 93.2}**

Zungumza Kirafiki na Kutoa Miito Binafsi. - Juhudi binafsi, za mtu mmoja mmoja na shauku kwa marafiki na majirani zako zitafanikisha mengi kuliko inavyoweza kukadiriwa. Ni kwa sababu ya kukosekana kwa aina hii ya kazi roho ambazo Kristo alikufa kwa ajili yake zinaangamia.... Kazi yako inaweza kufanikisha mema halisi mengi kuliko mikutano mikubwa zaidi, ikiwa itakosa juhudi za binafsi. Wakati vyote viwili vimeunganishwa, pamoja na baraka za Mungu, kazi timilifu na kamili zaidi inaweza kutendwa; lakini ikiwa tutakuwa na sehemu moja tu ya kufanywa, hebu na iwe kazi ya mtu binafsi kufungua Maandiko katika kaya, akitoa miito binafsi, na kuzungumza

kwa urafiki na washiriki wa familia, si juu ya mambo yenye umuhimu mdogo, bali juu ya mada kuu za ukombozi. Hebu na waone kwamba moyo wako umeelemewa na mzigo wa wokovu wa roho. - *The Review and Herald*, Machi 13, 1888. **{WM 93.3}**

Ufanisi wa Mbinu ya Maswali. - Ndugu zangu mnaohudumu, msifikiri kwamba kazi pekee unayoweza kufanya, njia pekee unayoweza kufanya kazi kwa ajili ya roho, ni kutoa hotuba. Kazi bora unayoweza kufanya ni kufundisha, kuelimisha. Wakati wowote unapoweza kupata fursa ya kufanya hivyo, kaa chini na baadhi ya familia, na waruhusu kuuliza maswali. Ndipo uwajibu kwa subira na unyenyekevu. Endeleza kazi hii kwa pamoja na mahubiri yenu ya hadhara. Hubiri kidogo, na kuelimisha

zaidi, kwa kufanya masomo ya Biblia na kwa kuomba pamoja na familia na makundi madogomadogo. — *Gospel Workers*, 193.**{WM 94.1}**

Kwa Sauti Iliyojaa Hisia za Kusababisha Huruma. - Hebu sauti ioneshe huruma na upole. Sauti ya Kristo ilikuwa imejaa hisia za kusababisha huruma. Kwa juhudi za kudumu tunaweza kuikuza sauti hiyo, tukiiondolea ukali wote. Hebu na tuombe kwa imani kwa ajili ya sauti iliyoongoka, ulimi ulioongoka, na huruma kama ya Kristo na upole, ili tuweze kuongoa roho kwa Ukweli tunaofundisha. - *The Review and Herald*, Novemba 11, 1902. **{WM 94.2}**

Ikiwa Wanakufungia Mlango Waziwazi, Nini Basi? – “Lakini” mtu

mmoja anasema, “fikiria kwamba hatutapata ruhusu ya kuingia katika nyumba za watu; na tunapodhani kuwa watainuka dhidi ya Ukweli tunaouwakilisha. Je! Hatutajisikia kuwa na kisingizio cha kutokuwafanyia juhudi zaidi?” Hasha! Na hata kama wakikufungia mlango waziwazi usoni pako, usiharakishe kuondoka kwa uchungu au hasira. Na kuacha kufanya juhudi zaidi ya kuwaokoa. Mwombe Mungu kwa imani akupe namna ya kuweza kuzifikia roho hizo hizo. Msiache juhudi zenu, bali chunguzeni na kupanga mikakati hadi mtakapopata njia nyingine za kuzifikia. Ikiwa hamtafanikiwa kwa matembezi ya binafsi, jaribu kuwatumia mjumbe wa kimya wa ile Kweli. Kuna kitu cha kujivunia sana katika dhana ya moyo wa

mwanadamu kwamba machapisho yetu mara nyingi hupata kibali cha kuingia mahali ambapo mjumbe anayeishi hawezi. - *Historical Sketches*, uk. 150. **{WM 94.3}**

Jinsi Kristo Alivyokutana na Watu. - Tutapata mafundisho mengi kwa ajili ya kazi yetu kutokana na kujifunza mbinu za kazi za Kristo na namna Yake ya kukutana na watu. Katika kisa cha injili tunayo rekodi ya jinsi alivyofanya kazi kwa matabaka yote, na jinsi ambavyo alifanya kazi katika miji na vijiji na maelfu walivutwa upande Wake kuja kusikia mafundisho Yake. Maneno ya Mwalimu yalikuwa wazi na kusikika kwa urahisi na yalisemwa kwa huruma na upole. Yalibeba hakika kwamba hapa palikuwa na Ukweli. Ilikuwa ni usahili, unyofu na

bidii ambayo kwayo Kristo alifanya kazi na kuzungumza ambayo iliwavuta wengi Kwake. - *The Review and Herald*, Januari 18, 1912. **{WM 95.1}**

Si Kutenda Kama Mashine Bila Kufikiri Kazini.-Wote wanaojihusisha katika kazi hii ya binafsi wanapaswa kuwa waangalifu sana wasiwe kama mashine katika namna yao ya kufanya kazi kama vile tu ambavyo ingempasa mchungaji anayelihubiri Neno. Daima wanapaswa kuwa wanajifunza. — *Gospel Workers*, 193. **{WM 95.2}**

Buni Mbinu Mpya. – Ninasema na Wakristo wanaoishi katika miji yetu mikubwa: Mungu amewafanya kuwa maghala ya ile Kweli, si kwamba mpate kuuzuilia, bali ili mweze kuwapa wengine. Mnapaswa kutembelea

nyumba hadi nyumba kama mawakili waaminifu wa neema ya Kristo. Kadiri mnavyofanya kazi, kubuni, na kupanga, mbinu mpya zitaendelea kujionesha katika akili zenu na kwa kutumika, uwezo wa akili zenu utaongezeka. Utendaji wa wajibu ulio vuguvugu, na mlegevu ni jeraha kwa roho ambaye Kristo amekufa kwa ajili yake. Ikiwa tunataka kuzipata lulu zilizofukiwa katika vifusi vya mijini, tunapaswa kusonga mbele tukiwa tayari kufanya kazi inayotakiwa na Bwana. - *The Review and Herald*, Juni 11, 1895. **{WM 95.3}**

Maisha Mapya na Mipango Mipya. - Watu wanahitajika ambao huomba kwa Mungu kwa ajili ya hekima, na ambao, chini ya uongozi wa Mungu, wanaweza kuweka uhai mpya

katika mbinu za zamani za kazi na wanaweza kubuni mipango mipya na mbinu mpya za kuamsha shauku ya washiriki wa kanisa na kuwafikia wanaume na wanawake wa ulimwengu. - *Manuscript* 117, 1907. **{WM 96.1}**

Katika Nguvu ya Ushawishi, Maombi, na Upendo. - Maskini wanapaswa kufarijiwa na kupewa afueni, wagonjwa kutunzwa, wenye huzuni na wafiwa kufarijiwa, wasiojua kufundishwa, wasio na uzoefu kushauriwa. Tunapaswa kulia pamoja na wale wanaolia na kufurahi pamoja na wale wanaofurahi. Ikiambatana na nguvu ya ushawishi, nguvu ya maombi, nguvu ya upendo wa Mungu, kazi hii haitakuwa, haiwezi, kuwa bila matunda. - *The Ministry of Healing*, 143, 144. **{WM 96.2}**

Sura ya Kumi na Mbili -Ufanisi wa Uinjilisti wa Kutembelea

Mahali pa Uinjilisti wa Kutembelea katika Kumaliza Kazi ya Mungu Duniani. - Kazi kubwa ya ujumbe wa malaika wa tatu inaweza kutimizwaje? Ni lazima itimizwe kwa kiasi kikubwa kwa juhudi za kudumu, za mtu mmoja mmoja, kwa kuwatembelea watu majumbani mwao. - *Historical Sketches*, uk. 150. **{WM 97.1}**

Njia mojawapo yenye ufanisi mno ambayo kwayo nuru inaweza

kuwasilishwa ni kwa juhudi binafsi, za faragha. Katika duru ya jamii nyumbani, kando ya moto nyumbani kwa jirani yako, kando ya kitanda cha mgonjwa, kwa namna ya utulivu unaweza kusoma Maandiko na kusema neno juu ya Yesu na Ukweli. Hivyo unaweza kupanda mbegu ya thamani ambayo itachipuka na kuzaa matunda. - *Testimonies for the Church*, 6:428, 429. **{WM 97.2}**

Inalipwa Mara Elfu. - Amkeni, ndugu na dada. Msiziogope kazi njema. Msichoke katika kutenda mema, kwa kuwa mtavuna kwa wakati unaofaa ikiwa hamtazimia.... Himizeni ndani yenu kuupenda ukarimu, ukaribishaji wa wageni, upendo wa kuwasaidia wale wanaohitaji msaada. **{WM 97.3}**

Mnaweza kusema mmedanganywa, kutoa mali zenu kwa wale wasiostahili fadhila zenu, na kwa hiyo umekata tamaa katika kujaribu kuwasaidia wahitaji. Ninamleta Yesu mbele yenu... Nafsi moja iliyovutwa kutoka katika kushika kwa nguvu kwa Shetani; nafsi moja mliyoifadhili; nafsi moja iliyotiwa moyo! Hii itawalipa mara elfu moja kwa juhudi zenu zote. Kwenu Yesu atasema, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi." Je! Hatupaswi kufanya yote tuwezayo kwa furaha katika kuiga maisha ya Bwana wetu wa Mbinguni/Kiungu?—*The Review and Herald*, Aprili 20, 1886. **{WM 97.3}**

Ni Muhimu kwa Majaliwa Yetu ya Milele. - Pale mnapojihusisha na kazi hii mnakuwa pamoja na wenzi

wasioonekana kwa macho ya kibinadamu. Malaika wa mbinguni walikuwa kando ya Msamaria yule aliyemtunza mgeni aliyejeruhiwa. Malaika kutoka katika nyua za mbinguni husimama kando ya wote wanaofanya utumishi wa Mungu katika kuwahudumia wanadamu wenzao. Na mnakuwa na ushirikiano wa Kristo Yeye Mwenyewe. Yeye Ndiye Mponyaji, na mnapofanya kazi chini ya usimamizi Wake, mtaona matokeo makubwa. Juu ya uaminifu wenu katika kazi hii, si tu ustawi wa wengine, bali pia majaliwa yako mwenyewe ya milele hutegemea.- *Christ's Object Lessons*, 388. **{WM 98.1}**

Kristo Anaingia katika Makazi Pamoja Nao. — Bwana anatamani kwamba Ukweli uje karibu na watu, na

hii inaweza kutimizwa tu kwa kazi binafsi. Mengi yanajumuishwa katika amri, "Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa." Kuna kazi ya kufanywa katika mwelekeo huu ambayo bado haijafanyika. Hebu wafanyakazi wa Mungu wafundishe Ukweli katika familia, wakikaribiana na wale ambao kwao wanafanya kazi. Ikiwa kwa jinsi hiyo watashirikiana na Mungu, Yeye atawavika uwezo wa kiroho. Kristo atawaongoza katika kazi yao, akiingia katika nyumba za watu pamoja nao na kuwapa maneno ya kusema ambayo yatazama ndani kabisa ya mioyo ya wasikilizaji. Roho Mtakatifu atafungua mioyo na akili ili ipate kupokea miale inayotoka kwenye Chanzo cha nuru yote.

- *The Review and Herald*, Desemba 29, 1904. **{WM 98.2}**

Leta Matumaini kwa Watu. — Haiwezekani kwa mtu anayemwamini Kristo kuona kazi ambayo inahitajika kufanywa na bado asifanye chochote au afanye sifuri. Kila siku tunapaswa kupokea kutoka Mbinguni zeri ya uponyaji ya neema ya Mungu ili tupate kuitoa kwa wahitaji na wanaoteseka. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kupata habari juu ya shida za maskini katika maeneo ya karibu nao na kujitahidi kuwaletea msaada. Wale ambao wana maisha ya giza na yasiyokubalika ndio wale ambao tunapaswa kuwaambia wapate kuwa na matumaini kwa sababu Kristo ni Mwokozi wao. Je, hakuna wale

ambao wanaweza kwenda nyumba kwa nyumba, kutoka familia moja hadi familia nyingine, na kutoa tena maarifa yale sahili yaani (ABC) ya uzoefu wa Kweli wa Kikristo?—*The Review and Herald,* Aprili 11, 1912. **{WM 98.3}**

Uzoefu wa E. G. White katika Kutembelea. — Ninakumbuka wakati ule ambapo uweza wa Mungu wa kuongoa ulinijia utotoni mwangu nilitaka kila mtu apate baraka ambayo nilikuwa nayo, na sikuweza kupumzika hadi nilipowaambia juu yake. Nilianza kwa kuwatembelea vijana marafiki wangu na kwenda nyumbani kwao kuzungumza nao na kuwaambia kuhusu uzoefu wangu, jinsi Mwokozi alivyokuwa wa thamani kwangu, na jinsi nilivyotaka kumtumikia, na jinsi nilivyotaka wao pia wapate kumtumikia. Hivyo

nilizungumza jinsi Kristo alivyo wa thamani kubwa sana, na ningesema, "Je! unaweza kupiga magoti pamoja nami na kuomba?" Baadhi wangepiga magoti na wengine wangekaa kwenye viti vyao, lakini kabla hatujasalimu amri, kila mmoja angekuwa amepiga magoti na tungeomba pamoja kwa saa kadhaa, hadi yule wa mwisho angesema, "Ninaamini kwamba Yesu amesamehe dhambi zangu." Wakati mwingine jua lingeanza kuonekana mbinguni kabla sijaacha mapambano. Kuna uweza mkubwa katika Yesu. - *Manuscript* 10, 1888. **{WM 99.1}**

"Kazi za Kwanza" Zinaleta Matokeo. — Sababu ya wengi kushindwa kupata mafanikio ni kwa kuwa kwa jumla wao wanajiamini wenyewe kupita kiasi, na hawahisi haja

chanya ya kukaa ndani ya Kristo, wanapokwenda kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. Mpaka wamekuwa na nia ya Kristo na kufundisha Kweli kama ilivyo katika Yesu, hawatafanikiwa sana....

Angahewa ya kanisa ina ubaridi mno, ari yake ni ya jinsi ile, ambapo wanaume na wanawake hawawezi kuhimili au kuvumilia mfano wa uchaji wa asili wa mbinguni. Joto la upendo wao wa kwanza limeganda, na isipokuwa wamenyweshewa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kinara chao cha taa kitaondolewa kutoka mahali pake, isipokuwa wametubu na kufanya kazi zao za kwanza. Kazi za kwanza za kanisa zilionekana wakati waumini walipotafuta marafiki, jamaa, na watu waliozoeana nao, na kwa mioyo

iliyofurika upendo, walisimulia kisa cha kile Yesu alikuwa kwao na kile walichokuwa kwa Yesu. -*Testimonies to Ministers and Gospel Workers*, 167, 168. **{WM 99.3}**

Wewe ni Barua; Iwasilishe!

-Mtume Paulo anawaambia wanafunzi wa Yesu, “Mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo,” “inayojulikana na kusomwa na watu wote.” Ndani ya kila mmoja wa watoto Wake Yesu ametuma barua kwa ulimwengu. Ikiwa wewe ni mfuasi wa Kristo, anatuma ndani yako barua kwa familia, kijiji, mtaa, unakoishi. Yesu, anayeishi ndani yako, anatamani kuzungumza na mioyo ya wale ambao hawajafahamiana Naye. Huenda hawasomi Biblia au hawaisikii sauti ile inayozungumza nao katika kurasa zake;

hawauoni upendo wa Mungu kupitia kazi Zake. Lakini ikiwa wewe ni mwakilishi wa Kweli wa Yesu, inawezekana kwamba kwa kupitia kwako wataongozwa kuelewa kitu fulani kuhusu wema Wake, na kuongolewa wapate kumpenda na kumtumikia. - *Steps to Christ*, 119. **{WM 100.1}**

Maandiko/Machapisho Tunayoyaacha Nyumbani kwa Watu Yatazaa Matunda. - "Miguu yako imefungiwa utayari tupatao kwa injili ya amani," utakuwa tayari kutembea nyumba kwa nyumba ukibeba Ukweli kwa watu. Wakati mwingine utaona kuwa ni usumbufu sana kufanya kazi ya aina hii; lakini ikiwa utasonga mbele kwa imani, Bwana atakutangulia, na nuru Yake itaangaza kwenye njia yako. Unapoingia katika nyumba za

majirani zako kuuza au kugawa maandiko yetu, na kwa unyenyekevu kuwafundisha Ukweli, nuru ya mbinguni itaambatana nawe. - *The Review and Herald*, Novemba 11, 1902. **{WM 100.2}**

Punde Mungu atafanya mambo makubwa kwa ajili yetu ikiwa kwa unyenyekevu na kuamini tutaanguka miguuni pake.... Zaidi ya watu elfu moja hivi karibuni wataongolewa kwa siku moja, wengi wao watafuatilia usadikisho wao wa mara ya kwanza na kugundua kuwa ulitokana na usomaji wa machapisho yetu. - *The Review and Herald*, Novemba 10, 1885. **{WM 101.1}**

Njia Iliyo Bora ya Kuzifikia Nafsi. - Katika vivuli vilevile vya

nyumba za Mungu kuna umati wa wenye dhambi wasiomcha Mungu, wasio na ujuzi wa Ukweli, wasio na tumaini…. Katika kila mji, katika kila makazi ambapo Wakristo hukutana kumwabudu Mungu, kuna wanaume na wanawake na watoto watakaopaswa kukusanywa kuingia ndani ya zizi. Wengi hawasikii kamwe mahubiri juu ya Neno la Mungu. Ni nani atakayechukua juu yake mzigo kwa ajili ya nafsi? Ni nani atakayejifunza kutoka kwa Mwalimu Mkuu kwamba njia bora ya kuzifikia roho ni ile ya moja kwa moja, mtu binafsi kuwasihi, wale wanaokosea, wale ambao wamekufa katika makosa na dhambi, kumtazama Mkombozi wao aliyeinuliwa, aliyesulubiwa, na wapate kuishi? Wakristo, hebu mioyo yenu na ijae huruma na upendo kwa wale

wasioujua Ukweli. - *Manuscript* 81, 1900. **{WM 101.2}**

Hali Zilizorekebishwa kwa Ajili ya Vipaji Vyetu. - Ikiwa walimu wa Neno Lake wako tayari, Bwana atawaongoza katika kuwa na uhusiano wa karibu na watu. Atawaongoza katika nyumba za wale wanaohitaji na kuutamani Ukweli, akiwaleta katika hali zinazofaa kabisa kwa vipaji vyao. - *Letter* 95, 1896. **{WM 101.3}**

Vipaji Vyote Vinahitajika. - Bwana anayo nafasi kwa kila mtu katika mpango Wake mkuu. Vipaji ambavyo havihitajiki huwa havitolewi. Kwa kila mtu Mungu hutoa talanta, ambazo zinapaswa kutumiwa vizuri kulingana na uweza Wake mbalimbali. Ukidhani kuwa talanta ni ndogo, Mungu anayo

nafasi kwa ajili yake; na talanta ile moja, ikitumiwa, itafanya kazi ile ile ambayo Mungu alikusudia ifanye. Vipaji vya mkulima au kibarua mnyenyekevu anayeishi kwenye nyumba ndogo mashambani vinahitajika katika kazi ya nyumba kwa nyumba na vinaweza kufanikisha zaidi katika kazi hii kuliko karama adhimu za watu wenye akili zilizosheheni Na yeye yule mwenye kuitumia vizuri ile talanta yake moja kwa hakika atalipwa kama yule anayetumia vizuri talanta tano. Ni kwa sababu ya kufanya kazi kulingana na uwezo uliotolewa ndiyo Mungu huwapa thawabu watumishi Wake. - *Letter* 41, 1899. **{WM 101.4}**

Jinsi ya Kupata Muda wa Kuwatembelea Majirani. - Ikiwa vijana wa kiume na vijana wa kike

wangejiweka wakfu kwa Mungu, kama wangejizoeza kujikana nafsi katika maisha ya nyumbani, kuwasaidia mama zao waliochoka, na kulemewa na masumbufu, ni mabadiliko ya jinsi gani yangelitokea katika makanisa yetu. Mama angeweza kupata muda wa kuwatembelea majirani. Kama fursa ingetolewa, watoto wangeweza kutoa msaada kwa kufanya, wakati wakiwa bado wadogo kabisa, safari fupi fupi za rehema na upendo kwa ajili ya kuwabariki wengine. Kwa jinsi hiyo maelfu ya nyumba za maskini na wahitaji zingeweza kufikiwa. Vitabu vinavyohusiana na afya na kiasi vingeweza kuwekwa katika nyumba nyingi. Usambazaji wa vitabu hivi ni kazi muhimu, kwani vina maarifa ya thamani kuhusiana na matibabu ya ugonjwa-

maarifa ambayo yatakuwa baraka kubwa kwa wale ambao hawawezi kulipia kutembelewa na daktari (au kumwona tabibu ofisini mwake).—*Manuscript* 119, 1901.**{WM 102.1}**

“Usisubiri Kuambiwa Wajibu Wako.” - Usisubiri kuambiwa wajibu wako. Fumbua macho yako uwaone wale walio karibu nawe, fahamiana na wasiojiweza, wenye shida, na wahitaji. Msijifiche kwao, wala msitafute kuyafungia nje mahitaji yao. Ni nani anayetoa ushahidi uliotajwa katika Yakobo, ya kuwa na dini safi, isiyotiwa doa na ubinafsi au ufisadi? -Testimonies for the Church 2:29. **{WM 102.2}**

Vunja Laana: "Nenda Kazini, Ikiwa Unajisikia au La.” - Ndugu na dada zangu, je, mnatamani kuvunja

laana inayowashikilia? Je! mnaweza kuamka kutoka katika uzito huu wa kujongea polepole kama konokono jambo ambalo hunafanana na usingizi wa kifo? Nenda kazini, iwe unajisikia kufanya hivyo au la. Jihusishe kwa juhudi binafsi katika kuleta roho kwa Yesu na katika kupata maarifa ya Ukweli. Katika kazi kama hiyo utapata kichocheo na dawa ya kutia afya na nguvu; itaamsha na kuimarisha. Kwa matumizi nguvu zako za kiroho zitakuwa na nguvu zaidi, ili kwamba kwa mafanikio mazuri zaidi uweze kuufanyia kazi wokovu wako mwenyewe. Usingizi wa kifo uko juu ya wengi wanaomkiri Kristo. Fanya kila juhudi kuwaamsha. Onya, sihi, zuia kwa maneno. Omba kwamba upendo wa Mungu ulio mtamu sana upate kutia joto na kulainisha asili

yao iliyotiwa barafu. Ingawa wanaweza kukataa kusikiliza, kazi yako haitapotea. Katika jitihada za kuwabariki wengine roho zenu wenyewe zitabarikiwa. - *Testimonies for the Church* 5:387. **{WM 103.1}**

Kubeba Angahewa ya Mbinguni. - Kuwatembelea wagonjwa, kuwafariji maskini na wenye huzuni kwa ajili ya Kristo, kutawaletea watendakazi miale angavu ya Jua la Haki, na hata uso utaonesha amani inayokaa ndani ya roho. Nyuso za wanaume na wanawake wanaozungumza na Mungu, ambaye Kwake ulimwengu usioonekana ni halisi, zinaonesha amani ya Mungu. Wanabeba angahewa laini na kunjufu ya mbinguni, na wanaieneza kwa matendo ya fadhili na kazi za upendo. Mvuto wao ni wa namna ya kuongoa roho kwa Kristo.

Ikiwa wote wangeweza kuona na kuelewa, na kuwa watendaji wa Maneno ya Mungu, amani gani, furaha gani, afya ya mwili na amani ya roho, yangekuwa ni matokeo yake! Angahewa changamfu, yenye wema wa upendo, wema wa Kristo wenye huruma ndani ya roho haiwezi kukadirika. Thamani ya upendo iko juu ya dhahabu na fedha na vito vya thamani, na huwafanya mawakala wa kibinadamu kuwa kama Yeye ambaye aliishi kwa kutokujipendeza Mwenyewe. - *Letter* 43, 1895. **{WM 103.2}**

"**Mamia na Maelfu Walionekana Wakitembelea Familia.**" - Katika maono ya usiku, maonesho yalipita mbele yangu ya vuguvugu kubwa la matengenezo miongoni mwa watu wa Mungu. Wengi walikuwa wakimsifu Mungu. Wagonjwa waliponywa, na

miujiza mingine ilitendeka. Roho ya kuwaombea wengine ilionekana, kama vile ilivyodhihirishwa kabla ya siku kuu ya Pentekoste. Mamia na maelfu walionekana wakitembelea familia na kufungua mbele yao Neno la Mungu. Mioyo ilisadikishwa na nguvu ya Roho Mtakatifu, na roho ya uongofu wa kweli ilidhihirika. Kila upande milango ilifunguliwa wazi kwa ajili ya tangazo la Ukweli. Ulimwengu ulionekana kumulikwa na uwezo wa mbinguni. Baraka kubwa zilipokelewa na watu wa Mungu walio wakweli na wanyenyekevu. Nilisikia sauti za shukrani na sifa, na ilionekana kuwa kuna matengenezo kama yale tuliyoyashuhudia mnamo mwaka 1844.-*Testimonies for the Church* 9:126. **{WM 104.1}**

Sura ya Kumi na Tatu - Kulipanga Kanisa kwa Ajili ya Huduma ya Ustawi

Kusudi la Mungu katika Mfumo wa Kanisa. - Kanisa la Kristo duniani lilipangwa kwa madhumuni ya umisionari, na Bwana anatamani kuona kanisa lote likibuni njia na namna ambazo kwazo watu wa juu na wa chini, matajiri na maskini, wanaweza kusikia ujumbe wa ile Kweli. — *Testimonies for the Church* 6:29.**{WM 105.1}**

Kuungana katika Zoezi la Kutoa Msaada. - Popote ambapo Ukweli umetangazwa na watu wameamshwa na kuongolewa, waumini mara moja wanapaswa kuungana katika kufanya

matendo ya wema (upendo na ukarimu). Popote ambapo Ukweli wa Biblia umewasilishwa, kazi ya uchaji Mungu kwa vitendo inapaswa kuanzishwa. Popote ambapo kanisa linaanzishwa, kazi ya umisionari inapaswa kufanywa kwa ajili ya wasiojiweza na wanaoteseka. —*Testimonies for the Church* 6:84, 85. **{WM 105.2}**

Wito kwa Watu Wanaoweza Kuongoza. - Isipokuwa kuna wale ambao watabuni njia za kugeuka au zenye kuleta tofauti katika kufikiria muda, nguvu, na akili za washiriki wa kanisa, kutakuwa na kazi kubwa iliyoachwa ambayo inapaswa kufanywa. Kazi ya ovyo ovyo haitaridhisha. Tunawataka watu kanisani ambao wana uwezo wa kuendelea katika mwelekeo wa kupanga na kutoa kazi ya vitendo

kwa vijana wa kiume na wa kike katika mwelekeo wa kupunguza shida za ubinadamu, na kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho za wanaume, wanawake, vijana, na watoto. - *Letter* 12, 1892.**{WM 105.3}**

Kama Shule ya Mafunzo. — Kila kanisa linapaswa kuwa shule ya mafunzo kwa wafanyakazi Wakristo. Washiriki wake wanapaswa kufundishwa jinsi ya kutoa masomo ya Biblia, jinsi ya kuongoza na kufundisha madarasa ya shule ya Sabato, jinsi bora ya kuwasaidia maskini na kuwatunza wagonjwa, jinsi ya kufanya kazi kwa wale ambao hawajaongoka. Kuwe na shule za afya, shule za mapishi, na madarasa katika nyanja mbali mbali za kazi ya msaada wa Kikristo. Haipaswi kuwapo na kufundisha peke yake, bali

kazi halisi chini ya walimu wenye uzoefu. Hebu walimu waongoze njia katika kufanya kazi miongoni mwa watu, na wengine, wakijiunga nao, watajifunza kutokana na mfano wao. ***Mfano mmoja*** ni wa thamani zaidi kuliko maagizo mengi. - *The Ministry of Healing*, 149.**{WM 105.4}**

Kuandaa Vijana Wetu kwa Ajili ya Utumishi wa Vitendo -Practical. - Mwalimu Mkuu anashirikiana na juhudi zote zinazofanywa ili kupunguza mateso kwa wanadamu. Wafundishe wanafunzi kufanyia mazoezi yale masomo waliyoyapokea kwa vitendo halisi. Wanaposhuhudia shida za mwanadamu na umaskini mkubwa wa wale wanaojaribu kuwasaidia, wataamshwa na huruma. Mioyo yao italainishwa na kutiishwa na kanuni za

kina, takatifu zilizodhihirishwa katika Neno la Mungu. Tabibu mkuu anashirikiana na kila juhudi inayofanywa kwa niaba ya wanadamu wanaoteseka, kutoa afya kwa mwili na nuru na urejesho kwa roho.... Ni lazima sasa tuone kitu gani kifanyike ili kuwaelimisha wanafunzi katika kazi ya umisionari kwa vitendo. - *Manuscript* 70, 1898. **{WM 106.1}**

Fundisha Kazi ya Umisionari wa Vitendo. - Katika matukio kama yale ya mikutano yetu ya makambi ya kila mwaka hatupaswi kamwe kupoteza fursa tulizopewa za kuwafundisha waumini jinsi ya kufanya kazi ya umisionari kwa vitendo mahali pale wanapoishi. Katika matukio mengi ingekuwa vyema kutenga watu fulani kubeba mzigo wa mielekeo mbalimbali

ya kazi ya elimu katika mikutano hii. Hebu wengine wawasaidie watu kujifunza jinsi ya kutoa masomo ya Biblia na kufanya mikutano ya nyumba kwa nyumba. Hebu wengine wabebe mzigo wa kuwafundisha watu jinsi ya kufuata kanuni za afya na kiasi na jinsi ya kutoa matibabu au tiba rahisi kwa wagonjwa. Bado wengine wanaweza kufanya kazi kwa manufaa ya kazi yetu ya majarida na vitabu. - *Testimonies for the Church* 9:82, 83. **{WM 106.2}**

Tengeneza Vikosi vya Wafanyakazi. – Utengenezaji wa vikosi vidogo vidogo kama msingi wa juhudi za Kikristo umewasilishwa kwangu na Yule ambaye hawezi kukosea. Ikiwa kuna idadi kubwa ya watu kanisani, hebu washiriki wapangwe katika vikosi vidogo vidogo,

ili wapate kufanya kazi si tu kwa ajili ya washiriki wa kanisa, bali pia kwa ajili ya wasioamini. Ikiwa katika sehemu moja wapo wawili au watatu tu ambao wanaujua Ukweli, hebu na watengeze kikundi cha wafanyakazi. Hebu wadumishe kifungo cha muungano wao kisivunjike, wakisonga mbele pamoja kwa upendo na umoja, wakitiana moyo kusonga mbele, kila mmoja akipata ujasiri na nguvu kutokana na msaada wa wengine. —*Testimonies for the Church* 7:21, 22.**{WM 107.1}**

Vikosi Vilivyopangwa Vizuri katika Kila Kanisa. — Hebu kuwepo katika kila kanisa vikosi vya wafanyakazi vilivyopangwa vizuri kufanya kazi katika maeneo ya karibu na kanisa hilo. Wekeni nafsi nyuma, na mruhusuni Kristo atangulie kama uzima na uwezo

wenu. Hebu kazi hii iingiwe bila kukawia, na Ukweli utakuwa kama chachu katika dunia. Wakati majeshi hayo yatakapowekwa kufanya kazi katika makanisa yetu yote, kutakuwa na uwezo wa kurekebisha, kuongoa, kuchangamsha katika makanisa, kwa sababu washiriki wanafanya kazi ile hasa ambayo Mungu amewapa waifanye. Hebu makanisa yetu yote yawe hai, yenye bidii, yaliyojazwa shauku na Roho na uweza wa Mungu. Ni matumizi ya akili ya fedha, vipaji, nguvu, mlizopewa na Mungu, zilizowekwa wakfu kwa huduma Yake, ndiyo yatakayoiathiri jamii ambazo mnaweza kuzifanyia kazi. Inawezekana kwamba mtalazimika kufanya mwanzo mdogo sana katika maeneo fulani; lakini msikate tamaa; kazi itaongezeka na

kuwa kubwa, nanyi mtakuwa mnafanya kazi ya mwinjilisti. Angalia namna ya Kristo ya kufanya kazi, na jitahidi kufanya kazi kama Yeye alivyofanya.- *The Review and Herald*, Septemba 29, 1891. **{WM 107.2}**

Fanya Kazi kwa Kutumia Jina Fulani. - Katika kazi yote ya Mungu kwa ajili ya mwanadamu anapanga kwamba mwanadamu atashirikiana na Yeye. Kwa kusudi hili Bwana anatoa wito kwa kanisa kuwa na uchaji Mungu wa juu, hisi ya haki zaidi juu ya wajibu, utambuzi wa wazi zaidi wa wajibu wao kwa Muumbaji wao. Anawaita wapate kuwa wafanya kazi walio safi, waliotakaswa. Na kazi ya Kikristo ya msaada ni njia mojawapo ya kulisababisha hili, kwa kuwa Roho Mtakatifu anawasiliana na wote

wanaoifanya kazi ya Mungu.... Napenda kusema: Endeleeni kufanya kazi kwa busara na uwezo. Waamsheni washiriki wenu kufanya kazi kwa kutumia jina fulani ambalo chini yake wanaweza kupangwa ili kushirikiana katika utendaji wa upatanifu. Wafanye vijana wa kiume na wa kike makanisani kufanya kazi. - *Testimonies for the Church* 6:266, 267. **{WM 108.1}**

Vijana Kujipanga na Kujifunza kwa Ajili ya Kazi ya Mwisho-Kufunga kazi. - Kuna mielekeo mingi ambako vijana wanaweza kupata fursa kwa ajili ya jitihada yenye msaada. Wanapojipanga katika vikosi kwa ajili ya huduma ya Kikristo, ushirikiano wao utathibitika kuwa msaada na kitu cha kutia moyo.... **{WM 108.2}**

Katika kazi hii ya mwisho ya injili kuna uwanja mkubwa sana unaopaswa kutwaliwa; na, zaidi kuliko ilivyowahi kuwa hapo awali, kazi hii inabidi kuandikisha wasaidizi kutoka kwa watu wa kawaida. Vijana na wale walio na umri mkubwa wataitwa kutoka mashambani, kutoka katika karakana, na kutumwa na Bwana ili wapate kutoa ujumbe Wake. Wengi wa hawa wanaweza kuwa walipata fursa ndogo tu elimu, lakini Kristo anaona ndani yao sifa ambazo zitawawezesha kutimiza kusudi lake. Ikiwa wataweka mioyo yao katika kazi na kuendelea kuwa wanafunzi, atawaandaa ili wafae kufanya kazi kwa ajili Yake. **{WM 108.3}**

Kwa maandalizi kama hayo wanayoweza kuyapata, maelfu kwa

maelfu ya vijana na wale wenye miaka mingi wanapaswa kuwa wanajitoa kwa ajili ya kazi hiyo. Tayari mioyo mingi inaitikia wito wa Mfanyakazi Mkuu, na idadi yao itaongezeka. **{WM 109.1}**

Wote wanaojihusisha katika huduma ni mkono wa Mungu wa msaada. Hakuna mwelekeo mwingine wa kazi ambapo inawezekana kwa kijana kupata faida kubwa zaidi. Wao ni wafanyakazi wenza na malaika; naam, wao ni mawakala wa kibinadamu ambao kupitia kwao malaika hutimiza utume wao. Malaika husema kupitia sauti za hao na kufanya kazi kwa mikono ya hao. Na wafanyakazi wanadamu, wanaposhirikiana na mawakala wa mbinguni, wana faida ya elimu na uzoefu wa hao [malaika]. Kama njia ya elimu ni "kozi gani ya chuo kikuu"

inaweza kuwa sawa na hii? Hebu fikiria tukiwa na jeshi kama hilo la wafanyakazi ambao ni vijana wetu waliofunzwa inavyotakiwa, Je, wanaweza kutimiza mengi kiasi gani, na hivyo kufanya mambo kwenda kwa kasi ili kupeleka ulimwenguni kote ujumbe wa Mwokozi aliyesulubiwa, aliyefufuka, na anayekuja upesi sana! —*The Youth's Instructor*, March 3, 1908.**{WM 109.2}**

Kazi Kubwa Itakayopasa Kufanywa na Watu Ambao kwa Sasa Hawatumiki. - Si kusudi la Mungu kwamba wachungaji waachwe kufanya sehemu kubwa ya kazi ya kupanda mbegu za Ukweli. Watu ambao hawajaitwa kwenye utumishi wa injili wanapaswa kuhimizwa na kutiwa moyo kufanya kazi ya Bwana kulingana na vipaji vyao mbalimbali. Mamia ya

wanaume na wanawake ambao kwa sasa hawatumiki, wangeweza kufanya huduma inayokubalika. Kwa kupeleka Ukweli ndani ya nyumba za marafiki na majirani zao, wangeweza kufanya kazi kubwa kwa Bwana. Mungu hana upendeleo. Atawatumia Wakristo wanyenyekevu, waliojitoa ambao wana upendo wa ile Kweli mioyoni mwao. Hebu watu kama hawa wajihusishe katika kumtumikia kwa kufanya kazi ya nyumba kwa nyumba. Wakiketi kando ya moto -wanapoota moto wakati wa baridi, watu kama hao ikiwa watakuwa wanyenyekevu, wenye busara, na wacha Mungu - wataweza kufanya zaidi katika kukidhi mahitaji halisi ya familia mbalimbali kuliko ambavyo angelifanya mchungaji. - *The Review and Herald*, Agosti 26, 1902. **{WM 109.3}**

Msaada Bora Ambao Wachungaji Wanaweza Kuutoa. - Msaada bora ambao wachungaji wanaweza kuutoa kwa washiriki wa makanisa yetu si kuhubiri bali kupanga kazi kwa ajili yao. Mpe kila mmoja kitu fulani cha kufanya kwa ajili ya wengine.... Ikiwa watawekwa kufanya kazi, waliokata tamaa punde watasahau kukata tamaa kwao; wanyonge watakuwa na nguvu; wasiojua au wajinga watakuwa wenye akili; na wote watakuwa tayari kuwasilisha Kweli kama ilivyo katika Yesu. — *Testimonies for the Church* 9:82. **{WM 110.1}**

Kila mtu anayeongezwa katika safu hii kwa uongofu anapaswa kupewa mahali pake pa kazi. Kila mtu anapaswa kuwa tayari kuwamo au kufanya

chochote katika vita hivi. — *Testimonies for the Church* 7:30. **{WM 110.2}**

Hebu Wote na Washirikiane. - Kumekuwapo na mahubiri mengi kwa makanisa yetu kiasi kwamba karibu wameacha kupendezwa na huduma ya injili. Wakati umefika ambapo mpangilio huu wa mambo unapaswa kubadilishwa. Hebu mchungaji na awaite washiriki mmoja mmoja wa kanisa ili wamsaidie kwa kufanya kazi ya nyumba kwa nyumba katika kupeleka Ukweli katika maeneo ya mbali. Hebu wote washirikiane na malaika wa mbinguni katika kuuwasilisha Ukweli kwa wengine. - *The Review and Herald*, Juni 11, 1895. **{WM 110.3}**

Wote kwa Umoja Kuimaliza Kazi. - Wale ambao wana usimamizi wa

kiroho wa kanisa wanapaswa kubuni njia na namna ambazo kwazo fursa inaweza kutolewa kwa kila mshiriki wa kanisa kutenda sehemu fulani katika kazi ya Mungu. Mara nyingi sana huko nyuma hili halijafanyika. Mipango haijawekwa wazi na kutekelezwa kikamilifu ambapo vipaji vya wote vinaweza kutumiwa katika utumishi hai. Kuna wachache tu ambao wanatambua ni kiasi gani kimepotezwa kwa sababu ya hili. **{WM 110.4}**

Viongozi katika kazi ya Mungu, kama majemadari wenye busara, wanapaswa kuweka mipango ya kusonga mbele katika njia yote. Katika mipango yao wanapaswa kufanya uchunguzi maalum kwa kazi ambayo inaweza kufanywa na walei kwa marafiki na majirani zao. Kazi ya Mungu katika dunia hii haiwezi

kukamilika mpaka wanaume na wanawake walei waliomo katika ushirika wa makanisa yetu wameungana katika kazi na kuunganisha juhudi zao na zile za wachungaji na maafisa wa kanisa. -*Testimonies for the Church* 9:116, 117. **{WM 111.1}**

Kristo Anaweza Kuwakilishwa katika Kazi Zote za Halali. - Wote wanapaswa kufundishwa jinsi ya kufanya kazi. Hasa wale ambao ni wapya kwenye imani wanapaswa kuelimishwa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Ikiwa jukumu hili limepuuzwa, kazi ya mchungaji haijakamilika. **{WM 111.2}**

Lakini Mungu hataki watu Wake **waning'inize** uzito wao juu ya wachungaji. Kama wakili wa neema ya Mungu, kila mshiriki wa kanisa

anapaswa kuhisi wajibu binafsi wa kuwa na maisha na mizizi ndani yake yeye mwenyewe. Wote ambao wamewekwa wakfu katika maisha ya Kristo wanaagizwa kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa wenzao. Yeye ampendaye Mungu kuliko vyote na jirani yake kama yeye mwenyewe hawezi kutulia kwa kuridhika na kutokufanya chochote. **{WM 111.3}**

Laiti waumini bayana katika Ukweli wangeliuishi Ukweli huo, leo wote wangekuwa wamisionari. Wengine wangekuwa wanafanya kazi katika visiwa vya bahari; wengine, katika nchi nyingine za ulimwengu. Wengine wangekuwa wanamtumikia Kristo kama wamisionari wa nyumbani. Si wote wanaitwa kwenda nchi za ng'ambo. Wengine wanaweza kufanikiwa katika

mielekeo ya biashara, na katika kazi hii wanaweza kumwakilisha Kristo. Wanaweza kuonesha kwa ulimwengu kwamba biashara inaweza kuendeshwa kwa kanuni za haki, kwa uaminifu na uadilifu mkubwa katika Ukweli. Kunaweza kuwa na wanasheria Wakristo, madaktari Wakristo, wafanyabiashara Wakristo. Kristo anaweza kuwakilishwa katika kazi zote zilizo halali. — *Manuscript* 19, 1900. **{WM 111.4}**

Mfano wa Kanisa Lenye Uaminifu. — Asubuhi ya siku ya Sabato, Novemba 10, 1900, tuliingia katika kanisa la San Francisco, na kulikuta limejaa kabisa. Niliposimama mbele ya watu nilifikiri juu ya ndoto na maagizo ambayo nilikuwa nimepewa miaka mingi iliyopita, na nilitiwa moyo

sana. Nikiwatazama watu waliokusanyika, nilijisikia kwamba ningeweza hasa kusema, "Bwana amelitimiza Neno Lake." **{WM 112.1}**

Katika miaka michache iliyopita "mzinga wa nyuki" [Hapa ninarejelea ufunuo ule wa 1876 ambapo shughuli za makanisa ambayo kwa kiasi yalikuwa ni mapya wakati ule katika San Francisco na Oakland ziliwakilishwa kama mizinga miwili ya nyuki.] katika San Francisco umekuwa ni mmoja wenye shughuli kwelikweli. Mielekeo mingi ya juhudi za Kikristo imesogezwa mbele na ndugu na dada zetu walioko huko. Hizi ni pamoja na kutembelea wagonjwa na wasiojiweza, kutafuta nyumba kwa ajili ya yatima na kufanya kazi kwa wasio na ajira, kuwaangalia wagonjwa, na kufundisha Ukweli nyumba kwa

nyumba, kusambaza maandiko mbalimbali, na kuendesha masomo juu ya maisha yenye kuleta afya na utunzaji wa wagonjwa. Shule kwa watoto imeendeshwa katika chumba cha chini cha nyumba ya mkutano katika Mtaa wa Laguna. Ambapo kwa muda palikuwa ni nyumba ya wafanyakazi na utume wa matibabu uliendelezwa. Kwenye Mtaa wa Market, karibu na ukumbi wa jiji, kulikuwa na vyumba vya matibabu, vilivyoendeshwa kama tawi la Sanitariamu ya St. Helena. Katika eneo hilo hilo kulikuwa na duka la vyakula vyenye kutia afya. Karibu na katikati ya jiji, si mbali na jengo letu la kazi, lilifanywa kuwa mgahawa wa chakula cha mbogamboga yaani bila mapishi ya nyama (vegeterian food), ambao ulifunguliwa kwa siku sita katika wiki na

kufungwa kabisa siku ya Sabato. Katika mwambao kazi ya utume wa meli iliendelezwa (ndani ya meli kunakuwa na mkakati wa utume* kama Luzeiro Brazil). Kwa nyakati mbalimbali wachungaji wetu walifanya mikutano katika kumbi kubwa jijini. Kwa jinsi hiyo ujumbe wa onyo ulitolewa na wengi. - *The Review and Herald*, Julai 5, 1906. **{WM 112.2}**

Kwa Kusudi Hili Kanisa Limepangwa. - Mtu fulani ni lazima atimize agizo la Kristo; mtu fulani ni lazima aendeleze kazi ambayo [Kristo] alianza kuifanya duniani; na kanisa limepewa upendeleo huu. Kwa kusudi hili [kanisa] limepangwa. Kwa nini, basi, washiriki wa kanisa hawajaukubali wajibu huo? Kuna wale ambao wameona kutokujali huku kukubwa; wameona

mahitaji ya wengi ambao wako katika mateso na uhitaji; wametambua katika roho hizi maskini wale ambao Kristo alitoa maisha Yake kwa ajili yao, na mioyo yao imechochewa na huruma, kila nguvu imeamshwa kuchukua hatua.... Wameingia katika kazi ya kuwaandaa wale ambao watashirikiana nao katika kuleta Ukweli wa injili mbele ya wengi ambao sasa wako katika uovu na udhalimu, ili waweze kukombolewa kutoka katika maisha ya ubadhirifu na dhambi. **{WM 112.3}**

Wale ambao wamekuwa wakijihusisha na kazi hii ya msaada wa Kikristo wamekuwa wakifanya kile ambacho Bwana anatamani angekifanya, Naye amezikubali kazi zao. Kile kilichofanyika katika mwelekeo huu ni kazi ambayo kila Mwadventista wa

Sabato anapaswa kukubaliana nayo kwa moyo wote na kuiunga mkono, na kuishikilia kwa bidii. - *Testimonies for the Church* 6:295, 296. **{WM 113.1}**

Sehemu ya V Kumsaidia Binadamu Anayeteseka

Wazo la Thamani

Ni maisha ya shughuli nyingi kiasi gani Kristo aliishi! Siku kwa siku Angeweza kuonekana akiingia katika makao duni ya wahitaji na wenye huzuni, akitamka tumaini kwa walioanguka na amani kwa

waliofadhaika. Maskini na walioteseka walipokea sehemu kubwa zaidi ya usikivu Wake. Watoto walimpenda. Walivutwa Kwake kwa sababu ya huruma Yake ya haraka. Kwa Maneno Yake sahili, ya upendo Alitatua matatizo mengi yaliyojitokeza miongoni mwao. Mara nyingi aliwachukua kwenye goti lake na kuzungumza nao kwa njia ambayo ilivutia mioyo yao. **{WM 116.1}**

Kazi Yake ilikuwa ni ya umisionari wa tiba ambayo anawaomba watu Wake waifanye leo. Mnyenyekevu, mwenye fadhili, mwema, mwenye huruma, Alizunguka huku na kule akitenda mema, akiwalisha wenye njaa, akiwainua walioinama, akiwafariji wenye huzuni. Wala hakuna yeyote aliyekuja Kwake kwa ajili ya msaada aliyeondoka bila kufarijiwa. Hakuna uzi

wowote wa ubinafsi uliosokotwa katika mfano ambao amewaachia watoto Wake kuufuata. Aliishi maisha ambayo angetaka wale wote wanaomwamini waishi. Ilikuwa ni chakula na kinywaji Chake kufanya mapenzi ya Baba Yake. Kwa wote waliokuja Kwake kwa ajili ya msaada alileta imani na tumaini na uzima. Popote alipokwenda alipeleka baraka. **{WM 116.2}**

Kwetu sisi ujumbe wa Kristo ni, "Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate." - *Manuscript* 115, 1902. **{WM 116.3}**

Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu, na kupoza wagonjwa.Luka 9:2

Sura ya Kumi na Nne - Katika Nyayo za Mwalimu

Mfano wa Kristo wa Huduma ya Tiba. - Kwa miaka mitatu wanafunzi walikuwa nao mbele yao Mfano wa ajabu wa Kristo. Siku kwa siku walitembea na kuzungumza Naye, wakisikia Maneno Yake ya furaha kwa wale waliochoka na kulemewa na mizigo na kuona udhihirisho wa uweza Wake kwa niaba ya wagonjwa na wanaoteseka. Wakati ulipofika wa Yeye kuwaacha, Aliwapa uwezo wa kufanya kazi kama Yeye alivyofanya. Aliwapa neema Yake, akisema, "Mmepata bure, toeni bure." Walipaswa kusonga mbele ulimwenguni kutawanya nuru ya injili Yake ya upendo

na uponyaji. Kazi aliyokuwa akiifanya walipaswa kuifanya. **{WM 117.1}**

Na hii ndiyo kazi tunayopaswa pia kuifanya ulimwenguni. Kwa utu wema na huruma tunapaswa kuwahudumia wale wanaohitaji msaada, tukitafuta kwa bidii bila ubinafsi kupunguza shida ya wanadamu wanaoteseka. Tunapojihusisha na kazi hii tutabarikiwa sana. Mvuto Wake hauzuiliki. Kwa hiyo roho zinaongolewa kwa Mkombozi. Utekelezaji wa kivitendo wa agizo la Mwokozi unadhihirisha uwezo wa injili. Kazi hii inahitaji bidii ya kuchosha (kazi ya mitulinga haswa), lakini inalipa; kwani kwa hiyo roho zinazoangamia zinaokolewa. Kupitia uwezo Wake wanaume na wanawake wenye vipaji wanapaswa kuletwa kwenye msalaba wa Kristo. **{WM 117.2}**

Mwanadamu ana mwili na pia roho vyote viwili vya kuokolewa. Vyote viwili vinapaswa kurejeshwa katika afya kwa njia za Mungu zilizo sahili lakini zenye ufanisi, ambazo zina mvuto kwa wanaume na wanawake wenye akili. Kupitia imani katika Ukweli roho zinaamshwa kuona hitaji la maandalizi kwa ajili ya majukumu ya maisha. Kadiri afya ya mwili inavyorejeshwa nguvu za akili zinatolewa ili zipate kufahamu kweli kuu za injili. - *Letter* 152, 1901. **{WM 117.3}**

Kwanza Kidhi Mahitaji ya Maisha. – Watu wanaoteseka na mafukara wa matabaka yote ni majirani zetu, na pale tunapopata taarifa ya mahitaji yao ni wajibu wetu kuyatuliza au kuleta afueni kwa kadiri iwezekanavyo. Kanuni imetolewa katika

mfano huu [wa Msamaria mwema] ambayo itakuwa vizuri kwa wafuasi wa Kristo kuichukua. Kwanza kidhi mahitaji ya maisha ya wahitaji na kuyatuliza mahitaji yao ya kimwili na mateso, na ndipo utakuwa umepata njia ya wazi ya kuufikia moyo, ambapo utaweza kupanda mbegu njema za maadili na dini. - *Testimonies for the Church* 4:226, 227. **{WM 118.1}**

Tuna Ulimwengu wa Kuokoa. - Kumbuka kwamba kuna ulimwengu wa kuokoa. Tunapaswa kutenda sehemu yetu, tukisimama karibu na kando ya Kristo kama wafanyakazi pamoja Naye. Yeye Ndiye kichwa; sisi ni mkono Wake wa msaada. Anakusudia kwamba sisi, kwa kufanya kazi ya umisionari wa tiba, tutaitengua/tutaiondoa mizigo mizito na kuwaacha walioonewa huru. Hebu sisi

tusifumbe macho yetu kwa shida zinazotuzunguka au kuziba masikio yetu kwa vilio vya dhiki ambavyo vinaendelea kupaa. Kristo ni mmisionari mkuu zaidi ambaye ulimwengu umewahi kumjua. Alikuja kuwainua na kuwachangamsha walio na huzuni na wenye shida, na katika kazi hii tunapaswa kushirikiana Naye. — *Manuscript* 31, 1901. **{WM 118.2}**

Zipate au zifuatilie Nyayo za Kristo katika Vibanda Vibovu vya Umaskini. - Wengi wanahisi kwamba itakuwa faida na fursa kubwa kwao kutembelea sehemu za matukio ya maisha ya Kristo duniani, kutembea mahali ambapo Yeye alikanyaga, kulitazama ziwa ambalo kando yake Yeye Alipenda kufundisha, na vilima na mabonde ambayo macho Yake mara

nyingi yalitua. Lakini hatuhitaji kwenda Nazareti, Kapernaumu, au Bethania ili tupate kutembea katika nyayo za Yesu. Sisi tutaziona na kuzigundua nyayo Zake kando ya kitanda cha mgonjwa, katika vibanda vibovu vya umaskini, katika vichochoro vya miji mikubwa vilivyojaa watu, na kila mahali ambapo pana mioyo ya wanadamu wanaohitaji faraja. Kwa kufanya kama Yesu alivyofanya alipokuwapo duniani, sisi tutakuwa tunatembea katika nyayo Zake Mwenyewe. —*The Desire of Ages*, 640. **{WM 118.3}**

Injili ya Kufunguliwa Kutoka Katika Mateso. - Kazi ya umisionari wa tiba huleta kwa wanadamu injili ya kufunguliwa kutoka katika mateso. Ni kazi tangulizi ya injili (inafungua njia, ni daraja la kufikia watu). Ni injili

inayohubiriwa kwa vitendo, injili inayotendwa, huruma ya Kristo iliyodhihirishwa. Kuhusu kazi hii kuna hitaji kubwa, na ulimwengu uko tayari kuipokea. Mungu na amekubali kwamba umuhimu wa kazi ya umisionari wa tiba utaeleweka na kwamba mashamba mapya yataweza kuingiwa mara moja. — *Manuscript* 55, 1901. **{WM 119.1}**

Anza katika Ujirani Wako Mwenyewe. - Mbele ya mwanamatengenezo wa kweli, kazi ya umisionari wa tiba itafungua milango mingi. Hakuna mtu anayepaswa kusubiri hadi ameitwa kwenda katika shamba fulani katika eneo la mbali kabla ya kuanza kuwasaidia wengine. Popote ulipo, unaweza kuanza mara moja. Fursa zipo karibu na kila mtu. Chukua kazi ambayo kwayo

unawajibika, kazi ambayo inapaswa kufanywa nyumbani kwako na katika ujirani wako. Usisubiri wati wengine wakusihi sana kuchukua hatua. Katika hofu ya Mungu songa mbele bila kuchelewa, ukizingatia wajibu wako binafsi Kwake Yeye aliyetoa uhai wake kwa ajili yako. Tenda kana kwamba ulimsikia Kristo akikuita wewe binafsi kufanya bidii katika utumishi Wake. Usiangalie kuona ni nani mwingine aliye tayari. Ikiwa umejiweka wakfu kweli kweli, Mungu, kupitia uwakala wako, atawaleta katika Ukweli wengine ambao Anaweza kuwatumia kama njia ya kupitisha nuru kwenda kwa wengi wanaopapasa papasa gizani.**{WM 119.2}**

Wote wanaweza kufanya kitu fulani. Katika kujaribu kutoa udhuru,

wengine wanasema: "Majukumu yangu ya nyumbani, watoto wangu, wanahitaji muda wangu na fedha zangu." Wazazi, watoto wenu wanapaswa kuwa mkono wako wa msaada, wakiongeza nguvu na uwezo wako wa kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Watoto ni washiriki wachanga wa familia ya Bwana. Wao

wanapaswa kuongozwa kujiweka wakfu kwa Mungu, ambaye wao ni Wake kwa uumbaji na kwa ukombozi. Wanapaswa kufundishwa kwamba nguvu zao zote za kimwili, kiakili, na kiroho ni Zake. Wanapaswa kufundishwa kusaidia katika njia mbalimbali za huduma isiyo na ubinafsi. —*Testimonies for the Church* 7:62, 63.**{WM 120.1}**

Kila Mtu Anatakiwa Kufanya Kila Liwezekanalo kwa Kadri

awezavyo. - Bwana anataka sana kila mfanyakazi afanye bidii. Wale ambao hawajapata mafunzo maalum katika moja ya taasisi zetu za matibabu wanaweza kufikiri kwamba wanaweza kufanya kidogo sana; lakini, wafanyakazi wenzangu wapendwa, kumbuka kwamba katika mfano ule wa talanta Kristo hakuwakilisha watumishi wote kama wanaopokea idadi sawa. Mtumishi mmoja alipewa talanta tano; mwingine talanta mbili; na mwingine talanta moja. Ikiwa una talanta moja tu, itumie kwa busara, ukiiongeza kwa kuiweka kwa watoao riba. Baadhi hawawezi kufanya mengi kama wengine, lakini kila mtu anapaswa kufanya yote awezayo kulirudisha nyuma wimbi la magonjwa na dhiki ambalo linaenea na kuufagia ulimwenguni mwetu. Jitokeze

kumsaidia Bwana, kumsaidia Bwana dhidi ya mamlaka za giza zenye nguvu (Waamuzi 5:26). Mungu anataka sana kila mmoja wa watoto Wake apate kuwa na akili na maarifa, ili kwamba kwa uwazi dhahiri na uweza utukufu Wake upate kudhihirishwa katika ulimwengu wetu. - *The Review and Herald*, Juni 9, 1904. **{WM 120.2}**

Wafanyakazi Pamoja na Mungu. - Upande mkubwa wa kazi ya Mungu unadhihirishwa na maneno "umisionari wa tiba." Kuwa mmisionari wa tiba kunamaanisha kuwa mtendakazi pamoja na Mungu. Kazi ya umisionari wa tiba, kazi ambayo inapaswa kuwa msaada mkubwa na nguvu kwa ajili ya kusudi, inapaswa kuendelezwa kwa uangalifu na hekima yote. Katika kazi hii kusiwepo uzi hata mmoja utakaoingizwa

ambao utaharibu mpangilio mzuri ambao Mungu anakusudia kwamba upate kutengenezwa. - *Manuscript* 139, 1902. **{WM 120.3}**

Kutangaza Ukweli kwa Wagonjwa na Wenye Afya. - Huduma ya injili ni mfumo au mpangilio wa utangazaji wa Ukweli kwa wagonjwa na kwa wenye afya. Inaunganisha kazi ya umisionari wa tiba na huduma ya Neno. Kwa nguvu hizi zilizounganishwa fursa zinatolewa za kuwasilisha nuru na kufikisha injili kwa matabaka yote na madaraja yote ya jamii. Mungu anawataka wachungaji na washiriki wa kanisa wapate kuwa na shauku ya dhati, iliyoazimiwa na iliyo hai katika kazi ya umisionari wa tiba. **{WM 121.1}**

Kuwafikia watu pale walipo, vyovyote iwavyo cheo au hali yao, hali yao yoyote, na kuwasaidia kwa kila njia inayowezekana - hii ni huduma ya injili. Wale ambao ni wagonjwa katika mwili karibu siku zote ni wagonjwa katika akili, na pale roho inapougua mwili pia unaathirika. - *Testimonies for the Church* 6:300, 301. **{WM 121.2}**

Sura ya hamsini na nane ya Isaya ina Ukweli wa sasa kwa watu wa Mungu. Hapa tunaona jinsi ambavyo kazi ya umisionari wa tiba na huduma ya injili vinapaswa kufungwa pamoja pale ujumbe unapotolewa kwa ulimwengu. Juu ya wale wanaoitunza Sabato ya Bwana limewekwa jukumu la kufanya kazi ya rehema na ukarimu (upendo kwa vitendo). Kazi ya umisionari wa tiba inapaswa kufungamanishwa pamoja na

ujumbe (wa malaika watatu na umishonari wa tiba), na kutiwa muhuri kwa muhuri wa Mungu. — *Manuscript* 22, 1901. **{WM 121.3}**

Kaskazini, Kusini, Mashariki, na Magharibi. - Kwa nini haijaeleweka kutoka katika Neno la Mungu kwamba kazi inayofanywa katika mielekeo ya umisionari wa tiba ni utimilizaji wa Andiko, "Toka upesi, uende katika njia kuu na vichochoro vya mji, ukawalete hapa maskini, na vilema, na vipofu, na viwete. Mtumwa akasema, Bwana, hayo uliyoagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa ingaliko nafasi. Bwana akamwambia mtumwa, Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba Yangu ipate kujaa."**{WM 122.1}**

Hii ni kazi ambayo makanisa katika kila eneo, kaskazini na kusini na mashariki na magharibi, yanapaswa kufanya. Makanisa yamepewa fursa ya kuiitikia kazi hii. Kwa nini hawajaifanya basi? Ni lazima mtu fulani alitimize agizo hili la utume. **{WM 122.2}**

Kazi ambayo ingepaswa kufanywa imeachwa. Wale ambao wamekuwa wakijishughulisha na kazi ya umisionari wa tiba wamekuwa wakifanya kazi ile hasa ambayo Bwana angeifanya..... **{WM 122.2}**

Oh, ni kiasi gani, ni kiasi gani kikubwa kimebaki kufanywa, na bado ni wangapi ambao wangeweza kutumia kwa usahihi vipaji vyao walivyopewa na Mungu hawafanyi karibu chochote kando ya kujitunza na kujipendeza

wenyewe. Lakini mkono wa Bwana bado umenyoshwa, na ikiwa watafanya kazi leo katika shamba Lake la mizabibu, Yeye ataukubali utumishi wao. - *Manuscript* 18, 1897. **{WM 122.3}**

Weka Mizani Sahihi. - Kazi ya umisionari wa tiba inapaswa kuendelezwa na kanisa katika juhudi zilizopangwa vizuri. Inapaswa kuwa kwa kusudi la Mungu kile ambacho mkono wa kulia ulivyo kwa mwili. Lakini kazi ya umisionari wa tiba haipaswi kuchukua umuhimu unaokiuka mipaka. Hii Inapaswa kufanywa bila kupuuza mielekeo mingine ya kazi. - *Letter* 139, 1898. **{WM 122.4}**

Kazi ya Mkono wa Kulia. - Mkono wa kulia hutumika kwa ajili ya kufungua milango ambayo mwili

unaweza kupata nafasi ya kuingia. Hii ndiyo sehemu ambayo kazi ya umisionari wa tiba inapaswa kutenda. Kwa kiasi kikubwa inapaswa kuandaa njia kwa ajili ya mapokezi ya ile Kweli wa wakati huu. Mwili usio na mikono hauna maana na hauna msaada. Katika kutoa heshima kwa mwili, heshima lazima pia itolewe kwa mikono ya kuusaidia, ambayo ni nguvu muhimu sana kiasi kwamba bila hiyo mwili hauwezi kufanya chochote. Kwa hiyo, mwili unaotenda bila kuujali mkono wa kulia, ukikataa msaada wake, hauwezi kutimiza chochote. - *Manuscript* 55, 1901. **{WM 122.5}**

Sehemu ya Kitu Kizima Kikubwa. - Kazi ya umisionari wa tiba ilipaswa kuwapo kila wakati katika kazi ya matengenezo. Lakini kamwe haifai

kuwa njia ya kuwatenga wafanyakazi walioko katika huduma kutoka katika kazi yao. Kristo aliunganisha matawi haya mawili katika kazi Zake zote. Kazi ya umisionari wa tiba ni sehemu ya kitu kizima kikubwa, kama mkono ulivyo sehemu ya mwili. Lakini mkono haupaswi kukiambia kichwa, Sikuhitaji wewe. Mwili unakihitaji kichwa kwa vyovyote vile, na mikono, ili uweze kufanya kazi ya kiutendaji, iliyo hai, na ya hima. Mwili haupaswi kuwa mkono. Kila kiungo kina kazi yake ambayo kiliteuliwa kipate kuifanya. — *Manuscript* 105, 1899. **{WM 123.1}**

Maombi ya Mmisionari wa Tiba. - Wachungaji na walimu wanapaswa kufanya kazi kwa akili katika mielekeo yao, wakiwafundisha washiriki wa kanisa jinsi ya kufanya kazi katika

mielekeo ya umisionari wa tiba. Pale wale wafuasi bayana wa Kristo wanapokuwa na Mwokozi anayekaa ndani, wataonekana wakitenda kama Kristo alivyotenda. Hawatakuwa na nafasi ya kuota kutu kwa kutulia bila kufanya kazi. Watakuwa na mambo mengi ya kutenda. Na kazi ambayo wanaifanya chini ya mwavuli wa kanisa itakuwa ni njia yao kubwa ya kuwasilisha nuru. **{WM 123.2}**

Mtu ambaye anafanya kazi kulingana na mpango wa Mungu ataomba, "Hebu na ijulikane leo katika kazi yangu kwa ajili ya wanadamu wanaoteseka kwamba kuna Mungu katika Israeli, na kwamba mimi ni mtumishi Wako. Hebu na ionekane kwamba ninafanya kazi, si kulingana na msukumo wangu na

hekima yangu, bali kulingana na Neno Lako.” **{WM 123.3}**

Wakati mwanadamu anapojiweka katika mtazamo huu, na kugundua kuwa anatendea kazi mpango wa Mungu, na kwamba Mungu anatenda mpango Wake kupitia kwake, hapo anakuwa na nguvu ya Bwana, ambayo haiwezi kushindwa. Nguvu zote za kupinga hazina thamani zaidi ya makapi ya sakafu ya kupuria. —*Manuscript* 115, 1899. **{WM 124.1}**

Italeta Uhai kwa Makanisa. - Kwa ndugu zangu wanaohudumu ningesema, Endeleeni na kazi hii kwa busara na uwezo. Wawekeni kufanya kazi vijana wa kiume na wa kike katika makanisa yetu. Unganisha kazi ya umisionari wa tiba na kutangaza ujumbe

wa malaika wa tatu. Fanya juhudi za kila siku, zilizopangwa kuyainua makanisa kutoka katika kiwango mfu ambacho wameanguka, na kubakia kwa miaka mingi. Peleka wafanyakazi kanisani ambao wataweka kanuni za matengenezo ya afya katika muunganiko wake na ujumbe wa malaika wa tatu mbele ya kila familia na mtu binafsi. Wahimize wote kushiriki katika kazi kwa wanadamu wenzao, na uone kama pumzi ya uhai haitarudi haraka kwa makanisa haya. - *Letter* 54, 1898. **{WM 124.2}**

Sura ya Kumi na Tano - Huduma ya Tiba katika Makazi ya Watu

Mlango wa Kuingia katika Makazi ya Watu. - Kazi ya umisionari wa tiba ni kazi ya utangulizi kwa injili (piooner), mlango ambao kupitia huo Ukweli kwa ajili ya wakati huu unapata mlango wa kuingia katika makazi mengi ya watu. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamisionari wa dhati/kweli wa tiba, kwani wanapaswa kujifunza kuyahudumia mahitaji ya roho na ya mwili. Ukarimu halisi kabisa unapaswa kuoneshwa na wafanyakazi wetu kwani, kwa maarifa na uzoefu unaopatikana kwa kazi ya vitendo, wanatoka kwenda kutoa tiba rahisi kwa wagonjwa. Pale wanapokwenda nyumba kwa nyumba watapata njia ya kufikia mioyo mingi. Wengi watafikiwa ambao vinginevyo kamwe hawangesikia ujumbe wa injili. -

The Review and Herald, Desemba 17, 1914. **{WM 125.1}**

Kristo Ataongoza katika Huduma Hii. - Kama wewe utajisogeza karibu na Kristo, huku ukivaa nira Yake, kila siku utajifunza kutoka Kwake jinsi ya kubeba ujumbe wa amani na faraja kwa wale walio na huzuni na waliokata tamaa, wenye huzuni na waliovunjika moyo. Unaweza kuwaelekeza wale waliokata tamaa kwenye Neno la Mungu na kuwapeleka wagonjwa kwa Bwana kwa maombi. Unapoomba, zungumza na Kristo kama unavyoweza kuzungumza na rafiki anayeaminika, anayependwa sana. Dumisha heshima tamu, huru, ya kufurahisha kama mtoto wa Mungu. Hii itatambuliwa. -*Testimonies for the Church* 6:323, 324. **{WM 125.2}**

Huduma ya Madaktari na Wauguzi Wanaofanana na Kristo.

– Laiti kama wote wanaoteseka wangeweza kuhudumiwa na matabibu na wauguzi walio kama Kristo, ambao wangeweza kuwasaidia kuweka miili yao iliyochoka, iliyoteswa na maumivu katika utunzaji wa Mponyaji Mkuu, kwa imani wakimtazama kwa ajili ya uponyaji na urejeshwaji. **{WM 125.3}**

Kila Mkristo wa dhati/kweli anamwinamia Yesu kama daktari wa kweli wa roho. Pale anaposimama kando ya kitanda cha mwenye shida kutakuwa na wengi siyo tu walioongolewa bali walioponywa. Ikiwa kupitia katika huduma ya busara mgonjwa anaongozwa kutoa roho yake kwa Kristo na kuleta mawazo yake katika utii kwa mapenzi ya Mungu, ushindi mkubwa

unapatikana. - *The Review and Herald*, Mei 9, 1912. **{WM 126.1}**

Muuguzi Mmisionari Nyumbani. - Bwana anawataka wanaume na wanawake wenye busara watendao kazi katika wadhifa wa wauguzi kuwafariji na kuwasaidia wagonjwa na wanaoteseka.... Kuna mielekeo mingi ya kazi inayopaswa kuendelezwa na muuguzi mmisionari. Kuna fursa kwa wauguzi waliofunzwa vizuri kwenda miongoni mwa familia na kujitahidi kuamsha shauku kuhusu Ukweli. Katika karibu kila jamii kuna idadi kubwa ambao hawahudhurii ibada yoyote ya kidini. Ikiwa watafikiwa na injili, ni lazima wapelekewe majumbani mwao. Mara nyingi msaada wa kuwapunguzia mahitaji yao ya kimwili ndio njia pekee ambayo kwayo

wanaweza kuendewa/kufikiwa. Pale wauguzi wamisionari wanapowajali wagonjwa na kupunguza shida za maskini, watapata fursa nyingi za kuomba pamoja nao, kuwasomea Neno la Mungu, kusema juu ya Mwokozi. Wanaweza kuomba pamoja nao na kuwaombea wale wasiojiweza ambao hawana nguvu ya utashi wa kudhibiti hamu ya chakula au kile ambacho shauku kali imeiharibu (uraibu). Wanaweza kuleta mwali wa matumaini katika maisha ya walioshindwa na kukatishwa tamaa. Upendo wao usio na ubinafsi, unaodhihirishwa katika matendo ya wema usio na ubinafsi au upendeleo, utafanya iwe rahisi kwa hawa wanaoteseka kuuamini upendo wa Kristo. - *kitabu kile kile*. **{WM 126.2}**

Wafundishe Watu Jinsi ya Kutunza Afya Njema. -Kazi ya umisionari wa tiba inatoa fursa nyingi za huduma. Kukosa kiasi katika kula na kutojua sheria za maumbile husababisha magonjwa mengi ambayo yapo na humpokonya Mungu utukufu unaomstahili.... Wafundishe watu kwamba ni bora kujua jinsi ya kutunza afya kuliko kujua jinsi ya kutibu ugonjwa (kuzuia ni rahisi kuliko kuponya). Tunapaswa kuwa waelimishaji wenye hekima, tukiwaonya wote dhidi ya kutimiza tamaa bila kujizuia-ulafi. Tunapoona umaskini, ulemavu, mpasuko, na magonjwa ambayo yamekuja ulimwenguni kama matokeo ya ujinga, Je, tunawezaje kuacha kufanya sehemu yetu kuwaelimisha watu wasiojua na

kuwafariji wanaoteseka? — *The Review and Herald*, Juni 6, 1912. **{WM 126.3}**

Kanuni Sahili Ambazo Wote Wanapaswa Kuzimudu. - Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamisionari wa kweli wa tiba. Wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya roho na ya mwili. Wanapaswa kujua jinsi ya kutoa matibabu sahili ambayo hufanya mengi sana katika kupunguza maumivu na kuondoa ugonjwa (tiba ya maji kama haidrotherapia, mazoezi nk). Wanapaswa kuwa wazoefu wa kanuni za matengenezo ya afya, ili waweze kuwaonesha wengine jinsi ambavyo, kwa mazoea sahihi ya kula, kunywa, na kuvaa, magonjwa yanaweza kuzuiwa na afya kupatikana tena. Maonesho ya thamani ya kanuni za matengenezo ya afya yatasaidia sana kuondoa chuki

dhidi ya kazi yetu ya kiinjili. Tabibu Mkuu, mwanzilishi wa kazi ya umisionari wa tiba, atambariki kila mmoja ambaye atasonga mbele kwa unyenyekevu na uaminifu, akimtumaini Yeye, na akitafuta kuwapa watu Ukweli wa wakati huu. - *The Review and Herald*, Mei 5, 1904.**{WM 127.1}**

Matengenezo Endelevu ni ya Lazima. -Matengenezo, matengenezo endelevu, ni lazima yadumishwe mbele ya watu, na kwa mfano wetu ni lazima tuyatie nguvu na kuyakazia mafundisho yetu. Dini ya Kweli na sheria za afya huenda pamoja. Haiwezekani kufanyia kazi wokovu wa wanaume na wanawake bila ya kuwasilisha kwao hitaji la kujitenga/kuikimbia furaha ya dhambi, hitaji la kuacha kuiendekeza dhambi, ambayo hiyo huharibu afya,

hudhoofisha roho, na kuishusha katika hali ya chini na duni na kuzuia ile Kweli ya Mungu kuvutia akili. Wanaume na wanawake ni lazima wafundishwe kuchunguza kwa makini kila tabia na mazoea, na mara moja kutupilia mbali vitu vile ambavyo husababisha hali mbaya kwenye afya ya mwili, na hivyo kutupa kivuli cha giza akilini. - *The Review and Herald*, Novemba 12, 1901. **{WM 127.2}**

Fundisha Kanuni za Upishi Wenye Kuleta Afya Njema. - Kwa sababu njia za kuelekea rohoni zimefungwa na chuki zenye ukatili, wengi hawajui kanuni za kuishi kwa namna ya kuleta afya. Huduma nzuri inaweza kufanywa kwa kuwafundisha watu jinsi ya kuandaa chakula chenye kuleta afya. Mwelekeo huu wa kazi ni

muhimu kama wowote ambao unaweza kufuatwa. Shule nyingi zaidi za upishi zinapaswa kuanzishwa, na wengine wanapaswa kufanya kazi kutoka nyumba hadi nyumba, wakitoa maelekezo katika sanaa ya kupika vyakula vizuri. Wengi, wengi wataokolewa kutokana na udhoofu wa kimwili, kiakili, na kimaadili kupitia katika mvuto wa matengenezo ya afya. Kanuni hizi zitapendwa na wale wanaotafuta nuru, na watu kama hao watasonga mbele kutoka hapo na kupokea Ukweli kamili kwa wakati huu. **{WM 128.1}**

Mungu anataka watu Wake wapate kupokea ili watoe. Kama mashahidi wasio na upendeleo, na wasio na ubinafsi, wanapaswa kuwapa wengine kile ambacho Bwana amewapa. Na pale unapoingia katika kazi hii, na kwa njia

yoyote ile iliyo katika uwezo wako ukijitahidi kufikia mioyo, hakikisha kuwa unafanya kazi kwa namna ambayo itaondoa upendeleo badala ya kuutengeneza. Fanya maisha ya Kristo kuwa somo lako la daima, na ufanye kazi kama alivyofanya, ukifuata mfano Wake. - *The Review and Herald*, Juni 6, 1912. **{WM 128.2}**

Tunahitaji elimu ya kweli katika sanaa ya mapishi.... Tengeneza madarasa, ambapo utaweza kuwafundisha watu jinsi ya kutengeneza ugali/mkate mzuri na jinsi ya kuweka pamoja viambato ili kufanya mchanganyiko wa chakula chenye kuleta afya kutokana na nafaka na mbogamboga. -*Manuscript* 150, 1905. **{WM 128.3}**

Fuata Njia Inayopendekeza Matengenezo. - Mengi ya maoni yanayoshikiliwa na Waadventista wa Sabato yanatofautiana sana na yale yanayoshikiliwa na ulimwengu kwa ujumla. Wale wanaoutetea Ukweli usiopendwa wanapaswa, na usio mashuhuri kuliko mwingine wote, kujitahidi kuwa waaminifu katika maisha yao wenyewe. Hawapaswi kujaribu kuona jinsi wanavyoweza kuwa tofauti na wengine, bali jinsi wanavyoweza kuja karibu na wale ambao wanataka kuwavutia, ili waweze kuwasaidia kufika katika nafasi ambazo wao wenyewe wanazithamini sana. Mwelekeo kama huo utafanya zile Kweli ambazo wanazishikilia zikubaliwe. **{WM 128.4}**

Wale ambao wanatetea matengenezo katika chakula wanapaswa, kwa chakula wanachoweka katika meza yao wenyewe, kuwasilisha faida za usafi kwa nuru iliyo bora. Wanapaswa kuonesha mfano wa kanuni zake ili kuzipendekeza kwa maamuzi ya akili zilizo nyofu.... **{WM 129.1}**

Pale ambapo wale wanaoyatetea matengenezo yenye kuleta afya wanalipeleka suala hilo mbali mno kupita kiasi au kwa kupitiliza, watu hawapaswi kulaumiwa ikiwa watachukizwa. Mara nyingi imani yetu ya kidini kwa jinsi hiyo hufikishwa katika sifa mbaya, na mara nyingi wale wanaoshuhudia maonesho kama hayo ya kutofautiana hawawezi kamwe baadaye kufikiria kuwa kuna kitu chochote kizuri katika matengenezo

hayo. Watu hawa wenye msimamo mkali ambao unapitiliza hufanya madhara makubwa zaidi katika miezi michache kuliko wanavyoweza kutangua katika maisha yao yote. Wanajishughulisha na kazi ambayo Shetani anapenda kuona inaendelea.... Mawazo finyu na kukazia sana mambo madogomadogo kumekuwa jeraha kubwa kwa kusudi la elimusiha (afya, usafi na kuzuia maradhi-Hygeine). - *Christian Temperance and Bible Hygiene,* 55-57. **{WM 129.2}**

Maoni ya Mtu Binafsi Hayapaswi Kuhimizwa. -Wale ambao wana uelewa mdogo tu wa kanuni za matengenezo mara nyingi ndio walio wagumu zaidi, si tu katika kutekeleza maoni yao wenyewe, lakini pia katika kuyahimiza juu ya familia zao

na majirani zao. Matokeo ya matengenezo yao yaliyokosewa, kama inavyoonekana katika afya yao mbaya wao wenyewe, na juhudi zao za kulazimisha maoni yao kwa wengine huwapa wengi mawazo ya uwongo juu ya matengenezo ya chakula na kuwaongoza katika kuyakataa kabisa. **{WM 129.3}**

Wale ambao wanaelewa sheria za afya na ambao wanaongozwa na kanuni wataepuka kupindukia/kupitiliza katika uendekezaji na uzuiaji vyote viwili. Chakula chao huchaguliwa, si tu kwa ajili ya kukidhi au kuendekeza hamu ya chakula, lakini kwa ajili ya ujenzi wa mwili. Wanajitahidi kuhifadhi kila nguvu katika hali bora zaidi kwa ajili ya huduma ya hali ya juu kabisa kwa Mungu na kwa mwanadamu. Tamaa

inakuwa chini ya udhibiti wa akili na dhamiri, nao huzawadiwa kwa afya ya mwili na ya akili. Ingawa hawahimizi maoni yao kwa jinsi ya kuchukiza kwa wengine, mfano wao ni ushuhuda unaounga mkono kanuni sahihi. Watu hawa wana mvuto mpana kwa ajili ya mema. **{WM 129.4}**

Kuna maarifa halisi ya kawaida katika matengenezo kuhusu elimu-lishe. Mada hii inapaswa kusomwa kwa upana na kwa kina, na hakuna mtu anapaswa kuwakosoa wengine kwa sababu utendaji wao, katika mambo yote, haulingani na wake yeye mwenyewe. Haiwezekani kutunga sheria isiyobadilika kwa ajili ya kurekebisha tabia ya kila mtu, na hakuna mtu anayepaswa kujiona kuwa ndiye kigezo cha wote. Wote hawawezi kula vitu

vilivyo sawa. Vyakula vinavyopendeza na vyenye kuleta afya kwa mtu mmoja vinaweza kuwa ni vya kuchukiza, na hata kuwa chenye madhara kwa mwingine. Wengine hawawezi kutumia maziwa, wakati wengine husitawi kwa kuyatumia. Watu wengine hawawezi kumeng 'enya njegere na maharage; wengine wanayaona kuwa hivyo ndivyo vyakula vya kutia afya. Kwa wengine mchanganyiko wa nafaka isiyosagwa kuwa unga au kuvunjwa vipande vidogo ni chakula kizuri kwao, wakati wengine hawawezi kukitumia. (mfano watu wengine hushindwa kula makande, ila wanawaza kula ugali na maharage) - *The Ministry of Healing,* 318-320. **{WM 130.1}**

Nuru kwa Ajili ya Wokovu wa Ulimwengu. - Wale wanaotenda kama

walimu wanapaswa kuwa na akili kuhusu magonjwa na sababu zake, wakielewa kwamba kila hatua ya wakala wa kibinadamu inapaswa kuwa katika upatanifu kamili na sheria za maisha. Nuru ambayo Mungu ameitoa juu ya matengenezo ya afya ni kwa ajili ya wokovu wetu na wokovu wa ulimwengu. Wanaume na wanawake wanapaswa kujulishwa juu ya makazi ya binadamu yaani miili yetu, makazi haya yaliyoandaliwa na Muumbaji wetu kama makao Yake, na ambayo kwayo Anataka sana tupate kuwa mawakili waaminifu. “Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu.” —*The*

Review and Herald, November 12, 1901. **{WM 130.2}**

Huamsha Imani. - Wengi hawana imani kwa Mungu na wamepoteza imani kwa mwanadamu, lakini wanathamini matendo ya huruma na msaada. Wanapomwona mtu ambaye havutiwi na sifa au fidia za kidunia akija nyumbani kwao, akiwahudumia wagonjwa, akiwalisha wenye njaa, akiwavisha walio uchi, akiwafariji wenye huzuni, na kwa upole akiwaelekeza wote kwa Yeye ambaye kwa ajili ya upendo na huruma Yake mfanyakazi wa kibinadamu ni mjumbe tu - wanapoliona hili mioyo yao inaguswa. Shukrani huchipuka, imani inawaka/inachochewa. Wanaona kwamba Mungu anawajali, na Neno Lake linapofunguliwa wanakuwa tayari

kulisikiliza. - *The Review and Herald*, Mei 9, 1912.**{WM 131.1}**

Wengi Wanaokolewa Kutoka katika Udhilifu. - Nimeoneshwa kuwa kazi ya umisionari wa tiba itawatambua, kutoka katika vina hasa vya udhilifu, watu ambao hapo awali walikuwa na akili nzuri, sifa nyingi, ambao wataokolewa, kwa kazi nzuri, kutoka kwa hali yao ya anguko. Ni Ukweli kama ulivyo katika Yesu ambao unapaswa kuletwa mbele ya akili za wanadamu baada ya kuwa wametunzwa kwa huruma na mahitaji yao ya kimwili kutimizwa. Roho Mtakatifu anafanya kazi na kushirikiana na wakala wa kibinadamu ambao wanafanya kazi kwa roho kama hizo, na baadhi watafurahia msingi ulio juu ya mwamba kwa ajili ya imani yao ya kidini. Hakupaswi kuwa na

mawasilisho ya kushangaza ya Mafundisho ya imani ajabu kwa watu hawa ambao Mungu anawapenda na huwahurumia; bali wanaposaidiwa kimwili na wafanyakazi wa umishonari wa tiba, Roho Mtakatifu hushirikiana na mhudumu wa nguvu za kibinadamu katika kuamsha nguvu za kimaadili. Nguvu za akili zinaamshwa zipate kushughulika, na roho hizi maskini, wengi wao, wataokolewa kuingia katika ufalme wa Mungu. **{WM 131.2}**

Hakuna kitu kinachoweza, au kitakachoweza, kutoa sifa kwa uzuri kwa kazi ya kuwasilisha Ukweli ili kuwasaidia watu pale walipo kama kazi ya Msamaria. Kazi inayofanywa vizuri kuwaokoa wenye dhambi maskini ambao wamepitwa na makanisa, itakuwa ndio njia ndogo ya kuingilia

ambayo kwayo Ukweli utapata nafasi ya kuweka mguu na kusimama. Utaratibu tofauti wa mambo unahitajika kuanzishwa kati yetu kama kanisa, na tabaka hili la kazi likifanywa, kutaundwa angahewa tofauti kabisa kuzunguka roho za wafanyakazi; kwa kuwa Roho Mtakatifu anawasiliana na wale wote wanaofanya kazi ya Mungu, na wale ambao Roho Mtakatifu anafanya kazi ndani yao watakuwa nguvu kwa Mungu katika kuinua, kuimarisha, na kuokoa roho ambazo ziko karibu na kuangamia. — *Special Testimonies,* series A, no. 11, uk. 32.**{WM 132.1}**

Ari na Uvumilivu Vinahitajika. - Kama Ningeweza kuwaamsha watu wetu kuwa na bidii ya Kikristo, kama ningewaongoza kujihusisha katika kazi ya umishonari wa tiba kwa ari takatifu

na uvumilivu wa Kiungu/Bwana, si katika maeneo machache, bali kila mahali, kuweka juhudi binafsi kwa ajili ya wale walio nje ya zizi, ningekuwa na shukrani iliyoje! Hii ni kazi halisi ya umishonari. Katika maeneo mengine inaambatana na mafanikio kidogo, inavyoonekana; lakini tena, Bwana hufungua njia, na mafanikio makubwa huambatana na juhudi hiyo. Maneno yananenwa ambayo ni kama misumari iliyofungwa/iliyogongelewa mahali pa uhakika. Malaika kutoka mbinguni hushirikiana na wakala wa kibinadamu, na wenye dhambi huongolewa kwa Mwokozi. - *Letter* 43, 1903. **{WM 131.2}**

Wanaume na Wanawake Watakatifu na Wacha Mungu Wanaitwa. - Watu watakatifu na

wacha Mungu, wanaume na wanawake wote, sasa wanatakiwa kwenda kama wamishonari wa tiba. Hebu na wakuze nguvu zao za kimwili na kiakili na uchaji wao kufikia upeo wa juu kabisa. Kila juhudi inapaswa kufanyika katika kuwatuma wafanyakazi wenye akili. Neema ile ile iliyotoka kwa Yesu Kristo kwenda kwa Paulo na Apolo, ambayo iliwafanya kuwa maarufu kwa ubora wao wa kiroho, inaweza kupokelewa sasa, nayo italeta katika tabaka la wafanyakazi wamishonari wengi waliojitoa. - *Special Testimonies Relating to Medical Missionary Work,* uk. 8. **{WM 131.2}**

Usisubiri. – Wafanyakazi - wamishonari wa tiba wainjilisti - wanahitajika sasa. Huwezi kuthubutu kutumia miaka mingi katika maandalizi.

Punde milango iliyo wazi kwa sasa kwa ajili ya Ukweli itafungwa milele. Beba ujumbe sasa. Usisubiri, na kumruhusu adui kuchukua milki ya maeneo ambayo kwa sasa yako wazi mbele yenu. Hebu vikundi vidogo viende kufanya kazi ambayo kwa ajili ya hiyo Kristo aliwateua wanafunzi Wake. Hebu na wafanye kazi kama wainjilisti, wakitawanya machapisho yetu, na kuzungumza kuhusu Ukweli kwa wale wanaokutana nao. Hebu na wawaombee wagonjwa, wakihudumia mahitaji yao, si kwa vidonge vya dawa za famasia, bali kwa tiba za asili, na kuwafundisha jinsi ya kupata afya tena na kuepuka magonjwa. —*Testimonies for the Church* 9:172.**{WM 133.1}**

[**Maoni:** Kwa mashauri ya kina zaidi kuhusu huduma ya tiba na uwasilishaji

wa ujumbe wetu wa afya angalia vitabu *Ministry of Healing*, *Medical Ministry*, *Counsels on Diet and Foods*, na *Counsels on Health*.—Wakusanyaji.] **{WM 133.2}**

Sura ya Kumi na Sita - Kujiandaa kwa Ajili ya Hatari na Majanga ya Siku za Mwisho

Hali Hizi za Siku za Mwisho Zinatushinikiza Kujiandaa. - Tunaishi katika wakati wa mwisho. Ishara zinazokamilika haraka za nyakati zinatangaza kwamba kuja kwa Kristo kumekaribia. Siku tunazoishi ni makini na muhimu. Roho wa Mungu pole pole lakini kwa hakika anaondolewa duniani.

Mapigo na hukumu tayari zinawaangukia wanaodharau neema ya Mungu. Majanga ya nchi kavu na baharini, hali isiyo na utulivu ya jamii, hofu za vita, ni ya kutisha. Zinatabiri matukio yanayokaribia yaliyo makubwa mno. **{WM 134.1}**

Mawakala wa uovu wanaunganisha nguvu zao na kujizatiti. Wanajiimarisha kwa ajili ya hatari kubwa ya mwisho. Mabadiliko makubwa punde yatatokea katika ulimwengu wetu, na mabadiliko ya hatua za mwisho yatakuwa ni ya haraka haraka. **{WM 134.2}**

Hali ya mambo ulimwenguni inaonesha kwamba nyakati za shida zimetukaribia hasa. Magazeti ya kila siku yamejaa dalili za upeo wa hatari mbaya katika siku chache za usoni.

Ujambazi wa waziwazi ni sehemu ya matukio ya mara kwa mara. Migomo ni jambo la kawaida. Wizi na mauaji hutendwa kila upande. Watu waliopagawa na mapepo wanaondoa maisha ya wanaume, wanawake, na watoto wadogo. Watu wamelewa kwa uovu, na kila aina ya uovu imetapakaa. - *Testimonies for the Church* 9:11. **{WM 134.3}**

Jambo Fulani Lenye Uwezo wa Kuamua Karibu Kutukia. - Sasa ni wakati uliojawa na shauku kubwa kwa wote walio hai. Watawala na viongozi wa siasa, watu ambao wako katika nafasi zenye dhamana na mamlaka, wanaume na wanawake wenye akili wa matabaka yote, wana umakini wao juu ya matukio yanayotukia kutuzunguka, yanayotokea juu yetu. Wanaangalia uhusiano

mgumu, wenye wahaka uliopo miongoni mwa mataifa. Wanaona nguvu ambayo inatawala kila kitu cha asili duniani, nao hutambua kuwa jambo fulani kubwa lenye uwezo wa kuamua linakaribia kutukia - kwamba ulimwengu uko ukingoni mwa hatari kubwa sana. **{WM 134.4}**

Malaika sasa wanazuia upepo wa vita, ili usiweze kuvuma mpaka ulimwengu umeonywa kuhusu hukumu yake inayokuja; lakini dhoruba inajikusanya, tayari kupasuka juu ya dunia; na wakati Mungu atakapowaamuru malaika Wake kuuachia huru upepo, kutakuwapo na mandhari ya vita ambayo hakuna kalamu inaweza kuchora taswira yake. — *Education*,179, 180.**{WM 135.1}**

Muda umekaribia ambapo

kutakuwapo na huzuni ulimwenguni ambayo hakuna zeri ya mwanadamu inaweza kuponya. Roho wa Mungu akiondolewa. Maafa baharini na katika nchi kavu hufuatana moja baada ya nyingine kwa mfuatano wa haraka haraka. Ni mara nyingi kiasi gani tunasikia kuhusu matetemeko ya ardhi na vimbunga, kuhusu uharibifu wa moto na mafuriko, na upotevu mkubwa wa maisha na mali! Inavyoonekana misiba hii ni milipuko yenye kugeuka geuka ya nguvu za asili ambazo hazina mpangilio, za ghafla, ambazo hazijarekebishwa na zilizo nje kabisa ya udhibiti wa mwanadamu; lakini katika hizo zote, kusudi la Mungu linaweza kusomwa. Hizo ni miongoni mwa mawakala ambao kwazo Yeye hutafuta kuwaamsha wanaume na wanawake wapate

kutambua hali yao ya hatari. — *Prophets and Kings*, 277.**{WM 135.2}**

Miji Mikubwa Itafutiliwa Mbali. - Kazi ambayo ilipaswa kwa muda mrefu kuwa katika utendaji hai wa kuongoa roho kwa ajili ya Kristo haijafanywa. Wakazi wa miji isiyomcha Mungu ambayo karibuni sana itapatilizwa kwa misiba wamepuuzwa kikatili. Muda unakaribia ambapo miji mikubwa itafutiliwa mbali, na wote wanapaswa kuonywa juu ya hukumu hizi zinazokuja. Lakini ni nani anayetoa kwa kusudi la kufanikisha kazi hii huduma kamili ambayo Mungu anaitaka? ... **{WM 135.3}**

Kwa wakati wa sasa hakuna sehemu moja katika elfu inayotendwa katika kuifanyia kazi miji mikubwa ambayo inapaswa kufanywa, na hiyo ingefanywa

kama wanaume na wanawake wangetekeleza wajibu wao wote. -Manuscript 53, 1910. **{WM 136.1}**

Laiti watu wa Mungu wangekuwa na hisia ya uharibifu wa maelfu ya miji, ambayo kwa sasa karibu imejitoa kuipenda ibada ya sanamu! ” — *The Review and Herald*, Septemba 10, 1903. **{WM 136.2}**

Maafa Yanayokaribia - Si muda mrefu uliopita tukio la kuvutia sana lilipita mbele yangu. Niliona mpira mkubwa wa moto ukianguka kati ya majumba makubwa mazuri kadhaa, na kusababisha uharibifu wao wa papo hapo. Nilimsikia mtu akisema, "Tulijua kwamba hukumu za Mungu zilikuwa zinakuja juu ya dunia, lakini hatukujua kwamba zingekuja mapema kiasi hicho."

Wengine wakasema kaw kujibu: Je! Mlijua? Kwa nini basi hamkutuambia? Sisi hatukujua.” Kila upande nilisikia maneno kama hayo yakisemwa.... **{WM 136.3}**

Hivi punde taabu za kusikitisha zitatokea miongoni mwa mataifa - taabu ambazo hazitakoma hadi Yesu atakapokuja. Kama ambavyo haijawahi kutokea hapo awali, tunatakiwa kusonga mbele kwa pamoja, tukimtumikia Yeye ambaye ameandaa kiti Chake cha enzi mbinguni na ambaye ufalme Wake unatawala juu ya yote. Mungu hajawaacha watu Wake, na nguvu yetu inakaa katika kutokumwacha Yeye. **{WM 136.4}**

Hukumu za Mungu ziko katika nchi. Vita na matetesi ya vita, uharibifu kwa

moto na mafuriko, hunena wazi kwamba wakati wa taabu, ambayo itakuwa ikiongezeka mpaka mwisho, umefika karibu sana. Hatuna muda wa kupoteza. Ulimwengu unachochewa na roho ya vita. Unabii wa Danieli kumi na moja karibu umefikia utimilifu wake wa mwisho. - *The Review and Herald*, Novemba 24, 1904. **{WM 136.5}**

Haielezeki. - Asubuhi ya Ijumaa iliyopita, mara tu kabla ya sijaamka, mandhari ya kuvutia sana iliwasilishwa mbele yangu. Nilionekana kama vile ninaamka kutoka usingizini lakini sikuwa nyumbani kwangu. Kupitia madirishani niliweza kuona moto mkubwa wa kutisha. Mabonge makubwa ya moto yalikuwa yakianguka juu ya nyumba, na kutoka katika mabonge haya mishale ya moto ilikuwa ikiruka

kwenda kila upande. Haikuwezekana kuisimamisha mioto iliyowashwa, na maeneo mengi yalikuwa yakiharibiwa. Hofu ya watu ilikuwa haielezeki. Baada ya muda niliamka na kujikuta niko nyumbani. - *Letter* 278, 1906. **{WM 136.6}**

Jiandae Fursa Ingalipo. - Kadiri uchokozi wa kidini unavyoangamiza uhuru wa taifa letu, wale ambao wangesimama kuutetea uhuru wa dhamiri watawekwa katika nafasi zisizofaa na zisizo thabiti. Kwa ajili yao wenyewe wanapaswa, wakati wanayo fursa, kuwa na akili kuhusu ugonjwa, chanzo chake, jinsi ya kuuzuia, na tiba yake. Na wale ambao wanafanya hivyo watapata uwanja wa kazi mahali popote. Kutakuwapo na wanaoteseka, wengi sana, ambao watahitaji msaada, si tu

miongoni mwa wale wa imani yetu wenyewe, lakini kwa kiasi kikubwa miongoni mwa wale ambao hawaujui Ukweli. -.Medical Missionary Nov, Dec 1892 **{WM 137.1}**

Tayari Kutoa Msaada wa Haraka. - Umaskini na dhiki katika familia zitafahamika kwetu, na wale walio na dhiki na wanaoteseka itabidi wafarijiwe. Tunajua kidogo sana kuhusu mateso ya wanadamu ambayo yapo kila mahali kutuzunguka, lakini tunapopata fursa tunapaswa kuwa tayari kutoa msaada wa haraka kwa wale ambao wako chini ya shinikizo kali. - *Manuscript* 25, 1894. **{WM 137.2}**

Mkono wa Mungu wa Msaada katika Kupunguza Mateso. - Kazi ya matengenezo ya afya ni njia ya Bwana ya

kupunguza mateso katika ulimwengu wetu na ya kulisafisha kanisa Lake. Wafundishe watu kwamba wanaweza kutenda kama mkono wa Mungu wa msaada kwa kushirikiana na Mfanyakazi Mkuu katika kurejesha afya ya kimwili na ya kiroho. — *Testimonies for the Church* 9:112, 113. **{WM 137.3}**

Kila Mshiriki Anapaswa Kushikilia Kazi ya Umisionari wa Tiba. - Tumeufikia wakati ambapo kila mshiriki wa kanisa anapaswa kushikilia kazi ya umisionari wa tiba. Ulimwengu ni nyumba ya wagonjwa iliyojaa waathiriwa wa maambukizi ya ukoma wa kimwili na kiroho (Lazar house). Kila mahali watu wanaangamia kwa kukosa maarifa ya Ukweli ambao umekabidhiwa kwetu. Washiriki wa kanisa wanahitaji uamsho, ili waweze

kutambua wajibu wao wa kuwapasha watu Kweli hizi. -*Testimonies for the Church* 7:62. **{WM 138.1}**

Mlango wa Kuingilia Miji Mikubwa. – Tangu sasa na kuendelea kazi ya umisionari wa tiba inabidi itekelezwe kwa bidii ambayo kwayo haijawahi kutekelezwa. Kazi hii ni mlango ambao kwa huo Ukweli utapata njia ya kuingia katika miji mikubwa. -*Testimonies for the Church* 9:167. **{WM 138.2}**

Kila mji unapaswa kuingiwa na wafanyakazi waliofunzwa kufanya kazi ya umisionari wa tiba. -*Testimonies for the Church* 7:59. **{WM 138.3}**

Katika kila jiji kubwa kunapaswa kuwapo na jeshi la wafanyakazi waliopangwa, wenye nidhamu nzuri; si

tu mmoja au wawili, bali makundi ya ishirini wanapaswa kuwekwa kufanya kazi. - *Letter* 34, 1892. **{WM 138.4}**

Sehemu ya Kazi ya Kila Kanisa. - Kazi ya umisionari wa tiba inapaswa kuwa na mwakilishi wake katika kila mahali kulingana na uanzishwaji wa makanisa yetu. - *Manuscript* 88, 1902. **{WM 138.5}**

Katika kila mji ambapo tuna kanisa kuna haja ya mahali ambapo matibabu yanaweza kutolewa. Miongoni mwa nyumba za washiriki wa kanisa letu zipo chache ambazo zina uwezo wa kuwa na chumba na vifaa vya utunzaji mzuri wa wagonjwa. Sehemu inapaswa kutolewa ambapo matibabu yanaweza kutolewa kwa magonjwa ya kawaida. Jengo linaweza kuwa si la kifahari na hata

kuwa sahili, lakini linapaswa kuwekewa samani na vifaa vya kutolea matibabu rahisi. - *Testimonies for the Church* 6:113. **{WM 138.6}**

Kazi ya umisionari wa tiba inapaswa kuwa sehemu ya kazi ya kila kanisa katika nchi yetu. Isipoungana na kanisa punde itakuwa mchanganyiko wa ajabu wa atomu zilizovurugika. Ingeweza kutumia, lakini si kuzalisha. Badala ya kutenda kama mkono wa Mungu wa kusaidia kupeleka mbele Ukweli Wake, ingedhoofisha uhai na nguvu kutoka kanisani na kuupunguza nguvu ujumbe. Ikiendeshwa kwa kujitegemea, haingetumia tu vipaji na fedha zinazohitajika katika nyanja zingine, bali katika kazi hasa ya kuwasaidia wasiojiweza mbali na huduma ya Neno, ingewaweka watu ambapo

wangeudhihaki Ukweli wa Biblia. — *Testimonies for the Church* 6:289.**{WM 139.1}**

Huduma ya Umisionari wa Tiba katika Mgogoro wa Mwisho. - Moyo wangu unahuzunishwa ninapoangalia makanisa yetu, ambayo yalipaswa kuunganika katika moyo na roho na kuifanya kazi ya umisionari wa tiba.... Napenda kuwaambia kwamba hivi karibuni hakutakuwa na kazi itakayofanywa katika mielekeo ya kichungaji bali kazi ya umisionari wa tiba. Kazi ya mchungaji ni kuhudumu. Wachungaji wetu wanapaswa kufanya kazi katika mpango wa injili wa kuhudumu. **{WM 139.1}**

Kamwe hamtakuwa wachungaji wa kulingana na mpango wa injili hadi pale mtakapoonesha shauku dhahiri katika

kazi ya umisionari wa tiba, injili ya uponyaji na baraka na uimarishaji. Jitokezeni kumsaidia Bwana, kumsaidia Bwana dhidi ya nguvu kubwa za giza, ili isije ikanenwa juu yenu, "Ulaanini Merozi, ... Walaanini kwa uchungu wenyeji wake; Kwa maana hawakuja kumsaidia Bwana, Kumsaidia Bwana juu ya hao wenye nguvu." Waamuzi 5:23.- *The General Conference Bulletin*, Aprili 12, 1901. **{WM 139.2}**

Sehemu ya VI Vuguvugu la Dorkasi Kanisani

Wazo la Thamani

Katika Yopa alikuwapo Dorkasi, ambaye vidole vyake vyenye ustadi vilikuwa katika utendaji kuliko ulimi

wake. Alijua ni nani alihitaji mavazi ya raha na ni nani alihitaji huruma, na alihudumia bure mahitaji ya matabaka yote mawili. Na Dorkasi alipokufa, kanisa la Yopa walitambua kile walichokipoteza. Haishangazi kwamba waliomboleza na kusikitika, wala kwamba machozi ya joto yalianguka juu ya udongo usio na uhai. Alikuwa ni wa thamani kubwa sana kiasi kwamba kwa nguvu za Mungu alirudishwa kutoka katika nchi ya adui, ili ustadi na nguvu zake bado ziendelee kuwa baraka kwa wengine. **{WM 142.1}**

Uaminifu kama huo wa subira, maombi, na wa kudumu kama waliokuwa nao watakatifu hawa wa Mungu ni nadra; lakini kanisa haliwezi kufanikiwa bila huo. Unahitajika kanisani, katika shule ya Sabato, na

katika jamii. Wengi huja pamoja katika uhusiano wa kanisa na sifa bainishi za asili za tabia zao ambazo hazijatiishwa; na katika upeo wa hatari, ugonjwa, au shida, wakati ambapo roho zenye nguvu, zenye matumaini zinahitajika, wanasalimu amri kwa kuvunjika moyo na kuleta mizigo kwa kanisa; na hawaoni kwamba hili si sahihi. Kusudi ya kazi ya Mungu, haina haja ya watu kama hao, kwa maana wao si watu wa kutegemewa; lakini daima kuna wito kwa ajili ya wafanyakazi imara, wacha Mungu, ambao hawatazimia roho katika siku ya shida. - *Testimonies for the Church* 5:304. **{WM 142.2}**

Na mwanafunzi mmoja alikuwako Yafa, jina lake Tabitha, tafsiri yake ni Dorkasi (yaani paa); mwanamke huyu alikuwa amejaa matendo mema na sadaka alizozitoa. Matendo 9:36

Sura ya Kumi na Saba - Wanawake Wameitwa Kazini

Vuguvugu la Dorkasi Leo. - Kwa hakika kunapaswa kuwa na idadi kubwa ya wanawake wanaojishughulisha na kazi ya kuwahudumia wanadamu wanaoteseka, kuwainua, kuwaelimisha jinsi ya kuamini - kumwamini kabisa, Yesu Kristo Mwokozi wetu. Na kadiri roho zinavyojitoa kwa Bwana Yesu, na kujisalimisha kikamilifu, watayaelewa mafundisho.... **{WM 143.1}**

Ninapata uchungu kwa sababu dada zetu huko Marekani si wengi wao wanaofanya kazi ambayo wangeweza kuifanya kwa Bwana Yesu. Kwa kukaa ndani ya Kristo, wangepokea ujasiri na nguvu na imani kwa ajili ya kazi hiyo.

Wanawake wengi wanapenda kuongea. Kwa nini wasizungumze Maneno ya Kristo kwa roho zinazoangamia? Kadiri tunavyohusiana na Kristo kwa karibu, moyo hujifunza unyonge wa roho ambazo hazimjui Mungu, na ambazo hazihisi aibu wanayomfanyia Kristo ambaye amezinunua kwa thamani. **{WM 143.2}**

Pale wanawake waumini watakapohisi mzigo wa roho, na mzigo wa dhambi ambao si wa kwao wenyewe, watakuwa wakifanya kazi kama Kristo alivyofanya. Hawataona dhabihu yoyote kuwa ni kubwa mno kuitoa kwa ajili ya kuongoa roho kwa Kristo. Na kila mtu aliye na upendo huu kwa roho, amezaliwa na Mungu; wao wako tayari kufuata nyayo Zake, na maneno yao na sauti yao vingekuwa talanta

zinazotumika katika kazi ya Bwana; lishe ile hasa inayotoka katika shina mama kuja katika roho zao wenyewe ingetiririka katika mifereji dhahiri ya upendo kwenda kwa roho ambazo zimenyauka na kukauka. **{WM 143.3}**

Katika kazi hii kuna elimu ya kudumu. Tamaa ya kutaka kuwa baraka hufichua udhaifu na uzembe wa mfanyakazi. Hii huongoza roho kwa Mungu katika maombi, na Bwana Yesu anatoa nuru na Roho Wake Mtakatifu, na wanaelewa kuwa ni Kristo anayeyusha na kuivunja mioyo migumu. - *Letter* 133, 1898. **{WM 144.1}**

Thamani ya Mfumo. - Kazi unayoifanya [Ilielekezwa kwa mwanamke mwenye uzoefu mpana wa umma ambaye alikuwa amejiunga na

Kanisa la Waadventista wa Sabato.] ya kuwasaidia dada zetu kuhisi uwajibikaji wao kwa Mungu ni kazi nzuri na muhimu. Kwa muda mrefu imepuuzwa. Lakini kazi hii itakapopangwa katika mielekeo ya wazi, rahisi, yenye mipaka, tunaweza kutarajia kwamba majukumu ya nyumbani, badala ya kupuuzwa, yatafanywa kwa akili zaidi. Bwana angependa daima tupate kusisitiza thamani ya roho ya mwanadamu kwa wale ambao hawaelewi thamani yake. **{WM 144.2}**

Ikiwa tunaweza kupanga kuwa na makundi ya watu yaliyopangwa, yenye kufuata sheria za dini, yaliyofundishwa kwa busara kuhusiana na sehemu ambayo wanapaswa kutenda kama watumishi wa Bwana, makanisa yetu yatakuwa na maisha na uhai ambao

wamehitaji kwa muda mrefu. Ubora wa roho ambayo Kristo ameiokoa utathaminiwa. Dada zetu kwa ujumla wana wakati mgumu na familia zao zinazoongezeka na majaribio yao yasiyopendeza. Nimetamani sana kuwa na wanawake ambao wangeweza kuelimishwa kuwasaidia dada zetu kuinuka kutoka katika kukata tamaa kwao na kuhisi kwamba wanaweza kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Hili huleta miale ya jua katika maisha yao wenyewe, ambayo inaakisiwa katika mioyo ya wengine. Mungu atakubariki na wote wanaoungana nawe katika kazi hii kubwa. - *Letter* 54, 1899. **{WM 144.3}**

Bwana Ana Kazi kwa Ajili ya Wanawake. - Bwana ana kazi kwa wanawake na wanaume pia. Wanaweza

kuchukua nafasi zao katika kazi Yake katika shida hii, na atafanya kazi kupitia kwao. Ikiwa wamejazwa na hisia ya wajibu wao, na wanafanya kazi chini ya mvuto wa Roho Mtakatifu, watakuwa na mali binafsi inayohitajika kwa ajili ya wakati huu. Mwokozi ataakisi juu ya wanawake hawa wanaojitoa mhanga nuru ya uso Wake, na atawapa uwezo unaozidi ule wa wanaume. Wanaweza kufanya katika familia kazi ambayo wanaume hawawezi kuifanya, kazi ambayo inafikia maisha ya ndani. Wanaweza kuja karibu na mioyo ya wale ambao wanaume hawawezi kuwafikia. Kazi yao inahitajika. - *The Review and Herald*, Agosti 26, 1902. **{WM 145.1}**

Wanawake Wana Majaliwa Makubwa. – Dada zangu, tunaweza kufanya kazi bora kwa Mungu ikiwa

tutapenda. Mwanamke hajui uwezo wake. Mungu hakukusudia kwamba uwezo wake wote upate kufyonzwa kwa kuhoji: Nitakula nini? Nitakuywa nini? na kwa gharama gani nitajivika nguo? Kuna kusudi la juu zaidi kwa ajili ya mwanamke, majaliwa makubwa zaidi. Anapaswa kuendeleza na kukuza uwezo wake, kwa kuwa Mungu anaweza kuutumia katika kazi kubwa ya kuokoa roho kutoka katika uharibifu wa milele. - *Testimonies for the Church* 4:642. **{WM 145.2}**

Tunaweza kusema kwa usalama kwamba heshima na umuhimu wa utume wa mwanamke na majukumu ya pekee ni ya asili iliyo tukufu na takatifu zaidi kuliko majukumu ya mwanaume.... Hebu mwanamke na atambue utukufu wa kazi yake na, katika nguvu na hofu ya

Mungu, apate kutenda utume wake. - *Testimonies for the Church* 3:565. **{WM 145.3}**

Ikiwa tutaweza kuvutia katika akili za dada zetu mema yale ambayo yako katika uwezo wao wa kutenda kupitia kwa Bwana Yesu Kristo, tutaona kazi kubwa ikitimizwa. - *Letter* 119, 1898. **{WM 145.4}**

Wanawake Wanaitwa Kuwa Wajumbe wa Rehema. - Tunawahitaji sana wanawake waliojiweka wakfu ambao, kama wajumbe wa rehema, watawatembelea akina mama na watoto majumbani mwao na kuwasaidia katika majukumu ya kila siku ya kaya, ikiwa ni lazima, kabla ya kuanza kuzungumza nao kuhusu Ukweli wa wakati huu.

Utagundua kwamba kwa mbinu hii utakuwa na roho kama matokeo ya huduma yako. - *The Review and Herald,* Julai 12, 1906. **{WM 146.1}**

Mbona Mmesimama Bila Kazi? - Bwana wa shamba la mizabibu anawaambia wanawake wengi ambao sasa hawafanyi chochote, "Mbona mmesimama hapa mchana kutwa bila kazi?" Wanawake wanaweza kuwa vyombo vya haki, wakitoa huduma takatifu. Alikuwa ni Mariamu aliyemhubiri Yesu aliyefufuka kwa mara ya kwanza; na mvuto utakasao, na wenye kulainisha wa wanawake Wakristo unahitajika katika kazi kubwa ya kuuhubiri Ukweli sasa. Ikiwa kungelikuwapo na wanawake ishirini pale ambapo kwa sasa pana mmoja ambao wangefanya wokovu wa roho

kuwa kazi yao inayohifadhiwa kwa upendo, tungelipaswa kuona wengi zaidi wakiongoka kuufuata Ukweli. Ari na bidii endelevu katika kusudi la Mungu ingefanikiwa kabisa, nayo ingewashangaza kwa matokeo yake. Kazi lazima itimizwe kupitia kwa saburi na uvumilivu, na katika hili inadhihirishwa upendo halisi kwa Mungu. Yeye Anataka matendo, na si maneno peke yake. **{WM 146.2}**

Kazi ya Mungu inastahili juhudi zetu bora.... Mara nyingi tumefungwa sana katika shauku zetu za ubinafsi kiasi kwamba mioyo yetu hairuhusiwi kuingiza ndani mahitaji na dhiki za ubinadamu; tumepungua katika matendo ya huruma na ukarimu, katika huduma takatifu na ya kijamii kwa wahitaji, walioonewa, na wanaoteseka.

— *The Signs of the Times*, Septemba 16, 1886.**{WM 146.3}**

Kazi Inayopasa Kufanyika. - Kuzubaa kwa kutotenda na uvivu mdogo-mdogo unadhoofisha nguvu ya maisha ya wanawake vijana. Wapo wale ambao wanatumia saa za thamani katika kitanda, ambacho hakiwabariki kwa kuongezeka kwa nguvu au kuwapunguzia wengine mizigo, bali huleta juu yao udhaifu na kuwathibitisha katika tabia mbaya. Saa hizi zilizopotezwa bila sababu kitandani haziwezi kupatikana tena. Dhambi ya muda uliopotezwa kwa jinsi hiyo hurekodiwa katika kitabu cha kumbukumbu. **{WM 146.4}**

Kuna mengi ya kufanya katika dunia yetu hii yenye shughuli nyingi. Wapo watu wengi katika familia kubwa ya

Mungu ambao wanahitaji huruma na msaada. Ikiwa kazi yetu wenyewe haidai muda wetu, kuna wagonjwa wa kutembelewa, maskini wa kusaidiwa na kutiwa moyo. —*The Health Reformer*, Juni, 1873. **{WM 147.1}**

Nafasi ya Pekee kwa Wanawake katika Kazi. - Kuna uwanja mpana ambao dada zetu wanaweza kumtumikia Bwana katika tanzu mbalimbali za kazi zinazohusiana na kusudi Lake. Kupitia katika kazi ya umisionari wanaweza kufikia tabaka ambalo wachungaji wetu hawawezi.... Kuna kazi iliyopuuzwa au iliyofanywa si kwa ukamilifu ambayo ingeweza kukamilishwa kabisa kwa msaada ambao dada zetu wanaweza kuutoa. Kuna aina nyingi za kazi ambazo ni ngumu sana kwa wanawake, ambazo ndugu zetu wanaitwa kujihusisha nazo,

kiasi kwamba tanzu nyingi za kazi za umisionari zimepuuzwa. Mambo mengi yanayohusiana na makanisa mbalimbali yameachwa bila kufanywa ambayo wanawake, ikiwa wangeelimishwa vizuri, wangeweza kuzishughulikia. Dada zetu wanaweza kutumika kama makarani wa kanisa, na shughuli za kanisa zisingepuuzwa kwa namna ya kusikitisha kiasi hicho. Kuna nafasi nyingine nyingi zilizounganishwa na kusudi la Mungu ambazo dada zetu wana sifa bora zaidi kuzijaza kuliko ndugu zetu, na ambazo kwa hizo wanaweza kufanya huduma yenye ufanisi. - *The Review and Herald*, Desemba 19, 1878. **{WM 147.2}**

Mawasiliano ya Kimisionari. - Wanawake wanaweza kufanya kazi nzuri katika uwanja wa umisionari, kwa

kuwaandikia marafiki, na kutambua hisia zao za kweli kuhusiana na kusudi la Mungu. Vitu vya thamani sana vinadhihirishwa kupitia njia hii. Wafanyakazi hawapaswi kutafuta kujitukuza wenyewe, bali kuwasilisha Ukweli katika usahili wake popote watakapopata fursa.-*The Signs of the Times*, Septemba 16, 1886. **{WM 147.3}**

Madai ya Mungu Juu ya Muda Wetu na Fedha. - Hatuna haki, dada zangu Wakristo, wa kupoteza muda wetu, na kutoa mfano kwa wengine ambao hawana uwezo kama sisi kupoteza muda wao na nguvu zao juu ya mapambo yasiyohitajika, juu ya mavazi au samani, au kujiingiza katika mazidio ya chakula. Tuna wajibu wa kidini wa kutekeleza, na ikiwa tutapuuza wajibu

huu, na kutoa muda wetu kwa mambo yasiyo ya lazima, tutadumaza akili na ziwe mbilikimo na kutenganisha mapenzi kutoka kwa Mungu. Mwanzilishi wa kuwepo kwetu ana madai juu ya muda wetu na fedha zetu. Anao maskini na wale wanaoteseka kote kutuzunguka ambao fedha zinaweza kuwatuliza, na maneno ya kuchangamsha, ya kutia moyo kuwabariki. Kristo anajitambulisha na mahitaji ya wanadamu wanaoteseka. Pale ulipopuuza kuwatembelea mjane na yatima waliojaribiwa katika tanuru la dhiki, mateso, uhitaji, na ufukara, hukutambua kwamba Kristo angeandika hali hizo dhidi yako katika kitabu cha kumbukumbu, kana kwamba ulikuwa umempuuza Yeye.- —*The Health Reformer*, Juni, 1873.**{WM 148.1}**

Jihusishe na Uinjilisti Binafsi. – Shida ya moja kwa moja inatoshelezwa na kazi ya wanawake ambao wamejitoa kwa Bwana na wanaondoka kwenda kuwasaidia watu wenye uhitaji, waliochoshwa na dhambi. Kazi ya uinjilisti wa binafsi inapaswa kufanywa. Wanawake ambao huchukua kazi hii hupeleka injili kwenye nyumba za watu katika barabara kuu na katika sehemu zisizofahamika vizuri, kwenye vijia vidogo. Wanasoma na kulifafanua Neno kwa familia, wakiomba pamoja nao, wakiwatunza wagonjwa, wakituliza mahitaji yao ya maisha. —*Testimonies for the Church* 6:118. **{WM 148.2}**

Sura ya Kumi na Nane - Sifa za Wanawake kwa Ajili ya Utumishi

Aina ya Wanawake Wanaoitwa kwenye Huduma. - Mungu anawaita wafanyakazi wanawake wenye bidii, wafanyakazi ambao wana busara, wenye moyo mkunjufu, moyo wenye jotojot, wapole, na waaminifu kwa kanuni. Anawataka wanawake wavumilivu ambao wataondoa akili zao kutoka katika nafsi na manufaa yao binafsi, na kuzilenga kwa Kristo.... Je, dada zetu watatokea kwa ajili ya dharura? Je, watafanya kazi kwa Bwana? -*Testimonies for the Church* 6:118. **{WM 149.1}**

Kujifunza katika Shule ya Kristo. - Bwana ana kazi ya kufanywa

na wanawake na wanaume pia. Wanaweza kufanikisha kazi nzuri kwa Mungu, ikiwa kwanza watajifunza katika shule ya Kristo somo la thamani kubwa, somo muhimu la upole. Hawapaswi tu kubeba Jina la Kristo bali pia kuwa na Roho Wake. Lazima watembee kama Yeye alivyotembea, wakitakasa roho zao kutokana na kila kitu kinachotia unajisi. Ndipo watakapoweza kuwanufaisha wengine kwa kuwasilisha utoshelevu wote wa Yesu. - *Manuscript* 119, 1907. **{WM 149.2}**

Kwa Msimamo Thabiti na Tabia Dhahiri. - Wanawake wenye msimamo au maadili thabiti na tabia dhahiri wanahitajika, wanawake ambao wanaamini kwamba kwa kweli tunaishi

katika siku za mwisho, na kwamba tunao ujumbe makini wa mwisho wa onyo wa kutolewa kwa ulimwengu. Wanapaswa kuhisi kwamba wanajihusisha na kazi iliyo muhimu katika kueneza miale ya nuru ambayo Mbingu imemwaga juu yao. Wakati upendo wa Mungu na Ukweli Wake ni kanuni ya kudumu, hawataruhusu chochote kuwazuia kutekeleza wajibu au kuwavunja moyo katika kazi yao. Watamcha Mungu na hawatavutwa kwingine kutoka katika kazi zao kwenye kusudi Lake kwa jaribu la hali yenye faida na matarajio ya kuvutia. Watahifadhi uadilifu wao kwa gharama yoyote kwa upande wao wenyewe. Hawa ndio watakaoiwakilisha dini ya Kristo kwa usahihi, ambao maneno yao yatanenwa kwa wakati unaofaa, kama

machungwa katika vyano vya fedha. Watu kama hao wanaweza kwa njia nyingi kufanya kazi ya thamani kwa Mungu. Yeye Anawataka waende katika shamba la mavuno na kusaidia katika kukusanya miganda. - *The Signs of the Times*, Septemba 16, 1886. **{WM 149.3}**

Busara, Mtazamo, Uwezo. - Wanawake Wakristo wanaitwa kwa ajili ya hayo. Kuna uwanja mpana ambao katika huo wanaweza kumtumikia Bwana. Kuna wanawake mashuhuri ambao wamekuwa na ujasiri wa kimaadili wa kuamua kuunga mkono Ukweli kutokana na uzito wa ushahidi. Wana busara, mtazamo, na uwezo mzuri, nao wangeweza kuwa wafanyakazi Wakristo wenye mafanikio. - *Kitabu hicho hicho*. **{WM 150.1}**

Mchanganyiko wa Sifa za Martha na Mariamu.- Wote wanaomfanyia Mungu kazi wanapaswa kuwa na mchanganyiko wa sifa za Martha na Mariamu - utayari wa kuhudumu na upendo wa dhati kwa ukweli. Nafsi na ubinafsi ni lazima viondolewe mbali. —*Testimonies for the Church* 6:118. **{WM 150.2}**

Wanawake Waungwana Wanahitajika. - Wanawake wanahitajika ambao hawajikwezi na kujiona wao ndiyo muhimu sana, bali ni wapole katika tabia na wanyenyekevu wa moyo, ambao watafanya kazi kwa upole wa Kristo popote wanapoweza kupata chochote cha kufanya kwa ajili ya wokovu wa roho. Wote ambao wamefanywa kuwa washirika wa manufaa ya mbinguni wanapaswa kuwa

na bidii na kuwa na shauku kwamba wengine ambao hawana upendeleo ambao wameufurahia, wanapaswa kuwa na ushahidi wa Ukweli ule uliowasilishwa mbele yao. Na hawatatamani tu kwamba wengine wapate faida hii, bali watahakikisha kwamba wanaipata, nao watafanya sehemu yao kuelekea utimilizwaji wa lengo hili. **{WM 150.3}**

Wale ambao watakuwa wafanyakazi pamoja na Mungu watakua katika nguvu za kimaadili na za kiroho, wakati ambapo wale wanaotumia muda wao na nguvu zao katika kujitumikia wenyewe watadumaa, na kunyauka, na kufa. — *The Signs of the Times*, Septemba 16, 1886.**{WM 151.1}**

Matumizi Mazuri ya Vipaji. - Dada zetu ... hawana upungufu katika uwezo, na kama wangeweka katika matumizi sahihi vipaji walivyonavyo tayari, ufanisi wao ungeongezeka sana. - *Testimonies for the Church* 4:629, 630. **{WM 151.2}**

Jasiri na Mwenye Kujitegemea. - Nyumba nyingi zinafanywa kukosa furaha sana kwa malalamiko yasiyo na maana ya mwanamke mkuu wa kaya au mama mwenye nyumba, ambaye anageuka kwa chuki kutoka katika kazi sahili, za kawaida za maisha yake ya nyumbani yasiyo ya kujifanya. Anayaangalia masumbufu na majukumu ya fungu lake kama taabu, na kile ambacho kwa njia ya uchangamfu kingeweza kufanywa kuwa si tu cha kupendeza na kuvutia bali chenye kuleta

faida, kinakuwa tu kazi ngumu kabisa. Anautazama utumwa wa maisha yake kwa kinyaa, na kujifikiria kuwa yeye ni mfiadini. **{WM 151.3}**

Ni kweli kwamba magurudumu ya urasimu wa nyumbani hayatakimbia kwa ulaini siku zote; kuna mengi ya kujaribu uvumilivu na kuelemea nguvu. Lakini wakati ambapo akina mama hawawajibiki kwa hali ambazo hawana udhibiti juu yake, ni bure kukataa kwamba mazingira huleta tofauti kubwa kwa akina mama katika kazi zao za maisha. Lakini lawama kwao ni pale mazingira yanaporuhusiwa kutawala na kuvuta kwingine msimamo wao, wakati wanapochoka na kukosa uaminifu kwa dhamana yao ya juu, na kupuuza wajibu wao unaojulikana. **{WM 151.4}**

Mke na mama ambaye kwa uadilifu anashinda shida ambazo kwa hizo wengine huzama kwa kukosa subira na ustahimilivu wa kuvumilia, si tu anakuwa na nguvu yeye mwenyewe katika kutekeleza wajibu wake, bali pia uzoefu wake wa kushinda majaribu na vikwazo unamfanya kuwa na uwezo wa kuwa msaada wenye ufanisi kwa wengine, kwa maneno na mfano. Wengi ambao wanafanya vizuri katika hali nzuri wanaonekana kupitia mabadiliko ya tabia chini ya shida na majaribio; wanas kwa kuwiana na shida zao. Mungu kamwe hakupanga kwamba tuwe mchezo wa mazingira. - *The Health Reformer*, Agosti, 1877.**{WM 151.5}**

Sifa za Lazima na Muhimu za Tabia ya Kikristo (Vipengele

muhimu katika Tabia ya Mkristo).
– Akina mama, mnakuza tabia. Mkombozi wenu Mwenye huruma anawaangalia kwa upendo na huruma, Naye Yuko tayari kusikia maombi yenu, na kuwapa msaada ambao mnauhitaji katika kazi yenu ya maisha. Upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, imani, na fadhila ni sifa za lazima na muhimu za tabia ya Kikristo. Neema hizi za thamani kubwa ni matunda ya Roho. Hizo ni taji na ngao ya Mkristo. Ndoto ya mchana ya juu kabisa na matamanio yaliyoinuliwa zaidi hayawezi kulenga katika chochote kilicho cha juu zaidi. Hakuna kitu kinachoweza kutoa maudhui kamili zaidi na kuridhika. Mafanikio haya ya mbinguni hayategemei hali, wala mapenzi au hukumu isiyo kamili ya mwanadamu.

Mwokozi wa thamani, ambaye anaelewa mapambano yetu ya moyo na udhaifu wa asili yetu, hutuhurumia, na kutusamehe makosa yetu na kutupatia neema ambazo tunazitamani kwa ari. – *Kitabu kile kile*. **{WM 152.1}**

Mwanamke Muungwana wa Kweli. - Je, unafanya makosa? Usiruhusu hili likukatishe tamaa. Bwana anaweza kukuruhusu kufanya makosa madogo madogo ili kukuokoa usifanye makosa makubwa. Nenda kwa Yesu, na umwombe akusamehe, kisha uamini kwamba anafanya hivyo. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." **{WM 152.2}**

Unaposemewa maneno yasiyo na fadhili, ya kukatisha tamaa, usilipize kisasi. Usijibu isipokuwa pale unapoweza kurudisha jibu zuri. Jiambie, "Sitamwangusha Mwokozi wangu." Mwanamke Mkristo ni muungwana. Katika midomo yake daima ni sheria ya wema. Hatamki maneno ya pupa. Kusema maneno ya upole unapokasirishwa kutaleta uchangamfu ndani ya mioyo yenu na kufanya njia yako iwe laini zaidi. Msichana wa shule, alipoulizwa juu ya fasili ya upole, alisema, "Watu wapole ni wale ambao hutoa majibu laini kwa maswali ya ukali." Kristo anasema, "Heri wenye upole; Maana hao watairithi nchi." Watakuwa raia wanaofaa kwa ufalme wa mbinguni, kwa kuwa wako tayari

kufundishwa. - *The Review and Herald*, Aprili 7, 1904. **{WM 153.1}**

Mwenye mwonekano wa kuvutia, Mwonekano mzuri, Wenye Ukarimu, na Neema kwa Watu, ni wa Kuheshimiwa/Kuheshimika (graceful and dignified). - Usichukulie maisha kama hekaya ya mahaba bali kama uhalisi. Timiza wajibu wako mdogo kabisa katika kumcha na kumpenda Mungu, kwa uaminifu na uchangamfu. Mungu anatamka, yule"Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia." **{WM 153.2}**

Jifunze maisha ambayo Kristo aliyaishi wakati akiwa hapa duniani. Hakupuuza wajibu mdogo kabisa, sahili kabisa.

Ukamilifu ulionekana katika yote aliyoyafanya. Mtegemee Yeye kwa ajili ya msaada, na utawezeshwa kutekeleza majukumu yako ya kila siku kwa neema na heshima ya yule anayetafuta taji ya uzima wa milele. *Kitabu kile kile*. (Shauri linaelekezwa kwa "Dada zangu Wanaojaribiwa na Kukata Tamaa.") **{WM 153.3}**

Mwaminifu katika Lililo Dogo Sana. - Ndugu na dada zangu, msipite kando vitu vidogo vidogo kwa kutafuta kazi kubwa. Unaweza kufanya kazi hiyo ndogo kwa mafanikio lakini ukashindwa kabisa katika kujaribu kufanya kazi kubwa, na ukaanguka katika kuvunjika moyo. Shikilia popote unapoona kwamba kuna kazi ya kufanywa. Ni kwa kufanya kwa nguvu zako lile ambalo mkono wako utakalolipata kulifanya

ndipo utakapokuza talanta na kipaji kwa ajili ya kazi kubwa. Ni kwa kudharau fursa za kila siku, na kupuuza vitu vidogo vidogo, ndipo wengi wanakosa kuzaa matunda na kunyauka. - *The Review and Herald*, Agosti 26, 1902. **{WM 153.4}**

Mwangalifu kwa Vitu Vidogo Vidogo. – Tunaeleza na kutafakari sana juu ya ukuu wa maisha ya Kristo. Tunazungumza juu ya mambo makuu aliyotimiza, juu ya miujiza aliyotenda, juu ya jinsi alivyozungumza utulivu kwa maji yaliyochafuka sana, akarejesha kuona kwa vipofu na kusikia kwa viziwi, na kufufua wafu. Lakini uangalifu Wake kwa vitu vidogo vidogo ni uthibitisho wa juu zaidi wa ukuu wake. Msikilize akiongea na Martha anapomwendea na ombi kwamba amwambie dada yake

amsaidie katika kutumikia. Anamwambia asiruhusu masumbufu ya kaya kuvuruga amani ya roho yake. "Martha, Martha," anasema, "unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi; lakini kinatakiwa kitu kimoja tu; na Mariamu amelichagua fungu lililo jema, ambalo hataondolewa." — *The Review and Herald*, Aprili 7, 1904. **{WM 154.1}**

Mwekevu/Mchumi au yule asiye mfujaji; Kusanya Vipande Vyote. - "Kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee chochote." Yeye ambaye alikuwa na rasilimali zote kwa amri Yake anatoa funzo kwamba hakuna hata kipande kimoja kinachopaswa kupotea. Yenye aliye navyo tele asitumie kwa kufuja. Hebu kisitumike vibaya kitu chochote ambacho kinaweza kumfaa

mtu yeyote/mwingine. Kusanya kila kipande, kwa kuwa mtu fulani atakihitaji. Masomo yanayohusu baraka za kiroho zilizotolewa yanapaswa kuthaminiwa kwa uangalifu. — *Manuscript* 60, 1897.**{WM 154.4}**

Nguvu ya Upole. - Kila mwanamke anapaswa kukuza akili yenye usawa na tabia iliyo safi, akiakisi yale tu yaliyo Kweli, mema, na mazuri. Mke na mama anaweza kuwafunga mumewe na watoto moyoni mwake kwa upendo usiobadilika, unaooneshwa kwa maneno ya upole na mwenendo wa heshima. Upole ni rahisi, lakini una nguvu ya kulainisha asili ambazo zingeweza kukua na kuwa ngumu na kali bila huo. Upole wa Kikristo unapaswa kutawala katika kila kaya. Ukuzaji wa uungwana ulio sawasawa, utayari wa kufanya kwa

wengine kama tunavyotaka wafanye kwetu sisi, ungeondoa nusu ya maovu ya maisha. — *The Signs of the Times*, Agosti 15, 1906.**{WM 154.3}**

Hakikisha kuwa Tunafanya Kazi kwa Ajili ya Yesu. - Dada zetu hawaachiliwi katika kushiriki kwenye kazi ya Mungu. Kila mtu ambaye ameonja nguvu za ulimwengu ujao ana kazi ya dhati ya kufanya katika nafasi fulani katika shamba la mizabibu la Bwana. Dada zetu wanaweza kuwa na uwezo wa kuweka vidole vyao daima katika shughuli ya kutengeneza vikorokoro vidogo vidogo vizuri kwa ajili ya kupamba nyumba zao au kutoa zawadi kwa marafiki wao. Kiasi kikubwa cha aina hii ya vifaa kinaweza kuletwa na kuwekwa juu ya jiwe la msingi, lakini je, Yesu ataiangalia aina hii yote ya kazi

nzuri kama dhabihu iliyo hai Kwake Mwenyewe? Je! Atatamka sifa juu ya wafanyakazi, "Nayajua matendo yako, na taabu yako, na subira yako," na jinsi "ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya Jina Langu, wala hukuchoka"? **{WM 155.1}**

Hebu dada zetu waulize, nitakutanaje katika Hukumu na hizi roho ambazo nimefahamiana au ningepaswa kufahamiana nao? Je, nimejua hali ya kila mmoja binafsi? Je, nimepata maarifa ya kutosha kutoka katika Biblia yangu kiasi kwamba ningeweza kuwafungulia Maandiko? ... .**{WM 155.2}**

Je, hii ndio kazi Mungu amekuteua uifanye kama mtumishi Wake wa kuajiriwa, kujifunza mitindo migumu,

mapambo ya kupendeza ya nakshi na mambo mengi yasiyoeleweka katika tabaka hili la kazi kwa kusudi la kuwa stadi kwa kile ambacho mtu mwingine amefanya au kuonesha kile unachoweza kufanya? Je! Hii ndio aina ya kazi ambayo Mungu atakupongeza kwa kuifanya, ambayo inashughulisha shauku yako, muda wako uliopewa na Mungu na talanta, kiasi kwamba huna ladha, upendo au elimu au kipaji cha kufanya kazi ya umisionari? Aina hii yote ya kazi ni nyasi kavu za ng'ombe, mbao, na mabua, ambayo moto wa siku ya mwisho utateketeza. Lakini matoleo yako kwa Mungu yako wapi? Iko wapi kazi yako ya saburi, ari yako ya dhati, inayokuleta katika uhusiano na Kristo, kubeba nira yake, kuchukua mizigo yake? Iko wapi dhahabu, fedha, na

mawe ya thamani ambayo umeweka juu ya jiwe la msingi, ambayo moto wa siku ya mwisho hauwezi kuteketeza, kwa sababu hivyo si vya kuharibika? — *The Review and Herald*, Mei 31, 1887. **{WM 155.3}**

Yesu Anajua Mizigo ya Wanawake. - Yeye ambaye alimrudishia mjane mwanawe wa pekee alipokuwa akipelekwa mazikoni, anaguswa leo na huzuni ya mama aliyefiwa. Yeye aliyewarudishia Mariamu na Martha ndugu yao aliyekwisha kuzikwa, ambaye alilia machozi ya huruma kwenye kaburi la Lazaro, ambaye alimsamehe Mariamu Magdalena, ambaye alimkumbuka mama Yake wakati akiwa amening'inia kwa uchungu msalabani, ambaye aliwatokea wanawake waliokuwa wakilia

baada ya Ufufuo Wake, na kuwafanya kuwa wajumbe Wake wa kumhubiri Mwokozi aliyefufuka akisema, "Enenda kwa ndugu Zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba Yangu Naye ni Baba yenu, kwa Mungu Wangu Naye ni Mungu wenu," ni rafiki bora wa mwanamke leo na Yuko tayari kumsaidia katika hitaji Lake ikiwa atamwamini. – *The Health Reformer*, Agosti, 1877. **{WM 156.1}**

Sura ya Kumi na Tisa - Mvuto wa Wanawake Wakristo

Utume wa Ajabu wa Wanawake. - Waadventista wa Sabato hawapaswi kwa namna yoyote ile kuishusha hadhi, au kuifanya ionekane duni au kuidharaua kazi ya mwanamke. - *Gospel Workers*, 453. **{WM 157.1}**

Ajabu ni utume wa wanawake walioolewa, akina mama, na wafanyakazi vijana wa kike. Ikiwa watapenda, wanaweza kutoa mvuto kwa ajili ya mema kwa wote wanaowazunguka. Kwa staha katika mavazi na mwenendo wa uangalifu wanaweza kushuhudia Ukweli katika usahili wake. Wanaweza kuruhusu nuru yao iangaze mbele ya wote ili wengine wapate kuona matendo yao mema na wamtukuze Baba yao aliye mbinguni. Mwanamke aliyeongoka kweli kweli ataweka mvuto wa nguvu wenye

kubadilisha kwa ajili ya wema. Akiwa ameunganishwa na mumewe, anaweza kumsaidia katika kazi yake na kuwa kwake njia ya kutia moyo na kubariki. Wakati nia na njia zinapoletwa chini ya utawala wa Roho wa Mungu, hakuna kikomo kwa mema ambayo yanaweza kufanikishwa/kupatikana. - *Manuscript* 91, 1908. **{WM 157.2}**

Kuwa na Sehemu ya Kutenda Katika Kazi ya Mwisho. - Dada zetu, vijana, wenye umri wa kati, na wale wa miaka mingi au wazee wanaweza kuchukua sehemu katika kazi ya mwisho kwa wakati huu; na kwa kufanya hivyo kadiri wanavyopata fursa watapata uzoefu wa thamani ya juu kabisa kwa ajili yao wenyewe. Katika kuwafikiria zaidi wengine kuliko wao wenyewe watakua katika neema. Kwa kufundisha

akili katika mwelekeo huu watajifunza jinsi ya kubeba mizigo kwa ajili ya Yesu. - *The Review and Herald*, Januari 2, 1879. **{WM 157.3}**

Kutumikia kwa Uaminifu na Utambuzi. - Wakati huu kila kipaji cha kila mfanyakazi kinapaswa kuangaliwa kama amana takatifu ya kutumika katika kupanua kazi ya matengenezo. Bwana alinielekeza kwamba dada zetu ambao wamepokea mafunzo ambayo yamewaandaa kwa ajili ya nafasi za kuwajibika wanapaswa kutumikia kwa uaminifu na utambuzi katika wito wao, wakitumia mvuto wao kwa busara na, pamoja na ndugu zao katika imani, kupata uzoefu ambao utawaandaa kwa ajili ya kutumika kwa ufanisi mkubwa zaidi.... **{WM 157.4}**

Katika nyakati za kale Bwana alifanya kazi kwa njia ya ajabu kupitia kwa wanawake waliowekwa wakfu ambao waliungana katika kazi Yake na wanaume ambao alikuwa amewachagua kusimama kama wawakilishi Wake. Yeye Aliwatumia wanawake kupata ushindi mkubwa na wa wazi. Zaidi ya mara moja wakati wa dharura aliwaleta mbele na kufanya kazi kupitia kwao kwa ajili ya wokovu wa maisha ya wengi. - *Letter* B-22, 1911. **{WM 158.1}**

Wajibu wa Kwanza wa Mama. - Ushawishi wa mama haukomi kamwe. Daima uko hai, iwe kwa wema au kwa uovu; na ili kazi yake ipate kusimama katika jaribio la Hukumu, ni lazima amfanye Mungu kuwa tegemeo Lake na kufanya kazi kwa jicho lililokazwa kwa ajili ya utukufu Wake Bwana. Wajibu

wake wa kwanza ni kwa watoto wake, kutengeneza tabia zao kiasi kwamba waweze kuwa na furaha katika maisha haya na kujipatia maisha yale ya baadaye, ya milele. Hapaswi kushawishiwa na kile ambacho Bibi fulani anakifanya, wala na maneno ya Bi A. au B. kwa kurejelea kuwa yeye ni wa ajabu sana, tofauti sana na watu wengine katika mavazi yake au katika mpangilio wa nyumba yake kwa ajili ya furaha badala ya maonesho au katika usimamizi wa watoto wake. **{WM 158.2}**

Mungu amempa mama, katika elimu ya watoto wake, wajibu mkubwa ulio juu ya kila kitu kingine. - *Good Health*, Juni, 1880. **{WM 158.3}**

Jamii Ina Madai Juu ya Wanawake. - Ni haki ya mwanamke kutunza maslahi ya mumewe, kuyahudumia mavazi yake, na kujitahidi kumfanya kuwa na furaha. Ni haki yake kuendeleza mawazo na tabia zake kuwa nzuri zaidi, kushirikiana na jamii, kuwa mchangamfu, na mwenye furaha, akieneza uchangamfu katika familia yake na kuifanya iwe mbingu ndogo. Na anaweza kuwa na shauku kwa ajili ya yaliyo zaidi ya "mimi na changu." Anapaswa kuzingatia kwamba jamii ina madai juu yake. - *The Health Reformer*, Juni, 1873. **{WM 158.4}**

Kazi Nje ya Nyumbani Kwetu. - Wanaume na wanawake hawatimizi mpango wa Mungu pale wanapoonesha upendo kwa familia zao peke yake, kwa jamaa na marafiki zao walio matajiri,

huku wakiwatenga kutoka katika upendo wao wale ambao wangeweza kuwafariji na kuwabariki kwa kupunguza mahitaji yao…. **{WM 159.1}**

Bwana anapotuambia tuwatendee mema wengine wale walio nje ya nyumbani kwetu, Hamaanishi kwamba upendo wetu wa nyumbani utapunguzwa, na kwamba tutawapenda jamaa zetu au nchi yetu kidogo kwa sababu anataka tueneze huruma zetu kwa wengine. Bali hatupaswi kufungia mapenzi na huruma yetu ndani ya kuta nne, na kufungia baraka ambayo Mungu ametupa, kiasi kwamba wengine hawatafaidika pamoja nasi katika kuifurahia. - *The Review and Herald*, Oktoba 15, 1895. **{WM 159.2}**

Kupanua Maeneo ya Kutumika kwa Ufanisi. - Wote hawana kazi sawa. Kuna wajibu dhahiri na wa mtu binafsi kwa kila mmoja kutekeleza; lakini bado pamoja na wajibu mbalimbali kunaweza kuwa na upatanifu mzuri, unaofunga pamoja kazi ya wote katika ubora kamili. Baba yetu wa mbinguni hataki kutoka kwa yeyote ambaye amempa talanta moja tu, ustawishaji wa kupata tano. Lakini ikiwa ile moja itatumiwa kwa busara, mmiliki wake punde atakuwa amepata zaidi, na anaweza siku zote kuongeza nguvu yake ya ushawishi na eneo la kutumika kwa ufanisi zaidi kwa kufanya matumizi bora ya talanta ambazo Mungu amempa. Upekee wake unaweza kuhifadhiwa kwa namna ya pekee, na bado anaweza kuwa sehemu ya jamii yote kubwa katika kuendeleza

kazi ya matengenezo inayohitajika sana. **{WM 159.3}**

Mwanamke, ikiwa atatumia vizuri muda wake, na vitivo na nguvu zake, akimtegemea Mungu kwa ajili ya hekima na nguvu, anaweza kusimama katika usawa na mumewe kama mshauri, mnasihi, mwenzi, na mfanyakazi mwenza, na bado asipoteze neema yoyote ya kuwa kwake mwanamke au staha. Anaweza kuinua tabia yake mwenyewe, na kadiri anavyofanya hivi anainua na kukuza tabia za familia yake na bila kutambua kutoa ushawishi wenye nguvu kwa wengine wanaomzunguka. - *Good Health*, Juni, 1880. **{WM 160.1}**

Kujifunza Kuwafikia Wanawake Wengine na Ukweli. - Wanawake wanaweza kujifunza kile kinachohitajika

kufanywa ili kuwafikia wanawake wengine. Wapo wanawake ambao wamejirekebisha hasa kwa ajili ya kufaa kwa kazi ya kutoa masomo ya Biblia, na wamefanikiwa sana katika kuliwasilisha Neno la Mungu kwa usahili wake kwa wengine. Hawa wanakuwa baraka kubwa katika kuwafikia akina mama na binti zao. Hii ni kazi takatifu, na wale wanaojihusisha nayo wanapaswa kuungwa mkono. - *Letter* 108, 1910. **{WM 160.2}**

Wajibu wa Kukusanya Miganda. - Hebu kila dada anayekiri kuwa mtoto wa Mungu ajisikie kuwa na wajibu wa kuwasaidia wote walio karibu yake. Mafanikio bora kabisa yanaweza kupatikana kupitia katika kujikana kwa vitendo na ukarimu kwa faida ya wengine. Akina dada, Mungu anawaita

mpate kufanya kazi katika shamba la mavuno na kusaidia katika kukusanya miganda na kuyaleta ghalani.... Katika mielekeo mbalimbali ya kazi ya umisionari wa nyumbani mwanamke wa kawaida, mwenye akili anaweza kutumia nguvu zake kwa manufaa ya juu kabisa. - *The Review and Herald*, Desemba 10, 1914.**{WM 160.3}**

Ushawishi katika Upande wa Matengenezo na Ukweli. - Kwa nini wanawake wasikuze akili? Kwa nini wasijibu kusudi la Mungu katika kuwepo kwao? Kwa nini hawawezi kuelewa nguvu zao wenyewe, na kwa kutambua kwamba nguvu hizi zimetolewa na Mungu, wajitahidi kuzitumia kwa ukamilifu kabisa katika kuwatendea wengine mema, katika kuendeleza kazi ya matengenezo, ya

Ukweli, na ya wema halisi ulimwenguni? Shetani anajua kwamba wanawake wana nguvu ya ushawishi kwa ajili ya mema au kwa ajili ya mabaya; kwa hiyo anajitahidi katika kuwaandikisha katika kazi yake. Anabuni mitindo mingi, na kuwajaribu wanawake wa siku hizi, kama alivyomfanya Hawa kuchuma na kula, kuchukua na kutumia mitindo hii inayobadilika daima, isiyoridhisha kamwe. **{WM 161.1}**

Akina dada na akina mama, tuna lengo la juu zaidi, kazi nzuri zaidi, kuliko kutafuta mtindo wa kisasa kabisa na kutengeneza mavazi na mapambo ya kutarizi na sindano kwa ubatili ili kuridhisha matakwa ya kiwango cha Moleki wa kisasa. Tunaweza kuwa watumwa wake, na kutoa juu ya madhabahu yake kuwa kafara sisi

wenyewe na furaha ya sasa na ya baadaye ya watoto wetu. Lakini tunapata faida gani mwishowe? Tumepanda katika mwili; tutavuna uharibifu. Kazi zetu haziwezi kustahimili ukaguzi wa Mungu. Tutaona hatimaye ni roho ngapi ambazo zingeweza kubarikiwa na kukombolewa kutoka katika giza na makosa kwa ushawishi wetu ambao, badala yake, uliwatia moyo kuwa na kiburi na maonesho ya nje kwa kupuuza mapambo ya ndani. - *Good Health*, Juni, 1880. **{WM 161.2}**

Kuweka Chachu ya Neno la Mungu katika Makazi ya Watu. - Wanawake pamoja na wanaume wanaweza kushiriki katika kazi ya kuuficha Ukweli pale ambapo unaweza kufanya kazi na kudhihirishwa.... Wanawake hawa wenye busara na

wanyenyekevu wanaweza kufanya kazi nzuri katika kuelezea Ukweli kwa watu katika nyumba zao. Neno la Mungu lililoelezwa kwa jinsi hiyo litaanza kazi yake ya kuchachua, na kupitia mvuto wake familia nzima zitaongolewa kuufuata Ukweli. — *Letter* 86, 1907. **{WM 161.3}**

Usichoke Katika Huduma ya Umisionari. - Dada zangu, msichoke katika usambazaji wa machapisho yetu. Hii ni kazi ambayo wote mnaweza kujihusisha nayo kwa mafanikio kama mtakuwa mmeungana/mmeshikamana na Mungu. Kabla ya kuwaendea marafiki na majirani zako au kuandika barua za kutafuta habari, inua moyo kwa Mungu kwa maombi. Wote ambao kwa moyo wa unyenyekevu wanashiriki katika kazi hii watakuwa wakijielimisha

kama wafanyakazi wanaokubalika katika shamba la mizabibu la Bwana. - *The Review and Herald*, Desemba 10, 1914. **{WM 162.1}**

Wanawake Wanaweza Kuifikia Mioyo. - Kwa hawa marafiki zetu ambao wanatarajia hivi karibuni kutoka kwetu kwenda katika nchi nyingine napenda kusema: "Kumbuka kwamba unaweza kuvunja upinzani mkali kabisa kwa kuwa na shauku binafsi kwa watu ambao unakutana nao. Kristo alikuwa na upendo binafsi kwa wanaume na wanawake wakati alipokuwa akiishi hapa duniani. Popote Alipokwenda Alikuwa mmishonari wa tiba. Sisi tunapaswa kwenda huku na kule tukifanya mema, kama vile alivyofanya. Tunaagizwa kuwalisha wenye njaa,

kuwavika walio uchi, na kuwafariji wenye huzuni." **{WM 162.2}**

Akina dada wanaweza kufanya mengi kufikia moyo na kuufanya kuwa laini. Popote mlipo, dada zangu, fanyeni kazi kwa usahili. Ikiwa uko katika nyumba ambamo kuna watoto, onesha kuvutiwa nao. Hebu na waone kuwa unawapenda. Ikiwa mtu ni mgonjwa, jitolee kumpa matibabu rahisi au msaada wa huduma ya kwanza; msaidie mama aliyechoka, mwenye wasiwasi apate kumfariji mtoto wake anayeteseka. - *The Review and Herald*, Novemba 11, 1902. **{WM 162.3}**

Kuungana na Wanawake Wengine Katika Kazi ya Kiasi. - Umoja wa Wanawake wa Kiasi cha Kikristo [*The Woman's Christian*

Temperance Union] ni shirika ambalo juhudi zake za kueneza kanuni za kiasi tunaweza kuungana nazo kwa nia njema. Nimepewa nuru kwamba hatupaswi kusimama mbali nao bila ya kuonyesha shauku, bali, wakati ambapo hakuna kanuni yoyote kwa upande wetu tunayopaswa kuiacha kwa makusudi, kadiri iwezekanavyo inabidi kuungana nao katika kufanya kazi kwa ajili ya matengenezo ya kiasi.... Tunapaswa kufanya kazi pamoja nao pale tunapoweza, na tunaweza kufanya hivi kwa hakika juu ya suala hili la kiasi, na hatimaye kile chumba kikubwa cha baa wanachouzia pombe kifungwe. **{WM 162.4}**

Kadiri wakala wa kibinadamu anapotiisha mapenzi yake kwa mapenzi ya Mungu, Roho Mtakatifu ataweka

mvuto juu ya mioyo ya wale anaowahudumia. Nimeoneshwa kuwa hatupaswi kuwaepuka wafanyakazi wa U.W.K.K. Kwa kuungana nao kwa ajili ya kuwa na kiasi kabisa juu ya kula na kunywa, hatubadili msimamo wetu kuhusu utunzaji wa siku ya saba, na tunaweza kuonesha kupendezwa kwetu na msimamo wao kuhusu mada ya kiasi. Kwa kufungua mlango na kuwaalika wapate kuungana nasi juu ya suala la kiasi tunapata msaada wao katika mielekeo ya kiasi; na wao, kwa kuungana nasi, watausikia Ukweli mpya ambao Roho Mtakatifu anasubiri kuutia mioyoni. - *The Review and Herald*, Juni 18, 1908. **{WM 163.1}**

Kushangazwa na Kutokujali Kwetu. - Nimewahi kuwa na fursa ya kuona manufaa makubwa

yatakayopatikana kwa kuunganika na wafanyakazi wa U.W.K.K., nami nimeshangazwa sana kadiri ambavyo nimeona kutokujali kwa viongozi wetu wengi kwa shirika hili. Ninatoa wito kwa ndugu zangu wapate kuamka. - *Letter* 274, 1907. **{WM 163.2}**

Tambua Mema Yanayotendwa na U.W.K.K. **-**Nuru imetolewa kwangu kwamba kuna wale wenye vipaji vya thamani sana na uwezo katika U.W.K.K. Muda mwingi na fedha vimefyonzwa miongoni mwetu kwa namna ambazo hazileti faida yoyote. Badala ya hili, baadhi ya talanta zetu bora zinapaswa kuwekwa kazini katika U.W.K.K., si kama wainjilisti, bali kama wale ambao wanathamini kabisa mema ambayo yamefanywa na shirika hili. Tunapaswa kujitahidi kupata imani ya wafanyakazi

walioko katika U.W.K.K. kwa kufanya upatanifu pamoja nao kadiri iwezekanavyo…. Watu hawa wamesheheni matendo mema. - *Manuscript* 91, 1907. **{WM 163.3}**

Mvuto Wenye Nguvu - Ushauri kwa Dada Fulani. - Ninatumai, dada yangu, kwamba utakuwa na ushawishi katika Umoja wa Kiasi wa Wanawake Wakristo. … Pata mafuta ya neema katika mvuto unaotambulika na usiotambulika wa maneno yanayosemwa, ukidhihirisha ukweli kwamba unayo nuru ya maisha ya kuangazwa kwa wengine kwa ushuhuda wa moja kwa moja, ulio chanya juu ya mada ambazo wote mnaweza kukubaliana, na hili litaacha mvuto wenye nguvu. Moyo wangu uko pamoja na moyo wako katika kazi hii ya kiasi.

Ninazungumza juu ya mada hii kwa uthabiti mno, nayo ina mvuto thabiti katika akili za wengine. - *Manuscript* 74, 1898. **{WM 164.1}**

Kufanya Kazi ya Umisionari Bila Kupuuza Wajibu wa Nyumbani. - Wanawake wa Kikristo wenye akili wanaweza kutumia talanta zao kwa manufaa ya juu kabisa. Wanaweza kuonesha kwa maisha yao ya kujikana na kwa nia yao ya kufanya kazi kwa uwezo wao wote kwamba wanauamini Ukweli na wanatakaswa kupitia kwa huo. Wengi wanahitaji kazi ya aina hii ili wapate kukuza uwezo walionao. Wake na akina mama hawapaswi kwa namna yoyote kuwapuuza waume zao na watoto wao, lakini wanaweza kufanya mengi bila kupuuza wajibu wa nyumbani, na si

wote walio na majukumu haya. **{WM 164.2}**

Ni akina nani wanaweza kuwa na upendo wa kina kwa roho za wanaume na wanawake ambao Kristo alikufa kwa ajili yao kama wale wanaoshiriki neema Yake? Ni akina nani wanaweza kuiwakilisha vizuri dini ya Kristo kuliko wanawake Wakristo, wanawake ambao wanafanya kazi kwa dhati na bidii kuleta roho katika nuru ya Ukweli? Nani mwingine ambaye amejirekebisha ili aendane vyema katika kufaa kwa kazi ya shule ya Sabato? Mama wa kweli ndiye mwalimu wa kweli, wa watoto. Ikiwa kwa moyo uliojaa upendo wa Kristo, anawafundisha watoto wa darasa lake, akiomba pamoja nao na kwa ajili yao, anaweza kuona roho zikiongoka na kukusanywa katika zizi la Kristo.

Sipendekezi kwamba mwanamke lazima ajitahidi kuwa mpiga kura au mmiliki wa ofisi; bali kama mmishonari, akifundisha Ukweli kwa njia ya barua, akisambaza masomo ya kujifunza, akizungumza na familia na kuomba na akina mama na watoto, anaweza kufanya mengi na kuwa baraka. - *The Signs of the Times*, Septemba 16, 1886. **{WM 164.3}**

Wanawake Hawana Udhuru kwa Sababu ya Mzigo wa Nyumbani. - Baadhi wanaweza kufanya zaidi ya wengine, lakini wote wanaweza kufanya kitu. Wanawake hawapaswi kuhisi kwamba wanasamehewa kwa sababu ya mzigo wa nyumbani. Wanapaswa kuwa na akili juu ya jinsi gani wanaweza kufanya kazi kwa mafanikio zaidi na kwa utaratibu

katika kuleta roho kwa Kristo. Kama wote wangetambua umuhimu wa kutenda kazi ya Mungu kwa uwezo wao wote, wakiwa na upendo wa kina kwa ajili ya roho, wakihisi mzigo wa kazi juu yao, mamia wangejihusisha kama wafanyakazi wachapakazi ambao hadi sasa ni goigoi na wasiovutiwa, wasiofanikisha chochote, au wenye kutimiza kidogo sana. **{WM 165.1}**

Katika hali nyingi takataka za ulimwengu zimefunga njia za kuingia rohoni. Ubinafsi hutawala akili na kupotosha tabia. Kama maisha yangekuwa yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu, utumishi Wake usingekuwa kazi ngumu ya kuchosha. Ikiwa moyo wote ungewekwa wakfu kwa Mungu, wote wangepata kitu cha kufanya na wangetamani kushiriki

katika kazi hiyo. Wangepanda kando ya maji mengi, wakiomba na kuamini kwamba matunda yangeonekana. Watenda kazi kwa matendo, wanaomcha Mungu watakua kuelekea juu, wakiomba kwa imani kwa ajili ya neema na hekima ya mbinguni ili waweze kufanya kazi waliyokabidhiwa kwa uchangamfu na akili iliyo tayari. Watatafuta miale ya nuru ya Bwana ili wapate kuangaza njia za wengine. *Kitabu kile kile* **{WM 165.2}**

Azimio Zuri, Lenye Kutengeneza Tabia. - Hebu kila mshiriki mmoja mmoja wa kanisa ajiulize, "Je! Ninaweza kuchukua nafasi gani ili niweze kuongoa roho kwa ajili ya Yesu Kristo?" "Nitafanya vile," linasema tabaka moja, "nitajilinda mwenyewe kiasi kwamba mahitaji yangu

yatawekewa mipaka kiasi kwamba hakuna pambo hata moja lisilohitajika litakaloiba senti na mashilingi ili kukidhi kiburi au kujionesha. Nitajiweka wakfu kwa Mungu, na hamu yangu ya kujifurahisha kwa ubinafsi itauawa kabla ya kuchipuka na kuchanua na kuzaa matunda.” Hili ni azimio zuri. Litampendeza Mwokozi aliyekununua.... **{WM 166.1}**

Mtu anaweza kusema, "Sina fursa ya kupata pesa, lakini nitajitenga mwenyewe. Nitajielimisha na kujifunza kiasi kwamba hakuna fursa yoyote itakayoruhusiwa kupita bila kutumiwa vizuri. Daima nimejishughulisha, lakini hata hivyo sijahisi kuridhika kwa jinsi ambavyo muda wangu umechukuliwa. Ninaona sasa kama ambavyo kamwe sijawahi kuona kwamba muda wangu

mwingi sana umetumika katika kufanya si kitu chochote isipokuwa mambo yale ambayo yalinipendeza mimi mwenyewe. Sasa ninatamani kumpendeza Mungu, nami nitatoa sehemu ya muda wangu katika kufanya utumishi halisi kwa Bwana. Nitawatembelea wagonjwa, nitajifundisha mwenyewe kuwa na shauku na huruma kwa wale wanaoteseka, na nitaongeza fadhila kadhaa ikiwezekana ili kuwafanya wawe na raha zaidi. Kwa kupitia njia hii ninaweza kufikia mioyo yao na kusema neno kama mtumishi wa Yesu Kristo. Kwa jinsi hiyo ninaweza kukuza sanaa ya kuhudumu/huduma, na kuweza kuongoa roho kwa Yesu.” Je! Huoni kwamba Yesu atasema, "Vema" kwa mwelekeo huu wa huduma? ” - *Letter* 12, 1892. **{WM 166.2}**

Sehemu ya VII Maskini

Wazo la Thamani

Mkristo wa kweli ni rafiki wa mtu maskini. Anashughulika na ndugu yake aliyefadhaishwa na mwenye bahati mbaya kama vile ambavyo mtu angeshughulikia na mmea dhaifu, nyeti, mwororo, laini, na ulio mwepesi kudhurika. Mungu anataka wafanyakazi Wake watembee miongoni mwa wagonjwa na wanaoteseka kama wajumbe wa upendo na huruma Yake. Yeye anatutazama, ili kuona jinsi

tunavyotendeana kila mtu na mwenzake, ikiwa sisi ni kama Kristo katika kushughulika kwetu na wote, walio juu au wa chini, tajiri au maskini, huru au mfungwa.... **{WM 168.1}**

Na mnapowakuta waliochoka kwa dhiki na uonevu, wasiojua ni wapi pa kugeukia ili kupata msaada, wekeni mioyo yenu katika kazi ya kuwasaidia. Si kusudi la Mungu kwamba watoto Wake watajifungia wenyewe, bila kujali ustawi wa wale wasio na hali nzuri kama wao. Kumbuka kwamba kwa ajili yao na kama ilivyo kwa ajili yako Kristo alikufa. Upatanisho na fadhili zitakufungulia njia ya kuwasaidia, kupata imani yao kwako, kuwatia moyo kwa tumaini na ujasiri. - *Letter* 30, 1887. **{WM 168.2}**

Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini?

Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake. Yakobo 2:15-17

Sura ya ya Ishirini – Huduma kwa Maskini

Injili Katika Uzuri Wake wa Kupendeza Sana. - Kwa maskini injili inapaswa kuhubiriwa. Injili haijawahi kamwe kuweka sura ya uzuri zaidi kuliko wakati inapoletwa katika maeneo yenye uhitaji na umaskini kabisa. Kwa watu wa kila hali ya maisha, injili inatoa maagizo yake, ambayo yanarekebisha wajibu wao, na ahadi Zake, ambazo huwapa ujasiri wa kutekeleza wajibu wao. Hapo ndipo nuru ya injili inapoangaza kwa udhahiri wake unaong'aa mno na kwa uwezo wake mkubwa kabisa. Ukweli kutoka katika

Neno la Mungu huingia kwenye kibanda kibovu cha mkulima na kutia nuru nyumba ndogo za kimasikini na hovyo zilizoko mashambani, za watu weusi na weupe. Miale kutoka kwa Jua la Haki huleta furaha kwa wagonjwa na wanaoteseka. Malaika wa Mungu wapo pale, na imani sahili inayooneshwa hufanya gamba la mkate na kikombe cha maji kuwa karamu ya anasa. Wale ambao wamechukiwa kabisa na kutelekezwa, wanainuliwa kwa njia ya imani na msamaha kufikia hadhi ya kuwa wana na binti za Mungu. Wakiwa wameinuliwa juu ya ulimwengu, wanakaa katika ulimwengu wa roho ndani ya Kristo Yesu. Hawa hawana hazina ya kidunia, lakini wameipata lulu ya thamani kubwa. Mwokozi anayesamehe dhambi anawapokea

maskini na wasiojua/wajinga, na kuwapatia mkate unaoshuka kutoka mbinguni kuwa chakula chao. Wanakunywa maji ya uzima. - *Letter* 113, 1901. **{WM 169.1}**

Yesu Alishirikiana na Maskini. - Imekuwa ni mtindo wa kisasa kuwadharau maskini.... Lakini Yesu, Bwana, alikuwa ni maskini, na Yeye anawahurumia maskini, waliotupwa, na walioonewa, Naye anatangaza kwamba kila tusi linalooneshwa kwao ni kana kwamba limeoneshwa Kwake Mwenyewe. Ninashangaa zaidi na zaidi ninapoona wale wanaokiri kuwa watoto wa Mungu wakiwa nao kidogo sana huruma, upole, na upendo uliomsukuma Kristo. Laiti kama kila kanisa, Kaskazini na Kusini, lingejawa na roho ya

mafundisho ya Bwana wetu! ” - *Manuscript* 6, 1891. **{WM 170.1}**

Kristo Alikuja Kuwahudumia Maskini. - Kristo Ndiye kichwa cha ubinadamu, Naye alisimama katika vazi la ubinadamu. Mtazamo Wake ulijawa na huruma na upendo kiasi kwamba maskini kabisa hawakuogopa kuja Kwake. Alikuwa mwema kwa wote, akikaribiwa kwa urahisi na watu wa hali ya chini. Alikwenda nyumba kwa nyumba, akiwaponya wagonjwa, akiwalisha wenye njaa, akiwafariji wanaoomboleza, akiwatuliza wanaoteseka, akiongea amani kwa wenye huzuni. — *Letter* 117, 1903. **{WM 170.2}**

“Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika

sinagogi kama ilivyokuwa desturi Yake, akasimama ili asome. Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa, Roho wa Bwana yu juu Yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.” **{WM 170.3}**

Haya ni maelezo ya ajabu ya kazi ya Kristo. Mafarisayo na Masadukayo waliwadharau maskini. Wenye elimu na matajiri waliwapuuza, kana kwamba utajiri na maarifa yao yaliwafanya kuwa na thamani zaidi ya wale ambao walikuwa maskini. Lakini Yesu alitangaza kwamba ilikuwa ni kazi Yake kutia moyo na kutoa faraja na msaada

mahali vilipohitajika zaidi. - *Manuscript* 65b, 1898. **{WM 171.1}**

Jinsi Kristo Alivyoamsha Njaa ya Roho. - Kazi kuu ya Kristo ilikuwa ni kuhubiri injili kwa maskini. Yeye Alichagua kuwahudumia maskini, wasiojua/wajinga. Kwa usahili alifungua mbele yao baraka ambazo wangeweza kuzipokea, na hivyo aliamsha njaa ya roho zao kwa ajili ya Ukweli, yaani ule mkate wa uzima. Maisha ya Kristo ni mfano kwa wafuasi Wake wote. - *Manuscript* 103, 1906. **{WM 171.2}**

Ushahidi wa Uungu wa Injili. - Kristo alikutana na mafanikio makubwa zaidi miongoni mwa maskini, na kwa tabaka hili kila mwanadamu, awe msomi au si msomi, anaweza kupata mengi ya kufanya. Maskini wanahitaji

faraja na huruma, kwani kuna wale ambao bila mkono wa msaada hawataweza kupata nafuu wenyewe. Kwa kufanya kazi kwa ajili ya hawa wanafunzi wa Kristo watatimiza utume wao. Hii ndio sifa ya juu kabisa ya huduma ya injili. Kama injili ingekuwa ni ya wanadamu, ingependwa na kuwa mashuhuri miongoni mwa matajiri na wenye nguvu; lakini inamimina dharau kwa matajiri na wenye nguvu, na inawataka wote wanaoikubali kufanya kazi za Kristo, kuwasaidia wale walio mafukara, waliodharauliwa, waliotelekezwa, wanaoteseka. **{WM 171.3}**

Wale wanaoshikilia kazi kwa sababu ya upendo kwa Kristo na upendo kwa roho za watu watafanya kazi katika mielekeo ya Kristo. Ulimwengu huu ni

nyumba ya maskini wenye ugonjwa wa maambukizo kama Ukoma, lakini Kristo alikuja kuwaponya wagonjwa, kuwafariji waliovunjika moyo, kutangaza ukombozi kwa mateka, kuwapa kuona walio vipofu. Injili ndio kiini hasa cha uponyaji, na Kristo angetaka tuwaambie waliovunjika moyo, wasio na tumaini, wenye dhiki, wazishike nguvu Zake; kwa kuwa mwaka wa Bwana uliokubalika umekuja. — *Manuscript* 65b, 1898. **{WM 171.4}**

Ukristo Faraja ya Maskini. - Kuna uhusiano kati ya dini ya Kristo na umaskini. Ukristo ni faraja ya maskini. Kuna dini ya uongo, inayohatarisha roho za wote wanaoiendeleza, ambayo inafundisha kwamba anasa na raha za ubinafsi ndio jumla ya furaha. Lakini mfano wa yule tajiri na Lazaro

unatuonesha kwamba huu ni uongo. Ilifika wakati ambapo yule tajiri angetoa vyote alivyokuwa navyo ili kubadilishana mahali na Lazaro, ambaye hapo awali alikuwa ni maskini, aliyefunikwa na vidonda. **{WM 172.1}**

Katika ubinadamu wa Kristo kuna nyuzi za dhahabu ambazo zinamfunga maskini anayemwamini, anayemtumaini katika roho Yake Mwenyewe yenye upendo usio na kikomo. Yeye Ndiye Tabibu Mkuu. Katika ulimwengu wetu alichukua udhaifu wetu na kubeba mizigo yetu. Yeye Ndiye Mponyaji Mkuu wa magonjwa yote. Alikuwa maskini, lakini bado alikuwa Ndiye kitovu cha wema wote, baraka zote. Yeye ni hazina/ghala ya nguvu kwa wote kuweka wakfu nguvu zao kwa ajili ya kazi ya

kufanyika kuwa wana wa Mungu. — *Manuscript* 22, 1898.**{WM 172.2}**

Kristo Aliondoa Unyanyapaa Kutoka kwa Umaskini. - Kristo daima amekuwa ni rafiki wa mtu maskini. Alichagua umaskini na kuuheshimu kwa kuufanya kuwa fungu Lake. Amevua milele aibu ya dharau kutoka Kwake kwa kuwabariki maskini, ambao ni warithi wa ufalme wa Mungu. Kazi kama hiyo ndio iliyokuwa kazi Yake. Kwa kujiweka wakfu kwa ajili ya maisha ya umaskini, aliukomboa umaskini kutoka katika aibu Yake. Alichagua kuwa pamoja na maskini ili apate kuondoa kutoka katika umaskini alama zile za aibu ambazo ulimwengu ulikuwa umeambatanisha Kwake. Alijua hatari ya upendo wa mali. Alijua kwamba upendo huu ni wenye kuharibu

kwa roho nyingi. Unawaweka wale ambao ni matajiri mahali ambapo wanaendekeza kila matamanio ya ukuu. Unawafundisha kuwatazama kwa dharau wale wanaoteseka kwa shinikizo la umaskini. Unakuza udhaifu wa akili za wanadamu na kuonesha kwamba, licha ya mali tele, walio matajiri si matajiri kwa Mungu. **{WM 172.3}**

Tabia za wengi zimekalibiwa na makadirio yasiyo sahihi yanayowekwa juu ya matajiri wa ulimwengu huu. Mtu aliyepagawa na nyumba na mashamba, anayesifiwa na kudanganywa na heshima anayopewa, anaweza kumtazama kwa dharau mtu maskini, ambaye ana fadhila ambazo mtu tajiri hana. Wanapopimwa katika mizani ya dhahabu ya Patakatifu, tajiri mbinafsi, mwenye tamaa atakutwa amepungua,

wakati mtu yule maskini, ambaye kwa imani amemtegemea Mungu peke Yake kwa ajili ya wema na fadhili Zake, atatangazwa kuwa mrithi wa utajiri wa milele katika ufalme wa Mungu. — *Manuscript* 22, 1898.**{WM 173.1}**

Watu Mashuhuri wa Dunia Hawawezi Kulitatua Tatizo Hili. - Katika miji mikubwa kuna watu wengi wanaoishi katika umaskini na unyonge, karibu na kukosa chakula, makazi, na mavazi; wakati katika miji hiyo hiyo kuna wale ambao wana zaidi ya kile moyo ungeweza kutamani, ambao wanaishi kwa anasa, wakitumia pesa zao kwa ajili ya nyumba zilizo na samani nyingi (luxury), kwa ajili ya mapambo binafsi, au mbaya zaidi, kwa ajili ya kuridhisha hamu ya kimwili, kwa ajili ya

pombe, tumbaku, na vitu vingine vinavyoharibu uwezo wa ubongo, kuchanganya akili, na kushusha thamani ya roho. Vilio vya wanadamu wenye njaa vinakuja mbele za Mungu.... **{WM 173.2}**

Si wengi, hata miongoni mwa waelimishaji na watawala, ambao wanaelewa sababu ambazo ni msingi kwa hali ya sasa ya jamii. Wale ambao wanashikilia hatamu za serikali hawawezi kutatua tatizo la ufisadi wa kimaadili, umaskini, ufukara, na kuongezeka kwa uhalifu. Wanajitahidi bure kuweka shughuli za biashara katika msingi ulio salama zaidi. Kama watu wangezingatia zaidi mafundisho ya Neno la Mungu, basiwangepata suluhisho la shida zinazowakanganya/zinazowafadhaisha.

— *Testimonies for the Church* 9:12, 13. **{WM 173.3}**

Mpango wa Mungu kwa Israeli wa Kuondoa Kutokuwa Sawa. - Ilipaswa kutiwa katika akili za wote kwamba maskini wana haki ya kupata nafasi katika ulimwengu wa Mungu kama walivyo wale walio matajiri zaidi. Hayo ndio yaliyokuwa masharti yaliyotolewa na Muumbaji wetu Mwenye huruma, kwa ajili ya kupunguza mateso, kuleta matumaini, kumulika mng'ao wa uchangamfu, katika maisha ya maskini na wenye huzuni. **{WM 174.1}**

Bwana angeweka udhibiti kwa upendo usio na mipaka wa mali na uwezo. Maovu makubwa yangetokana na kuendelea kujilimbikizia mali kwa tabaka moja na umaskini na udhilifu

kwa lingine. Bila kizuizi fulani uwezo wa matajiri ungekuwa ukiritimba, na maskini, ingawa kwa kila hali wanastahili kikamilifu machoni pa Mungu kama wao, wangechukuliwa na kutendewa kama walio duni kwa ndugu zao waliofanikiwa zaidi. Utambuzi wa uonevu huu ungeamsha hamaki za tabaka la walio maskini zaidi. Kungekuwapo na hisi ya kukata tamaa na kukosa matumaini ambayo ingekuwa na mwelekeo ambao ungeivunja moyo jamii na kufungua mlango kwa uhalifu wa kila aina. Kanuni ambazo Mungu alizianzisha zilikusudiwa kukuza usawa katika jamii. Masharti ya mwaka wa Sabato na Yubile yangeweza, kwa kipimo kikubwa, kurekebisha kile ambacho kwa kitambo kilikuwa

kimeharibika katika hali ya kijamii na kisiasa ya taifa. **{WM 174.2}**

Kanuni hizi zilikusudiwa kuwabariki matajiri si zaidi ya maskini (wote wabarikiwe). Zingezuia uchoyo na tabia ya kujikweza na zingekuza roho bora ya ukarimu; na kwa kukuza sifa njema na imani kati ya matabaka yote zingeweza kukuza utangamano wa jamii, uthabiti wa serikali. Sote tumefumwa pamoja katika mfumo mkubwa wa ubinadamu, na chochote tunachoweza kufanya kwa ajili ya kuwanufaisha na kuwainua wengine kitaakisiwa kama baraka juu yetu sisi wenyewe. Sheria ya kutegemeana hushughulikia matabaka yote ya jamii. Maskini hawawategemei zaidi matajiri kuliko matajiri wanavyowategemea maskini. Wakati tabaka moja linaomba mgao katika

baraka ambazo Mungu amewapa majirani zao matajiri, lingine linahitaji huduma ya uaminifu, nguvu ya ubongo na mifupa na misuli, ambayo ndio mtaji wa maskini…. **{WM 174.3}**

Kuna wengi ambao wanasisitiza kwa shauku kubwa kwamba watu wote wanapaswa kuwa na mgao sawa katika baraka za Mungu za dunia hii. Lakini hili halikuwa kusudi la Muumbaji. Tofauti katika hali ni mojawapo ya njia ambazo Mungu hupanga ili kuthibitisha na kukuza tabia. Lakini bado anakusudia kwamba wale ambao wana mali ya ulimwengu watajiona kama mawakili tu wa mali Yake, kama waliokabidhiwa mali inayotakiwa kutumika kwa ajili ya faida ya wanaoteseka na wahitaji. **{WM 175.1}**

Kristo amesema kwamba tutakuwa na maskini daima pamoja nasi, na anaunganisha shauku Yake na ile ya watu Wake wanaoteseka. Moyo wa Mkombozi wetu huwahurumia watoto wake walioko duniani walio maskini na wa hali ya chini kabisa. Yeye Anatuambia kwamba wao ni wawakilishi Wake duniani. Amewaweka miongoni mwetu ili kuamsha mioyoni mwetu upendo ule ambao Anauhisi kwa wanaoteseka na kuonewa. Huruma na ukarimu ulioonyeshwa kwao vinapokelewa na Kristo kana kwamba vimeonyeshwa Kwake. Kitendo cha ukatili au kupuuza kwao huchukuliwa kana kwamba kimefanywa Kwake. — *Patriarchs and Prophets*, 534-536. **{WM 175.2}**

Kristo Anaona Fursa katika Upeo wa Mateso ya Mwanadamu. - Moyo wa Kristo unachangamshwa kwa kuwaona wale ambao ni maskini katika kila maana ya neno hili; unachangamshwa kwa Yeye kuwatazama wale wanaoonewa ambao ni wapole na kwa kuwatazama wale walioinamishwa chini kwa huzuni ya kufiwa; unachangamshwa na wale wanaoonekana kutokuridhika na shauku ya kutafuta haki, na kutokuwa na uwezo wa kuanza kwa wengi. Hupokea, kana kwamba ilikuwa, ni hali halisi hasa ya mambo ambayo ingeweza kuwavunja moyo wachungaji wengi. Anaona fursa ya kuwasaidia wale ambao wanahitaji sana msaada kwa kukutana nao mahali pale walipo. **{WM 175.3}**

Bwana Yesu anasahihisha uchaji wetu wa makosa, akitoa mzigo wa kazi hii kwa ajili ya maskini na wahitaji walio katika maeneo yenye shida kwa wanaume na wanawake walio wepesi kubadilika kufuatana na mazingira ambao wana mioyo ambayo inaweza kuwahurumia wale wasiojua na wale ambao wako nje ya njia. Bwana anawafundisha jinsi ya kukabiliana na hali hizi. Wafanyakazi hawa watatiwa moyo waonapo milango ikifunguliwa kwa ajili ya wao kuingia mahali ambapo wanaweza kufanya kazi ya umisionari wa tiba. Wakiwa na ujasiri binafsi kidogo tu, wanampa Mungu utukufu wote, bila kuchukua hata kidogo katika huo kwa ajili yao wenyewe. Mwokozi Yupo ili kusaidia kufanya mwanzo kupitia kwa wale ambao mikono yao ni

ghafi na isiyo na ujuzi, lakini ambao mioyo yao ni miepesi kuhisi huruma na huamshwa kufanya kitu fulani ili kupunguza shida zilizo nyingi mno. Yeye Anafanya kazi kupitia kwa wale wanaoweza kutambua rehema katika taabu, faida katika upotevu wa vitu vyote. Nuru ya ulimwengu inapopita, faida kubwa huonekana katika shida zote, uadilifu na utaratibu katika machafuko, mafanikio na hekima ya Mungu katika kile ambacho kilionekana kushindwa katika uzoefu wa mwanadamu.... **{WM 176.1}**

Kristo hutamka baraka Yake juu ya wale ambao wana njaa na kiu ya haki. Katika Luka tunasoma, "Heri ninyi mlio maskini." Maskini hawana hata sehemu moja katika elfu ya majaribu yadanganyayo ya matajiri. Katika

Mathayo tunasoma, “Heri walio maskini wa roho, maana ufalme wa mbinguni ni wao.” Umaskini wa roho unaashiria utajiri utakaotolewa na utajiri wa neema ya Mungu. - *Letter* 100, 1902. **{WM 176.2}**

Kama Umaskini Ungeondolewa Duniani. – Uhitaji na umaskini vitakuwepo daima. Hata kama kiwango cha maarifa na maadili kitakuwa juu kiasi gani, kimo chochote tunachoweza kukifikia katika ustaarabu, umaskini utaendelea siku zote, kama onesho la utajiri wa neema ya Mungu, kumbukizi la kudumu kwa Ukweli wa maneno, "Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho Yangu, asema Bwana wa majeshi." Haitakuwa kwa faida ya Ukristo kwa Bwana kuondoa umaskini duniani. Hivyo mlango ungefungwa

ambao sasa uko wazi kwa ajili ya utekelezaji wa imani - njia ambayo kwayo mioyo ya wanaoteseka inaweza kufikiwa na injili ya wema. Kwa ukarimu wa Kikristo roho zinafikiwa ambazo zisingeweza kufikiwa kwa njia nyingine yoyote ile. Ni mkono wa msaada wa injili. - *Letter* 83, 1902. **{WM 177.1}**

Sura ya Ishirini na Moja - Maskini Waliomo Kanisani

Wahitaji wa Jamaa ya Waaminio. - Upendo wetu kwa Mungu unapaswa kuoneshwa katika kuwatendea mema wahitaji na

wanaoteseka walio katika jamaa ya waaminio ambao shida zao huja katika utambuzi wetu na kuhitaji kujali kwetu. Kila roho iko chini ya masharti ya pekee kwa Mungu kuwaweka maanani maskini wake wanaostahili kwa huruma ya pekee. Kwa vyovyote vile hakuna sababu ya kuzipita roho hizi. - *Testimonies for the Church* 6:271. **{WM 178.1}**

"Kwa hiyo, kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio." **{WM 178.2}**

Kwa namna ya pekee Kristo ameweka juu ya kanisa Lake jukumu la kuwatunza wahitaji walio miongoni mwa washiriki wake. Anaruhusu maskini wake kuwapo katika mipaka ya kila kanisa. Daima wanapaswa kuwamo miongoni mwetu, na Yeye ameweka juu

ya washiriki wa kanisa wajibu binafsi wa kuwatunza. **{WM 178.3}**

Kama vile washiriki wa familia halisi wanavyotunzana, wakiwahudumia wagonjwa, wakiwasaidia walio dhaifu, wakiwafundisha wasiojua, wakiwafunza wasio na uzoefu, ndivyo ambavyo "jamaa ya waaminio" wanapaswa kuwajali wahitaji na wasiojiweza. - *The Ministry of Healing*, 201. **{WM 178.4}**

Matabaka Mawili ya Kutunzwa. - Kuna matabaka mawili ya maskini ambao daima tunao ndani ya mipaka yetu - wale ambao wanajiharibu wenyewe kwa sababu ya mielekeo yao huru ya matendo na kudumu katika makosa yao, na wale ambao kwa ajili ya ile Kweli wameletwa katika hali ngumu. Tunapaswa kumpenda jirani yetu kama

nafsi yetu wenyewe, na kisha kwa matabaka haya yote mawili tutafanya jambo sahihi chini ya uongozi na ushauri wa busara. **{WM 178.5}**

Hakuna swali kuhusiana na maskini wa Bwana. Inabidi wasaidiwe katika kila hali ambayo itakuwa ni faida kwao. Mungu anataka watu Wake kuudhihirishia ulimwengu wenye dhambi kwamba hajawaacha waangamie. Jitihada za pekee zinapaswa kufanywa ili kuwasaidia wale ambao kwa ajili ya Ukweli wamefukuzwa nyumbani kwao na kulazimika kuteseka. Zaidi na zaidi kutakuwa na haja ya mioyo yenye huruma, iliyo wazi, yenye ukarimu, wale ambao wataikana nafsi na watashikilia hali za hawa ambao Bwana anawapenda. Maskini miongoni mwa watu wa Mungu hawapaswi

kuachwa bila riziki kwa ajili ya mahitaji yao. Njia fulani lazima ipatikane ambayo kwayo wanaweza kupata riziki. Baadhi watahitajika kufundishwa kufanya kazi. Wengine ambao wanafanya kazi kwa bidii, na wanasumbuka kwa uwezo wao wote ili wapate kuzisaidia familia zao, watahitaji msaada wa pekee. Tunapaswa kuwa na shauku katika hali hizi na kuwasaidia kupata kazi. Kunapaswa kuwepo na mfuko wa kusaidia familia maskini kama hizo zinazostahili ambazo zinampenda Mungu na kuzishika amri Zake. **{WM 179.1}**

Uangalifu lazima uchukuliwe kwamba fedha zinazohitajika kwa ajili ya kazi hii hazitachepushwa kwenda katika njia zingine. Inaleta tofauti kama tukiwasaidia maskini ambao kwa kushika amri za Mungu wanalazimishwa

kuwa na uhitaji na mateso, au kama tunawapuuza hawa ili kuwasaidia wenye kukufuru ambao wanazikanyaga chini ya miguu yao amri za Mungu. Na Mungu anaiheshimu tofauti hiyo. Watunzao Sabato hawapaswi kuwapita kando wale watesekao, wahitaji walio wa Bwana, ili kuchukua juu yao mzigo wa kuwasaidia wale wanaodumu katika uhalifu wa sheria ya Mungu, wale ambao wameelimika kutafuta msaada kwa mtu yeyote ambaye atawategemeza. Hii si aina sahihi ya kazi ya umishonari. Haipatani na mpango wa Bwana. **{WM 179.2}**

Popote kanisa linapoanzishwa washiriki wake wanapaswa kufanya kazi ya uaminifu kwa waumini wake wenye uhitaji. Lakini hawatakiwi kuachia hapa. Wanapaswa kuwasaidia na wengine pia,

bila kujali imani yao. Kama matokeo ya juhudi hizo baadhi ya hawa watapokea Kweli za pekee kwa ajili ya wakati huu. **{WM 180.1}**

"Kama akiwapo mtu maskini pamoja nawe, nduguzo mmojawapo, ndani ya malango yako mojawapo, katika nchi yako akupayo Bwana, Mungu wako, usifanye moyo wako kuwa mgumu, wala usimfumbie mkono wako nduguyo maskini; lakini mfumbulie mkono wako kwa kweli, umkopeshe kwa kweli yatoshayo haja yake katika ahitajiayo. Jitunze, msiwe na neno lisilofaa moyoni mwako, kusema, Umekaribia mwaka wa saba, mwaka wa maachilio; jicho lako likawa ovu juu ya nduguyo usimpe kitu; naye akamlilia Bwana juu yako, ikawa ni dhambi kwako. Mpe kwa kweli, wala moyo wako usisikitike utakapompa; kwa

kuwa atakubarikia Bwana, Mungu wako, kwa neno hili katika kazi yako yote, na katika kila utakalotia mkono wako. Kwa maana maskini hawatakoma katika nchi milele; ndipo ninakuamuru na kukuambia, Mfumbulie kwa kweli mkono wako nduguyo, mhitaji wako, maskini wako, katika nchi yako." Kumbukumbu la Torati 15:7-11. **{WM 180.2}**

Kupitia katika mazingira fulani, baadhi ya wale wanaompenda na kumtii Mungu wanakuwa maskini. Wengine si waangalifu; hawajui jinsi ya kusimamia. Wengine ni maskini kupitia kwa magonjwa na misiba. Haijalishi sababu, wao ni wahitaji, na kuwasaidia ni mwelekeo muhimu wa kazi ya umisionari. - *Testimonies for the Church* 6: 269-271. **{WM 180.3}**

Umaskini Unaweza Kutokana na Hali Mbaya. -Haijachukuliwa siku zote kuwa kama alama ya uzembe pale ambapo kupitia katika hali mbaya dhiki kali imefanya iwe lazima kwa ndugu kuingia katika madeni au kuteseka kwa ajili ya chakula na mavazi hata kama asingeweza kujiondoa katika madeni haya, kwa kujitahidi kadiri awezavyo. Mkono wa msaada umenyoshwa kwa watu kama hao, kuwaweka kusimama kwa miguu yao, wakiwa huru kutokana na shida, ili wapate kufanya kazi yao katika shamba la Bwana la mizabibu bila kukandamizwa na mawazo kwamba wingu la deni lilikuwa likining'inia juu yao. - *Manuscript* 34, 1894. **{WM 180.4}**

Wajibu wa Kanisa au Makanisa. - Ni wajibu wa kila kanisa kufanya

mikakati makini, na ya busara kwa ajili ya utunzaji wa maskini na wagonjwa wake. - *Letter* 169, 1901. **{WM 181.1}**

Mungu Anaruhusu maskini Wake kuwa katika mipaka ya kila kanisa. Daima wanapaswa kuwapo miongoni mwetu, na Bwana huwawekea washiriki wa kanisa wajibu binafsi wa kuwatunza. Hatupaswi kuweka wajibu wetu juu ya wengine. Kwenda kwa wale walio ndani ya mipaka yetu tunapaswa kudhihirisha upendo na huruma ile ile ambayo Kristo angedhihirisha kama angekuwa katika nafasi yetu. Hivyo tunapaswa kuwa na nidhamu, ili tuweze kuwa tayari kufanya kazi katika mielekeo ya Kristo. **{WM 181.2}**

Mchungaji anapaswa kuzielimisha familia mbalimbali na kuliimarisha

kanisa ili lipate kuwatunza wagonjwa na maskini wake. Anapaswa kuweka kazini vipaji vya watu vilivyotolewa na Mungu, na ikiwa kanisa moja linaelemewa kupita kiasi katika mwelekeo huu, makanisa mengine yanapaswa kutoa msaada kwake. Hebu washiriki wa kanisa watumie busara na ustadi katika kuwatunza hawa, watu wa Bwana. Hebu na wajinyime anasa, na mapambo yasiyo ya lazima, ili wapate kuwafanya wale wahitaji wanaoteseka kufarijika. Kwa kufanya hivi wanatekeleza maagizo yaliyotolewa katika sura ya hamsini na nane ya Isaya, na baraka zilizotamkwa pale zitakuwa zao. — *Testimonies for the Church* 6:272. **{WM 181.3}**

Kila Mshiriki wa Kanisa Kufanya Sehemu Yake. - Watu wa Bwana wanapaswa kuwa waaminifu

kabisa kwa kanuni. Yeye Ameonesha kazi iliyokabidhiwa kwa kila mshiriki wa kanisa. Anatangaza kwamba washiriki wa kanisa wanapaswa kutekeleza wajibu wao kwa uaminifu kwa wale walio ndani ya mipaka yao. Wanapaswa kwa ukarimu kuwasaidia maskini wao wenyewe. Wanapaswa kujihusisha katika kazi ya kimishonari hatua kwa hatua, wakiwafundisha watoto wao kushika njia ya Bwana na kufanya hukumu na haki. **{WM 182.1}**

Lakini nuru ambayo kwa miaka mingi imekuwa mbele ya makanisa imepuuzwa. Kazi ambayo ilipaswa kuwa imefanywa kwa ajili ya wanadamu wanaoteseka katika kila kanisa haijafanywa. Washiriki wa kanisa wameshindwa kutii Neno la Bwana, na hii imewanyima uzoefu ambao

wangepaswa kuupata katika kazi ya injili.-*The Review and Herald*, Machi 4, 1902. **{WM 182.2}**

Maskini na wahitaji wanapaswa kutunzwa. Hawa hawapaswi kupuuzwa, kwa gharama yoyote ile au kujitoa mhanga kwa upande wetu. — *The Youth's Instructor*, Agosti 26, 1897. **{WM 182.3}**

Kanisa Linapaswa Kubeba Mzigo. - Makanisa ambayo yana maskini miongoni mwao hayapaswi kupuuza uwakili wao na kutupa mzigo wa maskini na wagonjwa juu ya Sanitariamu (Kituo cha tiba rahisi). Washiriki wote wa makanisa kadhaa wanawajibika mbele za Mungu kwa ajili ya watu wao wanaoteseka. Wanapaswa kubeba mizigo yao wenyewe. Ikiwa wana

wagonjwa miongoni mwao, ambao wanataka wafaidike kwa matibabu, wanapaswa, ikiwa wanaweza, kuwapeleka katika Sanitariamu (vituo vya tiba rahisi). Kwa kufanya hivi hawatakuwa tu wakiifadhili taasisi ambayo Mungu ameianzisha bali watakuwa wakiwasaidia wale wanaohitaji msaada, wakiwatunza maskini kama Mungu anavyotaka tufanye. — *Testimonies for the Church* 4:551. **{WM 182.4}**

Maskini wa Bwana Wanapotelekezwa. – Maskini wa Bwana wanapotelekezwa na kusahauliwa au kusalimiwa kwa mwonekano wa ubaridi na maneno ya kikatili, hebu mwenye hatia akumbuke kwamba anamtelekeza Kristo katika nafsi ya watakatifu Wake. Mwokozi wetu

anafunganisha masilahi Yake na yale ya wanadamu wanaoteseka. Kama vile moyo wa mzazi unavyoona shauku kwa wema wenye huruma juu ya mmoja anayeteseka wa kundi Lake dogo, ndivyo moyo wa Mkombozi wetu unavyowahurumia watoto wake walioko duniani ambao ni maskini na wa hali ya chini kabisa. Amewaweka miongoni mwetu ili kuamsha ndani ya mioyo yetu upendo ambao Yeye anauhisi kwa wanaoteseka na kuonewa, Naye ataruhusu hukumu Zake kuangukia juu ya mtu yeyote anayewadhuru, kuwadharau, au kuwadhulumu. — *Testimonies for the Church* 4:620. **{WM 183.1}**

Tafuta Mahitaji. - Matamanio yenu (wishes!) mema tutawashukuru kwayo,

lakini maskini hawezi kuendelea kufarijika au kupata mahitaji yao kwa matamanio mema peke yake. Ni lazima wawe na ushahidi dhahiri wa wema wenu katika chakula na mavazi. Mungu hakusudii kwamba yeyote kati ya wafuasi Wake alazimike kuomba mkate. Amekupeni kwa wingi, ili mpate kuwakimu wale mahitaji yao, ambayo kwa bidii ya kazi na uwekevu hawawezi kutoa. Msiwasubiri kuvuta usikivu wenu kwa mahitaji yao. Tendeni kama Ayubu alivyofanya. Jambo ambalo hakulijua alilichunguza. Nenda kwenye ziara ya kukagua na ujifunze kinachohitajika na jinsi inavyoweza kutolewa kwa namna bora. - *Testimonies for the Church* 5:151. **{WM 183.2}**

Usisubiri Waje Kwetu. – Umaskini na dhiki katika familia

vitakuja katika ufahamu wetu, na wale walio na dhiki na wanaoteseka itabidi wasaidiwe.... Usisubiri hawa waje kwako. Chunguza mavazi yako yote uliyo nayo, kisha uwasaidie ikiwa wanahitaji msaada. Tunapaswa kuwekeza mali kwa ajili ya kuwasaidia vijana wa kiume na wa kike kupata elimu katika kupeleka injili kwa maskini, katika kuwasaidia wale ambao wamethubutu kwa imani kuchukua nafasi yao juu ya jukwaa la Ukweli wa milele, wakati ambapo kwa kufanya hivyo wamejiweka katika hali ya kujidhililisha. Pale ambapo kuna hali za uhitaji maalum, mchungaji lazima awe tayari kuwasaidia wale walio katika umaskini kwa ajili ya Ukweli. — *Manuscript* 25, 1894. **{WM 183.3}**

Msaada kwa Waongofu Wapya Ambao Hawana Ajira. - Katika kazi

yetu ya ukarimu msaada maalum unapaswa kutolewa kwa wale ambao, kupitia uwasilishaji wa Ukweli, wamesadikishwa na kuongoka. Ni lazima tuwe na utunzaji kwa wale ambao wana ujasiri wa kimaadili wa kuukubali Ukweli, ambao wanapoteza kazi zao kwa sababu hiyo, na wanakataliwa kufanya kazi ambayo kwayo wangezisaidia familia zao. Utoaji unapaswa kufanywa ili kuwasaidia maskini wanaostahili na kutoa ajira kwa wale wanaompenda Mungu na kutunza amri Zake. Hawapaswi kuachwa bila msaada, kuhisi kwamba wanalazimika kufanya kazi siku ya Sabato au kufa njaa. Wale ambao huchukua msimamo wao upande wa Bwana wanapaswa kuona ndani ya Waadventista wa Sabato watu wenye moyo mkunjufu, wenye kujikana nafsi,

wenye kujitoa, wanaowahudumia ndugu zao wenye uhitaji kwa uchangamfu na furaha. Ni kuhusu tabaka hili hasa Bwana anazungumzia pale anaposema: "Kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako." Isaya 58:7. - *Testimonies for the Church* 6: 85. **{WM 184.1}**

Kutoa Ardhi kwa Familia Maskini. - Mahali ambapo shule imeanzishwa [huko Australia] lazima kuwe na ardhi kwa ajili ya bustani ya matunda na bustani, ili wanafunzi wapate kuwa na mazoezi ya kimwili yakiunganishwa pamoja na ushughulishaji wa akili, na baadhi nusu na wengine kikamilifu hulipia kila gharama zao shuleni. Pia ardhi lazima inunuliwe, ili familia ambazo haziwezi kupata kazi katika miji kwa sababu ya

utunzaji wa Sabato ziweze kununua mashamba madogo na kujipatia riziki zao. Hili ni hitaji chanya katika nchi hii. Ni lazima elimu itolewe kuhusu kulima udongo, na ni lazima tutarajie kwamba Bwana atabariki juhudi hii. - *Manuscript* 23, 1894. **{WM 184.2}**

Wajibu Wetu kwa Familia Maskini. - Mara nyingi huulizwa Maswali kuhusu wajibu wetu kwa maskini ambao wanaupokea kwa moyo ujumbe wa malaika wa tatu; na sisi wenyewe kwa muda mrefu tumekuwa na shauku ya kutaka kujua jinsi ya kusimamia kwa busara masuala ya familia maskini ambao wanaikubali Sabato. Lakini nikiwa Roosevelt, New York, Agosti 3, 1861, nilioneshwa mambo fulani kuhusiana na maskini. **{WM 185.1}**

Mungu hataki ndugu zetu wawajibike na kila familia maskini ambayo itakubali ujumbe huu. Ikiwa watalazimika kufanya hivyo, wachungaji ni lazima wataacha kuingia katika maeneo mapya, kwa kuwa pesa zitamalizika. Wengi ni maskini kutokana na ukosefu wao wenyewe wa bidii na uwekevu; hawajui jinsi ya kutumia mali kwa usahihi. Kama watasaidiwa, watadhurika. Wengine daima watakuwa maskini. Ikiwa watapata nafasi bora kabisa, hali zao hazitasaidiwa. Hawana ukokotoaji mzuri, nao wangetumia mali zote ambazo wangeweza kupata, kama ni nyingi au kidogo. **{WM 185.2}**

Wengine hawajui chochote cha kujinyima na kubana matumizi ili waondokane na madeni na kusonga mbele kidogo kwa ajili ya wakati wa

hitaji. Ikiwa kanisa litalazimika kuwasaidia watu kama hao badala ya kuwaacha wategemee rasilimali zao wenyewe,wangewadhuriwa nao mwishowe, kwani wangeliangalia kanisa na kutarajia kupokea msaada kutoka kwao na hawaoneshi kujikana nafsi uwekevu wakati wameruzukiwa vizuri. Na ikiwa hawapati msaada kila wakati, Shetani huwajaribu, na wanakuwa na wivu na dhamira nyeti sana kwa ndugu zao, wakiogopa watashindwa kutekeleza wajibu wao wote kwao. Kosa ni kwa upande wao wenyewe. Wamedanganyika. Wao si maskini wa Bwana. **{WM 185.3}**

Maagizo yaliyotolewa katika Neno la Mungu kuhusu kuwasaidia maskini hayagusi mifano kama hiyo, bali ni kwa ajili ya wasiojiweza na wanaoteseka.

Mungu katika majaliwa Yake amewadhikisha watu mmoja mmoja ili apate kuwajaribu na kuwathibitisha wengine. Wajane na wasiojiweza wako kanisani ili kuwa baraka kwa kanisa. Wao ni sehemu ya njia ambazo Mungu amechagua ili kukuza tabia ya kweli ya wafuasi bayana wa Kristo na kuita katika utekelezaji sifa zile bainishi za thamani za tabia zilizooneshwa na Mkombozi wetu mwenye huruma. **{WM 186.1}**

Wengi ambao wanaweza kuishi lakini kwa shida kabla ya ndoa huchagua kuoa na kukuza familia wakati wanajua kuwa hawana chochote cha kuwasaidia. Na mbaya zaidi ya hili, hawana utawala wa kifamilia. Mwelekeo wao wote katika familia yao hupambanuliwa kwa tabia zao za ulegevu, na uzembe. Hawana utawala juu ya nafsi zao, na wanahamaki

kwa urahisi, hawana subira, na ni wenye kiherehere na hufadhaika au kuwa na jazba kirahisi. Wakati watu kama hawa wanapoukubali ujumbe wanahisi kuwa wanastahili msaada kutoka kwa ndugu zao walio matajiri zaidi; na ikiwa matarajio yao hayatimizwi, wanalalamika kwa kanisa na kuwashitaki kwa kutoishi kulingana na imani yao? Ni nani anayepaswa kupata hasara katika hali hii? Je ni lazima kusudi la Mungu lidhoofishwe, na hazina katika maeneo mbalimbali kumalizwa, kwa ajili ya kuzitunza familia hizi kubwa za maskini? Hapana. Wazazi lazima wawe ndio wenye kupata hasara. Hawatapungukiwa na kitu chochote kikubwa, kwa ujumla, baada ya kuikubali Sabato kuliko walivyokuwa hapo awali. **{WM 186.2}**

Kuna uovu miongoni mwa baadhi ya maskini ambao utathibitika kwa hakika kuwa uharibifu wao isipokuwa wameushinda. Wamekubali Ukweli pamoja na tabia zao rafu au zenye ujeuri, zenye fujo, zisizostaarabika, na inachukua muda kabla hawajaona na kutambua tabia zao zenye jeuri, na kwamba haikubaliani na tabia ya Kristo. Wanawaangalia wengine ambao ni wenye utaratibu na wastaarabu kama wenye majivuno/kiburi. Na unaweza kuwasikia wakisema: “Ukweli hutushusha chini wote katika usawa mmoja.” Lakini ni kosa kabisa kufikiria kwamba Ukweli unamshusha chini mpokeaji wake. Kwani Ukweli humwinua, husafisha hisia yake, hutakasa hukumu yake, na, ikiwa ataishi kulingana nao, daima humwandaa kwa

ajili ya jamii ya malaika watakatifu katika mji wa Mungu. Ukweli umekusudiwa kutuleta sote katika usawa wa juu. **{WM 186.3}**

Wenye uwezo zaidi wanapaswa daima kutenda sehemu njema, ya ukarimu katika kushughulika kwao na ndugu zao maskini, na wanapaswa pia kuwapa ushauri mzuri, na kisha kuwaacha wapigane vita vya maisha hadi kushinda. Lakini nilioneshwa kwamba wajibu mzito kabisa uko juu ya kanisa kuwa na huduma maalum kwa wajane wasio na mahitaji ya lazima, yatima, na wasiojiweza kama vile vilema. - *Testimonies for the Church* 1: 272-274. **{WM 187.1}**

Ushauri Kuhusu Kazi Yenye Uwiano. - Kristo hajatuagiza kutoa kazi

yetu yote na karama zetu zote kwa maskini. Tuna kazi ya kufanya kwa niaba ya wale wanaotimiza agizo Lake, "Nendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe." Ongezeko la huduma litahitaji ongezeko la fedha/mali .... **{WM 187.3}**

Unapotumia fedha, fikiria, "Je, ninahimiza ubadhirifu?" Unapowapa maskini na wanyonge fikiria, "Je! Ninawasaidia, au ninawadhuru?"...

Fikiria juu ya mahitaji ya maeneo yetu ya misioni ulimwenguni kote.... Wakati wa sasa umeelemewa na masilahi ya milele. Tunapaswa kutweka bendera ya Ukweli mbele ya ulimwengu unaoangamia katika dhambi. Mungu anawaita watu waandamane chini ya bendera ya Kristo yenye alama ya damu,

wape watu Biblia, zidisheni mikutano ya makambi katika maeneo mbalimbali, ionyeni miji, na tumeni maonyo kwenda mbali na karibu katika barabara kuu na sehemu zisizofahamika vizuri za ulimwengu. - *Manuscript* 4, 1899. **{WM 187.4}**

Sura ya Ishirini na Mbili - Maskini wa Dunia

Kutoa Mahitaji ya Maskini. - Kote kutuzunguka tunaona uhitaji na mateso. Familia zinahitaji chakula; watoto wanalia kwa ajili ya mkate. Nyumba za maskini hazina samani na matandiko ya kitanda yanayofaa. Wengi wanaishi katika vibanda vibovu tu,

ambavyo havina hali ya kufaa. Kilio cha maskini kinafika mbinguni. Mungu huona; Mungu husikia. —*Testimonies for the Church* 6:385. **{WM 188.1}**

Wakati ambapo Mungu kwa majaliwa Yake ameijaza dunia kwa neema Zake na amejaza ghala Zake kwa faraja za maisha, uhitaji na taabu ziko kila mahali. Majaliwa ya ukarimu yamewekwa mikononi mwa mawakala Wake wanadamu kwa wingi kwa ajili ya kutoa mahitaji ya wote, lakini mawakili wa Mungu si waaminifu. Katika ulimwengu wa Wakristo bayana kuna kiasi cha kutosha kinachotumiwa katika maonesho ya ubadhirifu ambacho kingekidhi mahitaji ya wote wenye njaa na kuwavisha wote walio uchi. Wengi ambao wamejitwalia Jina la Kristo wanatumia pesa Zake kwa ajili ya anasa

za ubinafsi, kwa ajili ya kukidhi hamu ya chakula au ulafi, kwa ajili ya vinywaji vikali na vitu vitamu vitamu, kwa ajili ya nyumba za fahari ya kupindukia na samani na mavazi, wakati ambapo kwa wanadamu wanaoteseka ni kwa nadra wanawaangalia kwa kuwasikitikia au kuwapa neno la huruma. **{WM 188.2}**

Ni taabu iliyoje iliyopo katika kiini kabisa cha nchi zetu zinazoitwa kuwa za Kikristo! Fikiria hali ya maskini katika miji yetu mikubwa. Katika miji hii kuna umati mkubwa wa wanadamu ambao hawapati utunzaji na kujaliwa kama wanavyopewa makatili. Kuna maelfu ya watoto wanyonge, waliovaa nguo zilizoraruka na walio karibu kufa kwa njaa, ambao uovu na upotovu umeandikwa kwenye nyuso zao. Familia zinakusanywa pamoja katika makundi

kwenye makao duni, mengi kati ya hayo yakiwa ni vyumba vya giza vilivyochimbwa chini vikinuka vibaya kwa unyevu na uchafu. Watoto wanazaliwa katika maeneo haya mabaya sana. Utoto na ujana hauoni kitu chochote cha kuvutia, hakuna chochote cha uzuri wa vitu vya asili ambavyo Mungu ameviumba kwa ajili ya kufurahisha akili. Watoto hawa wameachwa kukua wakitengenezwa na kukalibiwa tabia kwa maadili ya chini, ufukara, na mifano mibaya inayowazunguka. Wanasikia Jina la Mungu katika lugha chafu tu. Maneno machafu, harufu kali ya mvuke ya pombe na moshi wa tumbaku, udhilifu wa kimaadili wa kila aina, hukutana na jicho na kupotosha akili. Na kutoka katika maskani haya ya ufukara vilio vya

kuhuzunisha kwa ajili ya chakula na nguo hutumwa na wengi ambao hawajui kitu chochote kuhusu sala. **{WM 188.3}**

Karibu na makanisa yetu kuna kazi ya kufanywa ambayo wengi hawana habari nayo, kazi ambayo hadi sasa bado haijaguswa. "Nalikuwa na njaa," Kristo anasema, "mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia." Mathayo 25:35, 36. Baadhi wanafikiri kwamba wakitoa pesa kwa ajili ya kazi hii, ndio yote wanayotakiwa kufanya, lakini hili ni kosa. Michango ya pesa haiwezi kuchukua nafasi ya huduma ya mtu binafsi. Ni sawa kutoa mali zetu, na wengi zaidi wanapaswa

kulifanya hili; lakini kwa kadiri ya nguvu na fursa zao, huduma ya mtu binafsi inahitajika kwa wote. **{WM 189.1}**

Kazi ya kuwakusanya wahitaji, wanaoonewa, wanaoteseka, mafukara, ni kazi ambayo kila kanisa linalouamini Ukweli wa sasa linapaswa kuwa limekuwa likiifanya kwa muda mrefu. Tunapaswa kuonesha huruma ya upole ya Msamaria katika kutoa mahitaji ya kimwili, kuwalisha wenye njaa, kuwaleta maskini waliotupwa nje ndani ya nyumba zetu, tukikusanya kutoka kwa Mungu kila siku neema na nguvu ambayo itatuwezesha kufikia katika vina hasa vya mateso ya wanadamu na kuwasaidia wale ambao hawawezi kujimudu wenyewe. Katika kufanya kazi hii tunayo fursa yenye kufaa ya kumweka Kristo kama Yeye

aliyesulubiwa. — *Testimonies for the Church* 6:274-276. **{WM 189.2}**

Anza kwa Kusaidia Majirani Wako. - Kila mshiriki wa kanisa anapaswa kuhisi kuwa ni jukumu lake maalum kufanya kazi kwa ajili ya wale wanaoishi katika ujirani wake. Jifunze jinsi unavyoweza kuwasaidia vyema wale wasiopendezwa na mambo ya kidini. Unapowatembelea marafiki na majirani wako onesha shauku kuhusu maisha yao ya kiroho na pia ustawi wao wa maisha. Mwasilishe Kristo kama Mwokozi anayesamehe dhambi. Waalike majirani wako nyumbani kwako, na usome pamoja nao Biblia yenye thamani kubwa pamoja na vitabu vinavyoelezea Ukweli wake. Hii, ikiunganishwa na nyimbo sahili na maombi yenye ari, yatagusa mioyo yao. Hebu washiriki wa

kanisa wajielimishe kufanya kazi hii. Hii ni muhimu kama kuokoa roho zilizo gizani katika nchi za kigeni. Wakati ambapo baadhi wanahisi mzigo wa roho zilizo mbali, hebu wengi walio nyumbani wahisi mzigo wa roho za thamani zilizo karibu na wao na wafanye kazi kwa bidii kwa ajili ya wokovu wao. **{WM 190.1}**

Saa ambazo mara nyingi sana hutumika kwa ajili ya burudani ambazo hazichangamshi au kuleta nguvu mpya kwa mwili au roho zingepaswa kutumika katika kuwatembelea maskini, wagonjwa, na wale wanaoteseka, au kutafuta kumsaidia mtu fulani aliye na hitaji. **{WM 190.2}**

Katika kujitahidi kuwasaidia maskini, waliodharauliwa, waliotelekezwa, usifanye kazi kwa ajili

yao ukiwa umepanda juu ya kiburi cha hadhi yako na ukuu wako, kwani kwa njia hii hutatimiza chochote. Uwe mwongofu wa Kweli, na ujifunze kutoka Kwake Yeye aliye mpole na mnyenyekevu wa moyo. Ni lazima tumweke Bwana mbele yetu daima. Kama watumishi wa Kristo endeleeni kusema, msije mkasahau, "Nimenunuliwa kwa thamani." **{WM 190.3}**

Mungu hataki ukarimu wako peke yake bali pia uso wako uliochangamka, maneno yako yenye kutia matumaini, kushika kwa mkono wako. Unapowatembelea wale walioteswa wa Bwana utawakuta wengine ambao kwao tumaini limetoweka; warudishie uchangamfu. Wapo wale ambao wanahitaji mkate wa uzima; wasomee

kutoka katika Neno la Mungu. Juu ya wengine kuna ugonjwa wa roho ambao hakuna zeri ya kidunia inayoweza kuufikia au tabibu wa kuuponya; waombee hawa, na uwalete kwa Yesu. **{WM 190.4}**

Katika wakati maalum wengine huendekeza hisi za moyoni ambazo husababisha misukumo ya harara. Wanaweza kufikiri kwamba kwa njia hii wanafanya huduma kubwa kwa ajili ya Kristo, lakini sivyo. Bidii yao hufa mara, na kisha kazi ya Kristo hupuuzwa. Hii si huduma inayofaa ambayo Mungu anaikubali; si kwa matukio ya ghafla ya mhemko ya shughuli ndipo tunaweza kutenda wema kwa wanadamu wenzetu. Jitihada za vipindi visivyotabirika za kufanya mema mara nyingi husababisha

madhara zaidi kuliko faida.-*Testimonies for the Church* 6: 276-277. **{WM 191.1}**

Toa Msaada Unaostahili. - Mbinu za kuwasaidia wahitaji zinapaswa kuzingatiwa kwa uangalifu na kwa maombi. Tunapaswa kumtafuta Mungu kwa ajili ya hekima, kwa maana anajua vyema kuliko wanadamu wenye kufa wasioweza kuona mbali jinsi ya kuwatunza viumbe aliowaumba. Kuna baadhi ambao hutoa bila kuchagua kwa busara kwa kila mtu anayeomba msaada wao. Katika hili wanakosea. Katika kujaribu kuwasaidia wahitaji tunapaswa kuwa waangalifu ili kuwapa aina sahihi ya msaada. Wapo wale ambao wakisaidiwa wataendelea kujifanya kuwa malengo maalum ya uhitaji. Watakuwa tegemezi maadamu wataona chochote ambacho wanaweza

kukitegemea. Kwa kutoa muda na usikivu usiostahili kwa hawa tunaweza kuhimiza uvivu, kutokujiweza, ubadhirifu, na kukosa kiasi. **{WM 191.2}**

Tunapotoa kwa maskini tunapaswa kuzingatia, "Je! ninahimiza ubadhirifu? Je, ninawasaidia au ninawadhuru?" Hakuna mtu ambaye anaweza kupata riziki yake yeye mwenyewe aliye na haki ya kuwategemea wengine. **{WM 191.3}**

Methali, "Ninaudai ulimwengu uhai wangu," ina asili ya uwongo, ulaghai, na wizi ndani yake. Ulimwengu hauna deni na mtu yeyote aliye hai ambaye ana uwezo wa kufanya kazi na kujipatia riziki kwa ajili yake mwenyewe. Lakini kama mtu akija mlangoni petu na kuomba chakula, hatupaswi kumgeuza

aende zake akiwa na njaa. Umaskini wake unaweza kuwa ni matokeo ya bahati mbaya. **{WM 192.1}**

Tunapaswa kuwasaidia wale ambao wakiwa na familia kubwa za kutegemeza wanalazimika siku zote kupambana kwa unyonge na umaskini. Akina mama wajane wengi pamoja na watoto wao yatima hufanya kazi kuzidi nguvu zao ili kudumu kuwa na watoto wao na kuwapa chakula na mavazi. Wengi wa akina mama kama hao wamekufa kutokana na juhudi iliyopita kiasi. Kila mjane anahitaji faraja ya maneno ya matumaini, yenye kutia moyo, na kuna wengi sana ambao wanapaswa kupata msaada halisi. - *Testimonies for the Church* 6:227, 228. **{WM 192.2}**

Zingatia Kila Hali ya Uhitaji. - Ni kusudi la Mungu kwamba matajiri na maskini wataunganishwa pamoja kwa karibu kwa vifungo vya huruma na msaada. Anatuambia tuwe na shauku na kila hali ya mateso na uhitaji ambayo itafahamika kwetu. Usifikiri kuwa ni kushusha hadhi yako kuwahudumia binadamu wanaoteseka....! **{WM 192.3}**

Wengi wasio wa imani yetu wanatamani sana kupata msaada ambao Wakristo wana wajibu wa kuutoa. Kama watu wa Mungu wangeonesha shauku ya kweli kwa majirani wao, wengi wangefikiwa na Ukweli wa pekee wa wakati huu. Hakuna kitu kitakachotoa au kuweza kutoa sifa bainifu kwa kazi kama kuwasaidia watu pale walipo hasa. Maelfu wangeweza leo kuwa na furaha

katika ujumbe ikiwa wale wanaodai kumpenda Mungu na kushika amri Zake wangefanya kazi kama Kristo alivyofanya. - *Testimonies for the Church* 6:279, 280. **{WM 192.4}**

Njia Bora ya Kufikia Mioyo Leo. - Kwa kuonesha shauku katika mahitaji ya wanadamu wanaoteseka, tunaweza kufikia mioyo kwa namna bora. Ukuzaji na ukomavu wa akili na moyo hutimizwa kwa urahisi zaidi tunapohisi huruma kama hiyo kwa wengine kiasi kwamba tunatawanya faida na marupurupu yetu ili kupunguza mahitaji yao. - *Letter* 116, 1897. **{WM 192.5}**

Tunataka kumwakilisha Kristo kwa kuwafikia wengine. Tunapaswa kufanya kazi chini ya agizo ambalo Kristo aliwapa wanafunzi Wake, "Basi,

enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Hii, basi, ni kazi yetu, kuwafikia watu ambao wamepuuzwa, na kuwavuta waje kwa Kristo. **{WM 193.1}**

Hadi hivi karibuni watu wetu wamefanya kidogo tu au hakuna jitihada za kuwasaidia hawa. Kristo hakuja kuwaita watu wenye haki, bali wenye dhambi, ili wapate kutubu. Angetaka kila roho ipate kuzingatia kufaa kwa damu yake kuwa na thamani isiyo na kipimo, ikiwa na uwezo wa kuokoa kabisa wote ambao watashawishika kuja Kwake. Angetaka kila mtu mmoja

mmoja wa jamii yetu, aliyeumbwa kwa mfano wake, kukumbuka kwamba Mungu hana mwisho, na kwamba upendo wake uliodhihirishwa katika upatanisho wa Kristo, kwa ajili ya upendo kwa wanadamu wote, unadhihirisha thamani anayoiweka kwa wanadamu. Anawaalika waje Kwake ili wapate kuokolewa. Kwa Chanzo cha rehema zetu zote tunapaswa kuja. Atawatumia wanadamu kama mawakala wake kuwavuta wanadamu wenzao kutoka dhambini. - *Letter* 33, 1898. **{WM 193.2}**

Sura ya Ishirini na Tatu - Kuwasaidia Maskini Kujiweza

Waelimishe Maskini Kujitegemea. - Wanaume na wanawake wa Mungu, watu wa utambuzi na hekima, wanapaswa kuteuliwa kuwaangalia maskini na wahitaji, jamaa ya waaminio kwanza. Hawa watapaswa kutoa taarifa kwa kanisa na kushauri juu ya nini kifanyike. **{WM 194.1}**

Badala ya kuwatia moyo maskini kufikiria kwamba wanaweza kupewa chakula chao na kunywa bure, au karibu hivyo, tunapaswa kuwaweka mahali ambapo wanaweza kujimudu wenyewe. Tunapaswa kujitahidi kuwapa kazi, na ikiwa ni lazima, kuwafundisha jinsi ya kufanya kazi. Hebu washiriki wa kaya maskini wafundishwe jinsi ya kupika, jinsi ya kutengeneza na kurekebisha mavazi yao wenyewe, jinsi ya

kuhudumia wagonjwa, jinsi ya kutunza nyumba vizuri. Hebu wavulana na wasichana wafundishwe kabisa ufundi au kazi fulani muhimu. Tunapaswa kuwaelimisha maskini wapate kujitegemea. Huu utakuwa ndio msaada wa kweli, kwa kuwa hautawafanya waweze kujikimu tu bali utawawezesha kuwasaidia wengine. - *Testimonies for the Church* 6:278, 279. **{WM 194.2}**

Wito kwa Wanaume wa Fikira na Mali. - Swali mara nyingi litajitokeza: Ni nini kinachoweza kufanywa wakati ambapo umaskini umeenea na inabidi kupingana nao katika kila hatua? Chini ya hali hizi tunawezaje kuzivutia akili kwa mawazo sahihi ya kufanya vizuri zaidi? Hakika kazi hii ni ngumu; na isipokuwa walimu, watu wenye kufikiri, na watu ambao

wana mali watatumia talanta zao na kuinua kama vile ambavyo Kristo angeinua angekuwa katika nafasi yao kazi muhimu itaachwa bila kufanywa. Matengenezo yanayohitajika hayatafanyika kamwe isipokuwa wanaume na wanawake wamesaidiwa na nguvu iliyo nje yao. Wale ambao wana talanta na uwezo lazima watumie karama hizi kuwabariki wanadamu wenzao, wakijitahidi kuwaweka katika nafasi ambapo wanaweza kujimudu wao wenyewe. Ni hivyo ndivyo elimu inayopatikana katika shule zetu inapaswa kuwekwa katika matumizi bora kabisa. **{WM 194.3}**

Talanta zilizokabidhiwa na Mungu hazipaswi kufichwa chini ya pishi au chini ya kitanda. "Ninyi ni nuru ya ulimwengu," Kristo alisema. Mathayo

5:14. Kadiri mnavyoona familia zikiishi katika vibanda vibovu, wakiwa na samani na mavazi haba, bila zana, bila vitabu au alama nyingine za elimu katika nyumba zao, je utakuwa na shauku juu yao na kujitahidi kuwafundisha jinsi ya kuweka nguvu zao katika matumizi yaliyo bora kabisa, ili kuwepo na maendeleo, na kwamba kazi yao iweze kusonga mbele? - *Testimonies for the Church* 6:188, 189. **{WM 195.1}**

Neno la Mungu Linadhihirisha Suluhisho la Tatizo. - Kuna wanaume na wanawake wenye huruma ambao wanazingatia kwa hamu hali ya maskini na ni njia gani zinaweza kupatikana kwa ajili ya kuwa msaada wa kuwapunguzia dhiki yao. Jinsi ambavyo wasio na ajira na wasio na makazi wanaweza kusaidiwa kupata baraka za kawaida za

majaliwa ya Mungu na kuishi maisha ambayo alikusudia mwanadamu aoate kuyaishi, ni swali ambalo wengi wanajitahidi sana kulipatia jibu.... **{WM 195.2}**

Kama watu wangelizingatia zaidi mafundisho ya Neno la Mungu, wangepata suluhisho la shida hizi zinazowafadhaisha. Tunaweza kujifunza mengi kutoka katika Agano la Kale kuhusu suala la kazi na msaada kwa maskini. Katika mpango wa Mungu kwa Israeli kila familia ilikuwa na nyumba katika nchi, na ardhi ya kutosha kwa ajili ya kulima. Hivyo walipewa njia na kichocheo cha maisha yenye manufaa, ya bidii, na ya kujitegemeza. Na hakuna ubunifu wowote wa wanadamu umewahi kufanya vizuri zaidi ya mpango huo. Kwa ulimwengu kuondoka katika

huo, kwa kiwango kikubwa, ndio sababu ya umaskini na unyonge uliopo leo.... **{WM 195.3}**

Katika Israeli mafunzo ya ufundi yaliangaliwa kama wajibu. Kila baba alihitajika kuwafundisha wanawe ufundi fulani wenye manufaa. Watu mashuhuri katika Israeli walifundishwa kufanya shughuli fulani za uchumi. Ujuzi wa majukumu yanayohusu utunzaji wa nyumba ulizingatiwa kuwa ni muhimu kwa kila mwanamke. Na ustadi katika majukumu haya uliangaliwa kama heshima kwa wanawake wenye cheo cha juu kabisa. **{WM 196.1}**

Tasnia mbalimbali zilifundishwa katika shule za manabii, na wanafunzi wengi walijitegemeza kwa kazi za mikono.... **{WM 196.2}**

Mpango wa maisha ambao Mungu aliwapa Israeli ulikusudiwa kuwa somo linalofundishwa kwa vielezo kwa wanadamu wote. Kama kanuni hizi zingetekelezwa leo, ulimwengu huu ungekuwa mahali tofauti kiasi gani! — *The Ministry of Healing*, 183-188. **{WM 196.3}**

Watu Wengi Wanaweza Kupata Makazi Katika Nchi. - Katika mipaka mikubwa ya asili bado kuna nafasi kwa ajili ya wanaoteseka na wahitaji kupata makazi. Ndani ya kifua chake kuna rasilimali za kutosha kuwapatia chakula. Ndani kabisa ya dunia zimefichwa baraka kwa wote ambao wana ujasiri na bidii na uvumilivu wa kukusanya hazina zake. Kuulima udongo, kazi ambayo Mungu aliiagiza kwa mwanadamu katika Edeni, hufungua uwanja ambao

ndani yake kuna fursa kwa ajili ya watu wengi kupata riziki…. **{WM 196.4}**

Kama maskini ambao kwa sasa wamejaa mijini wangeweza kupata makazi katika ardhi, wasingeweza kupata riziki peke yake bali pia wangepata afya na furaha ambayo kwa sasa haijulikani kwao. Kazi ngumu, mlo sahili, uchumi wa kujinyima, mara nyingi shida na ufukara, vingekuwa ndio fungu lao. Lakini ni baraka kiasi gani wangekuwa nayo kwa kuuacha mji, pamoja na ushawishi wake kuelekea katika uovu, misukosuko yake na uhalifu, taabu na uchafu, kwa ajili ya utulivu na amani na usafi vinavyopatikana mashambani…. **{WM 196.5}**

Kama wangeweza kuwa na bidii na kujitegemeza, wengi sana lazima wangekuwa na msaada, kutiwa moyo, na mafunzo. Kuna familia maskini nyingi sana ambazo kwao hakuna kazi bora ya umisionari ingeweza kufanyika kuliko kuwasaidia katika kufanya makazi mashambani na katika kujifunza jinsi ya kuifanya ipate kuwatolea riziki. **{WM 197.1}**

Hitaji la msaada kama huo na mafunzo halijafungiwa mijini peke yake. Hata mashambani, pamoja na uwezekano wake wote kwa ajili ya maisha bora, watu wengi maskini wana uhitaji mkubwa. Jamii nzima hazina elimu katika mielekeo ya tasnia na usafi.... **{WM 197.2}**

Roho zilizoshushwa na kufikia kuwa katili, miili dhaifu na yenye maumbo mabaya, hudhihirisha matokeo ya urithi mbaya na tabia mbaya. Watu hawa ni lazima waelimishwe kuanzia kwenye msingi kabisa. Wameishi maisha ya kizembe, ya uvivu, mapotovu, na wanahitaji kufundishwa tabia sahihi. **{WM 197.3}**

Je! Wanawezaje kuamshwa juu ya umuhimu wa kufanya vizuri zaidi? Wanawezaje kuelekezwa katika maadili bora ya juu ya maisha? Wanawezaje kusaidiwa kuinuka? Kitu gani kinachoweza kufanywa pale ambapo umasikini umeenea, na unapaswa kupingwa katika kila hatua? — *The Ministry of Healing*, 188-193. **{WM 197.4}**

Kazi kwa Ajili ya Wakulima Wakristo. - Wakulima Wakristo wanaweza kufanya kazi halisi ya umisionari katika kuwasaidia maskini kupata maskani mashambani na kuwafundisha jinsi ya kuulima udongo na kuurutubisha. Wafundishe jinsi ya kutumia zana za kilimo, jinsi ya kulima mazao mbalimbali, jinsi ya kupanda na kutunza bustani za matunda. **{WM 197.5}**

Wengi ambao wanalima udongo hushindwa kupata faida ya kutosha kwa sababu ya kupuuza kwao. Bustani zao za matunda hazitunzwi vizuri, mazao hayawekwi kwa wakati unaofaa, na kazi ya juu juu tu inafanywa katika kuulima udongo. Mafanikio yao yasiyoridhisha wanadai kwamba ni kwa sababu ya ardhi kukosa rutuba. Ushuhuda wa

uwongo mara nyingi unatolewa katika kuilaani ardhi ambayo, kama ingetengenezwa vizuri, ingetoa faida nyingi. Mipango finyu, nguvu ndogo iliyowekwa, utafiti mdogo juu ya mbinu bora, huita kwa sauti kubwa kwa ajili ya kufanya matengenezo. - *The Ministry of Healing*, 193. **{WM 197.6}**

Hata maskini kabisa wanaweza kuboresha mazingira yao kwa kuinuka mapema na kufanya kazi kwa bidii.... Ni kwa kufanya kazi kwa bidii, kwa kutumia kwa hekima kabisa kila uwezo, kwa kujifunza kutokupoteza muda, ndipo watafanikiwa katika kuboresha majengo na maeneo yake na kuilima ardhi yao. - *Testimonies for the Church* 6:188, 189. **{WM 198.1}**

Uanzishwaji wa Tasnia. – Usikivu ni lazima utolewe katika uanzishwaji wa tasnia mbalimbali ili familia maskini ziweze kupata ajira. Mafundi seremala, wahunzi, na kwa kweli kila mtu anayeelewa mkondo fulani wa kazi yenye manufaa anapaswa kuhisi wajibu wa kuwafundisha na kuwasaidia wasiojua na wasio na ajira. **{WM 198.2}**

Katika huduma kwa maskini kuna uwanja mpana wa kufanya kazi kwa wanawake na pia kwa wanaume. Mpishi mzuri, msimamizi au mtunzaji wa nyumba, mshonaji, muuguzi - msaada wa wote unahitajika. ...**{WM 198.3}**

Familia za wamisionari zinatakiwa kukaa katika maeneo yasiyo na rutuba. Hebu wakulima, wafadhili, wajenzi, na

wale ambao wana ujuzi katika sanaa na ufundi anuwai waende kwenye mashamba yaliyotelekezwa ili wapate kuiboresha ardhi, kuanzisha tasnia, kuandaa nyumba duni kwa ajili yao wenyewe, na kuwasaidia majirani zao. - *The Ministry of Healing*, 194.**{WM 198.4}**

Wasaidie Watu Wapate Kujimudu. - Kwa mafunzo katika mielekeo ya kiutendaji tunaweza mara nyingi kuwasaidia maskini kwa ufanisi kabisa. Kwa kawaida wale ambao hawajafundishwa kufanya kazi hawana tabia ya tasnia, uvumilivu, uwekevu, na kujikana nafsi. Hawajui jinsi ya kusimamia. Mara nyingi kupitia ukosefu wa uangalifu na uamuzi wa busara hupotezwa kile ambacho kingeweza kukimu familia zao kwa heshima na

faraja kama kingetumiwa kwa uangalifu na uwekevu. "Chakula kingi kipo katika shamba la maskini; lakini kipo kikile kinachoharibiwa kwa kukosa busara." **{WM 198.5}**

Tunaweza kuwapa maskini, na kuwadhuru, kwa kuwafundisha kuwa tegemezi....**{WM 199.1}**

Wema wa Kweli huwasaidia watu kujimudu.... Ukarimu wa Kweli unamaanisha zaidi ya zawadi tu. Unamaanisha shauku ya Kweli kwa ajili ya ustawi wa wengine. Tunapaswa kujitahidi kuyaelewa mahitaji ya maskini na wenye dhiki, na kuwapa msaada ambao utawanufaisha kabisa. Kutoa mawazo na muda na juhudi binafsi kunagharimu zaidi mno kuliko kutoa fedha tu. Lakini hii ndio fadhila ya

kweli kabisa. - *The Ministry of Healing*, 194, 195. **{WM 199.2}**

Jitihada za Kimwili na Nguvu za Kimaadili Zinahitajika. - Jitihada za kimwili na nguvu za kimaadili zinapaswa kuunganishwa katika juhudi zetu za kufufua na kuongoa. Tunapaswa kujitahidi kupata maarifa katika mielekeo ya maisha na ya kiroho, ili tuweze kuyawasilisha kwa wengine. Tunapaswa kujitahidi kuiishi injili katika fani zake zote, ili baraka Zake za maisha na za kiroho ziweze kuhisiwa kote kutuzunguka. - *Testimonies for the Church* 6:189. **{WM 199.3}**

Kujeruhiwa Pasipo Kujua. - Tunaweza kukosea katika kutoa zawadi kwa maskini ambazo si baraka kwao, tukiwaongoza kuhisi kwamba hawahitaji

kujituma na kuwa wawekevu, kwa kuwa wengine hawatawaruhusu kuteseka. Hatupaswi kuunga mkono ugoigoi au kuhimiza tabia ya kujifurahisha kwa kutoa fedha kwa ajili ya kujiingiza katika uzoefu wa kujifurahisha. - *Historical Sketches*, uk. 293. **{WM 199.4}**

Unaweza kutoa kwa maskini, na kuwadhuru, kwa sababu unawafundisha kuwa tegemezi. Badala yake, wafundishe kujikimu. Hii ndio itakuwa ni msaada wa kweli. Wahitaji lazima wawekwe mahali ambapo wanaweza kujisaidia. — *Manuscript* 46, 1898. **{WM 199.5}**

Kutoungwa Mkono katika Uvivu. - Neno la Mungu linafundisha kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi, asile chakula. Bwana hataki mtu mchapa kazi kuwasaidia wale ambao

hawana bidii. Kuna upotezaji wa muda, ukosefu wa juhudi, ambao huleta umaskini na uhitaji. Ikiwa makosa haya hayataonekana na kusahihishwa na wale wanaoyaendekeza, yote ambayo yangeweza kufanywa kwa niaba yao ni kama kuweka hazina kwenye kikapu kilicho na matobo matobo. Lakini kuna umaskini usioepukika, na tunapaswa kudhihirisha upole na huruma kwa wale waliofikwa na bahati mbaya. - *The Review and Herald,* Januari 3, 1899. **{WM 200.1}**

Maskini Wanapaswa Kutafuta Ushauri. - Kuna tabaka la ndugu maskini ambao hawako huru kutokana na majaribu. Ni wasimamizi wabaya, hawana uamuzi wa busara, wanataka kupata mali bila kungojea mchakato wa polepole wa kufanya kazi kwa kuvumilia.

Baadhi yao wana haraka ya kuboresha hali zao kiasi kwamba wanajihusisha na shughuli mbalimbali bila ya kuomba ushauri kutoka kwa watu wenye busara na uzoefu. Matarajio yao hupatikana kwa nadra; badala ya kupata, wanapoteza, na kisha huja jaribu na moyo wa kuwaonea husuda matajiri. Wanataka hasa kufaidika na utajiri wa ndugu zao, na wanahisi kujaribiwa kwa sababu wao hawana. Lakini hawastahili kupokea msaada wowote maalum. Wana ushahidi kwamba juhudi zao zimetawanywa. Wamekuwa wakibadilika badilika katika shughuli nao wamejaa wasiwasi na masumbufu ambavyo huleta faida kidogo tu. Watu kama hao wanapaswa kusikiliza ushauri wa wale walio na uzoefu. Lakini kwa kawaida hawatafuti ushauri. Wanadhani

kuwa wana akili bora na hawawezi kufundishwa. **{WM 200.2}**

Hawa mara nyingi ndio wale hasa ambao hudanganywa na wachuuzi wale hodari, werevu wenye haki za hataza (kibali rasmi cha kutengeneza bidhaa) ambao mafanikio yao hutegemea sanaa ya udanganyifu. Hawa wanapaswa kujifunza kwamba hakuna imani yoyote inaweza kuwekwa juu ya wachuuzi kama hawa. Lakini ndugu ni wepesi kuyaamini bila ya kuwa na ushahidi mambo yale hasa waliyopaswa kuyashuku na kuepukana nayo. Hawapokei agizo la Paulo kwa Timotheo: "Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa." “Ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo.” Hebu maskini wasidhanie kuwa matajiri peke yao ndio wenye tamaa. Wakati ambapo

matajiri wanashikilia kile walicho nacho kwa uwezo wa kushika wa tamaa, na kujitahidi kupata zaidi na zaidi, maskini wako katika hatari kubwa ya kutamani utajiri wa matajiri. - *Testimonies for the Church* 1:480, 481. **{WM 201.1}**

Kuwa Tayari Kupokea Ushauri. - Wengi hukosa usimamizi na uwekevu wa hekima. Hawapimi mambo vyema, na kwenda kwa uangalifu. Watu kama hao hawapaswi kutegemea uamuzi wao mbaya, bali washauriane na ndugu zao ambao wana uzoefu. Wale ambao hawana uamuzi mzuri na uwekevu mara nyingi hawapendi kutafuta ushauri. Kwa ujumla wanafikiri kwamba wanaelewa jinsi ya kuendesha shughuli zao za maisha, na hawataki kufuata ushauri. Wanachukua hatua mbaya na kuteseka kwa matokeo yasiyofaa. Ndugu zao

wanahuzunika kuwaona wakiteseka, na kuwasaidia kutokana na shida hizo. Usimamizi wao usio wa hekima unaliathiri kanisa. Unachukua mali kutoka katika hazina ya Mungu ambayo ingepaswa kutumika kuendeleza kusudi la ukweli wa sasa. **{WM 201.2}**

Kama ndugu hawa maskini wangechukua njia ya unyenyekevu na kuwa tayari kujulishwa na kushauriwa na ndugu zao, na kisha kuletwa katika maeneo yenye dhiki, ndugu zao wanapaswa kuhisi kuwa ni jukumu lao kuwasaidia kutoka katika shida. Lakini wakichagua njia yao wenyewe na kutegemea akili zao wenyewe, inabidi waachwe kuhisi matokeo kamili ya njia yao isiyo ya hekima, na kujifunza kwa uzoefu ghali kwamba "kwa wingi wa washauri huja wokovu." Watu wa

Mungu wanapaswa kutegemeana kila mtu na mwenzake. Wanapaswa kushauriana kila mmoja na mwenzake, ili kwamba upungufu wa mmoja ujazilizwe na utoshelevu wa mwingine. - *The Review and Herald,* Aprili 18, 1871. **{WM 201.3}**

Maskini Walio Wengi Wangeweza Kujisaidia Wenyewe. -

Wapo wachache sana katika nchi yetu yenye neema ambao kwa kweli ni maskini kiasi cha kuhitaji msaada. Kama wangeliandama njia iliyo sahihi wangeweza karibu katika kila hali kuwa juu zaidi ya uhitaji. Wito wangu kwa matajiri ni huu, Watendeeni kwa ukarimu ndugu zenu walio maskini, nanyi tumieni mali zenu katika kuendeleza kusudi la Mungu. Maskini wanaostahili, wale ambao wamefanywa

kuwa maskini kwa sababu ya misiba na magonjwa, wanastahili utunzaji wenu maalum na msaada. “Hatimaye, iweni na nia moja, msikitikiane kila mtu na mwenzake; pendaneni kama ndugu, iweni na huruma, iweni wenye heshima.” - *Testimonies for the Church* 1:481. **{WM 202.1}**

Fuata Kanuni Iliyo Bora. - Mungu mara kwa mara humwinua mtu fulani ambaye atawakinga maskini wasije wakawekwa katika nafasi ambazo zitakuwa hasara kwao, hata kama itawaletea madhara. Huu ndio wajibu wa mwanadamu kwa mwanadamu mwenzake. Kujinufaisha kwa sababu ya ujinga wa mtu kwa sababu hawezi kutambua matokeo ya mwelekeo fulani wa utendaji si sawa. Ni wajibu wa ndugu yake yeye binafsi kuweka jambo hilo

wazi na kwa uaminifu mbele yake, katika hali zake zote, asije akatenda kwa uzembe, na kuharibu rasilimali ambazo ni zake kwa haki. Pale watu wanapoizingatia kanuni ile iliyo bora, Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo, shida nyingi zilizopo sasa zingerekebishwa haraka. - *Letter* 85, 1896. **{WM 202.2}**

Sura ya Ishirini na Nne - Maskini Kutenda Ukarimu

Si Kiasi, Bali ni Upendo Ule Unaochochea. - Maskini hawajatengwa kutoka katika faida kubwa ya kutoa. Wao, pamoja na matajiri, wanaweza kuwa na sehemu katika kazi hii. Somo ambalo Kristo

alilitoa kuhusiana na sarafu mbili za mjane linatuonesha kwamba sadaka ndogo kabisa za hiari za maskini, ikiwa zinatolewa kutoka katika moyo wa upendo, zinakubalika kama michango mikubwa kabisa ya matajiri. Katika mizani ya patakatifu zawadi za maskini, zilizotolewa kutokana na upendo kwa Kristo, zinakadiriwa, si kulingana na kiasi kilichotolewa bali kulingana na upendo unaochochea dhabihu hiyo. - *The Review and Herald*, Oktoba 10, 1907. **{WM 203.1}**

Dhabihu Pia Inahitajika Kutoka kwa Maskini. - Baadhi ambao ni maskini katika mali ya ulimwengu huu ni wepesi wa kuweka ushuhuda wote ulionyoka juu ya mabega ya watu wenye mali. Lakini hawatambui kwamba wao pia wana kazi ya kufanya. Mungu

anawataka wapate kutoa dhabihu. - *The Review and Herald*, Aprili 18, 1871. **{WM 203.2}**

Alifanya Alichoweza. - Mwokozi aliwaita wanafunzi Wake kuja Kwake na kuwaambia kuzingatia umaskini wa yule mjane. Ndipo maneno yake ya pongezi yakaanguka sikioni mwake [mjane]: "Hakika nawaambia, huyu mjane maskini ametia zaidi kuliko wote." Machozi ya furaha yalijaa machoni mwake alipohisi kwamba tendo lake lilieleweka na kuthaminiwa sana. Wengi wangemshauri atunze pesa yake ndogo kwa ajili ya matumizi yake mwenyewe. Kwa kuwekwa katika mikono ya makuhani waliolishwa vizuri, wala isingetambulika miongoni mwa zawadi nyingi za gharama kubwa zilizoletwa kwenye hazina. Lakini Yesu alielewa nia

yake. Aliamini kuwa huduma ya hekalu ilikuwa ni agizo la Mungu, na alikuwa na shauku ya kufanya yote aliyoweza kuihimili. Alifanya kile alichokiweza, na tendo lake lilikuwa liwe ni kumbukizi kwa kumbukumbu yake siku zote, na furaha yake katika milele. Moyo wake ulienda pamoja na zawadi yake; thamani yake ilikadiriwa, si kwa thamani ya sarafu, bali kwa upendo kwa Mungu na shauku katika kazi Yake ambavyo vilichochea tendo lile. **{WM 203.3}**

Yesu alisema juu ya mjane yule maskini, "Ametia zaidi kuliko wote." Matajiri walikuwa wametoa kutoka katika wingi wao, wengi wao ili waonekane na kuheshimiwa na watu. Michango yao mikubwa haikuwanyang'anya faraja, au hata anasa yoyote; hawakuhitaji kutoa

kafara, na wasingeweza kulinganishwa kwa thamani na sarafu ya mjane. **{WM 204.1}**

Ni nia ambayo inatoa sifa bainifu kwa matendo yetu, ikiyapiga mhuri kwa aibu au kwa thamani ya juu ya kimaadili. Si vitu vikubwa ambavyo kila jicho linaona na kila ulimi unavisifu ambavyo Mungu anavihesabu kuwa vya thamani mno. Majukumu madogo madogo yanayofanywa kwa uchangamfu, zawadi ndogo ndogo ambazo hazijioneshi, na ambazo kwa macho ya kibinadamu zinaweza kuonekana kutokuwa na thamani, mara nyingi husimama juu kabisa machoni Pake. Moyo wenye imani na upendo unapendwa mno na Mungu kuliko zawadi ya gharama kubwa. Mjane maskini alitoa riziki yake ili afanye kile

kidogo alichofanya. Alijinyima chakula ili kutoa sarafu hizo mbili kwa kusudi alilolipenda. Naye alifanya hivyo kwa imani, akiamini kwamba Baba yake wa mbinguni hataacha kutilia maanani hitaji lake kubwa. Ilikuwa ni roho hii isiyo na ubinafsi na imani kama ya mtoto ambayo iliyopata sifa ya Mwokozi. **{WM 204.2}**

Miongoni mwa maskini kuna wengi ambao wanatamani kuonesha shukrani zao kwa Mungu kwa neema na ukweli Wake. Wanatamani sana kushiriki na ndugu zao waliofanikiwa zaidi katika kuihimili huduma Yake. Roho hizi hazipaswi kurudishwa nyuma. Waache waweke sarafu zao katika benki ya mbinguni. Kama imetolewa kutoka

katika moyo uliojaa upendo kwa Mungu, hizi zinazoonekana kuwa ni pesa kidogo tu zinakuwa ni zawadi zilizowekwa wakfu, sadaka zenye thamani kubwa mno, ambazo Mungu anatabasamu kuziona na kubariki. - *The Desire of Ages*, 614-616. **{WM 204.3}**

Jinsi Kanisa la Makedonia Lilivyoitikia. - Paulo aliliandikia kanisa la Korintho: “Tena ndugu zetu, twawaarifu habari ya neema ya Mungu, waliyopewa makanisa ya Makedonia; maana walipokuwa wakijaribiwa kwa dhiki nyingi, wingi wa furaha yao na umaskini wao uliokuwa mwingi uliwaongezea utajiri wa ukarimu wao. Maana nawashuhudia kwamba, kwa uwezo wao, na zaidi ya uwezo wao, kwa

hiari yao wenyewe walitoa vitu vyao; wakituomba sana pamoja na kutusihi kwa habari ya neema hii, na shirika hili la kuwahudumia watakatifu. Tena walitenda hivi si kama tulivyotumaini tu, bali kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana; na kwetu pia, kwa mapenzi ya Mungu. Hata tukamwonya Tito kuwatimilizia neema hii kwenu kama vile yeye alivyotangulia kuianzisha." **{WM 205.1}**

Kulikuwa na njaa huko Yerusalemu, na Paulo alijua kwamba Wakristo wengi walikuwa wametawanyika katika nchi za ng'ambo, na kwamba wale waliobaki wangekuwa na uwezekano wa kunyimwa huruma ya kibinadamu na kuwekwa wazi kwa uadui wa kidini. Kwa hiyo aliwahimiza makanisa kutuma msaada wa fedha kwa ndugu zao waliokuwamo

Yerusalemu. Kiasi kilichochangwa na makanisa kilizidi matarajio ya mitume. Wakiwa wakibidishwa na upendo wa Kristo, waumini walitoa kwa ukarimu, na walijawa na furaha kwa sababu kwa jinsi hiyowaliweza kuonesha shukrani zao kwa Mkombozi na upendo wao kwa ndugu. Huu ndio msingi wa kweli wa upendo kulingana na Neno la Mungu. - *Testimonies for the Church*, 6:271, 272. **{WM 205.2}**

Kulingana na Talanta Zetu Zilizokabidhiwa. - Katika kanisa la Makedonia tunasoma kwamba "maana walipokuwa wakijaribiwa kwa dhiki nyingi, wingi wa furaha yao na umaskini wao uliokuwa mwingi uliwaongezea utajiri wa ukarimu wao." Sasa je, yeyote kati yetu anayekiri kuwa Mkristo atafikiri kwamba tutasamehewa kwa

kutokufanya chochote kwa ajili ya ukweli kwa sababu sisi ni maskini? Tunachukulia nuru ya ukweli kama hazina isiyoelezeka, isiyoweza kuisha. Tunapaswa kuweka ushawishi unaowiana na talanta zetu tulizokabidhiwa, tuwe matajiri au masikini, wa juu au wa chini, wajinga au wenye elimu. Sisi ni watumishi wa Yesu Kristo, na Bwana anatarajia kuwa tutafanya kila tuwezalo. - *The Review and Herald*, Septemba 4, 1894. **{WM 205.3}**

Wasinyimwe Baraka ya Kutoa. - Jukumu liko juu ya watumishi wa Kristo - wachungaji kuyaelimisha makanisa kuwa na ukarimu. Hata maskini wanapaswa kuwa na sehemu katika kuwasilisha sadaka zao kwa Mungu. Wanapaswa kuwa washirika wa neema

ya Kristo katika kuikana nafsi ili wapate kuwasaidia wale ambao hitaji lao ni kubwa zaidi kuliko lao. Kwa nini watakatifu maskini wakataliwe baraka ya kutoa misaada kwa wale ambao ni maskini kuliko wao wenyewe? Kazi ya kuwaelimisha watu katika mielekeo hii imepuuzwa, na makanisa yameshindwa kutoa kwa ajili ya shida za makanisa maskini zaidi, na kwa jinsi hiyo baraka imezuiliwa ambayo ilipaswa kuwa yao, na itazuiliwa hadi pale watakapokuwa na hisi ya kutambua kupuuza kwao. - *The Review and Herald*, Septemba 4, 1894. **{WM 206.1}**

Sehemu ya VIII Wenye Bahati Mbaya

Wazo la Thamani

Katika usiku wa giza la kiroho utukufu wa Mungu unapaswa kuangaza kupitia kwa kanisa Lake katika kuwainua walioinama chini na kuwafariji wale wanaoomboleza. Kote kutuzunguka kunasikika maombolezo ya huzuni ya ulimwengu. Kila upande kuna wahitaji na wenye dhiki. Ni jukumu letu kusaidia katika kutuliza na kulainisha shida na mateso ya maisha. Mahitaji ya roho, ni upendo wa Kristo peke yake ndio unaoweza kuyakidhi. Ikiwa Kristo anakaa ndani yetu, mioyo yetu itajaa huruma ya kiungu. Chemchemi zilizotiwa muhuri za upendo wa dhati, kama wa Kristo zitafunguliwa. —

Prophets and Kings, 718, 719.**{WM 208.1}**

Ayubu 29

12 Kwa sababu nalimwokoa maskini aliyenililia; Yatima naye, na yule asiyekuwa na mtu wa kumsaidia.
13 Baraka yake yeye aliyekuwa karibu na kupotea ilinijia; Nikaufanya moyo wa mjane kuimba kwa furaha.
14 Nalijivika haki, ikanifunika, Adili yangu ilikuwa kama joho na kilemba.
15 Nalikuwa macho kwa kipofu, Nalikuwa miguu kwa aliyechechemea.
16 Nalikuwa baba kwa mhitaji, Na daawa ya mtu nisiyemjua naliichunguza.

Sura ya Ishirini na Tano - Wajibu wetu kwa Wenye Bahati Mbaya

Huruma kwa Vipofu, Vilema, na Wanaoteseka. - Wale ambao wana huruma kwa wasiojiweza, vipofu, viwete, wenye shida, wajane, yatima, na wahitaji, Kristo anawakilisha kama watunzaji wa amri, ambao watakuwa na uzima wa milele. – *Testimonies for the Church* 3:512. **{WM 209.1}**

Huruma Zilizoganda. - Kwa mtazamo wa kile mbingu inachokifanya ili kuwaokoa waliopotea, inawezekanaje kwa wale ambao ni washiriki wa utajiri wa neema ya Kristo kuondoa shauku na huruma zao kutoka kwa wanadamu wenzao? Wanawezaje kuendekeza kiburi cha vyeo au tabaka na kuwadharau wale wenye bahati mbaya na maskini? **{WM 209.2}**

Lakini bado ni kweli mno kwamba kiburi cha cheo na ukandamizaji wa maskini ambao umeenea ulimwenguni, upo pia miongoni mwa wafuasi bayana wa Kristo. Kwa wengi huruma zile ambazo zilipaswa kutekelezwa kwa kipimo kamili kwa wanadamu zinaonekana kuganda. Watu hujitwalia wenyewe zawadi zile walizokabidhiwa kwa ajili ya kuwabariki wengine.

Matajiri huwaonea maskini na kutumia mali zinazopatikana kwa jinsi hiyo kuendekeza kiburi chao na kupenda kujionesha hata katika nyumba ya Mungu.... Isingekuwa kwamba Bwana amedhihirisha upendo wake kwa maskini na watu wa hali ya chini ambao ni wenye mioyo ya kutubu, ulimwengu huu ungekuwa mahali pa kusikitisha kwa mtu maskini. - *The Review and Herald*, Juni 20, 1893. **{WM 209.3}**

Fanya Hali ya Ndugu Yetu Asiyefanikiwa Kuwa Yetu Wenyewe. - Wakati mtu anapambana kwa jitihada za kweli ili apate kujitegemeza yeye na familia yake, na bado asiweze kulifanya hili, kiasi kwamba anateseka kwa ajili ya chakula na mavazi muhimu, Bwana hatawatangaza ndugu zetu

wanaohudumu kuwa hawana hatia ikiwa wataangalia kwa kutokujali au kuagiza masharti kwa ndugu huyu ambayo kwa kweli hayawezekani kutimizwa ... Tunapaswa kuifanya hali ya ndugu asiyejiweza kuwa yetu wenyewe. **{WM 210.1}**

Upuuzaji wowote kwa upande wa wale wanaokiri kuwa wafuasi wa Kristo, kushindwa kupunguza mahitaji ya ndugu au dada ambaye anabeba nira ya umaskini na uonevu, kunaandikishwa katika vitabu vya mbinguni kama vile imeoneshwa kwa Kristo katika nafsi ya watakatifu Wake. Ni hesabu iliyoje Bwana atakuwa nayo kwa wengi, wengi sana, ambao wanawasilisha maneno ya Kristo kwa wengine lakini wanashindwa kudhihirisha huruma laini na kumjali ndugu katika imani ambaye hana bahati

na mafanikio kama wao wenyewe.... **{WM 210.2}**

Ikiwa ulijua hali za ndugu huyu, na hukufanya juhudi za dhati za kumsaidia, na kubadilisha kukandamizwa kwake kuwa uhuru, hufanyi kazi za Kristo, na una hatia mbele za Mungu. Ninaandika wazi, kwa maana, kutokana na nuru niliyopewa na Mungu, kuna tabaka la kazi ambalo limepuuzwa. **{WM 210.1}**

{WM 210.3}

Kunaweza kuwa na shauku kubwa inayochukuliwa katika shughuli ya jumla ya kulilisha tabaka la wanyonge ambao wako katika umaskini. Yote haya sina pingamizi nayo, lakini ni bidii iliyoelekezwa vibaya ikiwa tutapita kando hali za hawa ambao ni wa jamaa ya waaminio na kuacha kilio chao cha

dhiki kkupanda juu kwa Mungu kwa sababu ya mateso ambayo tungeweza kutuliza makali yake, na kwa kufanya hivyo tukamwakilisha Yesu Kristo kwa huruma na upendo. Bwana anapingana na sisi juu ya kupuuza huku. Hawezi kusema juu ya mwanamume au mwanamke yeyote, "Vema," isipokuwa kama wamefanya vema katika kuwakilisha sifa za Kristo-wema, huruma, na upendo kwa wanadamu wenzao. - *Manuscript* 34, 1894. **{WM 210.4}**

Toa Nyumba kwa Wasio na Makazi - Miaka kadhaa iliyopita nilioneshwa kwamba watu wa Mungu watajaribiwa juu ya jambo hili la kutengeneza nyumba kwa wasio na makazi; kwamba kutakuwapo na wengi wasio na makazi kwa sababu ya wao

kuuamini ukweli. Upinzani na mateso vingewanyima waumini nyumba zao, na ilikuwa ni jukumu la wale ambao walikuwa na nyumba kuwakaribisha wale ambao hawana. Nimeoneshwa hivi karibuni sana kwamba Mungu angewajaribu kwa namna ya pekee ambao ni watu Wake bayana kwa kurejelea jambo hili. **{WM 211.1}**

Kristo kwa ajili yetu alikuwa maskini ili sisi kupitia umaskini wake tupate kufanywa kuwa matajiri. Alitoa dhabihu ili aweze kutoa nyumba kwa ajili ya wasafiri na wageni ulimwenguni wanaoitafuta nchi iliyo bora, yaani, ya mbinguni. Je! Wale ambao ni raia wa neema Yake, ambao wanatarajia kuwa warithi wa kutokufa, wakatae, au hata wahisi kusita, kushiriki nyumba zao na wasio na makazi na wahitaji? Je! Sisi,

ambao ni wanafunzi wa Yesu, tutawakatalia wageni kuingia kwenye milango yetu kwa sababu hawawezi kudai kufahamiana na wakazi? **{WM 211.2}**

Je! amri ya mtume haina nguvu katika zama hii: "Msisahau kuwafadhili wageni: maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua"? ... **{WM 211.3}**

Baba yetu wa mbinguni ameweka baraka zilizojificha katika njia yetu, lakini wengine hawatazigusa hizi kwa sababu wanaogopa zitapunguza furaha yao. Malaika wanasubiri kuona kama tunatumia kwa bidii fursa zile zilizopo karibu na sisi za kutenda mema-wakisubiri kuona iwapo tunawabariki

wengine, ili na wao pia wapate utubariki. ...**{WM 211.4}**

Nimewasikia wengi wakitoa udhuru wa kutokuwakaribisha nyumbani mwao na mioyoni mwao watakatifu wa Mungu. "Kwa nini, sijaandaa chochote, sijapika chochote; lazima waende mahali pengine." Na mahali hapo panaweza kuwa na udhuru mwingine uliobuniwa kwa ajili ya kutokuwapokea wale wanaohitaji ukarimu, na hisia za wageni zinahuzunishwa sana, nao wanaondoka na maoni yasiyopendeza kuhusu ukarimu wa hawa wanaokiri kuwa ndugu na dada. Ikiwa huna mkate, dada, uige mfano uliodhihirishwa katika Biblia. Nenda kwa jirani yako na useme, "Rafiki yangu, nikopeshe mikate mitatu; kwa sababu rafiki yangu amefika

kwangu, atoka safarini, nami sina kitu cha kuweka mbele yake." Hatuna mfano ambapo ukosefu huu wa mkate unafanywa kuwa kisingizio cha kukataa kumkaribisha kwa mwombaji. Wakati Eliya alipomjia mjane wa Sarepta, alishiriki chakula chake na nabii wa Mungu, naye alifanya muujiza, na kusababisha kwamba katika tendo hilo la kufanya nyumba kwa mtumishi wake, na kugawana chakula chake pamoja naye, yeye mwenyewe alihimiliwa, na maisha yake na yale ya mwanawe yalihifadhiwa. Hivyo ndivyo itakavyothibitika katika hali ya wengi, ikiwa watalifanya hili kwa furaha, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. - *Testimonies for the Church* 2:27-29. **{WM 212.1}**

Jamii ya Kanisa Kuwajibika kwa Ajili ya Uzembe wa Washiriki.

- Mungu ataliwajibisha kanisa, kama jamii, kwa sababu ya mielekeo mibaya ya washiriki wake. Ikiwa roho ya ubinafsi na isiyo na huruma imeruhusiwa kuwepo kwa washiriki wake wowote kwa wasiojiweza, mjane, yatima, kipofu, kilema, au wagonjwa wa mwili au akili, Yeye ataficha uso Wake kutoka kwa watu Wake hadi pale watakapotimiza wajibu wao na kuyaondoa makosa kutoka miongoni mwao. Ikiwa yeyote anayekiri Jina la Kristo hadi sasa anamwakilisha vibaya Mwokozi wao kwa kutokujali wajibu wao kwa wanaoteseka, au ikiwa kwa njia yoyote ile wanajitahidi kujinufaisha wenyewe kwa kuwadhuru wale wasiojiweza, na kwa hivyo kuwaibia

mali, Bwana analiwajibisha kanisa kwa dhambi ya washiriki wake hadi pale watakapokuwa wamefanya yote wawezayo kuurekebisha uovu uliopo. Yeye Hatasikiliza maombi ya watu Wake wakati yatima, waliofiwa na baba, vilema, vipofu, na wagonjwa wametelekezwa miongoni mwao. - *Testimonies for the Church* 3:517, 518. **{WM 212.2}**

Mbingu Hutunza Rekodi kwa Uaminifu. - Kristo anaona kuwa matendo yote ya rehema, ukarimu, na huruma ya kufikiria kwa asiyejiweza, kipofu, kiwete, mgonjwa, mjane, na yatima kama vile yamefanywa Kwake Yeye mwenyewe: na kazi hizi zimehifadhiwa katika rekodi za mbinguni na zitapewa thawabu. Kwa upande mwingine, rekodi itaandikwa

katika kitabu dhidi ya wale ambao hudhihirisha kutokujali kwa kuhani na Mlawi kwa asiyejiweza, na wale ambao hujinufaisha kwa misiba ya wengine. - *Testimonies for the Church* 2:512, 513. **{WM 213.1}**

Sura ya Ishirini na Sita - Msaada na Faraja kwa Wajane

Madai ya Wajane na Yatima. – Miongoni mwa wote ambao mahitaji yao yanahitaji shauku yetu, mjane na wale wasio na baba wana madai yenye nguvu kuhusu huruma na huduma yetu njema. “Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii: Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika

dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.” **{WM 214.1}**

Baba ambaye amekufa katika imani, akipumzika juu ya ahadi ya milele ya Mungu, amewaacha wapendwa wake akiwa na imani kamili kwamba Bwana atawatunza. Na Bwana hutoaje riziki kwa hawa waliofiwa? Yeye hafanyi muujiza kwa kutuma mana kutoka mbinguni; Hatumi kunguru kuwaletea chakula; bali hufanya muujiza katika mioyo ya wanadamu. Hufukuza ubinafsi kutoka katika roho; Hufungua chemchemi ya ukarimu. Anapima upendo wa wafuasi Wake bayana kwa kuwaweka kwa ajili ya huruma zao wale wanaoteseka na wafiwa, maskini na yatima. Hawa kwa namna ya pekee ndio wale wadogo ambao Kristo anawatazama, ambao ni kosa Kwake

kuwapuuza. Wale ambao huwapuuza wanampuuza Kristo katika nafsi ya wale wanaoteseka. Kila tendo la huruma linalotendwa kwao kwa Jina la Yesu linapokelewa na Yeye kana kwamba limetendwa Kwake Mwenyewe, kwani Yeye hutambulisha masilahi Yake na yale ya wanadamu wanaoteseka, Naye amekabidhi kwa kanisa Lake kazi kubwa ya kumtumikia Yesu kwa kuwasaidia na kuwabariki wahitaji na wanaoteseka. Juu ya wote watakaowahudumia kwa mioyo ya hiari baraka ya Bwana itatulia. - *The Review and Herald*, Juni 27, 1893. **{WM 214.2}**

Toa Msaada Halisi; Punguza Mizigo ya Wajane. – Akina mama wengi wajane wakiwa na watoto wao yatima wanajitahidi kubeba mizigo yao miwili/maradufu, mara nyingi

wakijitahidi kupita nguvu zao ili kuwaweka watoto wao kudumu/waendelee kuwa pamoja nao na kuwapatia mahitaji yao. Yeye anao muda mchache tu kwa ajili ya mafunzo na maelekezo yao, fursa ndogo ya kuwazunguka na mivuto ambayo ingechangamsha maisha yao. Huyu mama anahitaji kutiwa moyo, huruma, na msaada halisi. **{WM 215.1}**

Mungu anatuagiza tupate kuwapa watoto hawa, kadiri tuwezavyo, mahitaji ya utunzaji wa baba. Badala ya kujitenga, kulalamikia makosa yao, na matatizo wanayoweza kuyasababisha, wasaidie kwa kila njia inayowezekana. Jitahidi kumsaidia mama aliyechoka au kutaabika kwa dhiki. Punguza mizigo yake. - *The Ministry of Healing,* 203. **{WM 215.2}**

Kuwa Mifereji ya Baraka za Mungu. - Katika nyumba zilizojaliwa mahitaji na raha zinazoondoa ugumu wa maisha (comfort), katika mapipa na ghala zilizojaa matunda ya mavuno tele, katika bohari zilizosheheni mashine za ufumaji wa nguo, na ghala za chini zilimohifadhiwa dhahabu na fedha, Mungu ametoa uwezo wa jinsi ya kuwapa riziki wahitaji hawa. Yeye Anatuagiza tuwe mifereji ya baraka Zake. - *The Ministry of Healing*, 202. **{WM 215.3}**

Msaada kwa Mjane Umekabidhiwa kwa Wenye Ustawi/mafanikio. - Maskini, wasio na makazi, na wajane wako miongoni mwetu. Nilimsikia mkulima tajiri akielezea hali ya mjane maskini aliyekuwa kati yao. Alilalamikia hali

yake ngumu, na kisha akasema: "Sijui atakavyoiweza baridi na theluji katika majira yajayo ya baridi. Ana hali ngumu kwa sasa.” Watu kama hao wamemsahau aliye Mfano, na kwa matendo yao wanasema: "La, Bwana, hatuwezi kunywa kikombe kile cha kujinyima, unyenyekevu, na kujitoa kuwa dhabihu ulichokinywa, wala kubatizwa kwa mateso uliyobatizwa nayo. Sisi hatuwezi kuishi ili kuwatendea watu wengine mema. Wajibu na ‘biashara’ yetu ni kujishughulikia sisi wenyewe.” **{WM 215.4}**

Ni nani anayepaswa kujua jinsi mjane anavyopaswa kuendelea au kujikumu maisha isipokuwa kupitia wale ambao wamezijaza vyema ghala zao za nafaka? Uwezo wa kumfanya

kuendelea au kujikimu maisha uko karibu. Je wale ambao Mungu amewaweka kuwa mawakili Wake, ambao amewakabidhi mali, watathubutu kuwazuilia wanafunzi wa Kristo wenye uhitaji? Ikiwa ndivyo, basi wanamzuilia Yesu. Je! Unatarajia Bwana anyeshe nafaka kutoka mbinguni ili kuwapa wahitaji? Je! badala yake Hajaiweka mikononi mwako, ili apate kuwasaidia na kuwabariki kupitia kwako? Je! Yeye Hajakufanya wewe kuwa chombo Chake katika kazi hii nzuri ili apate kukujaribu wewe na kukupa fursa ya kujiwekea hazina mbinguni? - *Testimonies for the Church* 2:32, 33. **{WM 216.1}**

Ndugu, kwa ajili ya Kristo jazeni maisha yenu kwa matendo mema.... Vyote mlivyo navyo ni mali ya Mungu.

Jihadharini, msije kwa ubinafsi mkahodhi (mkajilundikia wenyewe) baraka ambazo Yeye amewapa kwa ajili ya mjane na wale wasio na baba. - *Testimonies for the Church* 4:627. **{WM 216.2}**

Wakristo Wanamiliki Mali Nyingi kwa Ajili ya Wahitaji. - Wakristo hawasameheki kwa kuruhusu vilio vya mjane na maombi ya yatima kupaa Mbinguni kwa sababu ya kuwa kwao wahitaji wakati ambapo Majaliwa ya ukarimu wa Bwana yamewekwa mikononi mwa Wakristo hawa kwa wingi ili waweze kuruzuku mahitaji yao. Hebu vilio vya mjane na yatima visije vikaita kisasi cha Mbingu kuja juu yetu sisi kama kanisa. Katika ulimwengu wa Mkristo bayana kuna kiasi cha kutosha cha ugavi, kinachotumika katika

maonesho ya ubadhirifu kwa kununua vito vya thamani na mapambo, badala ya kutoa mahitaji ya wote wenye njaa na kuwavika walio uchi katika miji na majiji yetu; na bado hawa wafuasi bayana wa Yesu aliye mpole na mnyenyekevu hawataki kujinyima chakula kinachofaa au mavazi mazuri. Je, washiriki hawa wa kanisa watasema nini wakati watakapokabiliwa na hukumu katika siku ile ya Mungu na maskini wanaostahili, wale wanaoteseka, na wajane na yatima, ambao wamepitia uzoefu wa uhaba wa mahitaji ya muhimu katika maisha yao, wakati hawa wanaokiri kwamba ni wafuasi wa Kristo, walikuwa na nguo zilizosheheni na mapambo yasiyo ya lazima yaliyopigwa marufuku kwenye Neno la Mungu, ambayo yalitosha

kabisa kushugulikia mahitaji ya hawa watu wenye shida. (asilimia 80% ya utajiri wote duniani unamilikiwa mikononi mwa Wakristo, ila huwapa wahitaji chenji, chenji zao tu, badala ya kuwapa mitaji midogo midogo ya kuinua maisha yao, Bwana amekuwa mwaminifu sana kwa waumini ila wao hawajakuwa waaminifu- Ron Sider, Rich Christian in the World of hunger)**{WM 216.3}**

Usiwapuuze Wale Walio Karibu. - Katika kila karama na utoaji kunapaswa kuwapo na lengo linalofaa mbele ya mtoaji, si kumuunga mkono yeyote katika uvivu au kuchochea ugoigoi, si ili kuonekana na wanadamu au kupata jina kubwa, bali kumtukuza Mungu kwa kuendeleza kusudi Lake. Baadhi ya watu wanatoa michango

mikubwa kwa ajili ya kusudi la Mungu, wakati ambapo ndugu yao karibu anateseka kimaisha na hawafanyi lolote kumletea afueni au kumsaidia. Matendo madogo madogo ya wema yanayofanywa kwa ndugu yao kwa namna ya siri yangefungamanisha mioyo yao pamoja na yangeonekana mbinguni. Niliona kwamba katika kipaumbele chao na mishahara, matajiri wanapaswa kuweka tofauti kwa faida ya wanaoteseka na wajane na maskini wanaostahili walio miongoni mwao. - *Testimonies for the Church* 1:194. **{WM 217.1}**

Mungu Husikia Maombi ya Mjane. - Sheria walizopewa Israeli zinalinda kwa namna ya pekee masilahi ya wale wanaohitaji msaada.

“Usimwonee mgeni, wala kumtendea jeuri; kwa kuwa ninyi mlikuwa wageni katika nchi ya Misri. Usimtese mjane yeyote aliyefiwa na mumewe, wala mtoto yatima. Ukiwatesa watu hao katika neno lolote, nao wakanililia Mimi, hakika Yangu nitasikia kilio chao, na hasira Yangu itawaka moto, Nami nitawaua ninyi kwa upanga; na wake wenu watakuwa wajane, na watoto wenu mayatima.” **{WM 217.2}**

Hebu wale walio katika makanisa yetu na wale wanaosimamia kazi zenye madaraka katika taasisi zetu wajifunze kutoka katika Maneno haya jinsi Bwana anavyoyalinda kwa uangalifu masilahi ya wale ambao hawawezi kujisaidia. Yeye Anasikia kilio cha mjane kwa ajili ya watoto Wake wasio na baba. Hakika Yeye atawahukumu wale ambao

wanapuuza sheria ambazo ameziweka ili kuwakinga na madhara. **{WM 217.3}**

Na bado, licha ya maonyo ambayo Mungu ameyatoa, kuna wale ambao hawaogopi kumdhulumu mjane na yatima-(kuwakosea haki). Neno la Bwana limewajia, lakini hawakubadilisha mwelekeo wao ili wapate kuwasaidia wahitaji. Waligeuza masikio yao mbali na ombi la yatima. Machozi na maombi ya mjane hayakuwa kitu kwao. — *Manuscript* 117, 1903. **{WM 218.1}**

Kumtembelea Mjane. - Kuwatembelea mjane na yatima ambako mtume aliamuru ni kuwa na huruma ya Kikristo, huruma iliyotakaswa kwao katika mateso yao. Wanapaswa kulinda masilahi yao kwa utakatifu, kuyafanyia

kazi kwa ajili yao, kujiweka katika usumbufu kwa ajili ya kuwafanyia fadhila. Wanapaswa kuwapa ushauri kama wa Kristo; wanapaswa kuungana nao katika maombi na kukumbuka daima kwamba Yesu Kristo Yupo katika ziara hizi zote, na kwamba rekodi ya uaminifu inawekwa kuhusu lengo na kazi iliyotimizwa. Wakristo watatoa ushahidi kwamba wao ni wanaume na wanawake walioongoka. Wataonesha kwamba wao ni wasomaji wa Biblia, waumini wa Biblia, na wanatii kila amri ya Neno la Mungu. Hawatajitahidi kutengeneza huruma kwa ajili yao wenyewe kwa kuzungumza kwa chuki juu ya mke au mume. Hawatakuwa watu wa kujiona na kujifikiria wenyewe kama ndiyo kitovu cha mambo yote, bali watakuwa na moyo wa kuwatendea

wengine mema na kuwa baraka kwa wanadamu, kwa kuwa huku ni kuwa kama Kristo. Watatembea kwa uangalifu na kuidhihirisha tabia ya Kristo. Katika kushughulika kwao kote na wajane na yatima watafanya kama vile ambavyo wangependa wengine wafanye kwa mke na watoto wao ikiwa wangewaacha wakiwa wajane na yatima. **{WM 218.2}**

Kweli zinapaswa kuzingatiwa na wote ambao wanadai kuwa ni watoto wa Mungu, kwamba kuna Mwangalizi katika kila shughuli ya biashara ambaye anarekodi kila tendo la mfanya biashara na kwamba rekodi hii itasimama kama ilivyoandikwa hadi siku kuu ambayo kila mtu atapokea kama kazi zake zilivyokuwa, isipokuwa pale ambapo makosa yao yatakuwa yametubiwa na kufutwa. Dhuluma yoyote inayofanywa

kwa mtakatifu au mwenye dhambi wakati huo italipwa ipasavyo. Kristo anatambulisha maslahi Yake katika mateso yote ya watu Wake. Mungu atalipiza kisasi kwa wale ambao watamtendea mjane au yatima kwa uonevu, au ambao watawaibia kwa namna yoyote ile. - *Letter* 36, 1888. **{WM 218.3}**

Hakuna Kupungua kwa Wajibu. - Kila nafsi maskini, iliyojaribiwa inahitaji mwanga, inahitaji maneno ya laini, yenye huruma, na ya matumaini. Kila mjane anahitaji faraja ya maneno ya kusaidia na ya kutia moyo ambayo wengine wanaweza kuyatoa.... **{WM 219.1}**

Kuna kazi kubwa ya kufanywa katika ulimwengu wetu, na tunapoukaribia

mwisho wa historia ya dunia,kazi haipungui kiwango hata kidogo; bali pale upendo kamili wa Mungu uko moyoni, mambo ya ajabu yatafanyika. Kristo atakuwamo moyoni mwa muumini kama kisima cha maji kinachobubujika kufikia uzima wa milele. - *The Review and Herald*, Januari 15, 1895. **{WM 219.2}**

Sura ya Ishirini na Saba - Matunzo ya Yatima

Baba na Mama Wakristo Wanahitajika. –Hadi kifo kitakapomezwa na ushindi kutakuwa na yatima wa kutunzwa, ambao watateseka kwa njia zaidi ya moja ikiwa huruma na fadhili za kanisa letu hazitatekelezwa kwa niaba yao. Bwana anatuambia,

"Kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako." Ukristo ni lazima uwapatie baba na mama hawa wasio na makazi. Huruma kwa mjane na yatima inayodhihirishwa katika sala na matendo itakuja kwa ukumbusho mbele za Mungu, nayo italipwa katika wakati unaokuja. - *The Review and Herald,* Juni 27, 1893. **{WM 220.1}**

Kristo Anasema, Wachukueni Watoto Hawa. - Watoto wasio na baba na wasio na mama wamewekwa katika mikono ya kanisa, na Kristo anawaambia wafuasi Wake: Wachukueni watoto hawa maskini, waleeni kwaajili Yangu, nanyi mtapokea mishahara yenu. Nimeona ubinafsi mwingi ukidhihirishwa katika mambo haya. Isipokuwa kuna ushahidi maalum kwamba wao wenyewe watafaidika kwa

kuwachukua katika familia zao wale ambao wanahitaji makazi, wengine hugeuka na kujibu: Hapana. Hawaonekani kujua au kujali kama watu kama hao wanaokolewa au wanapotea. Hiyo, wanafikiri, sio kazi yao. Pamoja na Kaini wanasema: “Mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?” (mimi siyo yaya wa ndugu yangu). Hawako tayari kusumbuliwa au kutoa dhabihu yoyote kwa ajili ya mayatima, na bila kujali wanawasukuma watoto kama hao mikononi mwa ulimwengu, ambao nyakati fulani uko tayari zaidi kuwapokea kuliko hawa Wakristo bayana/wanaokiri imani yao. Katika siku ya Mungu uchunguzi utafanywa kwa wale ambao Mbingu iliwapa fursa ya kuokoa. Lakini walitoa udhuru, na wala hawakujihusisha na kazi hii njema,

isipokuwa wangeweza kulifanya kuwa jambo la manufaa kwao. Nimeoneshwa kwamba wale wanaokataa fursa hizi za kutenda mema watasikia kutoka kwa Yesu: “Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea Mimi.” -*Testimonies for the Church* 2:33 **{WM 220.2}**

Fungueni Mioyo Yenu na Nyumba Zenu. - Mume wangu na mimi, ingawa tuliitwa kufanya kazi ngumu katika huduma, tulihisi kuwa ni faida kubwa kwetu kuwakusanya nyumbani kwetu watoto wale ambao walihitaji huduma, na kuwasaidia kuunda tabia inayofaa kwa ajili ya mbingu. Tusingeweza kuwalea watoto wachanga na kuwafanya kuwa wana, kwa maana hii ingetumia muda na umakini wetu na ingemwibia Bwana

huduma ambayo alihitaji kutoka kwetu katika kuwaleta wana na binti wengi Kwake. Lakini tulihisi kwamba maagizo ya Bwana katika Isaya 58 yalikuwa ni kwa ajili yetu, na kwamba baraka Zake zingeambatana nasi kwa kulitii Neno Lake. Wote wanaweza kufanya kitu fulani kwa ajili ya watoto wadogo wahitaji, kwa kusaidia kuwaweka katika kaya ambapo wanaweza kutunzwa. - *Manuscript* 35, 1896. **{WM 221.1}**

Kuna uwanja mpana wa kutumika ulio mbele ya wote ambao watafanya kazi kwa Bwana katika kuwatunza watoto hawa na vijana ambao wamenyimwa uongozi wenye hadhari wa wazazi na uwezo wa kutiisha wa nyumba ya Kikristo. Wengi wao wamerithi sifa bainifu mbaya za tabia; na ikiwa wataachwa kukua katika

ujinga, wataelekea katika ushirikiano utakaoongoza katika uovu na uhalifu. Watoto hawa wasioelekea kufanikiwa au wasionekana kuwa na tumaini wanahitaji kuwekwa katika nafasi nzuri itakayosaidia katika utengenezaji ya tabia sahihi, ili waweze kuwa watoto wa Mungu. **{WM 221.2}**

Je, ninyi ambao mnakiri kuwa watoto wa Mungu mnatenda sehemu yenu katika kuwafundisha hawa, ambao wanahitaji sana kufundishwa kwa uvumilivu jinsi ya kuja kwa Mwokozi? Je, mnatenda sehemu yenu kama watumishi waaminifu wa Kristo? Je, akili hizi changa, huenda zisizo sawasawa zinatunzwa kwa upendo ule ambao Kristo ameuonesha kwetu? Roho za watoto na vijana ziko katika hatari ya kufisha kama zitaachwa zenyewe.

Wanahitaji mafunzo yenye uvumilivu, upendo, na utunzaji mwororo/laini wa Kikristo. **{WM 221.3}**

Je! Hakukuwa na ufunuo wa kuonesha wajibu wetu, kile tukionacho hasa kwa macho yetu, na kile tunachokijua juu ya utendaji usioepukika wa kanuni ya chanzo na matokeo, kinapaswa kutuamsha kuwaokoa hawa wasiojiweza. Kama washiriki wa kanisa wangeleta katika kazi hii nguvu ile ile na busara na ustadi ambavyo wanavitumia katika uhusiano wa kawaida wa shughuli za maisha, ikiwa wangetafuta hekima kutoka kwa Mungu, na kujifunza kwa bidii jinsi ya kuzitengeneza akili hizi zisizo na nidhamu, roho nyingi ambazo zinakaribia kuangamia zingeweza kuokolewa.... **{WM 222.1}**

Ndugu na dada, ninawaomba mpate kulizingatia jambo hili kwa makini. Fikirini juu ya mahitaji ya wale wasio na baba na wasio na mama. Je! Mioyo yenu haisisimki mnaposhuhudia mateso yao? Angalia uone kama kitu hakiwezi kufanyika kwa ajili ya utunzaji wa wanyonge hawa. Kadiri inavyokuwa katika uwezo wako, fanya makazi kwa ajili ya wasio na makazi. Hebu kila mtu asimame tayari kushiriki katika kusaidia kuiendeleza kazi hii. Bwana alimwambia Petro: "Lisha wana-kondoo Wangu." Amri hii ni kwa ajili yetu, na kwa kufungua nyumba zetu kwa ajili ya mayatima sisi tunasaidia katika utimilizaji wake. Hebu Yesu asihuzunishwe na mwenendo wetu/wenu. **{WM 222.2}**

Chukueni watoto hawa na kuwaleta mbele ya Mungu kama sadaka yenye harufu nzuri. Ombea baraka Yake Bwana juu yao, na kisha walee, wafinyange na kuwatunza kulingana na utaratibu wa Kristo. Je, watu wetu wataikubali dhamana hii takatifu? Kwa sababu ya uchaji wetu wa juu juu na tamaa ya makuu ya kupenda anasa za dunia, je, wale ambao Kristo alikufa kwa ajili yao wataachwa kuteseka, na kwenda katika njia mbaya? - *Testimonies for the Church* 6: 282-284. **{WM 222.3}**

Wao ni Mali ya Mungu. - Mayatima ambao wamekopeshwa kwa Wakristo kama dhamana kwa Mungu mara nyingi hupitwa kando na kupuuzwa, na huku bado wakiwa wamenunuliwa kwa gharama kubwa, nao ni wa thamani machoni pa Mungu

kama sisi tulivyo…. Inabidi watunzwe; inabidi wapokee uangalifu wa pekee. Huwezi kutumia mali yako kwa namna iliyo nzuri zaidi kuliko kwa kufungua milango yako kwa ajili ya kuwapa hawa makao. Bwana atakapoona kuwa wewe ni mwaminifu katika kufanya kile unachoweza ili kupunguza mateso ya wanadamu, atawagusa wengine kutoa mali kwa ajili ya kuwatunza wale wanaohitaji msaada. Wale ambao wanapanua mioyo yao katika kazi ya namna hii hawafanyi zaidi ya kile kilicho wajibu wao. **{WM 222.4}**

Kristo Mfano Wetu. Alikuwa ni Mkuu wa mbinguni, lakini bado alifanya mengi kwa wanadamu wenzetu kuliko ambavyo yeyote kati yetu anaweza kufanya. "Ninyi ni watenda kazi pamoja na Mungu." Hebu matumizi yoyote

yasiyo ya lazima yasifanywe kwa ajili ya kuridhisha kiburi na ubatili. Wekeni michango yenu midogo na pesa zenu nyingi mbinguni. Wengi ambao wamepata fursa za thamani kubwa za kuvaa nira ya Kristo katika mwelekeo huu wa thamani kubwa wa kazi wamekataa kujitia katika nira hiyo. Haijapendeza kufanya kujizoeza kutokuwa na ubinafsi, na wamepuuza kufanya hali za maskini na wenye bahati mbaya kuwa zao wenyewe. Hawatilii maanani maagizo ya Kristo, na kutumia vizuri kila kipaji ambacho Bwana amewapa, wakishirikiana na malaika wa mbinguni katika kukusanya roho ambazo zitahudumu, zitatumika, zitaheshimu, na kulitukuza Jina la Kristo. -*The Review and Herald*, Januari 15, 1895.**{WM 223.1}**

Ushauri kwa Walezi wa watoto wasio wao. Ndugu na Dada D: Ziara yenu ya hivi karibuni na mazungumzo na sisi yamependekeza mawazo mengi, ambayo siwezi kuvumilia kuweka machache kwenye karatasi. Nilisikitika sana kwamba E hakuenenda kwa usahihi siku zote; lakini, ukifikiria, huwezi kutarajia ukamilifu kwa kijana wa umri wake. Watoto huwa na makosa, na wanahitaji mafundisho mengi ya uvumilivu. **{WM 223.2}**

Kwamba atakuwa na hisia ambazo mara zote si sahihi si zaidi ya kile kinachoweza kutarajiwa kwa mvulana wa umri wake. Unapaswa kukumbuka kwamba hana baba wala mama, hakuna mtu ambaye anaweza kushiriki naye hisia zake za ndani, huzuni zake, na majaribu yake. Kila mtu anahisi

kwamba anapaswa kuwa na mtu wa kumhurumia. Mvulana huyu amekuwa akitupwa hapa na pale, akinyanguliwa hapa na kupelekwa kule kwa ghafla bila mpangilio maalumu, naye anaweza kuwa na makosa mengi, njia nyingi potovu, pamoja na uhuru mkubwa, na anaweza kukosa heshima. Lakini yeye ni hodari kabisa wa kazi, na kwa mafundisho sahihi na kutendewa kwa huruma, Nina imani kamili kwamba hatayavunja matumaini yetu, bali kikamilifu atalipa kazi yote iliyotumika juu yake. Ukizingatia hali yake ngumu, ninadhani kuwa ni kijana mzuri sana. **{WM 224.1}**

Tulipokuomba wewe umchukue tulifanya hivyo kwa sababu tuliamini kabisa kuwa ni wajibu wako, na kwamba kwa kufanya hivyo ungebarikiwa.

Hatukutarajia kwamba ungelifanya hili ili tu upate kufaidika kwa msaada ambao ungeupata kutoka kwa mvulana huyu, bali kumnufaisha yeye, kufanya wajibu kwa yatima - wajibu ambao kila Mkristo wa Kweli anapaswa kujitahidi na kusubiri kwa shauku kutekeleza; wajibu, wajibu wa kujitoa kafara, ambao tuliamini ungekuwa heri kwako kuuchukua, kama ungeufanya kwa furaha/uchangamfu, kwa lengo la kuwa chombo mikononi mwa Mungu cha kuokoa roho kutoka katika mitego ya Shetani, ya kumwokoa mtoto ambaye baba yake aliyatoa maisha yake ya thamani kwa ajili ya kuzielekeza roho kwa Mwana-Kondoo wa Mungu achukuaye dhambi ya ulimwengu.... **{WM 224.2}**

Kuhusu E, nilikusihi, usisahau kwamba yeye ni mtoto tu mwenye uzoefu wa mtoto. Msimpime, yeye aliye kijana maskini, dhaifu, mnyonge, na nyinyi wenyewe, na mtarajie kutoka kwake kuwa kama ninyi. Ninaamini kabisa kwamba ni jambo lililo katika uwezo wenu kufanya jambo sahihi kwa yatima huyu. Mnaweza kuwasilisha vivutio kwake ili asihisi kuwa kazi yake haina furaha, isiyosaidiwa na miale yoyote ya kutia moyo. Enyi, ndugu na dada, mnaweza kufurahia imani ya kila mmoja wenu, mnaweza kuhurumiana ninyi kwa ninyi, kupendana na kufurahishana, na kusimuliana majaribu na mizigo yenu. Mnalo jambo la kuwachangamsha, wakati yeye yuko peke yake. Yeye ni mvulana mwenye kufikiri mno, lakini hana mtu wa

kumwambia siri zake au wa kumpa neno la kuchangamsha katikati ya kukatishwa tamaa kwake na majaribu makali, ambayo najua anayo sawa na wale wenye umri wa miaka mingi zaidi. **{WM 224.3}**

Ikiwa mtajifungia wenyewe kwa wenyewe, huo ni upendo wa ubinafsi, usioambatana na baraka za Mbinguni. Nina tumaini kubwa kwamba mtampenda yatima huyu kwa ajili ya Kristo, kwamba mtahisi kwamba mali yenu ni bure isipokuwa imetumika katika kufanya mema. Tendeni mema; mwe matajiri wa matendo mema, tayari kugawa, tayari kuwasiliana naye, tayari kutoa, mkijiwekea akiba msingi mzuri dhidi ya wakati ujao, ili mweze

kuushikilia uzima wa milele. Hakuna hata mtu mmoja atakayevuna mavuno ya thawabu ya uzima wa milele isipokuwa wale wenye kujitoa mhanga. Baba na mama waliokufa waliwaacha wapenzi wao wa moyoni kwa utunzaji wa kanisa, wapate kufundishwa kuhusu mambo ya Mungu na kuandaliwa kwa ajili ya mbingu. Wazazi hawa watakapowatafuta wapendwa wao, na mmoja akaonekana kuwa amepotea kwa sababu ya uzembe, kanisa litajibu nini? Kwa kiwango kikubwa linahusika na wokovu wa watoto hawa yatima. **{WM 225.1}**

Yamkini mmeshindwa kupata imani na upendo wa mvulana kwa kutompa ushahidi halisi wa upendo wenu kwa

kuzuia vivutio fulani. Kama msingetumia pesa yote, mngeweza angalau kwa njia fulani kumtia moyo kwa kumfanya afahamu kuwa hamkuwa wasioijali kwa hali yake. Kwamba upendo na urafiki vinapaswa kuwa vya upande mmoja tu ni kosa. Je! Mmejielimisha wenyewe kuonesha urafiki kiasi gani? Mmejifungia zaidi kwenu wenyewe kwa wenyewe na hamjisikii umuhimu wa kujizungushia angahewa ya ulaini na upole, ambayo hutokana na ubora wa Kweli wa roho. Ndugu na Dada F waliwaacha watoto wao chini ya uangalizi wa kanisa. Walikuwa na ndugu wengi wenye mali nyingi ambao waliwataka watoto hao, lakini hawakuwa waumini, na kama wangeruhusiwa kuwa na uangalizi huu, au kuwa walezi wa watoto hawa,

wangeiongoza mioyo yao mbali na Ukweli kwenda katika makosa, na kuhatarisha wokovu wao. Kwa sababu hawa jamaa hawakuruhusiwa kuwachukua watoto hao, hawakuridhika, na hawajafanya chochote kwa ajili yao. Imani ya wazazi kwa kanisa inapaswa kuzingatiwa, na isisahaulike kwa sababu ya ubinafsi. **{WM 225.2}**

Tunayo maslahi ya dhati kabisa kwa ajili ya watoto hawa. Mmoja tayari amekuza tabia nzuri ya Kikristo na kuolewa na mchungaji wa injili. Na sasa, kama malipo ya utunzaji na mizigo iliyobebwa kwa ajili yake, yeye ni mbebaji wa mzigo wa Kweli kanisani. Anatafutwa kwa ajili ya ushauri na nasaha na wale wasio na uzoefu, na hawatafuti bure. Anao unyenyekevu wa

Kweli wa Mkristo, pamoja na heshima ya kupendeza, ambayo inaweza tu kuhamasisha heshima na imani kwa wote wanaomjua. Watoto hawa wako karibu nami kama vile ni wangu mwenyewe. Sitaacha kuwaangalia, wala kusitisha utunzaji wangu kwa ajili yao. Ninawapenda kwa dhati, kwa upole, kwa urafiki. — *Testimonies for the Church* 2: 327-334. **{WM 226.1}**

Kuhukumiwa kwa Kile Ambacho Hawakukifanya (sin of ommission). - Kuna mayatima ambao wanapaswa kutunzwa; lakini baadhi ya watu hawatathubutu kukubali kuifanya kazi hii, kwa kuwa itawaletea kazi zaidi kuliko wanavyojali au kupenda kuifanya, kwani inawaachia muda mchache wa kujifurahisha wenyewe. Lakini pale Mfalme atakapofanya upelelezi, hawa

watu wasiofanya kitu chochote au wafanyao sifuri, nafsi bahili zenye ubinafsi watagundua kuwa mbingu ni kwa ajili ya wale ambao wamekuwa wafanyakazi, wale ambao wamejinyima kwa ajili ya Kristo. Hakuna masharti yaliyowekwa kwa wale ambao wamewahi kufanya kwa uangalifu maalum huo katika kujipenda na kujitunza wao wenyewe. Adhabu mbaya ambayo Mfalme aliitishia kwa wale walio katika mkono Wake wa kushoto, katika mfano huu, si kwa sababu ya makosa yao uhalifu wao mkubwa. Hawahukumiwi kwa ajili ya mambo waliyoyatenda, bali ni kwa yale ambayo hawakuyatenda. Kwamba Hukufanya mambo yale ambayo Mbingu ilikupa upate kuyafanya. Wewe ulikuwa unajifurahisha mwenyewe, basi nawe

unaweza kuchukua fungu lako pamoja na wale wanaojipendeza wenyewe. - *Testimonies for the Church* 2:27. **{WM 226.2}**

Mwe Mabinti wa Ukarimu. - Kwa dada zangu napenda kusema: Kuweni mabinti wa ukarimu. Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. Labda mmewaza kwamba ikiwa mngeweza kupata mtoto asiye na kosa, mngemchukua na kumtunza; lakini kufadhaisha akili yenu na mtoto anayekosea, kuondoa mawazo mengi na tabia kutoka kwake na kumfundisha upya, kumfundisha kujitawala, ni kazi ambayo unakataa kuifanya. Kuwafundisha wasiojua, kuwahurumia na kuwarekebisha wale ambao daima wamekuwa wakijifunza uovu, si kazi ndogo; lakini Mbingu imewaweka watu

kama hao haswa, katika njia yako. Na hao ni bahati inayojitokeza kwanza kwa sura ya balaa. **{WM 227.1}**

Wale walio na Moyo wa Mama wa Kweli. - Akina mama ambao wamewalea watoto wao kwa busara, wanahisi mzigo wa uwajibikaji, si tu kwa watoto wao wenyewe, bali kwa watoto wa jirani zao. Moyo wa kweli wa huruma wa mama huwaendea wote anaokutana nao. Kwa bidii ya dhati anajitahidi kuzigeuza roho kaidi kuja kwa Kristo. Kwa nguvu Zake Bwana anawezeshwa kutenda mengi. Na wale ambao hawana watoto wana wajibu wa kubeba. Mara nyingi wanaweza kuwapokea ndani ya nyumba zao watoto ambao ni yatima na wasio na makazi. Hawa wanaweza kujifunza kwa ajili ya Kristo kutekeleza mema yale yanayohitajika sana katika

ulimwengu wetu. -*Manuscript* 34, 1899. **{WM 227.2}**

Hebu hali ya watoto wadogo wasiojiweza ivutie moyo wa kila mama, ili aweze kutekeleza upendo wa mama kwa watoto yatima wasio na makazi. Kutokujiweza kwao huvutia kila sifa iliyotolewa na Mungu katika asili ya mwanadamu. — *The Medical Missionary*, Aprili, 1895. **{WM 228.1}**

Katika Angahewa ya Upendo wa Nyumba ya Kikristo. - Kuna watoto wengi ambao wamenyimwa kabisa uongozi wa wazazi na mvuto wa nyumba ya Kikristo. Hebu Wakristo wafungue mioyo yao na nyumba zao kwa wanyonge hawa. Kazi ile ambayo Mungu amewakabidhi kama wajibu wa mtu mmoja mmoja haipaswi kugeuzwa

kwenda kwa taasisi fulani za kukirimu au kuachwa kwa nasibu za fadhila ya ulimwengu. Ikiwa watoto hawana jamaa wanye uwezo wa kuwatunza, hebu washiriki wa kanisa watoe makazi kwa ajili yao. Yeye aliyetuumba alipanga kwamba tunapaswa kuunganishwa katika familia, na tabia ya mtoto itakua vizuri katika angahewa ya upendo ya nyumba ya Kikristo. **{WM 228.2}**

Wengi ambao hawana watoto wao wenyewe wangeweza kufanya kazi nzuri katika kuwatunza watoto wa wengine. Badala ya kutoa kipaumbele kwa wanyama vipenzi (pets), kutoa upendo mwingi mno kwa wanyama bubu, hebu na watoe usikivu wao kwa watoto wadogo, ambao tabia zao wanaweza kuziunda kulingana na mfanano wa kiungu. Weka upendo wako juu ya

washiriki wasio na makazi wa familia ya wanadamu. Angalia ni wangapi kati ya watoto hawa ambao unaweza kuwafunza katika malezi na maonyo ya Bwana. Wengi kwa jinsi hiyo wangefaidika sana. - *The Ministry of Healing*, 203, 204. **{WM 228.3}**

Kwa Nini Kimsingi Wajibu ni wa Kanisa. - Mungu ameweka katika utunzaji wetu maskini na wanaoteseka, na hawa wanapaswa kutunzwa kama Kristo alivyowatunza. Bwana angependa kazi hii ifanyike katika makanisa mbalimbali, badala ya kwamba hawa wenye bahati mbaya wazitegemee hasa taasisi mbalimbali; kwa sababu hii itachukua kutoka mikononi mwa makanisa kazi ile hasa ambayo Mungu amewaagiza kufanya. **{WM 228.4}**

Pale ambapo akina baba na akina mama wanapokufa na kuwaacha watoto wao bila uangalizi, mayatima hao wanapaswa kutunzwa na kanisa. Fungueni mioyo yenu, ninyi mlio na upendo wa Mungu, nanyi wachukueni nyumbani kwenu. - *Manuscript* 105, 1899. **{WM 229.1}**

Nyumba za Mayatima. - Wakati yote yanayoweza kufanyika yamefanyika katika kuwapa riziki mayatima katika nyumba zetu wenyewe, bado kutakuwa na wahitaji wengi ulimwenguni ambao wanapaswa kutunzwa. Wanaweza kuwa wamevaa nguo chakavu, wenye utovu wa adabu, na wanaoonekana kwa nje kutokuwa na mvuto wowote; lakini wamenunuliwa kwa bei, nao ni wa thamani kubwa mbele za Mungu kama vile walivyo watoto wetu wenyewe. Wao

ni mali ya Mungu, ambao kwa ajili yao Wakristo wanawajibika. Roho zao, Mungu anasema, "Nitaitaka mkononi mwako." **{WM 229.2}**

Kuwatunza wahitaji hawa ni kazi njema; lakini bado katika zama hii ya ulimwengu Bwana hatupi maelekezo sisi kama kanisa ya kuanzisha taasisi kubwa na za gharama kubwa kwa kusudi hili. Ikiwa, hata hivyo, kuna watu miongoni mwetu ambao wanahisi kuitwa na Mungu kuanzisha taasisi za utunzaji wa watoto yatima, hebu na wafuate msimamo wao katika wajibu. Lakini katika kuwatunza maskini wa ulimwengu, wanapaswa kuomba msaada kutoka kwa ulimwengu. Hawapaswi kuwakaribia watu wale ambao Bwana amewapa kazi muhimu zaidi iliyowahi kutolewa kwa

wanadamu, kazi ya kuleta ujumbe wa mwisho wa rehema mbele ya mataifa yote, kabila, lugha, na jamaa. Hazina ya Bwana ni lazima iwe na ziada ya ili kuendeleza kazi ya injili katika "maeneo ya ng'ambo au ya mbali na hapa tulipo." **{WM 229.3}**

Hebu wale wanaohisi mzigo wa kuanzisha taasisi hizi wawe na mawakili wenye busara wa kuwasilisha mahitaji yao na kufanya changizo la fedha. Hebu watu wa ulimwengu waamshwe, makanisa ya dhehebu mbalimbali yaweze kuamshwa na watu ambao wanahisi umuhimu kwamba kitu kinapaswa kufanyika kwa niaba ya maskini na yatima. Katika kila kanisa kuna wale wanaomcha Mungu. Hebu hawa wakate rufaa, kwa kuwa kwao Mungu ameitoa kazi hii.... **{WM 230.1}**

Kusudi la nyumba ya mayatima halipaswi kuwa tu kuwapa watoto chakula na mavazi bali kuwaweka chini ya uangalizi wa walimu Wakristo, ambao watawaelimisha katika kumjua Mungu na Mwanawe. Wale wanaofanya kazi katika mwelekeo huu wanapaswa kuwa wanaume na wanawake ambao ni wakarimu na wanaovutiwa na shauku katika msalaba wa Kalvari. Wanapaswa kuwa wanaume na wanawake ambao ni wastaarabu na wenye kujitoa mhanga, ambao watafanya kazi kama Kristo alivyofanya kazi kwa ajili ya kusudi la Mungu na kwa ajili ya wanadamu. - *Testimonies for the Church* 6:286, 287. **{WM 230.2}**

Taasisi Ndogo Ndogo kama za Nyumbani. - Taasisi kama hizo, ili zipate kuwa na ufanisi zaidi, zinapaswa

kuundwa zipate kufanana kwa karibu iwezekanavyo mfano wa nyumba ya Kikristo. Badala ya majengo makubwa, zinazokusanya idadi kubwa pamoja, hebu kuwepo na taasisi ndogo ndogo katika maeneo mbalimbali. Badala ya kuwa katika au karibu na mji fulani au jiji kubwa, zinapaswa kuwa mashambani, ambapo ardhi inaweza kupatikana kwa ajili ya kilimo na watoto wanaweza kukutanishwa na asili na wanaweza kuwa na faida ya mafunzo ya ufundi.

Wale wanaosimamia nyumba kama hiyo wanapaswa kuwa wanaume na wanawake ambao ni wakarimu, wastaarabu, na wenye kujitoa; wanaume na wanawake ambao hufanya kazi kutokana na upendo kwa Kristo, na ambao huwafundisha watoto kwa ajili

Yake. Chini ya utunzaji kama huo wengi wasio na makazi na waliotelekezwa wanaweza kuandaliwa kuwa washiriki wenye manufaa kwa jamii, kuwa heshima kwa Kristo wao wenyewe, na katika zamu yao kuwasaidia wengine. - *The Ministry of Healing*, 205-206. **{WM 230.4}**

Umuhimu wa Kutafuta Ushauri. - Mungu hatawabariki wale wanaofanya kazi bila kuchukua ushauri kutoka kwa ndugu zao. Mwadventista wa Sabato yeyote ambaye anadhani kwamba yeye mwenyewe ni mkamilifu kabisa, na kwamba wakati wote anaweza kufuata akili yake mwenyewe na hukumu, hafai kuaminiwa; kwa maana hatembei katika nuru kama Kristo alivyo katika nuru. Kutakuwapo na wengi ambao hawana utambuzi sahihi wa kile

wanachokifanya. Watu wanahitajika kuwa na mawazo dhahiri, hali ya kina ya mambo ya kiroho. Katika utumishi Wake Mungu anataka sana kila mtu aende kwa busara, akipima sababu zinazochochea matendo yake. - *Manuscript* 26, 1902. **{WM 231.1}**

Kama Tungelitii Mafundisho ya Mungu. - Neno la Mungu limejaa tele mafundisho kuhusu ni jinsi gani tunapaswa kumtendea mjane, yatima, na mhitaji, maskini anayeteseka. Kama wote wangelitii agizo hili, moyo wa mjane ungeimba kwa furaha; watoto wadogo wenye njaa wangelishwa; fukara angelivalishwa; na wale walio karibu kuangamia wangehuishwa. Malaika wa mbinguni wanatazama, na wakati, watakapojazwa na ari kwa ajili ya heshima ya Kristo, tunajiweka katika

mkondo wa majaliwa ya Mungu, wajumbe hawa wa mbinguni watatupa nguvu mpya ya kiroho, ili tuweze kupambana na shida na kuvishinda vizuizi. - *Testimonies for the Church* 6:284, 285.**{WM 231.2}**

Sura ya Ishirini na Nane-Kuasili Watoto

Hebu Familia na Ziwaasili/ziwachukue Watoto (adopt wasio na wazazi na kuwatunza kama ni wao wenyewe). - Kuna kazi maalum ya kufanywa kwa ajili ya watoto wenye

umri mkubwa. Hebu familia za imani yetu ambao makanisani wanaweza kufanya hivyo, wawaasili watoto hawa wadogo, nao watapata baraka kwa kufanya hivyo. - *Letter* 205, 1899. **{WM 232.1}**

Kuna watu ambao hawana watoto wao wenyewe, ambao wanaweza kufanya vyema kwa kuwapanga/kuwaasili watoto. Wale ambao hawana jukumu takatifu la kulitangaza Neno na kufanya kazi moja kwa moja kwa ajili ya wokovu wa roho, wana majukumu katika nyanja zingine za kazi. Ikiwa wamewekwa wakfu kwa Mungu, na wana sifa za kukalibu na kuunda akili za mwanadamu, Bwana atawabariki katika kuwatunza watoto wa wengine.**{WM 232.2}**

Lakini hebu watoto wa waumini wapate wema wetu wa kwanza. Wapo miongoni mwa Watunza Sabato familia nyingi sana za watoto ambazo hazitunzwi vizuri. Wazazi wengi hutoa ushahidi kwamba hawajajifunza kutoka kwa Kristo masomo ambayo yangewafanya kuwa watunzaji/walezi salama wa watoto. Watoto wao hawapati mafunzo sahihi. Na miongoni mwetu kuna watoto wengi ambao kifo kimewanyang'anya malezi ya wazazi wao. Wapo wale ambao wanaweza kuchukua baadhi ya watoto hawa na kujitahidi kuunda/kukalibu na kuunda tabia zao kulingana na kanuni za Biblia. - *Manuscript* 35, 1896. **{WM 232.3}**

Mungu ana watu katika ulimwengu huu, na wapo wengi ambao wanaweza kuwapanga/kuwaasili watoto na

kuwatunza kama hao walio wadogo wa Mungu. - *Letter* 68, 1899. **{WM 232.4}**

Watoto wa Waumini. - Bwana angependa kila kanisa lizingatie kuwa ni wajibu wa kidini ulio juu yao kuwapanga/kuwaasili watoto wa wale ambao wazazi wao wamekufa katika imani. Hebu familia na ziwachukue watoto hawa yatima. - *Manuscript* 44, 1900.**{WM 232.5}**

Ushauri kwa Wanandoa Wasio na Mtoto. - Hamjahisi kwamba iliwapasa kuwa na shauku na wengine, kufanya hali zao kuwa zenu wenyewe, na kudhihirisha shauku isiyo na ubinafsi kwa wale ambao hasa wako katika uhitaji mno wa msaada. Hamjaenda ili mpate kuwasadia wahitaji kabisa, wale wasiojiweza kabisa.**{WM 233.1}**

Kama mngelikuwa na watoto wenu wenyewe ambao wangelihitaji utunzaji, mapenzi, na upendo, msingejifungia wenyewe kiasi hicho kwa ajili ya masilahi yenu wenyewe. Ikiwa wale ambao hawana watoto, na ambao Mungu amewaweka kuwa mawakili wa mali, wangepanua mioyo yao ili wapate kuwatunza watoto ambao wanahitaji upendo, utunzaji, na mapenzi, na msaada kwa mali ya ulimwengu huu, wangekuwa na furaha zaidi kuliko walivyo leo. Maadamu vijana ambao hawana huduma ya upendo wa baba wenye kuhurumia wala upendo laini wa mama wanakabiliwa na ushawishi upotoshao wa siku hizi za mwisho, ni wajibu wa mtu fulani kutoa nafasi ya baba na mama kwa baadhi yao. Jifunze

kuwapa upendo, mapenzi na huruma. **{WM 233.2}**

Wote wanaokiri kuwa na Baba mbinguni, ambaye wanatumaini kuwa atawajali, na mwishowe kuwapeleka katika makao ambayo amewaandalia, wanapaswa kuhisi wajibu mzito ulio juu yao wa kuwa marafiki kwa wale wasio na marafiki na baba kwa mayatima, kuwasaidia wajane na kuwa na faida fulani ya kiutendaji katika ulimwengu huu kwa kuwanufaisha wanadamu. Wengi hawajayaona mambo haya katika nuru sahihi. Ikiwa wanaishi kwa ajili yao wenyewe tu, hawatakuwa na nguvu kubwa kuliko ile inayohitajika na jambo hili. —*Testimonies for the Church* 2:328, 329.**{WM 233.3}**

Je, Ni Mapenzi ya Mungu? - Suala la kumpanga/kumuasili mtoto, hasa mtoto mchanga, linahusisha wajibu mzito kabisa. Haupaswi kuangaliwa kwa juu juu.... Swali kwa kila mmoja kuamua ni, Je! Katika kufanya hivi nitakuwa nikitimiza matakwa yangu mwenyewe tu, au ni wajibu ambao Bwana amenipangia? Je! Hii ndiyo njia Yake, au njia ya uchaguzi wangu mwenyewe? Wote wanapaswa kuwa watenda kazi wa Mungu. Hakuna hata mmoja anayeachiliwa. Vipaji vyako si vyako mwenyewe, kutumia kama utakavyofikiria. Uliza, Bwana angetaka nifanye nini na vipaji Vyake alivyovikabidhi? -*Manuscript* 35, 1896. **{WM 233.4}**

Chunguza Nia. - Tunahitajika kwa uangalifu kuichunguza mioyo yetu na

kuzisoma nia zetu. Ubinafsi unaweza kuchochea hamu ya kufanya kile kinachoonekana kuwa ni kitendo kisicho na ubinafsi na cha kusifiwa. Sababu ambayo wengi huisukumiza kwa kutamani kumpanga mtoto, hamu ya kitu fulani ambacho wangeweza kukifanya kuwa kiini cha mapenzi yao, hudhihirisha ukweli kwamba mioyo yao haijalengwa kwa Kristo; haijazama katika kazi Yake. - *Manuscript* 35, 1896. **{WM 234.1}**

Je, Wachungaji Wawaasili Watoto. - Swali limeulizwa kama mke wa mchungaji anapaswa kuasili watoto wachanga. Ninajibu: Ikiwa hana mwelekeo au uwezo wa kushiriki katika kazi ya umisionari nje ya nyumbani kwake, na anahisi kuwa ni wajibu wake kuwaasili watoto yatima na kuwatunza,

anaweza kufanya kazi njema. Lakini hebu kwanza uchaguzi wa watoto ufanywe kutoka kwa wale ambao wameachwa yatima na wazazi watunzaji wa Sabato. Mungu atawabariki wanaume na wanawake pale ambapo kwa mioyo ya hiari wanashiriki nyumba zao pamoja na hawa wasio na nyumba. **{WM 234.2}**

Lakini kama mke wa mchungaji anaweza mwenyewe kushiriki katika kazi ya kuelimisha wengine, atapaswa kuweka wakfu nguvu zake kwa Mungu kama mfanyakazi Mkristo. Atapaswa kuwa msaidizi wa kweli wa mumewe, akimsaidia katika kazi yake, akitumia vyema akili yake, na kusaidia kutoa ujumbe. Njia iko wazi kwa ajili ya

wanawake wanyenyekevu, waliojiweka wakfu, wanaotukuzwa kwa neema ya Kristo, kuwatembelea wale wanaohitaji msaada na kutoa nuru kwa roho zilizokata tamaa. Wanaweza kuwainua walioinama chini kwa kuomba pamoja nao na kuwaelekeza kwa Kristo. Walio kama hao hawapaswi kutoa muda na nguvu zao kwa binadamu mmoja mdogo asiyejiweza ambaye anahitaji matunzo/utunzaji na uangalifu wa siku zote. Hawapaswi kwa jinsi hiyo kufunga mikono yao kwa hiari. —*Testimonies for the Church* 6:285.**{WM 234.3}**

Labda Mungu Ameizuia Baraka Hii. - Familia yenye utaratibu mzuri, yenye nidhamu itakuwa na ushawishi wenye nguvu kwa ajili ya mema. Lakini kama huna watoto wako mwenyewe, inawezekana kwamba Bwana ana kusudi

la hekima katika kukuzuilia baraka hii. Haipaswi kuchukuliwa kama ushahidi kwamba ni wajibu wako kuasili mtoto. Katika hali fulani hii inaweza kuwa jambo linalofaa. Ikiwa Bwana anakuambia umchukue mtoto mchanga umlee, basi wajibu huo utakuwa wazi mno kuweza kueleweka vibaya. Lakini kama kanuni, jambo hili halitakuwa busara kwa mke wa mchungaji kujifunga na mzigo mkubwa zaidi au vikwazo kwa jukumu kama hilo.... **{WM 235.1}**

Ikiwa mwenzi wa mchungaji ameungana na mumewe katika kazi ya kuokoa roho, hii ni kazi ya juu kabisa anayoweza kuifanya. Lakini utunzaji wa mtoto mdogo ungeweza kushughulisha usikivu wake, kiasi kwamba asingeweza kuhudhuria mikutano na kufanya kazi kwa mafanikio katika kutembelea watu

na juhudi za binafsi. Hata kama ataongozana na mumewe, mtoto huyu mara nyingi ndiye atakayekuwa kiini cha mawazo na mazungumzo, na ziara hiyo inafanywa kukosa matokeo yoyote. Wale ambao Mungu amewaita kuwa wafanyakazi pamoja na Yeye hawapaswi kuwa na sanamu za kushughulisha mawazo na mapenzi ambayo Angetaka yaelekezwe katika mielekeo mingine. - *Manuscript* 35, 1896. **{WM 235.2}**

Daima Weka Mtazamo Sahihi wa Wajibu. – Umuhimu mkubwa ni lazima uwekwe katika kazi ambayo tunaifanya. Hatupaswi kuchukua mizigo mikubwa katika utunzaji wa watoto wachanga. Kazi hii inafanywa na wengine. Tunayo kazi maalum ya kuwatunza na kuwaelimisha watoto umri mkubwa zaidi. Hebu familia

ambazo zinaweza kufanya hivyo ziwapange/ziwaasili watoto hao wadogo, nao watapata baraka kwa kufanya hivyo. —*Testimonies for the Church* 6:246, 247. **{WM 235.3}**

Sura ya Ishirini na Tisa - Utunzaji wa Wazee

Kutunzwa kwa Heshima na Upole au tabia nyororo. - Suala la kuwatunza ndugu na dada zetu wazee ambao hawana nyumba linasisitizwa kila wakati. Nini kifanyike kwa ajili yao? Nuru ambayo Bwana amenipa imerudiwa: Si jambo bora kuanzisha taasisi kwa ajili ya utunzaji wa wazee, ili wapate kuwa pamoja kama jamii. Wala

hawapaswi kupelekwa mbali na nyumbani kwa ajili ya kupata huduma. Hebu watu wa kila familia wawahudumie jamaa zao. Pale ambapo hili haliwezekani kazi ni ya kanisa, na inapaswa kupokelewa kama wajibu na kama upendeleo. Wote walio na roho ya Kristo watawachukulia walio dhaifu na wazee kwa heshima na upole wa pekee. —*Testimonies for the Church* 6:272. **{WM 237.1}**

Kubaki Kati ya Marafiki na Ndugu. - Wazee pia wanahitaji mivuto yenye kusaidia ya familia. Katika nyumba za ndugu na dada katika Kristo inawezekana kwa karibu kuwafidia kupotewa kwa nyumba zao wenyewe. Ikiwa watatiwa moyo kushiriki katika masilahi na kazi za kaya, itawasaidia kuhisi kuwa kufaa kwao hakujafikia

mwisho. Fanya wapate kuhisi kwamba msaada wao unathaminiwa, kwamba bado kuna kitu cha kufanya katika kuwahudumia wengine, na itachangamsha mioyo yao na kuyapa maisha yao shauku. **{WM 237.2}**

Kadiri inavyowezekana hebu wale ambao vichwa vyao vinageuka kuwa vyeupe na mvi na hatua zao kupungua nguvu kunaonesha kwamba wanakaribia kaburi wabaki miongoni mwa ushirika wa marafiki na ushirikiano uliozoeleka. Hebu na waabudu miongoni mwa wale ambao wamewajua na kuwapenda. Hebu na watunzwe kwa mikono ya upendo na iliyo laini/miororo.... **{WM 237.3}**

Uwepo katika nyumba zetu wa mmojawapo wa hawa wasiojiweza ni

fursa ya thamani ya kushirikiana na Kristo katika huduma Yake ya rehema na kukuza sifa bainifu na tabia kama Yake. Kuna baraka katika ushirikiano wa wazee na vijana. Vijana wanaweza kuleta uchangamfu katika mioyo na maisha ya wazee. Wale ambao kushikilia kwao maisha kunadhoofika wanahitaji faida ya mgusano na matumaini, nishati na uchangamfu wa vijana. Na vijana wanaweza kusaidiwa na hekima na uzoefu wa wazee. Zaidi ya yote, wanahitajika kujifunza somo la huduma isiyo ya ubinafsi. Uwepo wa mtu anayehitaji huruma na ustahimilivu na upendo wa kujitolea ungekuwa baraka isiyo kifani kwa kaya nyingi. Ingeyafanya kuwa matamu na kuyatakasa maisha ya nyumbani na kuleta kwa wazee na vijana neema zile

kama za Kristo ambazo zingewafanya kuwa wazuri kwa uzuri wa Bwana na kujaa tele hazina isiyoharibika ya mbinguni. - *The Ministry of Healing*, 204, 205. **{WM 238.1}**

Taasisi Si Mpango Bora. Watu hawapaswi kuajiriwa ili wapate kutoa muda na talanta zao kwa kazi ya kuwakusanya wazee au yatima pamoja katika shirika kwa ajili ya kuwalisha na kuwavika. Hii sio njia bora ya kuwasimamia kesi hizi....**{WM 238.2}**

Wala si vyema kabisa kusimamisha majengo kwa ajili ya wanaume na wanawake wazee, ili wapate kuwa pamoja katika shirika. Hebu wasaidiwe katika sehemu zile zile ambazo wanaweza kusaidiwa. Hebu ndugu wawatunze ndugu zao wenyewe walio

maskini, na kanisa litunze washiriki wake ambao ni wahitaji. Hii ndiyo kazi ambayo Mungu angependa kanisa liifanye, na watapata baraka katika kuifanya. - *Manuscript* 44, 1900. **{WM 238.3}**

Sura ya Thelathini - Wajibu Wetu kwa Vipofu

Mtendee Kipofu kwa Huruma. - Bwana anataka sana wale waliounganishwa na kazi ya umisionari wa tiba kuwa wamisionari wa kweli. Kwa maneno na matendo wanapaswa kuwa kama Kristo. Hawapaswi kuwa na huruma pale tu wanapohisi msukumo wa kuonesha rehema, wala hawapaswi kutenda kwa ubinafsi kwa wale ambao hasa ndiyo wanaostahili kabisa kazi ya

umisionari wa tiba. Vipofu, kwa mfano, wanapaswa kutendewa kwa huruma. Hebu wamisionari wa tiba watafakari juu ya matendo yao kwa vipofu, ili waweze kujifunza ikiwa kama wamisionari wa kweli kwa Mungu hawangeweza kulifanyia tabaka hili la watu wasio na bahati mambo mengi ambayo wameyaacha bila kufanywa. Kutokana na kile kilichowasilishwa kwangu ninajua kwamba wengi, watu wengi hawajapokea faraja ambayo Kristo angewapa kama angekuwa katika mahali pa wamisionari wetu wa tiba. **{WM 239.1}**

Bwana, Yeye ni Mungu. Anatambua matukio haya ya upuuzaji. Kila tendo baya kama hilo ni kuwasilisha visivyo rehema Zake, fadhili Zake, na ukarimu Wake. **{WM 239.2}**

Nimeagizwa kusema, "Tazama kwa uangalifu, kwa maombi, kwa makini, akili isije ikashughulishwa na shughuli nyingi muhimu za biashara kiasi kwamba utauwa wa kweli hautiliwi maanani, na upendo huzimwa kutoka rohoni, licha ya hitaji kubwa na la kusikitisha la wewe kuwa mkono wa Mungu wa msaada kwa vipofu na kwa wengine wote ambao wana bahati mbaya." Wale wasio na marafiki kabisa huhitaji kuzingatiwa mno. Tumia muda wako na nguvu katika kujifunza kuwa "mwenye bidii katika roho," kutendea kwa haki, na kupenda rehema, "ukimtumikia Bwana." Kumbuka kwamba Kristo anasema, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea

Mimi.” - *Manuscript* 109, 1902. **{WM 239.3}**

Wakati ambapo Mungu ni rafiki wa vipofu na wenye bahati mbaya. Wala hazitolei udhuru dhambi zao. Anataka wapate kushinda, na kukamilisha tabia ya Kikristo kwa jina la Yesu, ambaye alishinda kwa niaba yao. Lakini Yesu anasikitikia udhaifu wetu, na Yuko tayari kutoa nguvu za kustahimili katika jaribio na kupinga majaribu ya Shetani ikiwa tutatupa mzigo yetu Kwake. **{WM 240.1}**

Malaika Huwalinda Vipofu. - Malaika hutumwa kuwahudumia watoto wa Mungu ambao ni vipofu kimwili. Malaika hulinda hatua zao na kuwaokoa kutoka katika maelfu ya hatari, ambazo, bila kujulikana kwao, huzonga njia yao.

Lakini Roho Wake hataambatana nao isipokuwa watahifadhi kwa upendo mkuu roho ya fadhili na watafute kwa bidii kuwa na udhibiti juu ya asili zao na kuleta mapenzi yao na kila uwezo katika kumtii Mungu. Ni lazima wakuze roho ya upendo, na kuyatawala maneno na matendo yao. **{WM 240.2}**

Nilioneshwa kwamba Mungu anataka kuwa watu Wake wawe na huruma zaidi na kuwafikiria wale wenye bahati mbaya kuliko wao. “Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.” Hapa dini ya kweli inafafanuliwa. Mungu anataka kwamba uangalifu ule ule ambao

unapaswa kutolewa kwa mjane na yatima utolewe kwa vipofu na kwa wale wanaoteseka kwa mateso ya udhaifu mwingine wa kimwili. Ukarimu usio na upendeleo ni adimu sana katika zama hii ya ulimwengu. - *Testimonies for the Church* 3:516. **{WM 240.3}**

Waangalizi wa Wale Wasiojiweza. - Ikiwa wapo wale kanisani ambao wangesababisha vipofu kujikwaa, wanapaswa kufikishwa kwenye haki; kwa maana Mungu ametufanya sisi kuwa waangalizi wa vipofu, wenye shida, wajane, na yatima. Kikwazo kinachotajwa katika Neno la Mungu hakimaanishi pande kubwa la mti linalowekwa mbele ya miguu ya kipofu ili kumfanya ajikwae, bali

humaanisha mengi zaidi ya haya. Humaanisha mwelekeo wowote ambayo unaweza kufuatwa ili kudhuru mvuto wa ndugu yao kipofu, kutenda kazi dhidi ya masilahi yake, au kuzuia usitawi wake. **{WM 241.1}**

Ndugu ambaye ni kipofu na maskini na mgonjwa, na ambaye anafanya kila juhudi kujisaidia ili asiweze kuwa tegemezi, anapaswa kutiwa moyo na ndugu zake kwa kila njia inayowezekana. Lakini wale wanaodai kuwa ni ndugu zake, ambao wana matumizi ya viungo vyao vyote (vya kuwawezesha kuona, kusikia, kusema, kuelewa nk.), ambao si tegemezi, lakini ambao hadi sasa wanasahau wajibu wao kwa vipofu kiasi cha kuwatatanisha na

kuwatesa na kuzuia njia yao, wanafanya kazi ambayo itahitaji toba na urejeshwaji kabla Mungu hajakubali maombi yao. Na kanisa la Mungu, ambalo litaruhusu ndugu yao mwenye bahati mbaya kudhulumiwa, au kutendewa mabaya, litakuwa na hatia ya dhambi mpaka litakapofanya yote yaliyo katika uwezo wake kufanya kosa hilo kusahihishwa. -*Testimonies for the Church* 3:519, 520. **{WM 241.2}**

Mtazamo wa Rehema. - Ninatamani kwamba sote tungeweza kuona kama Mungu anavyoona. Ninatamani kwamba wote wangetambua jinsi ambavyo Mungu anawaangalia wale watu wanaokiri kuwa wafuasi wa Kristo, ambao wana baraka ya kuona na faida ya mali kwa faida yao, na ambao bado wanahusudu mafanikio

madogo anayofurahia kipofu maskini na ambao wangejinufaisha wenyewe, wakiongeza akiba zao za mali, kwa hasara ya ndugu yao anayeteseka. Hii inachukuliwa na Mungu kama ubinafsi wa jinai mbaya kabisa, na ni dhambi ya kukasirisha, ambayo hakika ataiadhibu. Mungu kamwe hasahau. Yeye haangalii mambo haya kwa macho ya kibinadamu na kwa hukumu baridi, isiyohisi, ya kibinadamu. Yeye haangalii mambo kutokana msimamo wa kidunia, bali kutokana na msimamo wa rehema, huruma, na upendo usio na kikomo. — *Testimonies for the Church* 3:514, 515. **{WM 241.2}**

Kipofu Mara Nyingi Hunyanyaswa. - Kwa wale wanaothubutu kushughulika bila huruma, Mungu atashughulika nao

kama walivyoshughulika na wale waliowaomba msaada. Nimeambiwa kwamba vipofu mara nyingi wameshughulikiwa kwa namna isiyo na huruma. **{WM 242.1}**

Huruma ya kweli kati ya mwanadamu na mwanadamu mwenzake inapaswa kuwa ndio ishara ya kuwapambanua wale wanaompenda na kumcha Mungu kutoka kwa wale ambao hawaijali sheria yake. - Manuscript 117, 1903. **{WM 242.2}**

Timiza Wajibu Wako kwa Wasiojiweza. - Ni ajabu kwamba Wakristo bayana wanapuuza mafundisho ya wazi, ya kujenga ya Neno la Mungu na hawahisi majuto ya dhamiri. Mungu anaweka juu yao wajibu wa kuwatunza wasiojiweza, vipofu,

vilema, mjane, na yatima; lakini wengi hawafanyi bidii kuuzingatia. Ili kuwaokoa watu kama hao, Mungu mara nyingi huwaleta chini ya fimbo ya mateso, na kuwaweka katika nafasi sawa na ya watu wale waliokuwa na haja ya msaada na huruma yao lakini ambao hawakuvipokea kutoka katika mikono yao. - *Testimonies for the Church* 3:517. **{WM 242.3}**

Sehemu ya IX Waliotengwa na Jamii

Wazo la Thamani

Kuna kazi inayopaswa kukamilishwa kwa ajili ya wengi ambao itakuwa si ya manufaa hata kidogo kwako wewe kwa kusema ukweli, kwa maana

wasingeweza kuielewa. Lakini unaweza kuwafikia kwa njia ya matendo ya ukarimu yasiyopendelea. Kuna waliotengwa na jamii, watu ambao wamepoteza sura ya Mungu, ambao lazima kwanza watunzwe, walishwe, wasafishwe, na kuvikwa kwa heshima. Halafu hawapaswi kusikia chochote isipokuwa kuhusu Kristo, upendo Wake mkuu na nia Yake ya kuwaokoa. Hebu roho hizi zinazoangamia wahisi kwamba yote uliyowafanyia yalifanywa kwa sababu ya upendo wako kwa ajili ya roho zao. **{WM 244.1}**

Bwana hutumia wakala wa mwanadamu. Uungu na ubinadamu vinapaswa kuungana, kuwa watenda kazi pamoja katika kazi ya kuinua na kurejesha sura ya kimaadili ya Mungu ndani ya mwanadamu.... Tembea kwa

akili na uvumilivu. Usivunjike moyo ikiwa mwanzoni hutakuwa na huruma na ushirikiano ambao unautarajia. Ikiwa unafanya kazi, ukimfanya Bwana kuwa tegemeo lako, uwe na hakika kwamba Bwana siku zote huwasaidia wanyenyekevu, wapole, na wanaojishusha. Lakini unahitaji utendaji wa Roho Mtakatifu juu ya moyo na akili yako mwenyewe, ili upate kujua jinsi ya kufanya kazi ya msaada wa Kikristo. Waombee sana wale unaojaribu kuwasaidia. Waruhusu kuona kwamba utegemezi wako uko juu ya mamlaka iliyo juu zaidi, nawe utaongoa roho. - *Letter* 24, 1898. **{WM 244.2}**

Yuda

[22] Wahurumieni wengine walio na shaka,
[23] na wengine waokoeni kwa kuwanyakua katika moto; na wengine wahurumieni kwa hofu, mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili

Sura ya Thelathini na Moja - Kufanya Kazi kwa Ajili ya Watu

Waliotengwa na Jamii

Mwaliko wa Injili kwa Matabaka Yote. - Kristo alionyesha baraka za kiroho za injili kwa karamu ya duniani, mwaliko wa kuja karamuni. Alionesha kujishusha kwa namna ya ajabu kwa Mungu katika mwaliko wa dhati wa bwana wa karamu kwa wote ambao wangekubali kuja. Wito maalum wa injili utakaotolewa karibu na mwisho wa historia ya dunia pia unawasilishwa. **{WM 245.1}**

Mwaliko kwanza ulipaswa kwenda kwenye njia kuu, kuwaalika wote kuja kwenye karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo. Ujumbe huo kwa watu

waliopendelewa sana ulikataliwa. **{WM 245.2}**

Wito uliofuata ulitolewa kwa tabaka la maskini zaidi - maskini, viziwi, walemavu, vipofu. Hawa hawakutukuzwa kwa miradi hii ya kutaka makuu. Ikiwa wangeukubali mwaliko huo, wangeweza kuja. Ujumbe huu ulitolewa, na watumishi walileta ripoti, "Bwana, hayo uliyoagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa ingaliko nafasi." **{WM 245.3}**

Kisha Bwana aliwaambia wafanyakazi Wake, "Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba Yangu ipate kujaa." - *Manuscript* 81, 1899.**{WM 245.4}**

"Washurutishe kuingia ndani," Kristo anatuambia.... Kwa kulitii Neno hili ni lazima twende kwa mataifa walio karibu nasi na wale walio mbali. "Watoza ushuru na makahaba" ni lazima wasikie mwaliko wa Mwokozi. Kupitia kwa fadhili na uvumilivu wa wajumbe Wake mwaliko huu unakuwa ni nguvu ya kubidisha ya kuwainua wale ambao wamezama katika kina cha chini kabisa cha dhambi. - *The Ministry of Healing*, 164. **{WM 245.5}**

Kristo Anatamani Sana Kutengeneza Upya Tabia. – Watu wengine haijalishi wawe chini- duni kiasi gani, wawe wameanguka kiasi gani, wawe wamefedheheshwa na kudhalilishwa kiasi gani, hatupaswi kuwadharau na kuwapita bila kujali; bali tunapaswa kuzingatia ukweli kwamba

Kristo amekufa kwa ajili yao....Kristo anataka sana kutengeneza upya tabia ya mwanadamu iliyoharibika, ili apate kurejesha sura ya kimaadili ya Mungu kwa wanadamu. - *The Review and Herald*, Oktoba 15, 1895. **{WM 246.1}**

Anawachukulia Kuwa ni Wenye Thamani Kubwa. - Kila nafsi ni lengo la shauku yenye kupenda ya Yeye aliyeyatoa maisha Yake ili awarudishe watu kwa Mungu. Shauku hii ya dhati na yenye kuvumilia iliyooneshwa na Baba yetu wa mbinguni inatufundisha kwamba wanyonge na waliotengwa na jamii hawapaswi kupitwa bila kujaliwa au kuonyeshwa kuwa wanabaguliwa. Wao ni wa Bwana kwa uumbaji na kwa ukombozi. Kama tungeachwa sisi wenyewe kuhukumu, tungewachukulia wengi ambao wamedhilika kuwa ni

wabaya wasioweza kuponyeka. Lakini Bwana anaona thamani ya fedha ndani yao. Ingawa hawatafuti msaada, Yeye anawaona kuwa ni wa thamani. Yeye anayeona yaliyofichika chini anajua jinsi ya kushughulika na akili za wanadamu. Anajua jinsi ya kuwaleta watu katika toba. Anajua kwamba ikiwa watajiona kuwa ni wenye dhambi, watatubu na kuongolewa na Ukweli. Hii ndiyo kazi tunayopaswa kujishughulisha nayo. - *Letter* 80, 1898. **{WM 246.2}**

Usiulize -"Je, Wanastahili?" - Kwa kuwasihi wale wanaokosea, wale wanaojaribiwa, na waathirika wanyonge wa uhitaji na dhambi, Mkristo haulizi, Je, wanastahili? bali, Ni jinsi gani ninaweza kuwanufaisha? Katika mnyonge kabisa, na yule aliyedhalilishwa kabisa, anaona roho

ambazo Kristo alikufa ili apate kuziokoa, na ambao kwa ajili yao Mungu amewapa watoto Wake huduma ya upatanisho. -*Mount of Blessing*, uk. 40. **{WM 246.3}**

Kugunduliwa na Kazi ya Umisionari wa Tiba. - Nimearifiwa kwamba kazi ya umisionari wa tiba itagundua, katika vina virefu sana vya uharibifu, wanaume ambao, ingawa wamesalimu amri kwa tabia potovu, isiyo na kiasi, wataitika kwa aina sahihi ya kazi. Lakini inabidi watambuliwe na kutiwa moyo. Juhudi thabiti, zenye subira, zenye ari, zitahitajika kwa ajili ya kuwainua. Hawawezi kujirejesha wenyewe. Wanaweza kusikia wito wa Kristo, lakini masikio yao ni mazito mno kuweza kuelewa maana yake; macho yao ni kipofu mno kuweza kuona kitu

chochote kizuri kilicho tayari kwa ajili yao. Wamekufa katika makosa na dhambi. Lakini bado hata hawa hawapaswi kuachwa nje ya karamu ya injili. Wanapaswa kupokea mwaliko: "Njoni." Ingawa wanaweza kujisikia kutokustahili, Bwana anasema: "Ukawashurutishe kuingia." Usisikilize udhuru wowote. Kwa upendo na huruma washikilie kwa usahihi.... Kazi hii, ikiendeshwa vizuri, itawaokoa wenye dhambi maskini wengi ambao wamepuuzwa na makanisa. - *Testimonies for the Church* 6:279, 280. **{WM 247.1}**

Katika kazi hii ya urejeshaji juhudi nyingi za uangalifu zitahitajika. Hakuna mawasiliano ya kushangaza ya Mafundisho ya Imani ajabu yanapaswa kufanywa kwa roho hizi, lakini pale

wanaposaidiwa kimwili Ukweli kwa ajili ya wakati huu unapaswa kuwasilishwa. Wanaume na wanawake na vijana wanahitajika kuiona sheria ya Mungu na masharti yake yenye athari nyingi. Si shida, wala kazi ya taabu, wala umaskini unaomdhalilisha mwanadamu; bali ni dhambi, uasi wa sheria ya Mungu. Jitihada zinazowekwa kwa ajili ya kuwaokoa waliotengwa na jamii na kudhalilishwa hazitafaa kitu isipokuwa madai ya sheria ya Mungu na hitaji la uaminifu Kwake yametiwa katika akili na moyo. Mungu hajaamrisha kitu chochote ambacho si muhimu katika kufunga ubinadamu pamoja Naye. "Sheria ya Bwana ni kamilifu, Huiburudisha nafsi. ... Amri ya Bwana ni safi, Huyatia macho nuru." "Kwa Neno la midomo yako," asema mwandishi wa

Zaburi, "Nimejiepusha na njia za wenye jeuri." Zaburi 19:7, 8; 17: 4. **{WM 247.2}**

Malaika wanasaidia katika kazi hii kuwarejesha wale walioanguka na kuwarudisha Kwake Yule ambaye ameyatoa maisha Yake kwa ajili ya kuwakomboa, na Roho Mtakatifu anashirikiana na huduma ya wakala wa kibinadamu ili kuamsha nguvu za kimaadili kwa kufanya kazi moyoni, kukemea dhambi, kuwajulisha kuhusu haki, na hukumu. — *Testimonies for the Church* 6:259, 260. **{WM 248.1}**

Kufanya Kazi kwa Ajili ya Wasio na Kiasi. [Maelezo zaidi na ushauri juu ya mada hii yatapatikana katika *The Ministry of Healing*, 171-182, na mkusanyiko kamili zaidi wa hivi karibuni uliopewa jina *Temperance*.] -

Jitihada kubwa zaidi zinapaswa kufanywa kwa niaba ya wale walio katika kifungo cha mazoea mabaya. Kila mahali kuna kazi ya kufanywa kwa ajili ya wale ambao kupitia kukosa kiasi wameanguka. Katikati ya makanisa, taasisi za kidini, na nyumba bayana za Kikristo, vijana wengi wanachagua njia ya uharibifu. Kupitia katika mazoea ya kukosa kiasi wanaleta magonjwa juu yao wenyewe, na kupitia katika uroho wa kupata pesa kwa ajili ya anasa za dhambi wanaanguka katika mazoea yasiyo ya uaminifu. Afya na tabia zimeharibika. Wakiwa ni wageni kwa Mungu, waliotengwa na jamii, roho hizi maskini zinahisi kwamba hawana tumaini kwa maisha haya au kwa maisha yajayo. Mioyo ya wazazi imevunjika. Watu husema juu ya hawa

wapotovu kama wasio na matumaini, lakini hivyo sivyo Mungu anavyowachukulia. Anaelewa hali zote ambazo zimewafanya kuwa kama walivyo, na anawaangalia kwa huruma. Hili ni tabaka linalohitaji msaada. Kamwe usiwape nafasi ya kusema, "hakuna mtu anayeijali roho yangu." **{WM 248.2}**

Miongoni mwa wahanga wa kukosa kiasi ni wanaume wa matabaka yote na taaluma zote. Watu wa hali vyeo vya juu, wenye vipaji adhimu, wenye mafanikio makubwa, wamesalimu amri katika kuendekeza hamu ya chakula, kiasi kwamba hawajiwezi kupinga majaribu. Baadhi yao ambao hapo awali walikuwa katika umiliki wa mali nyingi sasa hawana nyumba, hawana marafiki, wako katika mateso, taabu, magonjwa,

na udhilifu. Wamepoteza uwezo wao wa kujitawala. Isipokuwa mkono wa msaada umenyoshwa kwao watazama chini zaidi na zaidi. - *The Ministry of Healing*, 171, 172. **{WM 249.1}**

Vita Vilivyopiganwa Tena na Tena. - Hakuna kazi ya kubahatisha, ya ovyo ovyo, iliyo holela au isiyo na taratibu inayopaswa kufanywa. Kushikilia kwa uthabiti roho zinazokaribia kuangamia kunamaanisha zaidi ya kumwombea mlevi na kisha, kwa sababu analia na kukiri uchafuzi wa nafsi yake, kumtangaza kuwa ameokoka. Tena na tena vita hivi ni lazima vipiganwe. — *Testimonies for the Church* 8:196.**{WM 249.2}**

Ni lazima uwashikilie imara wale ambao unajaribu kuwasaidia, vinginevyo ushindi hautakuwa wako

kamwe. Daima watajaribiwa kutenda maovu. Tena na tena karibu watashindwa na kutamani sana kunywa kileo (uraibu); tena na tena wanaweza kuanguka; lakini kwa sababu ya hii, usiache juhudi zako. - *The Ministry of Healing*, 173. **{WM 249.3}**

Kazi Hii Si ya Bure. - Wakati wengine, juhudi zao za kibinadamu zikiwa zimeungana na za Mwenyezi Mungu, wanajitahidi kufikia vina vya majonzi na taabu za wanadamu, baraka za Mungu zitakaa juu yao kwa wingi. Ingawa ni wachache tu wanaokubali neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, kazi yao haitakuwa bure; kwa kuwa nafsi moja ni ya thamani, ya thamani sana, mbele za Mungu. Kristo angekufa kwa ajili ya nafsi moja ili mtu huyo apate kuishi enzi za umilele.... **{WM 249.4}**

Nafsi nyingi zinaokolewa, zinavutwa kwa ghafla kutoka mikononi mwa Shetani, na wafanyakazi waaminifu. Mtu fulani ni lazima awe na mzigo wa roho ili aweze kupata wale waliopotea kwa Kristo. Uokoaji wa roho moja ambaye Shetani ameshangilia ushindi juu yake husababisha furaha miongoni mwa malaika wa mbinguni. Wapo wale ambao wameharibu ndani yao sura ya kimaadili ya Mungu. Wavu wa injili ni lazima uwakusanye ndani maskini hawa waliotengwa na jamii. Malaika wa Mungu watashirikiana na wale wanajihusisha katika kazi hii, ambao hufanya kila juhudi ya kuokoa roho zinazoangamia, ili kuwapa fursa ambazo wengi hawajawahi kuwa nazo. Hakuna njia nyingine ya kuwafikia ila kwa njia ya Kristo. Yeye daima alifanya kazi ya

kutuliza mateso na kufundisha haki. Ni kwa njia hiyo tu wenye dhambi wanaweza kuinuliwa kutoka katika vina vya uharibifu. — *Testimonies for the Church* 8:72, 73. **{WM 249.5}**

Kufanya Kazi kwa Upendo. - Wafanyakazi ni lazima wafanye kazi kwa upendo, wakiwalisha, wakiwasafisha, na kuwavika wale wanaohitaji msaada wao. Kwa njia hii hawa waliotengwa na jamii wanaandaliwa kujua kwamba mtu fulani anazijali roho zao. Bwana amenionesha kuwa wengi wa maskini hawa waliotengwa kutoka katika jamii, kupitia katika huduma ya mawakala wa kibinadamu, watashirikiana na nguvu ya kiungu na kutafuta kurudisha sura ya kimaadili ya Mungu kwa wengine ambao kwa ajili yao Kristo amelipa bei ya damu Yake Mwenyewe. Wataitwa wateule wa

Mungu, wenye thamani, nao watasimama karibu na kiti cha enzi cha Mungu....**{WM 250.1}**

Bwana anafanya kazi kuwafikia wale walioharibika tabia kabisa. Wengi watajua maana ya kuvutwa kwa Kristo, lakini hawatakuwa na ujasiri wa kimaadili wa kupambana dhidi ya hamu ya kula na uroho/uchu. Lakini wafanyakazi hawapaswi kuvunjika moyo kwa sababu ya hili; kwa maana imeandikwa, "Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." 1 Timotheo 4:1. Je! Ni wale tu waliookolewa kutoka katika vina vya chini kabisa ambao hurudi nyuma? Wapo wale katika huduma ambao wamekuwa na nuru na maarifa ya

Ukweli, ambao hawatakuwa washindi. Hawazuii tamaa zao za chakula na uchu au kujikana kwa ajili ya Kristo. Watu maskini waliotengwa na jamii, hata watoza ushuru na wenye dhambi, watalishika tumaini lililowekwa mbele yao katika injili na wataingia katika ufalme wa mbinguni mbele ya wale ambao wamepata fursa kubwa na nuru kuu, lakini ambao wametembea gizani.... Ndugu na dada zangu, chukueni msimamo wenu upande wa Bwana, nanyi mwe watenda kazi pamoja na Kristo wenye ari, bidii, na ushujaa, mkifanya kazi Naye katika kuwatafuta na kuwaokoa waliopotea. —*Testimonies for the Church* 5:74, 75.**{WM 250.2}**

Kutokufuata Mbinu za Jeshi la Wokovu. - Bwana ameonesha njia yetu ya kufanya kazi. Kama kanisa hatupaswi

kuiga na kutumbukia katika mbinu za Jeshi la Wokovu. Hii si kazi ambayo Bwana ametupa kuifanya. Wala si kazi yetu kuwashutumu na kusema maneno makali dhidi yao. Kuna roho za thamani, na zenye kujitolea katika Jeshi la Wokovu. Tunapaswa kuwatendea kwa wema. Ndani ya Jeshi hili kuna roho zenye uaminifu, ambazo zinamtumikia Bwana kwa unyofu na ambao wataona nuru kubwa zaidi, wakisonga mbele kuukubali Ukweli wote. Wafanyakazi wa Jeshi la Wokovu wanajaribu kuwaokoa wale waliopuuzwa, waliokandamizwa. Usiwakatishe tamaa. Waache wafanye aina hiyo ya kazi kwa mbinu zao na kwa njia zao wenyewe. Lakini Bwana ameonesha wazi kazi ambayo Waadventista wa Sabato wanapaswa kuifanya. — *Testimonies for the Church*

8:184, 185.**{WM 251.1}**

Kuwasaidia Waliotengwa na Jamii Kupata Kazi Mpya. - Kadiri watoto wa Mungu wanavyojitoa kwa ajili ya kazi hii [kuwarejesha walioanguka], wengi wataushika mkono ulionyoshwa kwa ajili ya kuwaokoa. Wanalazimika kuziacha njia zao mbaya. Baadhi ya waliookolewa wanaweza, kwa njia ya imani kwa Kristo, kuinuka kufikia mahali pa juu pa huduma, na kukabidhiwa majukumu katika kazi ya kuokoa roho. Wanajua kwa uzoefu mahitaji ya wale ambao wanafanya kazi kwa ajili yao, nao wanajua jinsi ya kuwasaidia. Wanajua ni njia gani zinaweza kutumika kwa uzuri kabisa kuwapata tena wale wanaoangamia. Wamejazwa na shukrani kwa Mungu kwa ajili ya baraka walizozipokea. Mioyo

yao huhuishwa kwa upendo, na nguvu zao huimarishwa kwa ajili ya kuwainua wengine ambao hawawezi kuinuka pasipo msaada. Wakichukua Biblia kama kiongozi wao na Roho Mtakatifu kama msaidizi na mfariji wao, wanaipata kazi mpya ikifunguka mbele yao. Kila moja ya roho hizi ambazo zinaongezwa katika jeshi la wafanyakazi, ikipewa vifaa na maelekezo ya jinsi ya kuokoa roho kwa ajili ya Kristo, inakuwa mshirika wa wale waliomletea nuru ya Ukweli. Hivyo Mungu anaheshimiwa na Ukweli Wake kuendelezwa. — *Testimonies for the Church* 6:260. **{WM 251.2}**

Sura ya Thelathini na Mbili - Tahadhari Zilizotangazwa

Kazi katika Makazi duni na ovyo (slums) Zisipigiwe Chuku Kuwa ni Nzuri (zisitukuzwe kuwa ni nzuri).

- Tahadhari lazima zichukuliwe katika kazi hii ya mwisho ambayo

Mwanadamu anayekufa ataifanya. Kuna hatari ya kufanya kazi kwa taswira ya akili kwamba watu ambao hawafai kabisa kujihusisha katika kazi hii takatifu ya Mungu, watajiona wenyewe kuwa wameteuliwa na Mbingu kufanya kazi kwa ajili ya waliotengwa na walioanguka. Kama uzoefu wote, wa kufurahisha na wa kuchukiza ungefafanuliwa, kusingekuwa na watu wengi wanaovutwa na aina hii ya kazi. Wengi wanaingia katika kazi hii kwa sababu wanapenda kile ambacho ni cha mihemko na cha kusisimua. Lakini isipokuwa wameweka nguvu zao zote

katika kazi hii kuu, ya kuokoa roho, wanadhihirisha kwamba hawana roho ya kweli ya umisionari. —*Manuscript* 177, 1899. **{WM 253.1}**

Hatari katika Kufanya Kazi kwa Ajili ya Waliotengwa. - Katika kila juhudi ya kutunza roho kwa bidii yote, mwanadamu anahitaji uweza wa Mungu utunzao. Kuna hatari, hatari ya daima, ya maambukizi katika kazi miongoni mwa walioanguka na kudhilika. Kwa nini, basi, wanaume na wanawake ambao hawajajiandaa kupinga majaribu, na ambao hawana nguvu ya kutosha ya tabia kwa ajili ya kazi hiyo wanajiweka katika mgusano na hatari hii? **{WM 253.2}**

Katika akili za vijana wengi wanaojihusisha na kile kinachojulikana

kama kazi ya umisionari wa tiba matokeo tofauti kabisa ni husababishwa kuliko yale ambayo daktari au yoyote kati ya washirika wake hufikiria. [Marejeleo yamefanywa hapa kwa Dk. J. H. Kellogg, ambaye alikuwa akiongoza kazi iliyokuwa ikipanuka haraka kwa ajili ya waliopotoka na waliotengwa. - Wakusanyaji.] Yeye si mwangalifu kuchunga hila za Shetani zinazomwelekea katika kazi yake mpya na iliyo wazi, na polepole anajitenga na maisha ya nyumbani na mvuto mzuri. Mbele ya kila kijana kama huyo ishara ya hatari inapaswa kuinuliwa. Katika kila mahali ambapo wanaume na wanawake wanafanya kazi kwa ajili ya waliodhilika ni lazima mtu fulani abebe majukumu makubwa, ama sivyo wafanyakazi watakuwa hafifu katika

mtazamo wao, maneno yao, na kanuni zao. **{WM 253.3}**

Wengi watajiunga katika kazi hii, wakifikiri kwamba kwa kufanya hivyo watasaidiwa kutokana na maisha yao ya dhambi; na nafasi inapojitokeza hawa watafikiri kuwa ni sahihi kukwepa kusema Ukweli wote, kutokuwa waaminifu, au kufanya dhambi yoyote ambayo walikuwa na hatia nayo hapo zamani. Kwa kuona hili, wafanyakazi ambao hawaishi katika uhusiano wa karibu na Mungu watabadilishwa, si kutoka katika tabia njema kwenda njema zaidi, bali kutoka kwa tabia yenye kasoro kwenda katika iliyo mbaya zaidi. Watachukua njia na tabia za watendao dhambi kwa uwazi. Watajiunga na watenda maovu katika kukukuza kila taarifa mbaya, na kitambo watapoteza

upendo wote wa ufasaha wa lugha au tabia. Hofu yao kwa Mungu na kupenda haki huchanganywa na aina fulani ya homa ya kidini, ambayo haikubaliki mbele za Mungu. - *Manuscript* 177, 1899.**{WM 254.1}**

Wengi Hupotea kuliko Wanaookolewa. - Ni hatari kuwaweka vijana wa kiume na wa kike kazini miongoni mwa matabaka yaliyotelekezwa. Wanawekwa mahali ambapo wanakutana na kila aina ya uchafu/unajisi, na Shetani hutumia fursa hii kuzingira uharibifu wao. Kufikia hapo wengi hupotea kuliko wanaookolewa na wafanyakazi hawa. Jitihada nyingi zilizofanywa kwa ajili ya waliotelekezwa husababisha kupotea kwa usafi wa wafanyakazi hao. Wale ambao wanajihusisha na kutembelea

nyumba za ukahaba hujiweka katika majaribu ya kuogofya. Siku zote kazi hii ni ya hatari. Ni hila ya Shetani ya kuongoza roho katika majaribu na mazoea ya tamaa. “Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa Kwangu Wanangu wa kiume na wa kike.” **{WM 254.2}**

Kadiri vijana wa kiume na wa kike wanavyojiweka mbali na wale waliopotoka na vitu vya ulimwengu huu vinavyopotosha, ndivyo uzoefu wao wa baadaye utakavyokuwa bora na salama zaidi. Wafanyakazi wa umishonari wa tiba wanapaswa kusafishwa, kuadilishwa, kutakaswa, na kuinuliwa. Wanapaswa kusimama kwenye jukwaa la Ukweli wa milele. Lakini nimeagizwa

kwamba Ukweli haujafanywa kuonekana katika mapana na marefu yake ya Kweli. Matokeo ambayo hufanyiwa kazi huelekea kupotosha akili; kilicho kitakatifu hakitofautishwi na kile kikicho cha kawaida. - *Letter* 162, 1900. **{WM 255.1}**

Ilinde Kazi kwa Utakatifu. - Mambo mengi yamewasilishwa kwangu. Nilioneshwa kuwa kuna kazi ya kufanywa kwa tabaka lililodhilika mno, lakini kwamba jambo hili ni lazima lilindwe kwa uangalifu zaidi, ili kwamba kazi iliyowekwa kwake isiwe ya bure. Vijana wa kiume na wa kike hawapaswi kuwekwa wazi au kuanikwa, kama ambavyo wengi wamekuwa, katika kukutana na matabaka yaliyotelekezwa. Vizuizi thabiti vinapaswa kufanywa, kwani kuna hatari za hakika za kukutana

nazo. Kuna haja ya kuilinda kazi kwa utakatifu. Katika kazi kwa tabaka la chini tahadhari kali kabisa zinapaswa kuzingatiwa. Kuna wengi ambao hawapaswi kwenda katika miji mikubwa kufanya kazi kwa ajili ya waliopotoka zaidi. - *Manuscript* 17, 1901. **{WM 255.2}**

Sura ya Thelathini na Tatu - Wito wa Kazi Yenye Uwiano (kazi yenye balansi)

Dumisha Mtazamo Sahihi. - Kadiri kazi inavyoendelea, hatari zinaibuka ambazo inabidi kujilinda dhidi yake. Kadiri shughuli mpya zinapofunguliwa, kuna mwelekeo wa kufanya mkondo mmoja kuwa ni wenye

kushughulisha mno; kile ambacho kingepaswa kupewa nafasi ya kwanza kinafikiriwa katika nafasi ya pili. Kanisa linahitaji uwezo mpya na uhai, lakini kuna hatari kubwa ya kuchukua mielekeo mipya ya kazi ambayo itapoteza nguvu zao badala ya kuleta uhai kanisani. - *The Daily Bulletin of the General Conference*, Machi 2, 1899. **{WM 256.1}**

Kazi kwa Ajili ya Waliotengwa Si Kiini cha mzigo wa Kazi Yetu. – Hivi karibuni [1899] shauku kubwa imeamshwa kwa ajili ya matabaka kwa ajili ya kuwainua walioanguka na kudhilika. Hii kwa yenyewe ni kazi nzuri. Tunapaswa kuwa na Roho wa Kristo, na tunapaswa kufanya aina ile ile ya kazi ambayo aliifanya kwa wanadamu wanaoteseka. Bwana ana kazi ya

kufanywa kwa ajili ya wale waliotengwa na jamii. Hakuna swali ila kwamba ni wajibu wa wengine kufanya kazi kati yao na kujaribu kuokoa roho zinazoangamia. Hii itakuwa na nafasi yake kuhusiana na kutangazwa kwa ujumbe wa malaika wa tatu na kupokewa kwenye Ukweli wa Biblia. Lakini kuna hatari ya kumlemea kila mtu kwa tabaka hili la kazi, kwa sababu ya mkazo ambao unawekwa katika kuifanya. Kuna hatari ya kuwaongoza watu kuweka nguvu zao zote katika mwelekeo huu, wakati ambapo Mungu amewaita kwenye kazi nyingine.**{WM 256.2}**

Suala kubwa la wajibu wetu kwa ubinadamu ni suala lenye maana kubwa, na neema nyingi za Mungu zinahitajika katika kuamua jinsi ya kufanya kazi ili kukamilisha kiasi kikubwa kabisa cha

wema. Si wote walioitwa kuanza kazi yao kwa kufanya kazi miongoni mwa matabaka ya chini. Mungu hawahitaji wafanyakazi Wake kupata elimu na mafunzo yao ili wapate kujitoa kwa ajili ya matabaka haya peke yake. Utendaji wa Mungu unadhihirishwa kwa njia ambayo itaimarisha imani kwamba kazi hiyo ni ya ubunifu Wake, na kwamba kanuni thabiti ziko chini ya kila tendo. Lakini nimepata maagizo kutoka kwa Mungu kwamba kuna hatari ya kupanga kwa ajili ya waliotengwa na jamii kwa namna ambayo itasababisha matendo ya ghafla na ya kusisimua ambayo yanafanywa kiholela, hapa na pale. Haya hayataleta matokeo yenye manufaa hasa. Tabaka litatiwa moyo kufanya aina ya kazi ambayo itakuwa sawa na kiasi kidogo mno katika kuimarisha sehemu

zote za kazi kwa hatua yenye upatanifu. **{WM 256.3}**

Mwaliko wa injili unapaswa kutolewa kwa matajiri na maskini, walio juu na walio chini, na lazima tubuni njia za kupeleka ukweli katika maeneo mapya na kwa matabaka yote ya watu. Bwana anatuambia, "Bwana akamwambia mtumwa, Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa." Anasema, "Anzeni katika njia kuu; fanyeni kazi vizuri katika barabara kuu; andaeni kundi ambalo kwa kuungana pamoja nanyi linaweza kwenda kufanya kazi ile ile ambayo Kristo aliifanya katika kutafuta na kuwaokoa waliopotea." **{WM 257.1}**

Kristo alihubiri injili kwa maskini, lakini hakufunga kazi Yake kwa tabaka hili. Alifanya kazi kwa wote ambao wangelisikia Neno Lake - si tu kwa watoza ushuru na waliotengwa, bali pia kwa Farisayo tajiri na mwenye elimu, watu mashuhuri wa Kiyahudi, jemadari, na mtawala wa Kirumi. Hii ndio aina ya kazi ambayo daima nimeona kuwa inapaswa kufanywa. Hatupaswi kuchosha kila msuli na neva ya kiroho kufanya kazi kwa ajili ya matabaka ya chini, na kuifanya kazi hiyo kuwa ndio yote katika yote. Kuna wengine ambao tunapaswa kuwaleta kwa Bwana, roho ambazo zinahitaji Ukweli, ambao wanabeba majukumu, na ambao watafanya kazi kwa uwezo wao wote uliotakaswa kwa ajili ya mahali pa juu na pia kwa ajili ya sehemu duni.

Kazi kwa ajili ya matabaka maskini haina kikomo. Haiwezi kamwe kumalizwa, na ni lazima ichukuliwe kama sehemu ya kazi kubwa iliyo kamili. Kutoa usikivu wetu wa kwanza kwa kazi hii, wakati kuna sehemu kubwa za shamba la Bwana zilizo wazi kwa ajili ya utunzaji na bado hazijaguswa, ni kuanza mahali pasipostahili. Kama mkono wa kulia ulivyo kwa mwili, ndivyo kazi ya umisionari wa tiba ulivyo kwa ujumbe wa malaika wa tatu. Lakini mkono wa kulia haupaswi kuwa ndio mwili mzima. Kazi ya kuwatafuta waliotengwa na jamii ni muhimu, lakini haipaswi kuwa kiini kikuu cha utume wetu. - *Manuscript* 3, 1899. **{WM 258.1}**

Hatujaitwa Kujenga Nyumba kwa Ajili ya Wanawake Waliotelekezwa au Watoto. -

Lazima nizungumze wazi juu ya mambo kadhaa ambayo lazima yalindwe. Hatupaswi kuingia katika kazi ya kugharimia nyumba za wanawake waliotelekezwa au watoto wachanga. Jukumu hili linaweza kubebwa vizuri zaidi na familia, ambazo zitapaswa kuwatunza wale wanaohitaji msaada katika mwelekeo huu.-*Letter* 11, 1900. **{WM 258.2}**

Bwana hatupi maelekezo ya kujenga majengo kwa ajili ya utunzaji wa watoto, ingawa hii ni kazi nzuri, lakini si kazi ya wakati huu. Hebu dunia na ifanye yote inayoweza kufanya katika mwelekeo huu. Muda na fedha zetu lazima ziwekezwe katika mwelekeo tofauti wa kazi. Tunapaswa kuubeba ujumbe wa mwisho wa rehema kwa njia iliyo bora kabisa ya kuwafikia wale walio

makanisani ambao wana njaa na wanaomba kwa ajili ya kupata nuru.- Letter 232, 1899. **{WM 258.3}**

Geukieni Mashamba Yaliyo Tayari Kuvunwa. - Kazi hii inafanywa kuwa kazi ya kushughulisha mno, lakini hii haiko katika utaratibu wa Mungu. Ni kazi isiyoisha, na ikiwa itaendelezwa kama ilivyokuwa hapo zamani, nguvu zote za watu wa Mungu zitahitajika kuisawazisha ili ikae sawa, na kazi ya kuwaandaa watu wa kusimama katikati ya hatari za siku za mwisho haitafanywa kamwe. **{WM 258.4}**

Kazi yetu ni kuvaa silaha na kufanya vita vikali. Wafanyakazi hawapaswi kuhimizwa kufanya kazi katika mitaa duni na michafu ya miji, ambapo watapata waongofu wale tu ambao

wanahitaji kutunzwa, na kufanyiwa hivyo daima. Kuna mashamba yaliyoiva kabisa tayari kwa mavuno, na muda wote na fedha hazipaswi kutolewa kwa ajili ya kuwakusanya wale ambao kwa kuendekeza hamu ya chakula wamejielekeza wenyewe katika uchafu. Baadhi ya hawa wanaweza kuokolewa. Na wapo wale ambao wanaweza kufanya kazi katika matabaka duni kabisa ya dunia bila kuharibika tabia zao. Lakini si salama kuwapa vijana wa kiume na wa kike aina hii ya kazi wapate kuifanya. Jaribio hili litaweza kuwa lenye gharama kubwa mno. Kwa jinsi hiyo wale ambao wangeweza kufanya kazi katika barabara kuu wangeondolewa nguvu kwa ajili ya kufanya kazi ya aina yoyote.... **{WM 259.1}**

Hisia za watu zinaweza kuguswa sana wanapowaona wanadamu wakiteseka kama matokeo ya mwelekeo wa matendo yao wenyewe. Kuna wale ambao wanavutiwa kwa namna ya pekee kugusana moja kwa moja na tabaka hili, na Bwana anawapa agizo la kufanya kazi katika maeneo mabaya kabisa ya dunia, wakifanya kile wanachoweza ili wapate kuwakomboa waliotengwa na jamii na kuwaweka mahali ambapo watakuwa chini ya utunzaji wa kanisa. Lakini Bwana hajawaita Waadventista wa Sabato kuifanya kazi hii kuwa maalum. Asingewataka katika kazi hii kuwashughulisha wafanyakazi wengi au kutumia hazina yote. - *Manuscript* 16, 1900. **{WM 259.2}**

Msaada Kutoka Ulimwenguni Si Kutoka kwa Makanisa. - Kazi ya

daima inapaswa kufanywa kwa ajili ya waliotengwa na jamii, lakini kazi hii haipaswi kufanywa kuwa yenye kuteka na kushughulisha fikra kabisa na kisha kufanya mtu awe hoi.... Hakuna mtu anayepaswa sasa kutembelea makanisa yetu na katika shinikizo lililopo kupata kutoka kwao fedha za kuendeleza kazi ya kuwaokoa waliotengwa. Fedha za kuendeleza kazi hiyo zinapaswa kuja, na zitakuja, kwa kiasi kikubwa kutoka kwa wale ambao si wa imani yetu. Hebu makanisa na yajishughulishe na kazi yao iliyopangwa ya kuwasilisha Ukweli kutoka katika Maneno ya Mungu katika barabara kuu. - *Letter* 138, 1898. **{WM 259.3}**

Bwana haweki juu ya watu wake mzigo wote wa kufanya kazi kwa ajili ya tabaka ambalo limefanywa kuwa sugu

na dhambi kiasi kwamba wengi wao hawatafaidika wao wenyewe wala kuwanufaisha wengine. Ikiwa kuna watu ambao wataweza kujishughulisha kwa ajili ya hawa waliodhililika kabisa, ikiwa Mungu anaweka juu yao mzigo wa kufanya kazi kwa ajili ya umma kwa njia mbalimbali, hebu hawa na wasonge mbele na kukusanya kutoka ulimwenguni fedha zinazohitajika kwa ajili ya kuifanya kazi hii. Hebu wasiitegemee fedha ile ambayo Mungu anakusudia kwamba itaendeleza kazi ya ujumbe wa malaika wa tatu. — *Testimonies for the Church* 6:246.**{WM 260.1}**

Mataifa Yanaisubiri Nuru. - Kwa wale wanaodhani kwamba Bwana amewapa kazi ya kuutunza umati usio na taratibu wa waliotengwa na jamii,

ambao wamejiharibu wenyewe, ambao wengi wao wataendelea kufanya kama walivyofanya zamani, wakati huo huo wakijikimu kwa fedha walizopewa na Waadventista wa Sabato, Bwana anasema, Ni nani aliyekupa kazi hii? Kuna watu na mataifa ambao bado hawajapokea nuru ya ukweli kwa ajili ya wakati huu. Ujumbe wa injili unapaswa kuinuliwa na unapaswa kuleta athari nyingi na kufika mbali sana. **{WM 260.2}**

Katika kila mahali ambapo ujumbe unatangazwa, wafanyakazi wamisionari wanapaswa kusonga mbele na Biblia zao mikononi mwao. Roho zinapaswa kuongolewa na kuimarishwa katika ukweli. Nyumba ya kukutania itapaswa

kujengwa. Nuru inapaswa kuangaza kutoka kwa waumini, ambao watakuwa kama mji uliowekwa juu ya kilima. Kanisa linapaswa kuwa mahali hapo shahidi wa kile ambacho ukweli unaweza kufanya. - Letter 41, 1900. **{WM 260.3}**

Sehemu ya X Rasilimali ya Fedha kwa Ajili ya Kazi ya Ustawi

Wazo la Thamani

Ili mwanadamu asipoteze matokeo yenye baraka ya ukarimu, Mkombozi wetu aliweka mpango wa kumworodhesha kama mfanyakazi mwenza (mwenza Wake katika kazi). Kwa mlolongo wa hali ya mambo ambayo yangesababisha huruma Zake,

Anampa mwanadamu mali bora za kukuza ukarimu, na kumfanya kwa mazoea aendelee kutoa ili kuwasaidia maskini na kuendeleza kusudi Lake. Anawatuma maskini Wake kama wawakilishi Wake. Kwa mahitaji yao ulimwengu ulioharibika unatuvuta kutoka kwetu talanta za mali na za ushawishi, ili kuwasilisha kwao Ukweli, ambao kwa ajili ya huo wako katika uhitaji wa kuangamia. Na pale tunapoisikiza miito hii kwa kazi na kwa matendo ya ukarimu, tunafanywa kuwa sawa na mfano wa Yeye ambaye kwa ajili yetu alikuwa maskini. Katika kutoa tunawabariki wengine, na kwa hivyo tunalimbikiza utajiri wa kweli. — *Testimonies for the Church* 3:382, 383. **{WM 262.1}**

Matendo 4

32 Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala
hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu cho chote alicho nacho ni mali yake
mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika.
33 Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na
neema nyingi ikawa juu yao wote.
34 Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu
watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba waliviuza, wakaileta thamani ya vitu
vile vilivyouzwa,
35 wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji.

Sura ya Thelathini na Nne - Wajibu Wetu wa Mtu Moja Mmoja

Kazi ya Binafsi Iliyokabidhiwa kwa Wafuasi wa Kristo. - Kristo hukabidhi kwa wafuasi Wake kazi ya mtu binafsi - kazi ambayo haiwezi kufanywa na wakala au mwingine. Huduma kwa wagonjwa na maskini, utoaji wa injili kwa waliopotea, haipaswi kuachwa kwa kamati au misaada iliyopangwa. Wajibu wa mtu binafsi, juhudi ya mtu binafsi, kujitoa mhanga kwa mtu binafsi, ndio hitaji la injili. -

The Ministry of Healing, 147. **{WM 263.1}**

Mahitaji Hutolewa Kadiri Tunavyogawa. - Kristo ametuagiza, kupitia kwa nabii, "Kuwagawia wenye njaa chakula," na "kuishibisha nafsi iliyoteswa;" "ukimwona uchi, umfunike," na "kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani." Ametuambia, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Lakini ni mara ngapi mioyo yetu inazama na imani kupungua nguvu pale tunapoona jinsi hitaji lilivyo kubwa na jinsi fedha ni kidogo mikononi mwetu. Kama Andrea akitazama mikate mitano ya shayiri na samaki wawili wadogo, sisi tunasema, "Lakini hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa?" Mara nyingi tunasita, bila kutaka kutoa vyote

tulivyo navyo, tukiogopa kutumia na kutumika kwa ajili ya wengine. Lakini Yesu ametuambia, "Wapeni ninyi chakula." Agizo Lake ni ahadi, na nyuma yake kuna nguvu ile ile iliyowalisha umati kando ya bahari. **{WM 263.2}**

Katika tendo la Kristo la kutoa mahitaji ya wakati ule ya umati wa watu wenye njaa, limefungwa somo la kina la kiroho kwa wafanyakazi Wake wote. Kristo alipokea kutoka kwa Baba; Aliwapa wanafunzi; waliwapa umati; nao watu wakapeana wao kwa wao. Hivyo wote ambao wameunganishwa na Kristo watapokea kutoka Kwake mkate wa uzima, chakula cha mbinguni, na kuwapa wengine....**{WM 264.1}**

Wanafunzi walikuwa ni njia ya mawasiliano kati ya Kristo na watu. Hii

inapaswa kuwa jambo kubwa la kutia moyo kwa wanafunzi Wake leo. Kristo Ndiye kituo kikuu, chanzo cha nguvu zote. Wanafunzi Wake wanapaswa kupokea ugavi wao kutoka Kwake. Wale wenye akili sana, na wenye msimamo sana wa kiroho, wanaweza kutoa tu kadiri wanavyopokea. Peke yao hawawezi kutoa chochote kwa ajili ya mahitaji ya roho. Tunaweza kutoa tu kile tunachokipokea kutoka kwa Kristo, na tunaweza kupokea tu pale tunapotoa kwa wengine. Tunapoendelea kutoa tunaendelea kupokea; na kadiri tunavyotoa zaidi, ndivyo tutakavyopokea zaidi. Hivyo daima tunaweza kuwa tunaamini, tunatumaini, tunapokea, na kutoa. **{WM 264.2}**

Kazi ya kujenga ufalme wa Kristo itasonga mbele, ingawa kwa mwonekano

wote inasonga polepole na kutokuwezekana kunaonekana kushuhudia dhidi ya kusonga mbele. Kazi hiyo ni ya Mungu, Naye atatoa fedha na atawatuma wasaidizi, wanafunzi wa Kweli, wenye bidii, ambao mikono yao pia itajazwa na chakula kwa ajili ya umati wenye njaa. Mungu si msahaulifu kwa wale wanaofanya kazi kwa upendo katika kutoa Neno la uzima kwa roho zinazoangamia, ambao kwa upande wao wananyosha mikono yao kupata chakula kwa ajili ya roho zingine zenye njaa. – *The Desire of Age*s, 369, 370. **{WM 264.3}**

Mzigo Usihamishwe kwa Mashirika. -Katika kazi yetu kwa Mungu kuna hatari ya kutegemea sana kile ambacho mwanadamu pamoja na talanta na uwezo wake anaweza kufanya.

Hivyo, tunaacha kumwona Mfanyakazi Mkuu pekee. Mara nyingi mfanyakazi kwa ajili ya Kristo anashindwa kutambua jukumu lake la binafsi. Yuko katika hatari ya kuhamisha mzigo wake kwa mashirika, badala ya kumtegemea Yeye ambaye ndiye chanzo cha nguvu zote. Ni kosa kubwa kutegemea hekima ya kibinadamu au idadi katika kazi ya Mungu. Kazi yenye mafanikio kwa Kristo haitegemei sana idadi au talanta kama inavyotegemea usafi wa kusudi, usahili wa kweli wa imani ya dhati, iliyo tegemezi. Majukumu binafsi ni lazima yabebwe, wajibu binafsi ni lazima uchukuliwe, juhudi binafsi ni lazima zifanywe kwa ajili ya wale ambao hawamjui Kristo. Badala ya kuhamisha jukumu lako juu ya mtu ambaye unadhani amejaliwa kwa wingi kuliko

wewe, fanya kazi kulingana na uwezo wako. - *The Desire of Ages,* 370. **{WM 265.1}**

Mungu Atatoa Fedha. - Fedha tuliyo nayo inaweza kuonekana kuwa haitoshi kwa ajili ya kazi hiyo; lakini kama tutasonga mbele kwa imani, tukiamini katika nguvu toshelevu ya Mungu, rasilimali nyingi zitafunguka mbele yetu. Ikiwa kazi ni ya Mungu, Yeye Mwenyewe atatoa fedha kwa ajili ya ufanikishaji wake. Atatoa thawabu kwa kwa ajili ya utegemezi wa kweli, sahili Kwake. Kile kidogo kinachotumiwa kwa busara na kubana matumizi katika utumishi wa Bwana wa mbinguni kitaongezeka katika tendo lenyewe la kutoa. Katika mkono wa Kristo akiba ndogo ya chakula ilibaki bila kupungua hadi pale umati wa watu

wenye njaa walipotosheka. Ikiwa tutaenda kwa Chanzo cha nguvu zote, huku mikono yetu ya imani imenyoshwa ili ipate kupokea, tutaendelezwa katika kazi yetu, hata katika hali za kuogofya mno, na tutawezeshwa kuwapa wengine mkate wa uzima. - *The Desire of Ages*, 369, 371. **{WM 265.2}**

Thubutu Kutoa Kitu Fulani kwa Ajili ya Kuokoa Roho. - Kuna woga wa kuthubutu na kukubali kupata hasara katika kazi hii kubwa, kwa kuogopa kwamba matumizi ya fedha hayataleta faida. Je, kama fedha zinatumika, na bado hatuwezi kuona kwamba roho zimeokolewa na hiyo? Vipi ikiwa kuna hasara tupu ya sehemu ya fedha yetu? Ni bora kufanya kazi na kuendelea kufanya kazi kuliko kutokufanya chochote. Hamjui ni kipi

kitakachofanikiwa hiki au kile. Wanaume watawekeza katika haki za hataza (hatimiliki/patent rights) na kukutana na hasara kubwa, na inachukuliwa kwamba ndivyo mambo yanavyotarajiwa kuwa. Lakini katika kazi na kusudi la Mungu, watu wanaogopa kuthubutu. Fedha inaonekana kwao kuwa hasara tupu ambayo haileti faida ya haraka pale inapowekezwa katika kazi ya kuokoa roho. Fedha hizo hizo ambazo kwa sasa zinawekezwa kwa uchache sana katika kusudi la Mungu, na ambazo kwa ubinafsi zinazuiwa, kitambo, zitatupwa pamoja na sanamu zote kwao fuko na popo. Fedha zitashuka thamani kwa ghafla sana wakati Ukweli wa matukio ya milele utakapofunguka katika akili za mwanadamu. **{WM 266.1}**

Mungu atakuwa na watu ambao watathubutu kitu chochote na kila kitu kwa ajili ya kuokoa roho. Wale ambao hawatasonga mpaka waweze kuona kila hatua ya njia kwa uwazi mbele yao hawatakuwa na manufaa kwa wakati huu katika kuendeleza Ukweli wa Mungu. Ni lazima wawepo sasa wafanyakazi ambao watasonga mbele gizani na pia katika nuru, na ambao watashikilia kwa ujasiri hatika hali ya upinzani na matumaini yaliyokatishwa tamaa, na bado waendelee kufanya kazi kwa imani, kwa machozi na tumaini lenye subira, wakipanda kando ya maji yote, wakimtumaini Bwana kuleta ongezeko. Mungu anawataka watu wenye ujasiri, wenye matumaini, imani, na uvumilivu, kufanya kazi katika jambo

hili. — *The True Missionary*, Januari, 1874. **{WM 266.2}**

Kila Dola Inahitajika. - Mwisho wa vitu vyote umekaribia, na Mungu anawaita watu waje katika utumishi hai na kutenda wajibu wao kwa sababu anaitaka na ulimwengu unahitaji msaada wao. Chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu watu watakuwa na busara katika matumizi ya fedha nao watazitumia kulingana na ukubwa na umuhimu wa kazi ambayo inapaswa kufanywa.... Bwana Mungu wa mbinguni anatoa wito kwa wanadamu kuweka mbali sanamu zao, kukata kila tamaa ya kupita kiasi, kutokujiingiza katika kitu chochote ambacho ni cha maonesho na kuwavutia watu tu, na kubana matumizi katika ununuzi wa mavazi na samani. Usitumie hata dola

moja ya pesa za Mungu kununua bidhaa zisizohitajika. Fedha yako inamaanisha wokovu wa roho. Basi isitumike kwa vito, kwa dhahabu, au vito vya thamani....**{WM 267.1}**

Unaweza kutoa maelfu ya dola kwa ajili ya kusudi hilo, na bado dola hiyo ya ziada, paundi hiyo ya ziada, inaitwa. Kila paundi inahitajika, kila shilingi inaweza kutumika, na kuwekezwa kwa namna ile ambayo itakuletea hazina isiyoharibika. Rafiki zangu waapendwa, ambao wanampenda Mungu na wangemtumikia kwa moyo wote, ninawasihi mjihoji pale mnapotumia pesa kwa ajili ya kununua bidhaa, "Je! Ninamtukuza Mungu, au ninakidhi tu tamaa ya kibinadamu? Je! Niwekeze fedha hizi ambazo nimeshikilia mkononi mwangu ili kujipendeza mwenyewe,

kununua zawadi kwa ajili ya watoto wangu, au kwa ajili ya marafiki wangu, au nitakuwa mfanyakazi mwenza pamoja na Kristo, kielelezo kwa wote ambao wanajifunza kumtukuza Mungu?” Sheria imetolewa kwetu, " Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.” - *Letter* 90, 1895. **{WM 267.2}**

Sura ya Sura ya Thelathini na Tano – Kuachilia Mifereji ya Ukarimu

Kuwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Mungu. - Mungu ameweka mali mikononi mwa wanadamu ili wapate kujifunza kuwa na huruma, kuwa maafisa ustawi wa jamii Wake kwa ajili ya kupunguza mateso ya viumbe Wake

walioanguka dhambini. — *The Signs of the Times,* Juni 20, 1892.**{WM 268.1}**

Kuweka Mioyo Kuwa na Upendo na Huruma. - Matendo ya ukarimu na wema yalikusudiwa na Mungu kufanya mioyo ya watoto wa watu kuendelea kuwa yenye huruma, laini na wema na kusisitiza ndani yao shauku na upendo wa mtu kila mmoja na mwenzake kwa kumwiga Bwana, ambaye kwa ajili yetu alikuwa maskini, ili kwamba sisi kwa njia ya umaskini wake tuweze kufanywa kuwa matajiri. - *Testimonies for the Church* 3:547. **{WM 268.2}**

Mito ya Wema Kufanywa Iendelee Kutiririka. - Mito midogo ya wema ni lazima daima ifanywe kuendelea kutiririka ndani ya hazina. Upaji wa Mungu uko mbele sana,

ukisonga mbele kwa kasi kubwa zaidi ya ukarimu wetu. - *Manuscript* 26, 1891. **{WM 268.3}**

Mtiririko wa Kudumu wa Thawabu. - Fedha ambazo Mungu amekabidhi kwa wanadamu zinapaswa kutumiwa katika kuwabariki wanadamu, katika kupunguza shida za wanaoteseka na wahitaji. Watu hawapaswi kuhisi kwamba wamefanya jambo la ajabu sana wakati wanapokuwa wamewapa taasisi fulani au makanisa zawadi kubwa. Katika majaliwa ya hekima ya Mungu daima wanaowasilishwa mbele yao wale hasa ambao wanahitaji msaada wao. Wanapaswa kuwasaidia wanaoteseka, kuwavisha walio uchi, na kuwasaidia wengi ambao wako katika hali ngumu yenye kusumbua, ambao wanashindana kwa nguvu zao zote kujiweka wao

wenyewe pamoja na familia zao kutoka katika nyumba ya maskini. - *The Review and Herald,* Januari 4, 1898. **{WM 268.4}**

Tunaomba kwa Ajili ya Wengine. – Pale tunapoomba, "Utupe leo riziki yetu," tunaomba kwa ajili ya wengine pamoja na sisi pia. Na tunakiri kwamba kile Mungu anachotupa si kwa ajili yetu peke yetu. Mungu anatupa kwa dhamana, ili tuweze kuwalisha wenye njaa. Katika wema Wake ameandaa kwa ajili ya maskini. Na Anasema, "Ufanyapo chakula cha mchana au cha jioni, usiwaite rafiki zako, wala ndugu zako, wala jamaa zako, wala jirani zako wenye mali. ... Bali ufanyapo karamu waite maskini, vilema, viwete, vipofu, nawe utakuwa heri, kwa kuwa hao hawana cha kukulipa; kwa maana utalipwa katika

ufufuo wa wenye haki.” - *Mount of Blessing*, uk.163, 164. **{WM 269.1}**

Maandishi ya Mungu Juu ya Kila Dola (nembo Yake ipo kwenye kila noti). –Bila kujali jumla ya talanta zetu, iwe moja, mbili, au tano, hakuna hata sarafu moja yenye thamani ndogo ya fedha zetu inapaswa kutumika kwa ubadhirifu juu ya ubatili, kiburi, au ubinafsi. Kila dola ya malimbikizo yetu imepigwa muhuri kwa sura na maandishi ya Mungu. Maadamu kuna wenye njaa katika ulimwengu wa Mungu wa kulishwa, walio uchi wa kuvikwa, roho zinazoangamia kwa kukosa mkate na maji ya wokovu, kila anasa isiyo ya lazima, kila kuzidi kwa mtaji, husihi kwa kuomba kwaajili ya maskini na walio uchi. —*The Signs of the Times*, Juni 20, 1892. **{WM 269.2}**

Mito ya Fadhili Hukaushwa. – Kadiri mtu anavyotumia fedha zaidi katika mavazi, ndivyo wanavyoweza kidogo kuwalisha wenye njaa na kuwavalisha walio uchi; na mito ya wema, ambayo inapaswa kuwa inainatiririka daima, hukaushwa. Kila dola inayookolewa kwa mtu kujinyima mapambo yasiyo na maana yoyote inaweza kutolewa kwa wahitaji au inaweza kuwekwa katika hazina ya Bwana ili ipate kuendeleza injili, kutuma wamisionari kwenda katika nchi za kigeni, kuzidisha machapisho ili kubeba miale ya nuru kwa roho zilizo katika giza la makosa. Kila dola inayotumiwa isivyo lazima inamnyima mtumiaji wake fursa ya thamani ya kutenda mema. - *Testimonies for the Church* 4:645, 646. **{WM 269.3}**

Mungu Anataka Kujikana. -
Mungu anawaita vijana wajinyime mapambo yasiyo ya lazima na bidhaa za mavazi, hata kama yanagharimu sarafu chache tu, na waweke kiasi hicho kwenye sanduku la sadaka ya hisani (charity box). Pia anatoa wito kwa wale wa umri mpevu kutulia pale wanapoichunguza saa ya dhahabu au mkufu au bidhaa fulani ya gharama kubwa ya samani na kujiuliza swali: Je! Itakuwa sawa kutumia kiasi kikubwa kiasi hicho kwa kile ambacho tunaweza kuishi bila kuwa nacho au wakati ambapo bidhaa ya bei nafuu inaweza pia kukidhi kusudi letu? Kwa kujikana na kuinua msalaba kwa ajili ya Yesu, ambaye kwa ajili yenu alikuwa maskini, unaweza kufanya mengi katika kupunguza mateso ya maskini walio

miongoni mwetu; na kwa kuiga namna hiyo mfano wa Bwana wako na Mwalimu utapokea kibali Chake na baraka. - *Testimonies for the Church* 4:511. **{WM 270.1}**

Si Jambo Dogo Kuwa Wakili wa Bwana. – Vipi kama wataona imeandikwa juu ya mapambo yao ya gharama kubwa zilizo katika nyumba zao, picha, na samani, "Walete maskini waliotupwa nje nyumbani kwako"! Katika chumba cha kulia, ambapo meza imejaa chakula tele, kidole cha Mungu kimenakili, "Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? " **{WM 270.2}**

Hebu wote, wazee na vijana, wazingatie kuwa si jambo jepesi kuwa

wakili wa Bwana na kushtakiwa katika vitabu vya mbinguni kwa kutumia kwa namna ya ubinafsi. Wahitaji, na wale walioonewa, wameachwa katika uhitaji, wakati ambapo pesa za Bwana zinatumika ovyo kwa ubinafsi katika ubadhirifu na anasa. Laiti wote wangekumbuka kwamba Mungu hana upendeleo! Ni jambo kubwa kuwa wakili, mwaminifu na wa kweli, mbele ya Mungu Mwenye haki asiye na upendeleo, ambaye hatasamehe ndani ya yeyote kati ya mawakili Wake udhalimu au wizi wowote Kwake. - *Manuscript* 11, 1892. **{WM 270.3}**

Matengenezo ya Ajabu Yameahidiwa. - Wakati neema ya Kristo inapooneshwa katika maneno na kazi za waumini, nuru itawaangazia wale walio gizani; kwani kuwa wakati

midomo inazungumzia sifa za Mungu, mkono utanyoshwa kwa wema kwa ajili ya msaada wa wanaoangamia. Tunasoma kwamba katika siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu aliposhuka juu ya wanafunzi, hakuna mtu aliyesema kwamba kitu chochote alichokuwa nacho kilikuwa chake mwenyewe. Vyote walivyokuwa navyo vilitolewa kwa ajili ya maendeleo ya matengenezo ya ajabu. Na maelfu waliongolewa kwa siku moja. Wakati roho ile ile itakapowachochea waumini leo, nao wakamrudishia Mungu kutokana na kile kilicho Chake Mwenyewe kwa ukarimu huo huo, kazi kubwa na yenye athari nyingi itatimizwa. - *Manuscript* 95, 1907.**{WM 271.1}**

Sura ya Thelathini na Sita - Fedha Maalum kwa Ajili ya Kazi ya Ustawi

Wakristo Kutenda Kama Watunza Hazina wa Mungu. - Maskini ni urithi wa Mungu. Kristo alitoa maisha Yake kwa ajili yao. Anawataka wale ambao amewateua kutenda kama mawakili Wake, kutoa kwa ukarimu mali walizokabidhiwa ili kusaidia maskini na kusaidia kazi Yake duniani. Bwana ni mwingi wa rasilimali. Amewateua watu kufanya kazi kama watunza hazina Wake katika ulimwengu huu. Kile ambacho amewapa wanapaswa kukitumia katika utumishi Wake. - *Manuscript* 146, 1903. **{WM 272.1}**

Sadaka ya Shukrani kwa Ajili ya Maskini.- Katika kila kanisa kunapaswa kuanzishwa hazina kwa ajili ya maskini. Kisha hebu kila mshiriki awasilishe sadaka ya shukrani kwa Mungu mara moja kwa wiki au mara moja kwa mwezi, kama ilivyo rahisi zaidi. Sadaka hii itaonesha shukrani zetu kwa zawadi za afya, chakula, na mavazi mazuri. Na kadiri Mungu alivyotubariki kwa hali njema hizi (comfort!) ndivyo nasi tutakavyoweka akiba kwa ajili ya maskini, wanaoteseka, na wenye dhiki. Ningependa kwa namna ya pekee kuhusiana na jambo hili kuvuta nadhari yenu. Wakumbukeni maskini. Achilia baadhi ya anasa zako, ndio, hata raha, na kuwasaidia wale ambao wanaweza kupata chakula na nguo kidogo sana. Kwa kutenda kwa ajili yao unafanya kwa

ajili ya Yesu katika nafsi ya watakatifu Wake. Anajitambulisha na wanadamu wanaoteseka. Usisubiri hadi pale matakwa yako yote ya kufikirika yametoshelezwa. Usiamini hisia zako na kutoa pale unapojisikia na kuzuia wakati hujisikii. Toa mara kwa mara, ama senti kumi, ishirini, au hamsini kwa wiki, kama ungependa kuona katika rekodi ya mbinguni katika siku ile ya Mungu. - *Testimonies for the Church* 5:150, 151. **{WM 272.2}**

Sanduku la Kujinyima Nyumbani (self denial box). - Kila mtu awe na sanduku la kujinyima nyumbani kwake, na pale anapotumia peni na shilingi katika kujifurahisha, akumbuke wahitaji na wenye njaa wa Afrika na India na wale walio karibu na mlango wake mwenyewe. Wapo maskini

miongoni mwetu. Fanyeni mazoea ya kubana matumizi, na katika kila mwelekeo wasilisheni suala lenu kwa Mungu. Mwombeni awape roho ya Kristo, ili mwe katika kila maana ya neno hilo wanafunzi wa Kristo na kupokea baraka Zake. Pale unapogeuka kutoka kwenye kuiabudu nafsi na kujaribu kuwasaidia wanadamu wanaoteseka, mwombeni Mungu apate kuwapa kazi halisi ya umisionari ya kufanya kwa ajili ya roho. Ndipo wale wanaokuja kuabudu katika nyumba ya Mungu watawaona watu waliovaa mavazi ya staha yenye upatanifu na imani na Neno la Mungu. Ni mambo haya ndiyo ambayo hupokonya upendo na uaminifu na ujasiri wa watu wa Mungu kutoka Kwake, na kuharibu uzoefu wa kidini na kukuza ubinafsi

ambao Mungu hawezi kuutazama. -*Manuscript* 52, 1898. **{WM 273.1}**

Zaka ya Pili. - Ili kukuza kukusanyika kwa watu kwa huduma ya kidini, na pia kutoa kwa maskini, zaka ya pili ya maongeo yote ilihitajika. Kuhusu zaka ya kwanza, Bwana alikuwa ametangaza, " Na wana wa Lawi, nimewapa zaka yote katika Israeli." Lakini kuhusiana na ile ya pili aliamuru, "Nawe utakula mbele za Bwana, Mungu wako, mahali atakapochagua apakalishe Jina Lake, zaka ya nafaka zako, na divai yako, na mafuta yako, na wazaliwa wa kwanza wa makundi yako ya ng'ombe na ya kondoo; ili upate kujifunza kumcha Bwana, Mungu wako, daima." Fungu hili la kumi, au thamani yake katika fedha, walitakiwa kwa miaka miwili kulileta mahali ambapo hema takatifu liliwekwa.

Baada ya kuwasilisha sadaka ya shukrani kwa Mungu na sehemu iliyotajwa bayana kwa kuhani, watoaji walipaswa kutumia salio kwa karamu ya kidini, ambayo Mlawi, mgeni, yatima, na mjane walipaswa kushiriki....**{WM 273.2}**

Kila mwaka wa tatu, hata hivyo, zaka hii ya pili ilitakiwa kutumika nyumbani, kwa kumkirimu Mlawi na maskini, kama Musa alivyosema, "Wapate kula ndani ya malango yako, na kushiba." Zaka hii ingetoa fedha kwa ajili ya matumizi ya hisani na ukarimu. -*Patriarchs and Prophets,* 530. **{WM 274.1}**

Kuweka wakfu kwa Mungu kwa zaka ya maongeo yote, iwe ni ya shamba la miti ya matunda na shamba la mazao,

makundi ya kondoo na mbuzi na ng'ombe, au kazi ya ubongo au mkono; kuweka wakfu zaka ya pili kwa ajili ya misaada ya maskini na kwa matumizi mengine ya ukarimu, kulielekea kuweka upya mbele ya watu Ukweli juu ya umiliki wa Mungu wa yote na fursa yao ya kuwa mifereji ya baraka Zake. Ilikuwa ni mafunzo yaliyotengenezwa kwa ajili ya kuua ubinafsi wote wa uchoyo na kukuza upana na ubora wa tabia. - *Education,* 44. **{WM 274.2}**

Zawadi na Sadaka kwa Ajili ya Kazi ya Ustawi. - Matendo ya huruma lazima yafanyike; maskini na wanaoteseka ni lazima wasaidiwe. Zawadi na sadaka zinapaswa kutengwa kwa kusudi hili. Hasa katika nyanja mpya, ambapo bendera ya Ukweli haijawahi kuinuliwa, kazi hii ni lazima

ifanyike. — *Special Testimonies, series* A, no. 9, uk. 68.**{WM 274.3}**

Wamishonari wa tiba wanaweza kupata uwanja ambao utasaidia kupunguza shida za wale ambao wanadhoofika chini ya magonjwa ya kimwili. Wanapaswa kuwa na fedha ili waweze kuwavika walio uchi na kuwalisha wenye njaa. Kazi ya Wakristo ya kutoa msaada itafanya zaidi ya hotuba za mahubiri. - *The Review and Herald*, Desemba 24, 1895. **{WM 274.4}**

Itakuwa muhimu kwamba mfuko upate kuundwa ili wafanyakazi wapate fedha za kuwasaidia wale walio katika umaskini na dhiki, na huduma hii ya vitendo itafungua mioyo yao kuitika kwa

ukweli. - *The Review and Herald*, Januari 28, 1896. **{WM 274.5}**

Watu wanateuliwa kwa ajili ya kuutangaza ukweli katika maeneo mapya. Watu hawa ni lazima wawe na fedha za kujikimu. Na ni lazima wawe na mfuko ambao kutoka humo watachukua kwa ajili ya kuwasaidia maskini na wahitaji ambao wanakutana nao katika kazi zao. Ukarimu ambao wanauonesha kwa maskini unatoa ushawishi kwa juhudi zao za kuutangaza Ukweli. Utayari wao wa kuwasaidia wale walio katika uhitaji unawapatia shukrani za wale wanaowasaidia na kibali cha Mbingu. - *Letter* 32, 1903. **{WM 275.1}**

Kusaidiwa Kutokana na Michango Maalum, Sio Mapato ya Kawaida ya Kanisa. - Katika sura ya sita ya Matendo

tunaoneshwa jinsi ambavyo pale ambapo watu wangelichaguliwa ili kujaza nafasi kanisani, suala hilo lililetwa mbele za Bwana, na maombi ya dhati kabisa yalitolewa kwa kwa ajili ya uongozi. Wajane na yatima walipaswa kusaidiwa na michango kutoka kanisani. Mahitaji yao hayakupaswa kutulizwa na kanisa bali kwa michango maalum. Zaka ilipaswa kuwekwa wakfu kwa Bwana, na daima ingetumika kusaidia huduma. Wanaume ni lazima wachaguliwe kwa ajili ya kusimamia kazi ya kuwatunza maskini, kusimamia mgawanyo sahihi wa mali iliyopo, ili kwamba asiwepo yeyote kati ya waumini anayeteseka kwa ajili ya mahitaji ya maisha. - *Letter* 9, 1899. **{WM 275.2}**

Hakuna Anayeumia Ikiwa Mipango ya Mungu Inafuatwa. - Hakuna kitu chochote, baada ya utambuzi wao wa madai ya Mungu, ambacho kinatambulisha zaidi sheria zilizotolewa na Musa kuliko roho ya wema, upendo, na ukarimu iliyoamriwa kwa ajili ya maskini. Ingawa Mungu alikuwa ameahidi kuwabariki sana watu Wake, haikuwa mpango Wake kwamba umaskini ungepaswa kukosekana kabisa miongoni mwao. Alitangaza kwamba maskini hawatakoma kamwe katika nchi. Daima kungelikuwapo miongoni mwa watu Wake wale ambao wangehitaji huruma, upendo, na ukarimu wao. Wakati ule, kama ilivyo sasa, watu walikuwa wakipatwa na msiba, magonjwa, na upotevu wa mali; lakini maadamu walifuata maagizo

yaliyotolewa na Mungu, hakukuwa na ombaomba miongoni mwao, wala yeyote aliyeteseka kwa sababu ya kukosa chakula. — *Patriarchs and Prophets,* 530, 531.**{WM 275.3}**

Sura ya Thelathini na Saba - Utajiri wa Mataifa

Kutochukua Fedha Kutoka Katika Kusudi. - Zaka imetengwa kwa ajili ya matumizi maalum. Haipaswi kuchukuliwa kama hazina ya kusaidia masikini. Inapaswa kuwekwa wakfu hasa kwa ajili ya kuwasaidia wale ambao wanabeba ujumbe wa Mungu kwa ulimwengu, na haipaswi kugeuzwa kutoka katika kusudi hili. -*Review and Herald, Supplement*, Desemba 1, 1896. **{WM 277.1}**

Kusudi la Mungu halipaswi kupuuzwa ili maskini wapate uangalifu wetu wa kwanza. Kristo aliwahi kuwapa wanafunzi Wake somo muhimu sana juu ya jambo hili. Mariamu alipomimina marhamu kichwani mwa Yesu, Yuda mwenye kutamani alitoa ombi kwa ajili ya maskini, akinung'unika kwa kile alichokiona kuwa ni upotevu wa fedha. Lakini Yesu alithibitisha tendo lile, akisema: “Mbona mnamtaabisha mwanamke? Maana ni kazi njema aliyonitendea Mimi.” “Kila patakapohubiriwa Injili hii katika ulimwengu wote, tendo hilo alilolitenda huyu litatajwa pia kwa kumbukumbu lake." Kwa hili tunafundishwa kwamba Kristo anapaswa kuheshimiwa kwa kuweka wakfu mali zetu zilizo bora. Ikiwa usikivu wetu wote utaelekezwa

kwenye kupunguza shida za maskini, kusudi la Mungu lingepuuzwa. Hakuna hata mmoja atakayeteseka ikiwa mawakili wake watatekeleza wajibu wao, lakini kazi ya Kristo inapaswa kuja kwanza. — *Testimonies for the Church* 4:550, 551.**{WM 277.2}**

Dai la Mungu linapaswa kuchukua umuhimu wa kwanza juu ya dai lingine lolote na ni lazima litekelezwe kwanza. Ndipo maskini na wahitaji wanapaswa kutunzwa. — *The Youth's Instructor*, August 26, 1897.**{WM 277.3}**

Kupokea Kutoka Katika Vyanzo vya Nje. - Mungu atatufungulia njia kutoka katika vyanzo nje ya watu wetu wenyewe. Siwezi kuona jinsi ambavyo mtu yeyote anaweza kukerwa na kupokea zawadi kutoka kwa wale wasio wa imani yetu. Wanaweza tu kufanya

hivyo kwa kuchukua misimamo mikali na kwa kusababisha masuala ya ushindani ambayo hawana mamlaka ya kuyafanya. — *Special Testimonies to Ministers and Workers* 3:43**{WM 277.4}**

Mungu Huwasukuma Wasioamini Kutoa Msaada. - Mnauliza kuhusiana na heshima na usahihi wa kupokea zawadi kutoka kwa Mataifa au wapagani. Swali hili si geni; lakini napenda kuwauliza, "Ni nani anayeumiliki ulimwengu wetu?" Ni nani hasa walio wamiliki wa nyumba na ardhi? Je, si Mungu? Yeye Anao wingi katika ulimwengu wetu ambao ameuweka mikononi mwa wanadamu, ambao kwa huo wenye njaa wanaweza kupewa chakula, walio uchi mavazi, na wasio na makazi nyumba. Bwana

angewasukuma walimwengu, hata waabudu sanamu, kutoa kutoka katika wingi walio nao kwa ajili ya kuisaidia kazi hiyo, ikiwa tungewaendea kwa busara na kuwapa fursa ya kufanya mambo hayo ambayo ni fursa, upendeleo na faida kubwa kwao kufanya. Kile ambacho wangetoa tunapaswa kuwa na haki ya kukipokea. **{WM 278.1}**

Tunapaswa kufahamiana na watu walio katika nafasi za juu, na kwa kutumia hekima ya nyoka na upole wa njiwa tunaweza kupata manufaa kutoka kwao, kwa kuwa Mungu angesukuma akili zao kufanya mambo mengi kwa niaba ya watu Wake. Ikiwa watu sahihi wangeweka mbele ya wale ambao wana mali na uwezo, mahitaji ya kazi ya Mungu kwa nuru sahihi, watu hawa

wangeweza kufanya mengi katika kuliendeleza kusudi la Mungu katika ulimwengu wetu. Tumeweka mbali na sisi fadhila na faida ambazo tungeweza kuwa na faida yake, kwa sababu tulichagua kusimama kwa kujitegemea mbali na ulimwengu. Lakini hatupaswi kutoa kafara kanuni hata moja ya Ukweli pale tunapotumia kila fursa kuendeleza kazi ya Mungu. — *Special Testimonies to Ministers and Workers* 3:29 **{WM 278.2}**

Omba Msaada kwa Watu Wakuu na Wema Wapate Kutusaidia. - Kuna ulimwengu unaopaswa kuonywa, nasi tumekuwa dhaifu sana kuhusu kuwaomba msaada watu matajiri, wawe ni washiriki wa kanisa au walimwengu, kutusaidia katika kazi. Tungependa kwamba

Wakristo bayana wote wangelisimama pamoja nasi. Tungependa kwamba roho zao zingeweza kuvutwa kwa ukarimu kutusaidia katika kuujenga ufalme wa Mungu katika ulimwengu wetu. Tunapaswa kuwaita watu wakuu na wema kutusaidia katika kazi yetu ya juhudi ya Kikristo. Wanapaswa kualikwa kwa ajili ya kuunga mkono juhudi zetu katika kutafuta kukiokoa kile kilichopotea. — *The Origin and Development of the Thanksgiving Plan,* 5.**{WM 279.1}**

Zawadi Kama Hizo Hazipaswi Kukataliwa. - Tunapoonesha kwa ulimwengu, kwa malaika, na kwa wanadamu kwamba kufanikiwa kwa kusudi la Mungu ndilo wazo letu la kwanza, Mungu atatubariki. Wakati mwingine Yeye hufanya kazi kupitia kwa

wasioamini, na misaada isiyotarajiwa huja. Bwana anaweka ndani ya mioyo ya wanadamu haja ya kusaidia. Fedha zinazokuja kwa njia hii hazipaswi kukataliwa. Fedha zinapotoka kwa wasioamini zinapaswa kutumiwa na wakala wa kibinadamu kumheshimu Mungu. Kila mtoaji mwenye mawazo ya kiroho, anayetoa kwa moyo wote atatumia kwa usahihi kila talanta iliyokabidhiwa na Mungu.**{WM 279.2}**

Bwana halazimiki kutegemea mali zetu. Hatawekewa mipaka na wakala wa kibinadamu. Njia Yake daima ndiyo njia iliyo bora, na msaada wowote ambao unaweza kuja kwa ajili ya kuendeleza kusudi Lake na kazi Yake katika mojawapo ya taasisi zetu unapaswa kutumika kama iliyokuja kutoka Kwake. Zawadi kutoka kwa wasioamini

hazipaswi kukataliwa. Fedha ni mali ya Bwana, na inapaswa kupokelewa kwa shukrani. Hebu Mungu na afanye kazi na atoe kupitia kwa amtakaye.... Tunaamini muda unakwisha. Umilele umekaribia. Utoaji wetu wa mali ni mdogo, na kazi inayopaswa kufanywa ni kubwa. Ni sasa ndipo mahali ambapo imani inapaswa kutumika. Utoshelevu wetu uko kwa Mungu. - *Manuscript* 47, 1899.**{WM 279.3}**

Matajiri Watatoa Vifaa. – Hebu wale wanaofanya kazi kwa ajili ya faida ya kusudi la Mungu waweke mambo muhimu ya kazi hiyo - mbele ya matajiri wa ulimwengu. Fanya hivi kwa busara. Waambie kile unachojaribu kukifanya. Omba michango kutoka kwao. Ni mali za Mungu ambazo wanazo, mali ambazo

zinapaswa kutumika katika kuuelimisha ulimwengu. **{WM 280.1}**

Katika ardhi imetunzwa hazina kubwa za dhahabu na fedha. Utajiri wa watu umejilimbikiza. Nenda kwa watu hawa kwa moyo uliojaa upendo kwa Kristo na kwa wanadamu wanaoteseka na uwaombe wakusaidie katika kazi unayojaribu kuifanya kwa ajili ya Bwana. Watakapoona kuwa unadhihirisha mawazo ya ukarimu wa Mungu, hisia itaguswa ndani ya mioyo yao. Watatambua kuwa wanaweza kuwa mkono wa msaada wa Kristo kwa kufanya kazi ya umishonari wa tiba. Wataongozwa kushirikiana pamoja na Mungu, kutoa vifaa muhimu kwa ajili ya kuanzisha utendaji wa kazi ambayo inahitajika kufanywa. - *Manuscript* 40, 1901.**{WM 280.2}**

Kuvutiwa na Roho Kutoa. - Matabaka ya juu yamepuuzwa kwa namna ya ajabu. Katika mapito ya juu ya maisha watapatikana wengi ambao watauitikia Ukweli kwa sababu ni thabiti, kwa sababu unabeba muhuri wa tabia ya juu ya injili. Si wachache wa watu wenye uwezo wanaoongolewa kwa jinsi hiyo katika kusudi watakaoingia kwa nguvu katika kazi ya Bwana. **{WM 280.3}**

Bwana anatoa wito kwa wale walio katika nafasi za dhamana, wale ambao kwao amekabidhi thawabu Zake za thamani kubwa, kutumia talanta zao za akili na mali katika huduma Yake. Wafanyakazi wetu wanapaswa kuwasilisha mbele ya watu hawa maelezo dhahiri ya mpango wetu wa kazi, tukiwaambia kile tunakichohitaji ili

kuwasaidia maskini na wahitaji na kwa ajili ya kuiweka kazi hii juu ya msingi imara. Baadhi ya hawa watavutiwa na Roho Mtakatifu kuwekeza mali za Bwana kwa njia ambayo itaendeleza kusudi Lake. Watalitimiza kusudi Lake kwa kusaidia kutengeneza vituo vya mvuto katika miji mikubwa. - *Testimonies for the Church* 7:112. **{WM 280.4}**

Pesa Itatolewa. - Uzoefu wa siku za mitume utatujia ikiwa watu watafanyiwa kazi na Roho Mtakatifu. Bwana ataondoa baraka Zake pale ambapo shauku za ubinafsi zinaendekezwa, lakini atawaweka watu wake katika milki ya mema ulimwenguni kote ikiwa watatumia bila ubinafsi uwezo wao kwa ajili ya kuwainua wanadamu. Kazi Yake inapaswa kuwa ishara ya ukarimu Wake,

ishara ambayo itajipatia ujasiri na imani ya ulimwengu na kuleta rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya injili. – *Special Testimonies, series* B 1:20.**{WM 281.1}**

Ni Pesa za Mungu. - Kwa nini usiwaombe Mataifa msaada? Nimepokea maagizo kwamba kuna wanaume na wanawake ulimwenguni ambao wana mioyo ya huruma, na ambao wataguswa na huruma pale mahitaji ya wanadamu wanaoteseka yatakapowasilishwa mbele yao.... **{WM 281.2}**

Jambo hilo limewasilishwa kwangu katika nuru hii. Kazi yetu inapaswa kuwa ya hima. Fedha ni za Bwana, na ikiwa matajiri watafikiwa kwa njia sahihi, Bwana ataigusa mioyo yao na kuwavutia kutoa mali zao. Fedha za

Mungu ziko mikononi mwa watu hawa, na baadhi yao watasikia maombi kwa ajili ya msaada.**{WM 281.3}**

Zungumzieni hili, na kufanya yote yaliyo chini ya uwezo wenu kupata zawadi. Hatupaswi kuhisi kwamba haingekuwa jambo la kufanya kuwaomba fedha watu wa ulimwengu, kwani ni jambo la kufanya tu. Mpango huu ulifunguliwa mbele yangu kama njia ya kuwasiliana na matajiri wa ulimwengu. Kupitia katika njia hii si wachache watakaopendezwa, na wanaweza kusikia na kuamini Ukweli wa wakati huu. - *Stewardship Series,* no. 1, uk. 15, 16. **{WM 281.4}**

Jinsi ya Kufanya katika Njia ya Kuwafikia. - Watu wengi ambao wamefanikiwa ulimwenguni na ambao

kamwe hawajishushi chini kufikia kwa aina za kawaida za uovu bado wanaangamizwa kupitia katika upendo wa utajiri....**{WM 282.1}**

Watu hawa wanahitaji injili. Wanahitaji macho yao kugeuzwa kutoka katika ubatili wa vitu vya kimwili ili wapate kuona thamani kubwa ya utajiri wa udumuo. Wanapaswa kujifunza furaha ya kutoa, uheri wa kuwa wafanyakazi wenza wa Mungu. **{WM 282.2}**

Watu wa tabaka hili mara nyingi ndio walio wagumu mno kufikiwa, lakini Kristo atafungua njia ambazo kwazo wanaweza kufikiwa. Hebu watenda kazi wenye hekima hasa, wenye imani hasa, wenye matumaini hasa wazitafute roho hizi. Kwa hekima na busara iliyozaliwa

na upendo wa Bwana, kwa uungwana na heshima ambavyo hutokana tu na uwepo wa Kristo katika roho, hebu wafanye kazi kwa wale ambao, kwa kutiwa kiwi machoni kwa mng'aro wa utajiri wa dunia, hawaoni utukufu wa hazina ya mbinguni. Hebu wafanyakazi wajifunze Biblia pamoja nao, wakisisitiza Ukweli mtakatifu barabara mioyoni mwao. Wasomee maneno ya Mungu: "Bali kwa Yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi." "Bwana asema hivi, mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya

kwamba ananifahamu Mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni Bwana, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana Mimi napendezwa na mambo hayo, asema Bwana." "Katika Yeye Huyo, kwa damu Yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema Yake." "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri Wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu." 1 Wakorintho 1:30; Yeremia 9:23, 24; Waefeso 1:7; Wafilipi 4:19. **{WM 282.3}**

Kusihi kwa jinsi hiyo, kunakofanywa kwa roho ya Kristo, hakutafikiriwa kuwa hakuhusiani na kinachonenwa. Kutavuta akili za wengi walio katika matabaka ya juu. **{WM 283.1}**

Kwa juhudi zinazowekwa kwa hekima na upendo, matajiri wengi wanaweza kuamshwa kila mmoja kutambua majukumu yake na uwajibikaji wake kwa Mungu. Inapowekwa wazi kwamba Bwana anawatarajia wao kama wawakilishi wake kuwasaidia wanadamu wanaoteseka, wengi wataitikia na watatoa mali zao na huruma yao kwa faida ya maskini. Wakati akili zimevutwa kwa jinsi hiyo, yaani mbali na shauku zao za ubinafsi, wengi wataongozwa kujisalimisha kwa Kristo. Kwa talanta zao za ushawishi na mali watajiungana kwa furaha katika kazi ya ukarimu pamoja na mmisionari yule mnyenyekevu ambaye alikuwa wakala wa Mungu katika uongofu wao. Kwa matumizi sahihi ya hazina yao ya dunia

wataweka "akiba isiyopungua katika mbingu, mahali pasipokaribia mwivi, wala nondo haharibu." Watajipatia hazina ambayo hekima hutoa, hata "utajiri udumuo, na haki pia.” - *Testimonies for the Church* 6: 256-258. **{WM 283.2}**

Sura ya Thelathini na Nane - Mauzo ya Chakula

Mauzo ya Chakula Yaliyofadhiliwa na Kanisa Hayalaumiwi. - Maonesho ya Jimbo yalipofanyika Battle Creek, watu wetu walileta majiko matatu au manne ya kupikia kwenye viwanja vile na kuonesha jinsi milo mizuri inavyoweza kuandaliwa bila matumizi ya nyama.

Tuliambiwa kwamba tulitengeneza mlo bora kabisa katika uwanja ule. Wakati wowote mikusanyiko mikubwa inapofanyika, ni fursa yenu kubuni mipango ambayo kwayo mnaweza kuwapa wale wanaohudhuria chakula kizuri, na unapaswa kufanya juhudi zako kuwa za kuelimisha. – *Manuscript* 27, 1906. **{WM 284.1}**

Uzoefu wa Pekee katika Elimu ya Afya. - Ilikuwa ni katika tukio la ziara ya nyumba kuu ya wanyama wa maonesho ya Barnum katika mji huu mnamo tarehe 28 ya Juni [1877], ambapo wanawake wa Woman's Christian Temperance Union walipiga pigo lenye nguvu kwa ajili ya kiasi na matengenezo kwa kuandaa mgahawa mkubwa wa kiasi kwa ajili ya kuwapatia nafasi umati wa watu ambao

walikusanyika kutoka mashambani kwa ajili ya kutembelea nyumba ya wanyama, hivyo kuwazuia kutembelea baa/vilabu na maduka ya vyakula, ambapo wangeweza kuwa wazi kwa majaribu. Hema lile kubwa, lenye uwezo wa kuchukua watu elfu tano lililotumiwa na Konferensi ya Michigan kwa makusudi ya mkutano wa makambi, lilitolewa kwa ajili ya tukio hilo. Chini ya hekalu hili kubwa la turubai kulisimikwa meza kumi na tano au ishirini kwa ajili ya kuwapa nafasi wageni.**{WM 284.2}**

Kwa mwaliko Sanitariamu iliweka meza kubwa katikati ya banda hili kubwa, lililowekewa kwa wingi matunda matamu, nafaka, na mboga mboga. Meza hii ilitengeneza kivutio kikuu na kwa kiasi kikubwa zaidi ilitembelewa kuliko nyingine yoyote. Ingawa lilikuwa

na urefu wa zaidi ya futi thelathini, watu walisongamana kiasi kwamba ililazimu kuweka nyingine kama theluthi mbili ya urefu wake, ambayo pia ilijaa watu waliobanana. - *Testimonies for the Church* 4:275. **{WM 284.3}**

Kupanga kwa Ajili ya Dhifa/Karamu. - Jana nilikuwa na mazungumzo ya saa mbili na A pamoja na mke wake, ambao wanafanya kazi hapa katika Sanitariamu. Ninadhani kwamba mahojiano hayo yalikuwa ni yenye faida. Walizungumza juu ya mpango walio nao akilini - wa kuwa na karamu katika Sanitariamu na kuwaalika wakazi mashuhuri wa St. Helena - mawakili, wafanyakazi wa benki, na wachungaji. Wanatumaini kwamba kwa jinsi hiyo wanaweza kufanya kitu fulani ili kuondoa hisia

ambayo inayoonekana kubebwa na baadhi ya watu katika St. Helena - kwamba taasisi hii ni mahali ambapo mapunguani na wakongwe peke yao hutunzwa. Ndugu B, meneja wa San Francisco Vegetarian Cafe, atakuja kusimamia maandalizi ya dhifa/karamu hii. **{WM 285.1}**

Sikuona pingamizi lolote kwa mpango huu. Nuru ya matengenezo ya afya ilipotujia kwa mara ya kwanza tulizoea, katika matukio ya sikukuu, kuchukua majiko ya kupikia kwenda nayo katika viwanja ambapo watu walikuwa wamekusanyika, na pale pale kuoka mikate isiyotiwa chachu – Skonzi za unga maalumu (gems) na skonzi za kawaida. Na ninadhani kuwa uzuri ule ulikuwa ni matokeo ya juhudi zetu, ingawa, bila shaka, hatukuwa na

maandalizi ya vyakula vya afya ambayo tunayo sasa. Wakati ule ndio tulikuwa tunaanza kujifunza jinsi ya kuishi bila kutumia nyama. **{WM 285.2}**

Wakati mwingine tulitoa burudani, na tulikuwa waangalifu sana kwamba yote tuliyoyaandaa kwa ajili ya mlo yalikuwa matamu na kuandaliwa vizuri. Katika msimu wa matunda tungeweza kupata maberi/maforosadi ya rangi ya blue (blueberries) na rasiberi yaliyotoka mashambani moja kwa moja, na stroberi yaliyochumwa moja kwa moja kutoka kwenye mizabibu. Tulifanya mlo juu ya meza kuwa kielelezo ambacho kiliwaonesha wale waliokuwepo kwamba lishe yetu, ingawa ilikuwa imeandaliwa kulingana na kanuni za matengenezo ya afya, ilikuwa tofauti kabisa na kuwa haba (walikuwa na vingi

vilivyosheheni meza, yaani nyama siyo kitu pekee cha kuweka mezani au chenye ladha). **{WM 285.3}**

Wakati mwingine hotuba fupi ya kiasi ilitolewa kuhusiana na matumbuizo/takrima hizi, na kwa jinsi hiyo watu walifahamu kanuni zetu za maisha. Kwa kadiri tulivyofahamu, wote walifurahishwa na wote walielimishwa. Daima tulikuwa na kitu cha kusema juu ya umuhimu wa kutoa chakula chenye kuleta afya, kisichokobolewa au kusindikwa na kukiandaa kwa namna sahili/kawaida, na bado kukifanya kuwa kitamu sana na cha kutamanisha ili wale wanaokila wapate kuridhishwa. Ulimwengu umejaa majaribu ya kuendekeza hamu ya chakula, na maneno ya kuonya, ya dhati na yanayolenga moja kwa moja kwenye

wazo kuu, yamefanya mabadiliko ya ajabu katika familia na kwa watu binafsi. - *Letter* 166, 1903. **{WM 286.1}**

Hatari ya Kufanya Faida ya Fedha Inayotokana na Kuuza Chakula Kuwa Lengo la Kwanza. - Nuru pia ilitolewa kwamba katika miji kutakuwapo na fursa ya kufanya kazi sawa na ile tuliyoifanya kwenye viwanja vya maonesho ya Battle Creek. Kwa upatanifu na nuru hii, migahawa ya afya, usafi na kuzuia magonjwa imeanzishwa (Hygenic Restaurant). Lakini kuna hatari kubwa kwamba wafanyakazi wetu wa kwenye migahawa hii ya afya watajazwa na roho ya kibiashara kiasi kwamba watashindwa kuitoa nuru ile ambayo watu wanaihitaji. Migahawa yetu inatukutanisha na watu wengi, lakini

ikiwa tutaruhusu akili zetu kushughulishwa kabisa na mawazo ya faida ya kifedha, tutashindwa kutimiza kusudi la Mungu. Yeye Angependa tutumie vizuri kila fursa kuwasilisha Ukweli ambao utawaokoa wanaume na wanawake kutokana na kifo cha milele. - *Manuscript* 27, 1906. **{WM 286.2}**

Kristo Aliwafikia Watu Katika Dhifa na Karamu Zao. - Kristo Ndiye Bwana wetu. Kwa maagizo dhahiri aliwaandaa wafuasi Wake kwa ajili ya kazi yao kabla ya kuwaacha. Mara tu alipoweza kuzungumza, Kristo alitumia talanta ya usemi, katika familia na miongoni mwa marafiki na wale waliozoeana, kwa namna ambayo haikuwa na makosa. Hakuna hata Neno moja chafu liliponyoka kutoka midomoni Mwake. Kamwe hakufanya

tendo baya, kwa kuwa alikuwa ni Mwana wa Mungu. Ingawa alikuwa na umbo la mwanadamu, lakini bado hakuwa na doa la dhambi. **{WM 286.3}**

Alipoalikwa, pale kazi Yake ilipoanza, kwenye dhifa au karamu na Farisayo au mtoza ushuru aliukubali mwaliko huo. Alishutumiwa na viongozi wa kidini kwa ajili ya kula pamoja na watoza ushuru, na walimshutumu kwamba alikuwa kama wao. Lakini katika fursa kama hizo Kristo alitawala mazungumzo ya mezani, na kutoa masomo mengi ya thamani. Wale waliokuwepo walimsikiliza; Je, Yeye hakuwa amewaponya wagonjwa wao, amewafariji ndugu zao wenye huzuni, amewachukua watoto wao mikononi Mwake na kuwabariki? Watoza ushuru

na wenye dhambi walivutwa Kwake, na pale alipofungua midomo Yake kusema, usikivu wao ulikazwa Kwake. **{WM 287.1}**

Kristo aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuenenda wanapokuwa pamoja na wale ambao hawakuwa wa kidini na wale ambao walikuwa. Aliwafundisha kwa mfano kwamba wanapohudhuria mkutano wowote wa umma, hawatakiwi kukosa kitu cha kusema. Lakini mazungumzo Yake yalitofautiana sana na yale ambayo yalikuwa yamesikilizwa katika karamu katika siku zilizopita. Kila Neno alilotamka lilikuwa ni harufu ya uzima iletayo uzima kwa wasikilizaji Wake, nao walisikiliza kwa usikivu mtulivu, kana kwamba walikuwa wanataka sana kusikia kusudi. **{WM 287.2}**

Heshima iliyooneshwa kwa Kristo katika karamu alizohudhuria ilikuwa ni tofauti kabisa na jinsi waandishi na Mafarisayo walivyotendewa, na hii iliwafanya kuwa na wasiwasi. Kristo alitoa masomo yaliyoendana na mahitaji ya wasikilizaji Wake. Ilikuwa ni wakati alipokuwa kwenye karamu ambapo alitoa mfano wa karamu kuu, na kuonesha jinsi ambavyo mwaliko wa mfalme ulitendewa.... **{WM 287.3}**

Mwalimu mkuu huyu alizungumza kama mtu mwenye mamlaka. Aliwaelekeza wanafunzi Wake kuhusiana na wajibu na kanuni za maisha halisi ya kijamii, ambazo ni sawa na sheria za ufalme wa Mungu. Kristo alisema Maneno Yake kwa usahili/uwazi mkubwa na usahili, na bila sauti yoyote yenye mashaka. Maneno Yake yalikuwa

kama machungwa ya dhahabu katika vyano vya fedha. -*Manuscript* 19, 1899. **{WM 287.4}**

Fursa katika Mikusanyiko Mikubwa. - Nilipewa maelekezo kwamba tunapokaribia mwisho kutakuwa na mikutano mikubwa katika miji yetu, kama ilivyofanyika hivi karibuni huko St. Louis, na kwamba maandalizi lazima yafanyike ili kuwasilisha Ukweli katika mikutano hii. Kristo alipokuwa hapa duniani alitumia vizuri fursa kama hizo. Popote idadi kubwa ya watu walipokusanyika kwa ajili ya kusudi lolote, sauti Yake ilisikika, wazi, dhahiri na kwa namna ya pekee, ikitoa ujumbe Wake. Na kwa sababu hiyo, baada ya kusulubiwa na kupaa

Kwake, maelfu waliongoka kwa siku moja. Mbegu iliyopandwa na Kristo ilizama ndani ya mioyo, na kuota, na wakati ule wanafunzi walipopokea kipawa cha Roho Mtakatifu, mavuno yalikusanywa.... **{WM 288.1}**

Katika kila mkutano mkubwa baadhi ya wachungaji wetu wanapaswa kuhudhuria. Wanapaswa kufanya kazi kwa busara ili kupata nafasi ya kusikilizwa na kutoa nuru ya Ukweli mbele ya wengi kadiri iwezekanavyo.... **{WM 288.2}**

Tunapaswa kutumia vizuri kila fursa ya namna ile iliyotolewa na Maonesho ya St. Louis. Katika mikutano kama hiyo ni lazima wawepo watu ambao Mungu anaweza kuwatumia. Vipeperushi vyenye nuru ya Ukweli wa sasa

vinapaswa kutawanywa miongoni mwa watu kama majani ya majira ya kupukutika kwa najani (fall). Kwa wengi wanaohudhuria katika mikutano hii vipeperushi hivi vitakuwa kama majani ya mti wa uzima, ambayo ni kwa ajili ya kuwaponya mataifa. - *Letter* 296, 1904. **{WM 288.3}**

Sura ya Thelathini na Tisa - Mbinu za Kupata Pesa Zinazokatazwa

Tamaa ya Hamu ya Chakula na Upendo wa Anasa ni Mvuto Usiofaa wa Kupata Pesa.

-Tunayaona makanisa ya siku zetu yakihimiza karamu, uroho, na ufujaji, kwa chakula cha jioni, maonesho, dansi, na karamu zinazoandaliwa kwa kusudi la kukusanya fedha katika hazina ya

kanisa. Hii ni mbinu iliyobuniwa na akili za tamaa ya kimwili ili kupata fedha pasipo kujitoa mhanga.**{WM 289.1}**

Mfano kama huo unaathiri akili za vijana. Wanaona kwamba bahati nasibu na maonesho na michezo huidhinishwa na kanisa, na wanadhani kuwa kuna kitu kinachovutia sana katika njia hii ya kupata fedha.... **{WM 289.2}**

Hebu na tusimame mbali kabisa na upotovu wote huu wa kanisa, ufujaji, na matamasha, ambayo yana ushawishi wa kuharibu tabia kwa vijana na wazee. Hatuna haki ya kutupa juu yao vazi la utakatifu kwa sababu fedha inapaswa kutumika kwa makusudi ya kanisa. Sadaka kama hizo ni vilema na zilizo gonjwa na zinabeba laana ya Mungu. Hizo ni thamani ya roho. Mimbari

inaweza kutetea kutumika kwa matamasha, dansi, bahati nasibu, maonesho, na karamu za kifahari, bao, kwa ajili ya kupata fedha kwa makusudi ya kanisa, lakini hebu tusishiriki katika hata moja ya mambo haya; kwa kuwa tukifanya hivyo, chuki ya Mungu itakuwa juu yetu. Hatupendekezi kukimbilia tamaa ya chakula au kutumia burudani za kimwili kama kishawishi kwa wafuasi bayana wa Kristo ili wapate kutoa fedha ambazo Mungu amewakabidhi. Kama hawatatoa kwa hiari, kwa sababu ya upendo wa Kristo, sadaka hiyo kwa namna yoyote haitakubalika kwa Mungu. - *The Review and Herald,* Novemba 21, 1878. **{WM 289.3}**

Kanisa Limenajisiwa. - Wakati fedha zinapochangwa kwa ajili ya

makusudi ya kidini, makanisa mengi hukimbilia njia zipi? Mnada/kunadi, chakula cha jioni, maonesho ya fahari, hata bahati nasibu na mbinu nyingine kama hizo. Mara nyingi mahali palipotengwa kwa ajili ya ibada kwa Mungu huchafuliwa kwa chakula na kunywa, kununua, kuuza, na kufurahi. Heshima kwa nyumba ya Mungu na kicho kwa ibada Yake hupunguzwa katika akili za vijana. Vizuizi vya kujizuia vinadhoofishwa. Ubinafsi, uchu wa chakula, kupenda kujionesha, hukimbiliwa, na vinapata nguvu kadiri vinavyoendekezwa. - *Testimonies for the Church* 9:91.**{WM 290.1}**

Wasioamini Wanavutiwaje? - Na ni picha gani inawekwa katika akili za wasioamini? Kiwango kitakatifu cha Neno la Mungu kinashushwa hadi chini

mavumbini. Dharau huelekezwa kwa Mungu na kwa Jina la Kikristo. Kanuni chafu kabisa zinaimarishwa na njia hii isiyo ya ki-Maandiko ya kuchanga fedha. Na hivi ndivyo Shetani angetaka iwe. Watu wanarudia dhambi ya Nadabu na Abihu. Wanatumia moto wa kawaida badala ya moto mtakatifu katika utumishi wa Mungu. Bwana haikubali sadaka kama hiyo. **{WM 290.2}**

Mbinu zote hizi za kuleta fedha katika hazina Yake ni chukizo Kwake. Ni upendo wa bandia ambao unachochea ubunifu wote kama huo. Ni upofu ulioje, ni kupumbazwa kulikoje ku juu ya wengi wanaokiri kuwa ni Wakristo! Washiriki wa kanisa wanafanya kama walivyofanya wakazi wa ulimwengu katika siku za Nuhu, wakati ambapo mawazo ya mioyo yao yalikuwa ni

mabaya tu siku zote. Wote wanaomcha Mungu watachukia mazoea hayo kama uwasilishaji usio wa dini ya Yesu Kristo. - *The Review and Herald,* Desemba 8, 1896. **{WM 290.3}**

Kutoa kwa Ajili ya Mambo ya Ubinafsi. - Katika mikutano bayana ya Kikristo Shetani anaweka vazi la kidini juu ya anasa zinazodanganya na matamasha yasiyo matakatifu ili kuyapa mwonekano wa utakatifu, na dhamiri za wengi hutulizwa kwa sababu fedha zinachangwa ili kugharimia matumizi ya kanisa. Watu wanakataa kutoa kwa ajili ya upendo kwa Mungu, lakini kwa ajili ya upendo wa anasa na kuendekeza hamu ya chakula kwa sababu za ubinafsi wataachana na fedha zao. **{WM 290.4}**

Je! Ni kwa sababu hakuna nguvu katika masomo ya Kristo juu ya ukarimu, na katika mfano Wake, na neema ya Mungu moyoni kuwaongoza watu kumtukuza Mungu kwa mali zao, kwamba njia kama hiyo lazima itumike ili kulihimili kanisa? Dhara linalopatikana katika afya ya kimwili, kiakili, na kimaadili katika matukio haya ya burudani na uroho si dogo. Na siku ile ya hesabu ya mwisho itaonesha roho zilizopotea kupitia katika ushawishi wa matukio haya ya sherehe na upuuzi. **{WM 291.1}**

Ni Ukweli wa kusikitisha kwamba mambo matakatifu na ya milele hayana nguvu ile ya kufungua mioyo ya wafuasi bayana wa Kristo kutoa sadaka za hiari ili kuendeleza injili, kama hongo ya majaribu ya karamu na furaha ya jumla.

Ni Ukweli wa kusikitisha kwamba vishawishi hivi vitaenea wakati vitu vitakatifu na vya milele havitakuwa na nguvu ya kushawishi moyo kushiriki katika kazi za ukarimu. **{WM 291.2}**

Mpango wa Musa jangwani wa kuchangiza mali ulifanikiwa sana. Hakukuwa na umuhimu wa ulazimishwaji. Musa hakufanya karamu yoyote kubwa. Hakuwaalika watu kwenye matukio ya sherehe, kucheza, na burudani ya jumla. Wala hakuanzisha bahati nasibu au kitu chochote cha mpango huu mchafu ili kupata fedha ya kujenga maskani ya Mungu jangwani. Mungu alimwamuru Musa kuwaalika wana wa Israeli wapate kuleta sadaka. Musa alipaswa kupokea zawadi za kila mtu ambaye alitoa kwa hiari kutoka moyoni mwake. Sadaka hizi za hiari

zilikuja kwa wingi sana kiasi kwamba Musa alitangaza kuwa ilitosha. Inabidi waache kutoa zawadi zao, kwa kuwa walikuwa wametoa kwa wingi, zaidi ya kile walichoweza kutumia.**{WM 291.3}**

Majaribu ya Shetani hufanikiwa kwa wafuasi bayana wa Kristo juu ya suala la kuendekeza anasa na hamu ya chakula. Akiwa amevaa kama malaika wa nuru, atanukuu Maandiko ili kuhalalisha majaribu anayoyaweka mbele ya watu ili wapate kuendekeza hamu ya chakula, na anasa za dunia ambazo hupendeza moyo wa kimwili. Wafuasi bayana wa Kristo ni dhaifu katika nguvu za kimaadili na wanavutiwa na hongo ambayo Shetani ameiwasilisha mbele yao, naye anapata ushindi. **{WM 292.1}**

Je! Mungu anayaangaliaje makanisa ambayo yanategemezwa na fedha kama hizo? Kristo hawezi kukubali sadaka hizi, kwa sababu hazikutolewa kupitia upendo wao na kujitoa Kwake bali kupitia ibada yao ya sanamu kwa nafsi. Lakini kile ambacho wengi hawangefanya kwa upendo wa Kristo watafanya kwa upendo wa anasa za kupendeza ili wapate kukidhi hamu ya chakula na upendo wa burudani za dunia ili kufurahisha moyo wa kimwili. - *The Review and Herald,* Oktoba 13, 1874. **{WM 292.2}**

Sababu ya Kutoa Inaandikwa. - Nilioneshwa kwamba malaika anayetunza kumbukumbu anaweka rekodi ya uaminifu ya kila sadaka inayotolewa kwa Mungu, na kuwekwa katika hazina, na pia ya matokeo ya

mwisho ya mali zilizotolewa kwa jinsi hiyo. Jicho la Mungu huzingatia kila sarafu inayotolewa kwa ajili ya kusudi Lake na utayari au kusita kwa mtoaji. Sababu ya kutoa pia huandikwa. Wale wanaojitoa mhanga, waliojiweka wakfu ambao humrudishia Mungu vitu ambavyo ni Vyake, kama anavyotaka kutoka kwao, watalipwa kulingana na kazi zao. -— *Testimonies for the Church* 2:518, 519.**{WM 292.3}**

Sehemu ya XI Matunda ya Huduma ya Ustawi

Wazo la Thamani

Watu wanaowaangalia na kuwapima wale wanaodai kuuamini Ukweli maalum kwa wakati huu Wanatazama

wapate kuona jinsi maisha na mwenendo wao unavyomwakilisha Kristo. Kwa kujishughulisha kwa unyenyekevu na kwa bidii katika kazi ya kutenda mema kwa wote, watu wa Mungu watatoa ushawishi ambao utakuwa na nguvu katika kila mji na jiji ambapo Ukweli umeingia. Ikiwa wote wanaoujua Ukweli watashikilia kazi hii kadiri fursa zinavyowasilishwa, siku kwa siku wakitenda matendo madogo ya upendo katika ujirani wanakoishi, Kristo atadhihirika kwa majirani zao. Injili itadhihirika kama nguvu hai na si kama hadithi zilizotungwa kwa werevu au mawazo ya kipuuzi. Itadhihirika kama Ukweli, na wala si matokeo ya fikira au shauku. Hii itakuwa na umuhimu kuliko mahubiri au maungamo au kanuni za

imani. - *Testimonies for the Church* 6:264. **{WM 294.1}**

2 Wakorintho 9

11 mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu
shukrani kwa kazi yetu.
12 Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa
tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu;
13 kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo, wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii
wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha
wao na watu wote.
14 Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu
ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu.

Sura ya Arubaini – Mvuto wa Huduma ya Ujirani

Ruhusu Ulimwengu Uone. - Ruhusu ulimwengu uone kwamba sisi kwa ubinafsi hatujafanywa kuwa waangalifu kwa ajili ya masilahi yetu ya pekee na furaha za kidini, bali kwamba sisi ni wakarimu, na tunataka washiriki baraka na fadhila zetu, kupitia katika utakaso wa Ukweli. Hebu waone

kwamba dini ambayo tunaikiri haifungi au kuganda kwenye njia zielekeazo rohoni, na kutufanya kuwa wasio na huruma, bahili na washurutishaji. Hebu wote wanaodai kuwa wamempata Kristo, wahudumu kama alivyofanya kwa faida ya mwanadamu, wakihifadhi kwa upendo mkubwa roho ya ukarimu wa busara. Ndipo tutakapoona roho nyingi zikifuata nuru ile inayoangaza kutoka katika maadili na mfano wetu. -*Testimonies for the Church* 4:59. **{WM 295.1}**

Kazi ya Msaada wa Kikristo Ina Ufanisi Zaidi ya Kuhubiri. - Matendo mema ya watoto wa Mungu ndiyo hubiri lenye ufanisi kabisa alilo nalo yule asiyeamini. — *Spiritual Gifts* 2:235.**{WM 295.2}**

Hebu na wafanye kazi ya msaada wa Kikristo, wakiwalisha wenye njaa na kuwavika nguo walio uchi. Hii itakuwa na ushawishi mkubwa zaidi kwa ajili ya mema kuliko kuhubiriwa kwa hotuba za injili. - *Testimonies for the Church* 7:227, 228. **{WM 296.1}**

Mawazo yetu ya ukarimu wa Kikristo ni lazima yafanyiwe kazi ikiwa tunataka yaongezeke. Kazi ya vitendo itafanikisha mengi zaidi ya mahubiri. - *Testimonies for the Church* 6:302. **{WM 296.2}**

Mvuto wa Maisha ya Huduma ya Kikristo. - Maisha ya Mkristo yatashuhudia kwamba anatawaliwa na sheria zingine zaidi ya zile ambazo ulimwengu unazitii - sheria za daraja la juu kuliko zile zinazowaongoza wapenda ulimwengu. Mapenzi ya Mungu,

Muumbaji wetu, yanapaswa kudhihirishwa ndani yetu, si tu katika jina tunaloitwa, lakini katika maisha yetu ya kujikana nafsi au kujinyima. Tunapaswa kutoa ushahidi kwamba tunavutiwa na kuongozwa na kanuni zisizo za ubinafsi. Makusudi na shughuli zetu zote zinapaswa kusimama kwa tofauti dhahiri kinyume na ubinafsi wa ulimwengu. **{WM 296.3}**

Umoja na Kristo huwawezesha wanadamu kuwa na mvuto mkubwa kuliko ule wa watu mashuhuri wa ulimwengu huu. Wanapoiga mfano wa Kristo, wanakuwa, kwa neema Yake, na nguvu ya kutoa faida kwa kanisa na jamii. Ushawishi wao unaonekana kulingana tu na udhahiri wa mpaka unaowatenga katika roho na kanuni kutoka kwa ulimwengu. **{WM 296.4}**

Kwa kuwa umoja ni nguvu, Yeye aliye Chanzo cha uwezo wote, cha wema wote, rehema, na upendo, huwachukua wanadamu wenye ukomo, katika ushirika na Yeye kwa kusudi la kutoa nguvu Yake ya mbingu/Kiungu kwa mawakala wanadamu, wapate kuutawanya mvuto Wake na kuueneza mbali na karibu. Mtu anapounganishwa na Kristo, mshirika wa asili ya Kiungu, shauku yake inatambulishwa na ile ya wanadamu wote wanaoteseka. Tunapouangalia msalaba wa Kalvari ipasavyo, kila mshipa wa fahamu wa moyo na ubongo utasisimka kwa huruma kwa shida ya wanadamu katika sehemu zote za ulimwengu wetu. Wale ambao wameumbwa upya katika Kristo Yesu watatambua aibu ya dhambi na huruma ya Kiungu ya Kristo katika

kafara Yake isiyo na mwisho kwa ajili ya mwanadamu aliyeanguka. Ushirika na Kristo unawapa ulaini wa moyo; kutakuwa na huruma katika kutazama kwao, katika toni za sauti; na bidii ya unyenyekevu, upendo, na nguvu, katika juhudi zao, ambazo zitawafanya kuwa na nguvu kupitia kwa Mungu katika kuongoa roho kwa ajili ya Kristo. — *The Medical Missionary,* Juni, 1891. **{WM 296.5}**

Mvuto Uliotukuzwa wa Matendo ya Kukirimu. - Ikiwa ulimwengu ungekuwa nao mbele yao mfano ule ambao Mungu anawataka wale wanaomwamini wauweke, wangelifanya kazi za Kristo. Kama Yesu angewekwa mbele, msulubiwa miongoni mwetu, kama tungeutazama msalaba wa Kalvari katika nuru ya Neno la Mungu,

tungekuwa wamoja na Kristo kama Yeye alivyokuwa umoja na Baba. Imani yetu ingekuwa tofauti kabisa na imani inayooneshwa sasa. Ingekuwa imani inayofanya kazi kwa upendo kwa Mungu na kwa wanadamu wenzetu, na kuisafisha roho. Ikiwa imani hii ingeoneshwa na watu wa Mungu, wengi zaidi wangemwamini Kristo. Mvuto uliotukuzwa ungewekwa na matendo ya kukirimu ya watumishi wa Mungu, nao wangeangaza kama taa ulimwenguni. – *Special Testimonies, series* A 10:2.**{WM 297.1}**

Una Nguvu Kuliko Upanga au Mahakama za Haki. - Upendo wa Mungu moyoni, ukidhihirishwa katika kazi ya umishonari wa kweli, isiyo na ubinafsi, utakuwa na nguvu zaidi kuliko upanga au mahakama za haki katika

kushughulika na mtenda maovu. Mmisionari hai, moyo wake ukiwa umefurika na upendo wa Mungu, anaweza kubomoa vizuizi. Mmisionari wa tiba, anatejishughulisha na kazi yake aliyopangiwa, hawezi kupunguza magonjwa ya mwili peke yake, bali kupitia katika upendo na neema ya Kristo anaweza kuponya roho yenye ugonjwa, yenye ukoma wa dhambi. Mioyo ya wanadamu mara nyingi huwa migumu chini ya karipio, lakini hawawezi kuhimili upendo unaooneshwa kwao katika Kristo. - *Manuscript* 60, 1897. **{WM 297.2}**

Utumishi wa Upendo Utapunguza Chuki. - Utukufu wa mbingu ni katika kuwainua walioanguka, kuwafariji wenye huzuni. Na popote Kristo anapokaa ndani ya

mioyo ya wanadamu atadhihirishwa kwa njia hiyo hiyo. Popote inapofanya kazi dini ya Kristo, itabariki. Popote inapofanya kazi kuna mwangaza.... **{WM 298.1}**

Hata iweje tofauti katika imani ya kidini, wito kutoka kwa wanadamu wanaoteseka ni lazima usikilizwe na kujibiwa. Mahali pale ambapo uchungu wa hisia upo kwa sababu ya tofauti ya dini, mema mengi yanaweza kufanywa na huduma ya mtu binafsi. Utumishi wa upendo utavunja upendeleo na kuongoa roho kwa Mungu. - *Christ's Object Lessons,* 386.**{WM 298.2}**

Lazima Tuivunje Nguvu Chuki. - Wafuasi wa Kristo, kadiri wanavyoukaribia wakati wa taabu, [watapaswa] kufanya kila juhudi

kujiweka katika nuru sahihi mbele ya watu, kuvunja nguvu za chuki. — *The Great Controversy,* 616. **{WM 298.3}**

Kama njia ya kuishinda chuki na kupata nafasi ya kuzifikia akili za watu kazi ya umisionari wa tiba ni lazima ifanyike…. Tunapaswa kufanya kazi kama wamisionari wa tiba wa injili kuponya roho zenye ugonjwa wa dhambi kwa kuwapa ujumbe wa wokovu. Kazi hii itaibomoa chuki kuliko inavyoweza kufanyika na kitu kingine chochote. — *Testimonies for the Church* 9:211. **{WM 298.4}**

Ushahidi wa Maisha Maadilifu, Yasiyo na Ubinafsi. – Matendo mema ya watu wa Mungu yana mvuto wenye nguvu kuliko maneno. Kwa maisha yao maadilifu na matendo yao yasiyo ya ubinafsi mtazamaji anaongozwa

kutamani haki ile ile ambayo ilizaa matunda mazuri kama hayo. - *The Review and Herald,* Mei 5, 1885. **{WM 298.5}**

Matendo ni Makubwa Kuliko Kanuni za Imani. - Ukweli wa Bwana una ushawishi mdogo kwa ulimwengu, wakati ambapo ulipaswa kuwa na ushawishi mwingi kupitia katika utendaji wetu. Maungamo tu ya dini yamejaa tele, lakini hayana uzito wa maana. Tunaweza kudai kuwa wafuasi wa Kristo, tunaweza kudai kuamini kila Ukweli katika Neno la Mungu; lakini hii haitamfaa chochote jirani yetu isipokuwa imani yetu imechukuliwa katika maisha yetu ya kila siku. Ungamo/kukiri kwetu kunaweza kuwa kwa hali y ajuu kama kufikia mbingu, lakini halitatuokoa sisi wenyewe wala

wenzetu isipokuwa tumekuwa Wakristo. Mfano sahihi utatenda zaidi kwa ajili ya faida ya ulimwengu kuliko maungamo yetu yote. – *Christ's Object Lessons,* 383. **{WM 299.1}**

Mivuto Inayotoka Katika Nyumba Yenye Upendo. - Wale ambao wanakuza upendo katika maisha ya nyumbani watatengeneza tabia zinazofana na mfano wa Kristo, nao watabidishwa kuweka mvuto wenye kusaidia ng'ambo ya mzunguko wa familia, ili wapate kuwabariki wengine kwa utumishi wa wema, wenye kufikiria, kwa maneno ya kufurahisha, na huruma kama ya Kristo, na matendo ya ukarimu. Watakuwa wepesi katika kuwapambanua wale walio na mioyo yenye njaa, nao watafanya karamu kwa ajili ya wale walio wahitaji na wenye

dhiki. Wale ambao wana utambuzi wa mbinguni, ambao humjali kila mshiriki wa familia, katika kutekeleza wajibu wao wote, watajiandaa kufanya kazi ambayo itazichangamsha nyumba nyingine nao watawafundisha wengine kwa kanuni na mfano kile ambacho kitafanya nyumba kuwa na furaha. - *The Review and Herald,* Oktoba 15, 1895. **{WM 299.2}**

Mifano ya Mvuto. - Kwa hekima yao na haki, kwa usafi na ukarimu wa maisha yao ya kila siku, kwa kujitoa kwao kwa masilahi ya watu – watu hao, waabudu sanamu - Yusufu na Danieli walijidhihirisha kuwa waaminifu kwa kanuni za mafunzo yao ya awali, wakweli Kwake Yeye ambaye walikuwa ni wawakilishi Wake. Watu hawa, kote huko Misri na Babeli, taifa lote liliwaheshimu; na ndani yao taifa la

kipagani, na mataifa yote ambayo walihusiana nao, waliona kielelezo cha wema na ukarimu wa Mungu, kielelezo cha upendo wa Kristo. **{WM 299.3}**

Ilikuwa kazi ya maisha iliyoje hawa Waebrania waungwana waliitenda! Walipokuwa wakiiaga maskani ya utoto wao, ni kidogo kiasi gani walikuwa na ndoto ya hatima/majaliwa yao ya juu! Wakiwa waaminifu na wenye msimamo thabiti, walijisalimisha katika uongozi wa Bwana, kiasi kwamba kupitia kwao Mungu aliweza kutimiza kusudi Lake. **{WM 300.1}**

Kweli zile zile kuu ambazo zilidhihirishwa kupitia kwa watu hawa, Mungu anataka kuzidhihirisha kupitia kwa vijana na watoto wa leo. Historia ya Yusufu na Danieli ni kielelezo cha kile

atakachokifanya kwa wale wanaojisalimisha Kwake na kwa moyo wote kujitahidi kutimiza kusudi Lake. **{WM 300.2}**

Hitaji kuu kabisa la ulimwengu ni hitaji la watu - watu ambao hawatanunuliwa au kuuzwa; watu ambao ndasni kabisa ya nafsi zao ni wakweli na waaminifu; watu ambao hawaogopi kuiita dhambi kwa Jina lake sahihi; watu ambao dhamiri zao ni za kweli kwa wajibu kama mshale wa dira kwenye ncha ya dunia; watu ambao watasimama kuitetea haki hata kama mbingu zitaanguka. — *Education,* 56, 57. **{WM 300.3}**

Sura ya Arubaini na Moja - Baraka Zinazojirejea

Kanuni ya Tendo na Mjibizo (action and Reaction). - Hekima ya Bwana imeweka katika mpango wa wokovu kanuni ya tendo na mjibizo, ikifanya kazi ya ukarimu, katika matawi yake yote, kubarikiwa mara mbili. Yeye ambaye hutoa kwa wahitaji huwabariki wengine, na hubarikiwa yeye mwenyewe kwa kiwango kikubwa zaidi. Mungu angeweza kufikia lengo Lake la kuwaokoa wenye dhambi pasipo msaada wowote wa mwanadamu, lakini alijua kwamba mwanadamu asingeweza kuwa na furaha bila kuwa na sehemu ya kutenda katika kazi hii kubwa ambayo katika hiyo angekuwa anakuza tabia ya kujinyima na ukarimu. Mtu huyo anaweza asipoteze matokeo

yaliyobarikiwa ya ukarimu, Mkombozi wetu alitengeneza mpango wa kumwandikisha kama mfanyakazi mwenza. - *Testimonies for the Church* 3:382. **{WM 301.1}**

Ni kadiri tunavyojitoa kwa Mungu kwa ajili ya huduma ya wanadamu ndivyo na Yeye anavyojitoa kwetu. Hakuna mtu anayeweza kutoa nafasi katika moyo wake mwenyewe na maisha kwa ajili ya mkondo wa baraka za Mungu kutiririka kwenda kwa wengine bila kupokea ndani yake mwenyewe thawabu nyingi. - *Mount wa Blessing,* uk. 81, 82. **{WM 301.2}**

Kuwasaidia Wengine Kutakuza Tabia. - Ni katika kufanya kazi za Kristo, tukitumikia kama alivyofanya kwa wanaoteseka na wenye dhiki, ndipo

tutakapokuza tabia ya Kikristo. Ni kwa ajili ya faida yetu Mungu ametuita kuwa na desturi ya kujinyima kwa ajili ya Kristo, kubeba msalaba, kufanya kazi na kujitoa katika kujitahidi kukiokoa kile kilichopotea. Huu ni mchakato wa Bwana wa kutakasa, kusafisha na kuondolea mbali vitu vilivyo duni, ili sifa bainishi za tabia za thamani ambazo zilikuwa ndani ya Kristo Yesu, ziweza kuonekana ndani ya muumini.... Kupitia katika neema ya Kristo juhudi zetu za kuwabariki wengine si tu njia ya ukuaji wetu katika neema, bali zitazidisha nguvu ya furaha yetu ijayo ya milele. Kwa wale ambao wamekuwa wafanyakazi wenza wa Kristo itasemwa, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu: ulikuwa mwaminifu kwa machache; nitakuweka juu ya mengi.” —

The Review and Herald, Juni 27, 1893. **{WM 301.3}**

Roho ya kufanya kazi bila ubinafsi kwa wengine hutoa kina, uthabiti, na uzuri kama wa Kristo kwa tabia na huleta amani na furaha kwa mwenye nayo. — *Testimonies for the Church* 5:607.**{WM 302.1}**

Chanzo cha Furaha ya Kweli. - Katika kuwatendea wengine uzoefu wa kuridhika kunakopendeza utapatikana, amani ya ndani ambayo itakuwa thawabu ya kutosha. Wanaposukumwa na tamaa ya hali ya juu na iliyo bora ya kuwatendea wengine mema, watapata furaha ya kweli katika utekelezaji kwa uaminifu wa wajibu mbalimbali katika maisha. - *Testimonies for the Church* 2:132. **{WM 302.2}**

Furaha ya kweli inapatikana tu katika kuwa mwema na kutenda mema. — *The Youth's Instructor,* Desemba 5, 1901. **{WM 302.5}**

Furaha yetu italingana na kazi zetu zisizo na ubinafsi, zinazochochewa na upendo wa Bwana, kwa kuwa katika mpango wa wokovu Mungu ameagiza kanuni ya tendo na mjibizo. — *The Signs of the Times,* Novemba 25, 1886. **{WM 302.4}**

Kazi ya Ustawi Inaleta Afya. - Wale ambao hutoa uthibitisho wa kiutendaji wa ukarimu wao kwa utu wema wao na matendo ya huruma kwa maskini, na wanaoteseka, na wenye bahati mbaya, si tu kwamba wanawatuliza watesekao, lakini wanachangia kwa kiasi kikubwa furaha yao wenyewe, na wako katika njia ya

kupata afya ya roho na ya mwili. Isaya... ameieleza wazi kazi ambayo Mungu ataikubali na kuwabariki watu Wake kwa kuifanya. — *Testimonies for the Church* 4:60. **{WM 302.5}**

Ninavuta usikivu wenu katika matokeo ya hakika ya kutii onyo la Bwana la kuwatunza wenye shida: "Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara." Je, si hiki sisi sote tunakihitaji? Ndio, kuna afya na amani katika kuyafanya mapenzi ya Baba yetu wa Mbinguni. "Haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde. Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, naye atasema, Mimi hapa. Kama ukiiondoa nira; isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu; na kama ukimkunjulia

mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui." — *The Medical Missionary*, Juni, 1891. **{WM 302.6}**

Jinsi Kazi ya Ustawi Inavyosababisha Afya. - Raha ya kufanya mema kwa wengine hutoa mwanga kwa hisia ambao unamulika katika mishipa ya fahamu, huhuisha mzunguko wa damu, na kusababisha afya ya kiakili na ya kimwili. - *Testimonies for the Church* 4:56. **{WM 303.1}**

Makubaliano yaliyopo kati ya akili na mwili ni makubwa sana (viungo vinasaidiana na kuoneana huruma). Moja inapoathirika, nyingine inaitikia. Hali ya akili inategemeana sana na afya ya mfumo wa kimwili. Kama akili ni huru na yenye furaha, katika ufahamu wa kutenda mema na hisia ya kuridhika kwa sababu ya kusababisha furaha kwa wengine, itasababisha uchangamfu ambao utaugusa mfumo mzima, na kusababisha mzunguko huru zaidi wa damu na kuupa siha mwili mzima. Baraka ya Mungu ni mponyaji, na wale ambao wamejaa tele katika kuwanufaisha wengine wataitambua baraka hiyo ya ajabu katika mioyo yao na maisha yao. - *Testimonies for the Church* 4:60. **{WM 303.2}**

Tiba ya Magonjwa. - Baadhi wanakiri afya yao mbaya- wangependa kutenda kama wangekuwa na nguvu. Watu kama hao kwa muda mrefu wamejifungia wenyewe na kufikiri sana juu ya hisia zao hafifu na kuzungumza sana juu ya mateso yao, majaribu, na dhiki kiasi kwamba inakuwa ndio Ukweli wao wa sasa. Hawawezi kumfikiria mtu mwingine yeyote isipokuwa nafsi zao, hata kama wengine wanaweza kuwa wanahitaji huruma na msaada kiasi gani. Wewe ambaye unateseka na afya mbaya, kuna dawa kwa ajili yako. Ikiwa utawavika walio uchi, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako, na kuwapa wenye njaa chakula chako, " Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara." Kutenda

mema ni dawa bora ya maradhi. Wale ambao wanajihusisha na kazi hiyo wanaalikwa kumwita Mungu, na ameahidi Mwenyewe kuwajibu. Nafsi zao zitashiba wakati wa ukame, nao watakuwa kama bustani iliyotiwa maji, ambayo maji yake hayapunguki. — *Testimonies for the Church* 2:29. **{WM 303.3}**

Haya ndiyo maagizo na kichocheo ambacho Kristo ameagiza kwa roho zile zinazozimia, zenye mashaka, na zinazotetemeka (This is the recipe that Christ has prescribed for the fainthearted, doubting, trembling soul. Let the sorrowful ones, who walk mournfully before the Lord, arise and help someone who needs help. —Testimonies for the Church 6:266.) .

Hebu wenye huzuni, ambao hutembea kwa majonzi mbele za Bwana, wainuke na kumsaidia mtu fulani ambaye

anahitaji msaada. - *Testimonies for the Church* 6:266. **{WM 304.1}**

Huruma Huzalisha Mema Mengi. - Huruma ya mwanadamu inapochanganywa na upendo na ukarimu na kutakaswa na Roho ya Yesu, inakuwa msingi ambao unaweza kusababisha mema makubwa. Wale wanaokuza ukarimu si tu kwamba wanafanya kazi nzuri kwa wengine na kuwabariki wale wanaopokea matendo hayo mazuri, bali pia wanajinufaisha wenyewe kwa kufungua mioyo yao kwa ajili ya mvuto mwema wa ukarimu wa kweli. Kila mwale wa nuru unaotolewa kwa wengine utaonekana katika mioyo yetu wenyewe. Kila aina ya neno la huruma linalonenwa kwa mwenye

huzuni, kila tendo la kumsaidia aliyeonewa, na kila zawadi kwa ajili ya kukimu mahitaji ya wanadamu wenzetu, iliyotolewa au kufanywa kwa kulenga katika utukufu wa Mungu, itasababisha baraka kwa mtoaji. Wale ambao wanafanya kazi kwa jinsi hiyo wanatii sheria ya mbinguni na watapokea kibali cha Mungu.... **{WM 304.2}**

Yesu alijua uwezo wa ukarimu juu ya moyo na maisha ya mfadhili, na alitaka kutia kwenye akili za wanafunzi Wake faida zitakazopatikana kutokana na utekelezaji wa fadhila hii. Anasema: "Ni heri kutoa kuliko kupokea." Anaelezea roho ya ukarimu wa furaha, ambayo inapaswa kutumiwa kwa marafiki, majirani, na wageni, kwa mfano wa mtu yule aliyesafiri kutoka Yerusalemu

kwenda Yeriko. - Testimonies for the Church 4:56, 57. **{WM 305.1}**

Katika Kumwokoa Jirani Yake Alijiokoa Mwenyewe. - Kanisa linalofanya kazi ni kanisa linalokua. Washiriki hupata kichocheo na dawa ya kuchangamsha mwili katika kuwasaidia wengine. Nimesoma juu ya mtu ambaye, akisafiri siku moja ya majira ya baridi kupitia njia ya mkondo wa theluji, alitiwa ganzi na baridi ile, ambayo bila kutambua ilikuwa karibu kugandisha nguvu zake uhai. Alikaribia kufa kwa kutiwa baridi na alikuwa karibu kuacha kupambania maisha, aliposikia kelele za msafiri mwenzake ambaye pia alikuwa akiangamia kwa baridi. Huruma yake iliamshwa, na alidhamiria kumwokoa. Alisugua maungo ya mtu asiyejiweza yaliyokuwa na baridi ya barafu, na

baada ya juhudi kubwa akamwinua asimame kwa miguu yake. Kwa kuwa mgonjwa yule hakuweza kusimama, alimchukua katika mikono ya huruma kupitia kwenye mkondo ule ule ambao alifikiri kwamba hangeweza kamwe kuupitia peke yake. **{WM 305.2}**

Alipomfikisha msafiri mwenzake katika mahali pa usalama, Ukweli uliangaza ndani yake kwamba kwa kumwokoa jirani yake alikuwa pia amejiokoa mwenyewe. Jitihada zake za dhati za kumsaidia mwingine zilisisimua damu iliyokuwa imeanza kuganda kwenye mishipa yake mwenyewe na kusafirisha joto la afya katika mikono na miguu ya mwili wake. **{WM 305.3}**

Somo kwamba katika kuwasaidia wengine sisi wenyewe tunapokea

msaada, ni lazima lisisitizwe kwa waumini wachanga kila wakati, kwa kanuni na mfano, ili katika uzoefu wao wa Kikristo wapate matokeo bora. Hebu wale wanaokata tamaa, wale wanaopenda kufikiri kwamba njia ya uzima wa milele ni ngumu na yenye usumbufu, waende kazini kuwasaidia wengine. Jitihada kama hizo, zikiunganishwa na maombi kwa ajili ya nuru ya kiungu, zitasababisha mioyo yao wenyewe kugonga kwa uwezo unaosisimua wa neema ya Mungu, mapenzi halisi zaidi, yenye bidii zaidi, na yenye maombi zaidi. — *Gospel Workers,* 198, 199.**{WM 305.4}**

Kanisa Linabarikiwa. - Hebu washiriki wa kanisa katikati ya juma watende kwa uaminifu, na siku ya Sabato waelezane uzoefu wao. Hapo

ndipo kukutanika kutakuwa kama chakula kwa wakati unaostahili, na kuwaletea wote waliopo maisha mapya na nguvu mpya. Watu wa Mungu wanapoona hitaji kuu la kufanya kazi kama Kristo alivyofanya kazi kwa ajili ya uongofu wa wenye dhambi, ushuhuda unaotolewa nao katika huduma za Sabato utajazwa nguvu. Kwa furaha watashuhudia thamani ya uzoefu ambao wameupata katika kufanya kazi kwa ajili ya wengine. — *Gospel Workers,* 199. **{WM 306.1}**

Hisani Zetu Wenyewe Zinatumika. – Kama kamwe kusingekuwa na kitu chochote ulimwenguni cha kufanya kazi katika malengo yanayopishana nasi, saburi, ustahamilivu, upole, unyenyekevu, na uvumilivu visingeitwa katika utendaji.

Kadiri tunavyozishughulisha hisani hizi, ndivyo zitakavyoongezeka na kuimarishwa zaidi. Kadiri tunavyogawa chakula chetu cha kimwili kwa wenye njaa, kadiri tunavyowavika walio uchi, kuwatembelea wagonjwa, na kuwafariji yatima na mjane katika shida zao, ndivyo tutakavyotambua kwa uwazi baraka za Mungu. - *Manuscript* 64, 1894.**{WM 306.2}**

Kwa Nini Baraka Zinazuiliwa. - Baraka ya Mungu haiwezi kuja juu ya wale ambao ni wavivu katika shamba lake la mizabibu. Wakristo bayana ambao hawafanyi chochote wanahafifisha juhudi za wafanyakazi halisi kwa ushawishi na mfano wao. Wanafanya kweli kuu na muhimu wanazodai kuziamini, zionekane kuwa ni kinzani, na kuzifanya kuwa bure.

Wanawasilisha isivyo tabia ya Kristo. Je! Mungu anawezaje kuruhusu mvua ya neema Yake ije juu ya makanisa ambayo yana sehemu kubwa ya washiriki wa aina hii? Hayana matumizi yoyote katika kazi ya Mungu. Bwana anawezaje kuwaambia watu kama hao, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu: ... ingia katika furaha ya Bwana wako," wakati ambapo hawajawa wema wala waaminifu? Mungu hawezi kusema uongo. Nguvu ya neema ya Mungu haiwezi kutolewa kwa kiasi kikubwa kwa makanisa hayo. Ingefedhehesha tabia yake mwenyewe iliyo tukufu kwa kuruhusu mito ya neema iwafikie watu ambao hawataivaa nira ya Kristo, ambao hawatabeba mizigo Yake, ambao hawatajinyima, ambao hawatauinua msalaba wa Kristo. Kwa sababu ya uvivu

wanakuwa kizuizi kwa wale ambao wangetoka kwenda kuifanya kazi hiyo kama wasingelizuia njia. - *The Review and Herald,* Julai 21, 1896. **{WM 306.3}**

Uwe **Kijito Hai cha Matendo Mema.** - Ikiwa Mungu na Kristo na malaika wanafurahi wakati hata mwenye dhambi mmoja tu anatubu na kuwa mtiifu kwa Kristo, je! Mtu hapaswi kujawa na roho ile ile, na kufanya kazi siku zote kwa juhudi thabiti ya kuokoa, si tu nafsi yake mwenyewe, bali pia roho za wengine? Ikiwa tutafanya kazi katika mwelekeo huu kwa shauku ya moyo wote kama wafuasi wa Kristo, tukitoa kila wajibu, tukitumia vizuri kila fursa, roho zenu wenyewe zitakuwa zikipatana polepole na tabia ya Mkristo mkamilifu. Moyo hautakuwa mkavu na usiohisi.

Maisha ya kiroho hayatadumazwa. Moyo utang'aa kwa chapa ya mfano wa Kiungu/Bwana, kwa kuwa utakubaliana kwa karibu na Mungu. Maisha yote yatafurika kwa utayari wa furaha katika mifereji ya upendo na huruma kwa wanadamu. Nafsi (umimi) itasahaulika, na njia za tabaka hili zitawekwa imara ndani ya Mungu. Katika kuwanywesha maji watu wengine roho zao wenyewe zitanyweshwa. Kijito kinachotiririka kupitia roho zao kinatoka kwenye chemchemi iliyo hai na kinatiririka kwenda kwa wengine kwa matendo mema, kwa bidii, kwa juhudi isiyo na ubinafsi kwa ajili ya wokovu wao. Ili kuwa mti wenye kuzaa matunda, roho ni lazima ipate msaada na lishe kutoka katika Chemchemi ya Uhai na lazima iwe na mapatano/amani na Muumbaji.

— *The Review and Herald,* Januari 2, 1879. **{WM 307.1}**

Sababu za Utasa. - Hakuna kanisa letu hata moja linalotakiwa kuwa tasa na lisilozaa matunda. Lakini baadhi ya ndugu na dada zetu wako katika hatari ya kufa njaa kiroho hata pale ambapo wanasikia kila wakati Ukweli unaowasilishwa na wachungaji wetu, kwa kuwa wanapuuza kukitoa kile wanachokipokea. Mungu anahitaji kila mmoja wa mawakili wake kutumia talanta aliyokabidhiwa. Yeye hutupa karama nyingi juu yetu ili tuweze kuzitoa bure kwa wengine. Daima anaufanya moyo kufurika kwa nuru ya uwepo Wake, ili tuweze kumdhihirisha Kristo kwa wanadamu wenzetu. Wale ambao wanakunja mikono yao katika raha, wakiridhika na kutokufanya

chochote, Je, wanawezaje kutarajia Mungu kuendelea kuwapa mahitaji yao? Washiriki wa makanisa yetu yote wanapaswa kufanya kazi kama wale ambao ni lazima watatoa hesabu. - *The Review and Herald,* Novemba 11, 1902. **{WM 308.1}**

Majaliwa Yetu Yanahusika. - Ni kazi ile ambayo tunaifanya au hatuifanyi ndiyo inayosema kwa nguvu kubwa kuhusu maisha yetu na yale yatakayotutokea mwishomi/hatimaye. Mungu anataka tutumie vizuri kila fursa kwa manufaa ambayo tumepewa. Kupuuza kufanya hivi ni hatari kwa ukuaji wetu wa kiroho. — *Testimonies for the Church* 3:540.**{WM 308.2}**

Yeye Anayeishi kwa Ajili ya Kujipendeza Yeye Mwenyewe si

Mkristo. - “Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe?” Ni kiasi gani cha maagizo haya yamefanyika! Ni wangapi wamefunga macho na kufunga mlango wa moyo, isije ushawishi fulani ulainishao ukawachochea kufanya matendo ya wema na fadhili! Kazi ya Kristo haikomi kamwe. Upendo Wake wa upole na wema ni nyingi mno; rehema Yake iko juu ya watoto wote wa wanadamu. Bwana Yesu anamaanisha kwamba mtabarikiwa katika kutoa kwa wahitaji Wake, wanaoteseka. Amewafanya watu kuwa wabia wenza Wake. "Ninyi ni watenda kazi pamoja na Mungu." Je! Kristo, kwa kanuni na

mfano, hajatufundisha wazi nini tunapaswa kufanya? Tunapaswa kufanya kazi, tukiwa tumejazwa na Roho Wake, tunapotazama msalabani, tukiwa tayari ikiwa atatuagiza, kuyaacha yote kwa ajili Yake. Yeye anayeishi kwa ajili ya kujipendeza mwenyewe si Mkristo. Hajaumbwa upya katika Kristo Yesu. **{WM 309.1}**

Mkristo anajisikia kwamba hakuna kiumbe mwingine katika ulimwengu aliye na madai kwake kama yale ambayo Yesu anayo. Yeye ni mali iliyonunuliwa, iliyonunuliwa kwa bei ya gharama kubwa ya damu ya Mwana-Kondoo. Anapaswa kujitoa kikamilifu kwa Kristo; mawazo yake, maneno yake, na kazi zake zote zinapaswa kuwa chini ya mapenzi ya Kristo. — *The Medical Missionary*, Juni, 1891.**{WM 309.2}**

Kuridhika Hapa na Malipo ya Milele Baada ya Hapa. - Ili kuwa na furaha, ni lazima tujitahidi kufikia tabia ile ambayo Kristo aliionesha. Sifa moja ya pekee ya Kristo ilikuwa ni kujikana na ukarimu wake. Hakuja kutafuta Mambo Yake Mwenyewe. Alizunguka huku na huko akitenda mema, na hii ndio ilikuwa chakula na kinywaji Chake. Tunaweza, kwa kufuata mfano wa Mwokozi, kuwa katika ushirika mtakatifu pamoja Naye; na kwa kujitahidi kila siku kuiga tabia yake na kufuata mfano wake tutakuwa baraka kwa ulimwengu na kujipatia utoshelevu hapa na thawabu ya milele baadaye. — *Testimonies for the Church* 4:227. **{WM 309.3}**

Sura ya Arubaini na Mbili - Thawabu za Sasa na za Milele

Huduma Huleta Thawabu. - Wakati ambapo thawabu kubwa ya mwisho inatolewa wakati wa kuja kwa Kristo, huduma ya moyo wa kweli kwa Mungu huleta thawabu hata katika maisha haya.-*Testimonies for the Church* 6:305, 306. **{WM 311.1}**

Kuletwa Karibu Zaidi na Yesu. - Mnapowasaidia maskini, kuwahurumia wenye dhiki na walioonewa, na kufanya urafiki na yatima, mnajiweka wenyewe katika uhusiano wa karibu na Yesu. - *Testimonies for the Church* 2:25. **{WM 311.2}**

Uzoefu Mwingi Zaidi Umeahidiwa. -Kutekeleza kanuni za upendo ambazo Kristo alizifundisha kwa

kanuni na mfano kutafanya uzoefu wa kila mtu anayemfuata kuwa kama uzoefu wa Kristo. - *The Review and Herald,* Januari 15, 1895. **{WM 311.3}**

Unapofungua mlango wako kwa ajili ya wahitaji wa Kristo na wanaoteseka, unawakaribisha malaika wasioonekana. Unakaribisha ushirika wa viumbe wa mbinguni. Hawa wanaleta angahewa takatifu ya furaha na amani. Wanakuja na sifa midomoni mwao, na wimbo unaojibu unasikika mbinguni. Kila tendo la rehema husababisha muziki huko. — *The Desire of Ages,* 639. **{WM 311.4}**

Utasisimka kwa Kuridhika. - Kuna kazi ya dhati kwa kila jozi ya mikono kufanya. Hebu kila pigo liseme kwa ajili ya kuuinua ubinadamu. Wapo

wengi sana ambao wanahitaji kusaidiwa. Moyo wa yeye anayeishi, sio kwa ajili ya kujipendeza mwenyewe, bali kwa ajili ya kuwa baraka kwa wale ambao wana baraka chache, utasisimka kwa kuridhika. Hebu kila mvivu na aamke na kukabiliana na hali halisi ya maisha. Chukua Neno la Mungu na kuchunguza kurasa zake. Ikiwa wewe ni mtendaji wa Neno hili, maisha yatakuwa kweli hai kwako, na utagundua kwamba thawabu ni tele. - *Manuscript* 46, 1898. **{WM 311.4}**

Matatizo Yanayofadhaisha Yatatatuliwa. - Kama utamtafuta Bwana na kuongoka kila siku, kama wewe kwa uchaguzi wako mwenyewe wa kiroho utakuwa huru na mwenye furaha katika Mungu, kama kwa ridhaa yenye furaha ya moyo kwa wito Wake wa

neema, utakuja ukiwa umeibeba nira ya Kristo - nira ya utii na huduma - manung'uniko yenu yote yatatulizwa, shida zenu zote zitaondolewa, matatizo yote yanayofadhaisha ambayo kwa sasa yanawakabili yatatatuliwa. –Thoughts from the Mount of Blessing.101. **{WM 312.1}**

Mara Nyingi Hulipwa kwa Sarafu ya Ufalme. - Ile kanuni bora hufundisha, kwa kudokeza, ukweli ule ule ambao unafundishwa mahali pengine katika mahubiri ya mlimani, kwamba "kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa." Kile tunachokitenda kwa wengine, kiwe ni chema au kibaya, hakika kitakuwa na mjibizo kwetu wenyewe, kwa kubariki au kwa kulaani. Chochote tunachokitoa tutakipokea tena. Baraka za kidunia

ambazo tunatoa kwa wengine zinaweza kulipwa, na mara nyingi, hulipwa kulingana na jinsi tulivyotenda. Kile tunachokitoa, mara nyingi kinarudi kwetu, wakati wa shida, kwa kipimo cha mara nne kwa sarafu ya ufalme. Lakini, zaidi ya hayo, zawadi zote hulipwa, hata katika maisha haya, kwa ukamilifu wa upendo Wake, ambao ni jumla ya utukufu wote wa mbinguni na hazina yake. —*Thoughts from the Mount of Blessings,* 136. **{WM 312.2}**

Mungu Atalipa. - Mbinguni kitabu kimeandikwa kwa ajili ya wale ambao wanajishughulisha na mahitaji ya wanadamu wenzao, kitabu ambacho kumbukumbu zake zitafunuliwa siku ambayo kila mtu atahukumiwa

kulingana na matendo yaliyoandikwa ndani yake. Mungu atalipa kila tendo la dhuluma lililofanywa kwa maskini. Wale ambao wanaonesha kutokujali au dharau kwa wenye bahati mbaya hawapaswi kutarajia kupokea baraka ya Yeye aliyetamka, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi." - *Letter* 140, 1908. **{WM 312.3}**

Matendo Yote Mema Yamerekodiwa. - Mungu hajawa msahaulifu wa matendo mema, matendo ya kujinyima, ya kanisa katika siku za hapo zamani. Yote yameandikishwa juu. - *Testimonies for the Church* 5:611. **{WM 313.1}**

Kila utendaji kwa uaminifu, bila ubinafsi wa wajibu unawekwa maanani na malaika na kung'aa katika rekodi ya maisha. - *Testimonies for the Church* 2:132. **{WM 313.2}**

Malaika wanaagizwa wapate kuwa wasaidizi wetu. Wanapita kati ya dunia na mbingu, wakibeba kwenda juu rekodi ya matendo ya watoto wa wanadamu. — *The Southern Watchman,* Aprili 2, 1903. **{WM 313.2}**

Katika Rekodi ya Mbinguni Isiyoharibika. - Kila tendo la upendo, kila neno la wema, kila ombi kwa niaba ya wanaoteseka na wanaoonewa, inaripotiwa mbele ya kiti cha enzi cha milele na kuwekwa kwenye rekodi isiyoharibika ya mbinguni. —

Testimonies for the Church 5:133. **{WM 313.4}**

Ilikuwa ni vyema ... kuikumbuka rekodi iliyohifadhiwa kwenye kitabu cha juu ambacho ndani yake hakuna jambo lililoachwa, hakuna makosa, na ambacho kutokana nacho watahukumiwa. Mle kila nafasi iliyopuuzwa ya kufanya huduma kwa ajili ya Mungu imeandikwa; na pia, kila tendo la imani na upendo linakumbukwa milele. — *Prophets and Kings,* 639. **{WM 313.5}**

Thawabu kwa Ajili ya Kazi ya Ustawi. - Wale watakaopokea thawabu nyingi zaidi watakuwa ni wale ambao wamechanganya pamoja na shughuli na

ari zao, huruma yenye neema, kwa maskini, yatima, walioonewa, na wenye dhiki…. Wapo watu kutuzunguka ambao wana roho ya upole na ya unyenyekevu, Roho wa Kristo, ambao hufanya vitu vingi vidogo vidogo kwa ajili ya kuwasaidia wale walio kando yao, na bila kufikiria chochote juu ya hilo [wanalotenda]; watashangaa mwishowe kuona kwamba Kristo alitambua neno jema lililosemwa kwa waliovunjika moyo, na kuzingatia zawadi ndogo kabisa iliyotolewa kuwa msaada kwa maskini, ambayo ilimgharimu mtoaji kujinyima. - *The Review and Herald,* Julai 3, 1894. **{WM 313.6}**

Mungu Anafahamu/anayaona Matendo ya Huruma. - Kila tendo la haki, rehema, na ukarimu hufanya tuni za nyimbo mbinguni. Baba kutoka

kwenye kiti Chake cha enzi anawaona wale wanaofanya matendo haya ya rehema na kuwahesabu pamoja na hazina Zake za thamani hasa. "Nao watakuwa Wangu, asema Bwana wa majeshi, katika siku ile niifanyayo." Kila tendo la rehema kwa wahitaji, wanaoteseka, linachukuliwa kana kwamba limetendwa kwa Yesu. — *Testimonies for the Church* 2:25. **{WM 314.1}**

Thawabu kwa Vitu Vidogo Vidogo Visivyotiliwa Maanani kwa Kawaida. - Katika Siku ya hukumu wale ambao wamekuwa waaminifu katika maisha yao ya kila siku, ambao wamekuwa wepesi kuiona kazi yao na kuifanya, bila kufikiria sifa au faida, watasikia maneno haya, " Njoni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini

ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu." Kristo hawasifu kwa sababu ya hotuba yenye lugha ya kushawishi ambayo wameitoa, uwezo wa kiakili ambao wameuonesha, au michango ya ukarimu ambayo wameitoa. Yeye anawasifu sababu ya kufanya mambo madogo madogo ambayo kwa kawaida hayatiliwi maanani wanapewa thawabu. — *The Youth's Instructor*, Januari 17, 1901. **{WM 314.2}**

Wakati kesi za wote zinapokaguliwa mbele za Mungu, swali, Walikiri nini? halitaulizwa, bali, Wamefanya nini? Je, wamekuwa watendaji wa Neno? Je! Wameishi kwa ajili yao wenyewe, au wamejizoeza katika matendo ya ukarimu, katika matendo ya huruma na upendo, wakiwapendelea wengine kabla

ya wao wenyewe, kujinyima ili waweze kuwabariki wengine? Ikiwa rekodi itaonesha kuwa haya ndio yamekuwa maisha yao, kwamba tabia zao zimedhihirishwa na upole, kujinyima, na ukarimu, watapokea ahadi yenye baraka na baraka kutoka kwa Kristo, "Vema." “Njoni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu.” - *Testimonies for the Church* 3:525. **{WM 314.3}**

Sababu Sahihi ni Muhimu. - Nia ndio inayathibitisha matendo yetu, kwa kuyatia muhuri wa fedheha au wa thamani ya juu ya kimaadili. Si vitu vikubwa ambavyo kila jicho linaona na kila ulimi unasifu ambavyo Mungu anavihesabu kuwa na thamani zaidi. Wajibu mdogo unaofanywa kwa uchangamfu, zawadi ndogo ndogo

ambazo hazifanyi tamasha, na ambazo kwa macho ya kibinadamu zinaweza kuonekana kuwa hazina thamani, mara nyingi husimama juu zaidi machoni Pake. Moyo wenye imani na upendo una thamani kubwa kwa Mungu kuliko zawadi ya gharama kubwa zaidi. — *The Desire of Ages,* 615.**{WM 315.1}**

Tutahukumiwa Kulingana na Nia Yetu. –Tafakari ya kila siku juu ya matendo yetu, ili kuona kama dhamiri inathibitisha au inahukumu, ni muhimu kwa wote wanaotaka kufikia ukamilifu wa tabia ya Kikristo. Matendo mengi ambayo hupita kama matendo mema, hata matendo ya ukarimu, yatakapochunguzwa kwa makini, yataonekana kuwa yamechochewa na nia mbaya.**{WM 315.2}**

Wengi hupigiwa makofi kwa ajili ya wema ambao hawana. Mchunguzaji wa mioyo hupima nia, na mara nyingi matendo ambayo yamepongezwa sana na wanadamu yanarekodiwa na Yeye kama yaliyochipuka kutokana na ubinafsi na unafiki wa mbaya. Kila tendo la maisha yetu, liwe bora na la kusifiwa au linalostahili lawama, linahukumiwa na Mchunguzaji wa mioyo kulingana na nia ambayo ililisababisha. — *Gospel Workers,* 275.**{WM 315.3}**

Makasia Mawili - Imani na Matendo. - Ikiwa sisi ni waaminifu katika kufanya sehemu yetu, kwa kushirikiana Naye, Mungu atatenda kupitia kwetu [kufanya] uradhi wa mapenzi Yake. Lakini hawezi kutenda kupitia kwetu ikiwa hatufanyi bidii yoyote. Ikiwa tutaupata uzima wa

milele, ni lazima tufanye kazi, na tufanye kazi kwa bidii.... Hebu tusidanganyike na madai yanayorudiwa mara nyingi, "Unachotakiwa kufanya ni kuamini." Imani na kazi ni makasia mawili ambayo ni lazima tuyatumie kwa usawa ikiwa [tungetaka] kusonga mbele katika njia yetu dhidi ya mkondo wa kutokuamini. “Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa.” Mkristo ni mtu wa kuwaza na kutenda. Imani yake hukaza mizizi yake kwa uthabiti ndani ya Kristo. Kwa imani na matendo mema anaweka hali yake ya kiroho imara na kuwa yenye afya, na nguvu zake za kiroho zinaongezeka kadiri anavyojitahidi kufanya kazi za Mungu. - *The Review and Herald,* Juni 11, 1901. **{WM 315.4}**

Taji Zetu Zinaweza Kung’aa au Kufifia. - Ingawa hatuna ustahili

wowote ndani yetu, katika wema mkuu na upendo wa Mungu tunapewa thawabu kana kwamba stahili hiyo ni yetu wenyewe. Wakati tumefanya mema yote tunayoweza kufanya, bado sisi ni watumwa wasio na faida. Tumefanya tu kile ambacho kilikuwa ni wajibu wetu. Kile tulichokamilisha kimefanyika tu kupitia katika neema ya Kristo, na hakuna thawabu yoyote tunayoistahili kutoka kwa Mungu katika msingi wa ustahili wetu. Lakini kwa ustahili Wake Mwokozi wetu, kila ahadi aliyoahidi Mungu itatimizwa, na kila mtu atalipwa kwa kadiri ya matendo yake. **{WM 316.1}**

Thawabu za thamani za siku zijazo zitawianishwa na kazi ya imani na kazi ya upendo katika maisha ya sasa. "Apandaye haba atavuna haba;

apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu." Tunapaswa kushukuru zaidi kwamba sasa katika wakati wa majaribio [rehema] kupitia katika rehema isiyo na kipimo ya Mungu tunaruhusiwa kupanda mbegu kwa ajili ya mavuno yetu ya baadaye. Tunapaswa kufikiria kwa uangalifu mavuno yatakuwaje. Kama taji ya furaha yetu ya milele itang'aa au kufifia itategemeana na mwelekeo wetu wa utendaji. Tunaweza kufanya wito wetu na uteuzi wetu kuwa wa hakika, na tunaweza kumiliki urithi mwingi, au tunaweza kujipunja uzito uzidio mno na ulio wa milele wa utukufu. - *The Review and Herald,* Juni 27, 1893.**{WM 316.2}**

Kukutana na Wale Waliookoka kwa Sababu ya Juhudi Zetu. - Wakati waliokombolewa watakaposimama mbele za Mungu, roho za thamani zitaitikia majina yao wale walioko pale kwa sababu ya juhudi za uaminifu, zenye subira zilizotolewa kwa ajili yao, kusihi na ushawishi wa dhati wa kukimbilia Ngome. Hivyo ndivyo wale ambao katika ulimwengu huu wamekuwa watenda kazi pamoja na Mungu watapata thawabu yao. — *Testimonies for the Church* 8:196, 197. **{WM 317.1}**

Waliokombolewa watakutana na kuwatambua wale ambao usikivu wao waliuelekeza kwa Mwokozi aliyeinuliwa. Ni mazungumzo ya baraka kiasi gani

watakayokuwa nayo na roho hizi! "Nilikuwa mwenye dhambi," itasemwa, "bila Mungu na bila tumaini ulimwenguni; na ulikuja kwangu, na kuelekeza mawazo yangu kwa Mwokozi wa thamani kama tumaini langu pekee." ... **{WM 317.2}**

Wengine watatoa shukrani zao kwa wale ambao waliwalisha wenye njaa na kuwavika walio uchi. "Wakati kukata tamaa kuliifunga roho yangu kwa kutokuamini, Bwana alikutuma kwangu," wanasema, "kusema maneno ya matumaini na faraja. Ulinileta chakula kwa mahitaji yangu ya kimwili, na ukanifungulia Neno la Mungu, ukaniamsha kkutambua mahitaji yangu ya kiroho. Ulinitendea kama ndugu. Ulinihurumia katika huzuni zangu na kuirejesha roho yangu iliyochubuliwa na

kujeruhiwa kiasi kwamba niliweza kuushika mkono wa Kristo ulionyooshwa kuniokoa. Katika kutokufahamu kwangu ulinifundisha kwa uvumilivu kwamba nilikuwa na Baba mbinguni aliyenijali." - *Testimonies for the Church* 6:311. **{WM 317.3}**

"Njoni, Mliobarikiwa na Baba Yangu." - Wakati mataifa yatakapokusanyika mbele Yake kutakuwa na matabaka mawili tu, na majaliwa yao ya milele yataamuliwa na kile walichokifanya au walichopuuza kufanya kwa ajili Yake katika nafsi ya maskini na wanaoteseka. Katika siku ile Kristo hatawasilishi mbele ya wanadamu kazi kubwa ambayo amewafanyia katika kuyatoa maisha Yake kwa ajili ya ukombozi wao.

Atawasilisha kazi ya uaminifu ambayo wametenda kwa ajili Yake. **{WM 318.1}**

Kwa wale ambao atawaweka katika mkono Wake wa kuume atasema, "Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia.” Lakini wale ambao Kristo anawasifu hawajui kwamba wamekuwa wakimtumikia. Kwa maswali yao ya kukanganyikiwa anajibu, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi."... **{WM 318.2}**

Wale ambao Kristo anawasifu katika hukumu inawezekana kuwa walijua teolojia kidogo tu, lakini walihifadhi kanuni Zake. Kupitia katika mvuto wa Roho Mtakatifu wamekuwa baraka kwa wale waliowazunguka. Hata miongoni mwa wapagani wapo wale ambao wamehifadhi roho ya wema; kabla maneno ya uzima hayajaanguka masikioni mwao, wamefanya urafiki na wamisionari, hata kuwahudumia kwa kuhatarisha maisha yao wenyewe. Miongoni mwa wapagani wapo wale wanaomwabudu Mungu bila kujua, wale ambao kwao nuru haijawahi kuletwa na wakala wa kibinadamu, lakini bado hawataangamia. Ingawa hawaijui sheria ya Mungu iliyoandikwa, wameisikia sauti Yake ikisema nao katika asili, na wamefanya mambo ambayo sheria

ilihitaji. Matendo yao ni ushahidi kwamba Roho Mtakatifu ameigusa mioyo yao, nao wanatambuliwa kama watoto wa Mungu. **{WM 318.3}**

Ni jinsi gani watashangazwa na kufurahishwa watu wa hali ya chini miongoni mwa mataifa, na miongoni mwa wapagani, kusikia kutoka katika midomo ya Mwokozi, " Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi." Ni furaha iliyoje kuwa moyo waYeye aliye Upendo Usio na Kipimo wakati wafuasi Wake wanatazama juu kwa mshangao na furaha kwa kusikia maneno yake ya kukubali.-*Tumaini la Vizazi Vyote*, 637, 638. **{WM 319.1}**

Kiambatisho

Uzoefu Binafsi wa Ellen G. White Kama Mfanyakazi wa Ustawi

[Wakati ambapo katika maisha yake yote Mama White alikuwa akikumbuka mahitaji ya wale waliomzunguka, kulikuwa na nyakati ambapo mahitaji haya yalibana hasa hivyo mambo kuwa magumu. Hakuna jaribio linalofanywa katika kurasa zifuatazo la kutoa maelezo makamilifu, bali badala yake kuwasilisha uzoefu fulani wa mfano ambao alitokea kuuandika katika kumbukumbu ya shajara yake au katika

barua zake. Dondoo hizi zinawasilisha uwanja mpana wa huduma yake ya ustawi, kwa msisitizo mkubwa zaidi juu ya vipindi viwili katika uzoefu wake wa maisha, kimoja awali na kingine baadaye katika maisha yake. **{WM 321.1}**

Katika "kumbukumbu" kutoka katika shajara ya 1859 tunamwona Mama White kama mama wa miaka thelathini na moja akiwa na watoto wavulana watatu wachangamfu na wenye nishati tele, akibeba mizigo ya kaya, akiandika, akisafiri, na kuhubiri, na wakati huo huo akiwasaidia wale walio karibu naye ambao walikuwa wakiteseka au wana uhitaji. Hadi mwishoni mwa miaka ya tisini (1890 na) tunamwona huko Australia wakati wa mgororo mkali na wa muda mrefu wa kiuchumi, na

mahitaji ya kuvunja moyo kila upande. Pamoja na haya msomaji pia atapata taarifa kadhaa ambazo husaidia kufuatilia mlolongo wa shughuli zake za ustawi katika maisha yake yote. **{WM 321.2}**

Msomaji ataona kwamba maingizo ya shajara ya E. G. White ni yameandikwa kumbukumbu katika mtindo wa shajara ya maneno machache - ya mkato, wakati mwingine katika virai vifupi vifupi na mara nyingi katika wakati uliopo (present tense). Hakika pia itatambuliwa kuwa maelezo ya kuhusu wasifu halisi kama Ellen White alivyorekodi shughuli zake za siku kwa siku hayatoi maagizo kwa kanisa na kwa hivyo hayapaswi kuchukuliwa kama ushuhuda wenye mamlaka. Hii ni kweli pia kuhusu marejeleo ya wasifu

yanayotolewa kutoka katika barua za E. G. White. Hata hivyo, mfano wa Ellen White unaongeza msisitizo kwa kanuni zake. **{WM 321.3}**

Mzigo wa moyo uliobebwa na Mama White, kuthamini kwake wajibu wake kwa wale walio katika mateso na uhitaji waliomzunguka, na shauku yake ya kusaidia, ingawa inaonekana kuwa daima ilikwamishwa na rasilimali ndogo, inapaswa kumtia moyo kila Mwadventista wa Sabato kushiriki zaidi katika Huduma ya Ustawi/welfare ministry.] **{WM 321.4}**

E. G. White Aliagizwa Kuweka Mfano. -Baada ya ndoa yangu niliagizwa kwamba ni lazima nioneshe shauku ya pekee kwa watoto wasio na mama na wasio na baba, nikichukua

baadhi yao chini ya utunzaji wangu kwa muda, na kisha kutafuta maskani kwa ajili yao. Hivyo ningekuwa nawapa wengine mfano wa kile wanachoweza kukifanya. **{WM 321.5}**

Ingawa niliitwa kusafiri mara kwa mara, na kuwa na mambo mengi ya kuandika, nimechukua watoto wa umri wa miaka mitatu na miaka mitano, na nimewatunza, nimewaelimisha, na kuwafundisha kwa ajili ya nafasi zenye wajibu. Nimechukua nyumbani kwangu mara kwa mara wavulana kutoka miaka kumi hadi kumi na sita, nikiwalea kama mama na kuwapa mafunzo kwa ajili ya utumishi. [Kutoka katika kalamu ya wafanyakazi wawili ambao katika ujana wao walikaa miezi mingi nyumbani kwa White tuna maoni yafuatayo ya kile

walichokishuhudia wao wenyewe. - Wakusanyaji. **{WM 321.6}**

"Si tu kwamba Mama White alikuwa mshauri mwenye nguvu kwa mumewe, kumlinda dhidi ya kufanya makosa ambayo yangehatarisha kusudi kwa sehemu yoyote, lakini alikuwa mwangalifu zaidi katika kuyatekeleza kwa wakati wake mambo yale aliyowafundisha wengine. Kwa mfano, mara nyingi alielezea sana katika mazungumzo yake ya umma juu ya wajibu wa kuwatunza wajane na yatima, akiitaja Isaya 58:7-10 kwa wasikilizaji wake kwa; Na alionesha mfano wa mashauri yake kwa kuchukua wahitaji nyumbani kwake kwa ajili ya kuwapa makazi, chakula, na mavazi. Ninakumbuka vizuri wakati fulani yeye kuwa nao, kama watu wa familia yake,

mvulana na msichana na mjane na binti zake wawili. Zaidi ya hayo, nimemtambua akigawa kwa watu maskini nguo mpya alizonunua kwa kusudi hilo zenye thamani ya mamia ya dola.” - J. O. Corliss, *The Review and Herald,* Agosti 30, 1923. **{WM 322.1}**

“Mzee White mwenyewe alikuwa ni mtu mwenye huruma sana. Daima aliishi katika nyumba kubwa, lakini hakukuwa na vyumba vilivyo wazi ndani yake. Ingawa familia yake ya karibu ilikuwa ndogo, nyumba yake daima ilijawa na wajane na watoto wao, marafiki maskini, ndugu maskini walioko katika utumishi, na wale ambao walihitaji maskani. Moyo wake na pochi yake vilikuwa wazi kila wakati, na alikuwa tayari kuwasaidia wale waliohitaji msaada. Kwa hakika aliweka

mfano bora zaidi kwa dhehebu letu katika wema wake na ukarimu wa roho.” — *The Medical Missionary,* Februari, 1894.]

Nimejisikia kuwa ni wajibu wangu kuleta mbele ya watu wetu kazi hiyo ambayo wale walio katika kila kanisa wanapaswa kuhisi wajibu. **{WM 327.1}**

Wakati nikiwa Australia niliendelea na mwelekeo huu huu wa kazi, kuwachukua watoto yatima nyumbani kwangu, wale ambao walikuwa katika hatari ya kukumbwa na majaribu ambayo yangeweza kusababisha kupotea kwa roho zao. - *The Review and Herald,* Julai 26, 1906. **{WM 327.2}**

Ellen G. White katika Kazi ya Vitendo ya Dorkasi

(Kumbukumbu kutoka katika shajara ya E. G. White ya 1859)

Januari 2, Jumapili. – Dada Augusta Bognes alitumwa kunisaidia kujiandaa kwa ajili ya safari nyingine. Alitengeneza kanzu kwa ajili ya Edson. Ataandamana nasi. Tulijaribu kumfariji Augusta. Amesononoshwa na kuvunjika moyo, afya duni na hakuna mtu wa kumtegemea. Ameweka kando silaha zake na ngao ya imani. Bwana na aiimarishe mikono dhaifu na kuyatia nguvu magoti dhaifu. Nilimpa Dada Irving nguo ya joto na vazi na mambo mengine machache kwa ajili yake. **{WM 322.2}**

Januari 3, Jumatatu. – Nilienda ofisini. Niliitwa katika familia ya Ndugu Loughborough na ya dada yangu.

Niliandika kurasa saba kwa Daktari Naramores, kisha nikala chakula cha jioni kwa dada yangu. Nilikuwa na mahojiano mazuri na baba na mama yangu. Nilienda ofisini tena baada ya chakula cha jioni, na kuandika kurasa nne kwa familia ya Ndugu Orton. Pia niliandika kurasa nne kwa familia ya Ndugu Howland na kumwandikia Dada Ashley, na familia ya Ndugu Collin. Nilimlipa mjane Cranson $ 1.00 kwa ajili ya kutengeneza mashati kadhaa. Nilimlipa Dada Bognes $ 1.00 kwa ajili ya kushona kanzu. Hakuwa tayari kuichukua, lakini nilijisikia kuwa ni wajibu kumkabidhi. Yeye ni maskini na dhaifu. Bwana na amhurumie na kumtunza. Yesu alisema, "Maana siku zote mnao maskini pamoja nanyi." Bwana na atuondolee ubinafsi na

atusaidie kujali shida za wenzetu na kuwafariji.**{WM 322.3}**

Januari 6, Alhamisi. - Kumtengenezea Edson kofia na fulana. Usiku nimechoka sana. Mpe Agnes gauni ambalo si chakavu sana kwa ajili ya mama yake. Wao ni maskini. Mume na baba ni wagonjwa. Mazao yao yaliharibika. wanapaswa kununua mkate na hawana cha kununulia. Agnes ndiye msaada wao mkuu. Ana miaka kumi na saba tu. Kuna watoto wanne sasa nyumbani. Ni lazima wateseke isipokuwa kanisa limepata shauku kwa niaba yao. Bwana na awarehemu wahitaji, na kuiweka katika mioyo ya watoto wake ili wapate kuwatolea msaada kwa mkono wa ukarimu. **{WM 323.1}**

Februari 3, Alhamisi. - Mgonjwa sana siku nzima kwa ugonjwa wa maumivu ya kichwa. Henry Pierce kutoka Monterey nyumbani kwetu. Tuma kwa Dada Leander Jones vitu kadhaa kwa ajili ya watoto wake na Jenny anamtumia kofia yake bora. Bwana na atuwezeshe kuona mahitaji ya maskini na atupe moyo ulio tayari na wenye utayari wa kuwakimu. **{WM 323.2}**

Februari 28, Jumatatu. - Mary Loughborough alikuja hapa. Alikaa nasi kwa chakula cha jioni. Mtoto wake ni alikuwa mgonjwa mchana huu. Nilienda kwa Dada Ratel. Tulikuwa na mahojiano mazuri. Mtoto wake amevaa nguo nyeupe chakavu. Hiyo ndiyo bora aliyonayo isipokuwa ile moja ambayo anaivaa siku zote wanapotoka kwenda

nje pamoja naye. Anazungumza kuhusu watoto wake waliokufa miaka miwili iliyopita. Hataki wawe hai tena. Familia yote ni maskini. Binti mkubwa kabisa anaithamini sana zawadi ya Biblia niliyompa. Anawasomea wazazi wake kutoka humo. Afya ya Dada Ratel ni duni sana. Ametema damu leo. Nina hofu hatajaza nafasi yake katika familia yake kwa muda mrefu. Anajaribu kutenda haki. Mumewe ni maskini, ni mtu mwovu, mtu mwenye hamaki na [Ratel] ana majaribio makubwa. Bwana na amhimili. Anatuomba tumwombee ili aweze kutenda haki wakati wote. **{WM 323.3}**

Machi 1, Jumanne. - Nilikwenda ofisini. Niliitwa kuonana na Dada Sarah

na mama yake. Sarah alinipa nguo chache na aproni mbili kwa ajili ya mtoto mchanga wa Dada Ratel. Kisha nikamwagiza Dada Aurora Lockwood aje. Nilikuwa na mahojiano mazuri naye. Yeye ni dada mzuri, anayependwa na Mungu na anayeheshimiwa na kanisa lote. **{WM 324.1}**

Nilienda mjini na kununua vitu kadhaa. Nilinunua nguo chache kwa ajili ya mtoto mchanga wa Dada Ratel. Nilienda ofisini, nikawasaidia kidogo pale, kisha nilikwenda nyumbani kula mlo mkuu. Nilituma vikorokoro hivyo vichache kwa Dada Ratel. Mary Loughborough anamtumia nguo nyingine, kwa hiyo sasa mambo yake yatakuwa mazuri sana. Laiti wote

wangejua utamu wa kutoa kwa maskini, kusaidia kuwatendea wengine mema, na kuwafurahisha wengine. Bwana anaufungua moyo wangu kufanya yote yaliyo chini ya uwezo wangu kuwasaidia wale wanaonizunguka. “Nipe kuhisi shida ya ndugu yangu.” **{WM 324.2}**

Machi 8, Jumanne. - Ni siku ambayo udhaifu unajitahidi kupata ushindi. Ninapata maumivu sana kwenye bega langu la kushoto na mapafu. Hisia zangu za ubongo zina huzuni. Ndugu John Andrews anaondoka leo. Anakuja kututembelea jioni. Tulikuwa na mahojiano mazuri. Tukaandaa vitu vichache kwa ajili yake kuchukua nyumbani. Kumtumia Angeline nguo mpya ya kaliko (kitambaa cha pamba) kwa shilingi tisa, na jozi madhubuti ya viatu vya ngozi ya

ndama. Baba analipia utengenezaji wa viatu na utengenezaji wa masanduku mawili kwa Ndugu John Andrews. Ninamtumia yule kijana mdogo shati zuri la flana na uzi wa kufumia soksi. Ninamtumia Dada au Mama Andrew kofia kubwa nzuri, iliyofumwa vizuri apate kuvaa. Nimetengeneza mfuko wa kitambaa cha taulo kwa ajili ya kuviweka. Nikaandika kurasa tatu ndogo kwa Dada Mary Chase. Ndani yake maneno yenye [maelezo ya upishi (viambaupishi) yaliyopatikana kutoka nyumbani kwa John|. **{WM 324.3}**

Machi 10, Alhamisi. - Nilikwenda mjini na kurudi. Nilikuwa nimechoka sana. Nilimnunulia John F. suruali moja. Mchana Dada Irving alikuja.... **{WM 324.4}**

Kwa majuma kumi binti ameishi nasi, na tulimlipa shilingi tisa kwa juma. Amekabidhi zote hizi kwa mama yake isipokuwa dola moja. Nguo zake ni hafifu, lakini bado hatengi fedha yoyote kwa ajili matumizi yake mwenyewe. Anajisahau katika kujitoa kwake na kujinyima kwa ajili ya wazazi wake. Ilikuwa ni kama kuonesha onesho ambalo sijawahi kushuhudia. Kusita kwa mama kupokea mishahara, mishahara yote ya binti yake, katika shida na utayari na uhuru wa binti kutaka yote iende kwa wazazi wake maskini wanaoteseka. Mama na binti walilia, na sisi tulilia. Tuliwasaidia kidogo; na wakawa wao ndio wenye kushinda. Tulilipa nusu kwa ajili ya buti kwa ndugu mdogo. Dola moja. Nililipa mia moja hamsini kwa ajili ya viatu vya

mama. Mume wangu alimpa dola moja kwa pesa taslimu. Henry alimpa senti kumi. Edson, senti kumi, na Willie mdogo kumi. Mume alimpa ishirini na tano zaidi kwa ajili ya kumnunulia mgonjwa tunu chache. Tulitoa mavazi kadhaa ya zamani ila yasiyo chakavu kwa ajili ya kusaidia. **{WM 324.5}**

Aprili 21, Alhamisi. – Nilifanya kazi ya kutengeneza zulia. Nikaandika barua kwa Daniel Bourdeau. Asubuhi hii kuna hisia ya huruma miongoni mwa baadhi ya kundi kwa ajili ya familia ya Ndugu Benedict. Tumechangia kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya kuwasaidia, karibu dola saba. Tukawanunulia vitu mbalimbali vya kula, na kuwapelekea. Kaka na Dada Benedict walitutembelea siku nzima. Tulikuwa na mahojiano ya kuvutia sana

na ya kupendeza. Mama yangu alikuja kuniona, jambo ambalo lilikuwa faraja kubwa kwangu. **{WM 325.1}**

Huduma ya Ustawi Katika Miaka Yote

E. G. White Aomba Msaada. - Ndugu na Dada wapendwa: Hazina katika Mfuko wa Maskini, iliyo na nguo, na kadhalika, kwa wale walio wahitaji, imekaribia kuisha. Na kwa kuwa kuna matukio ya ufukara ambayo daima hujitokeza, na moja jipya limejitokeza hivi karibuni, Niliwaza kuwa itakuwa vyema kwa wale ambao wana mavazi, matandiko, au fedha za kuweza kutoa kuzituma hapa mara moja. Tunatarajia hakutakuwa na ucheleweshaji, kwa kuwa tutawasaidia wengine ambao ni wahitaji mara tu tutakapokuwa

tumeweka mambo sawa. Tumenia michango yenu kwa Sr. Uriah Smith au mimi mwenyewe. *The Review and Herald,* Oktoba 30, 1860. **{WM 325.2}**

James na Ellen White Huchanganya Maombi na Kazi. - Kabla ya Sanitariamu-hospitali yoyote kuwepo miongoni mwetu, mume wangu pamoja nami tulianza kufanya kazi katika mwelekeo wa wamishonari wa tiba. Tungewaleta nyumbani kwetu wagonjwa ambao walikuwa wameachwa wafe na waganga. Tulipokuwa hatujui kabisa kitu gani cha kuwafanyia tungemwomba Mungu kwa bidii zaidi, na kila wakati alituma baraka Zake. Yeye Ndiye Mponyaji hodari, na alifanya kazi pamoja nasi. Hatukuwahi kuwa na

muda au fursa ya kuchukua kozi ya matibabu, lakini tulifanikiwa pale tuliposogea kwa kicho cha Mungu na kumtafuta kwa ajili ya hekima katika kila hatua. Hii ilitupa ujasiri katika Bwana. **{WM 325.3}**

Hivyo tuliunganisha maombi na kazi. Tulitumia matibabu sahili ya maji, na kisha tukajaribu kuyakaza macho ya wagonjwa Kwake Mponyaji Mkuu. Tuwaambia kile ambacho angeweza kuwatendea. Ikiwa tungeweza kuwatia moyo wagonjwa kwa matumaini, hii ni kwa faida kubwa kwao. Tunataka wote ambao wana sehemu yoyote ya kutenda katika Sanitariamu-taasisi za tiba rahisi zetu, wawe na ufahamu thabiti juu ya uweza Wake Yeye asiye na mwisho. Tunamwamini na kuamini uweza wa Neno Lake. Tunapofanya kila

liwezekanalo kwa ajili ya kupona kwa wagonjwa, basi tunaweza kumtafuta awe pamoja nasi, ili tuweze kuuona wokovu Wake. Tunaweka imani ndogo sana katika uweza wa mkono ule unaoutawala ulimwengu. - *Manuscript* 49, 1908. **{WM 326.1}**

Katika Huduma ya Nyumba kwa Nyumba. - Kabla ya Sanitariamu - yaani vituo vyetu vya tiba rahisi havijaanzishwa mimi na mume wangu tulikwenda nyumba kwa nyumba kutoa matibabu. Chini ya baraka za Mungu tuliyaokoa maisha ya wengi waliokuwa wakiteseka. - *Letter 45, 1903*. **{WM 326.2}**

Shauku kwa Mjane Maskini. - Kuhusu Nellie L., mnajua kuwa yeye ni mjane anyewahudumia watoto watatu,

naye anajitahidi ili aweze kupata ujuzi kusudi aweze kukaa na watoto wake wa umri huo katika kazi ya chekechea, ambapo angeweza kuwatunza watoto wake wakiwa pamoja naye. Hebu tusiione roho hii maskini ikishugulika kupambana kwa ajili ya maisha yake na kuitoa kafara afya yake kwa kufanya hivi. Nimefikiria michango ya ukarimu ambayo imetolewa kwa watu ambao wameoa huko Oakland. Laiti marafiki hawa wangetumia fedha zao na kuonesha huruma zao kumbariki mjane na yatima ambao wanastahili uangalifu wao na huruma kubwa. Je, hali kama hizi hazina madai juu yetu? **{WM 326.3}**

Nitamsaidia Nellie dola mia moja ikiwa mtafanya vivyo hivyo. Dola mia mbili itakuwa baraka kubwa kwake

sasa hivi. Je, mwaweza kufanya hivi kwa ajili ya Kristo? Je! Utawatia wengine moyo wapate kumsaidia kupata mwanzo katika maisha? Ingekuwa bora zaidi kufanya hivyo kuliko kungojea na kuruhusu Nellie achoshwe na wasiwasi na masumbufu na kuanguka katika mapambano, akiwaacha watoto wake wakiwa hawajiwezi, wasio na mama, ili watunzwe na wengine.**{WM 326.4}**

Dola mia moja kutoka kwenu haitakuwa kiasi kikubwa, lakini itakuwa baraka kubwa kwake. Je, utafanya hivi? Hebu na tulifanye hili kama zawadi ya bure na tusiruhusu hofu ya deni iwe juu yake yeye ambaye anapambana chini ya vikwazo kama hivyo. Kama utafanya hivyo, tafadhali nenda ukachukue pesa kwa jina langu kutoka Signs Office dola mia moja kwa ajili ya Nellie L. Hebu

wote wawili tulitathmini jambo hili na Bwana atatubariki. Ninajua kuwa atapambana kwa nguvu zake zote kuweza kujitegemeza/kujikimu kimaisha. Battle Creek, Mich., Machi 28, 1889 Ndugu C. H. Jones: **{WM 327.1}**

Tafadhali lipa kwa hundi ———– $ 100.00 (Dola mia moja) kama zawadi kutoka kwa Bwana ambaye amenifanya kuwa wakili Wake wa fedha. “Ellen G. White” (*Letter* 28, 1889). **{WM 327.2}**

Kuwa Watangulizi Nchini Australia

Chuki Inaondolewa na Huduma ya Ustawi. - Tulipitia uzoefu mwingi wa kuvutia tulipokuwa Australia. Tulisaidia kuanzisha shule kutoka kwenye msingi, kwenda kwenye misitu

ya mikalitusi na kupiga kambi wakati miti hii ilipokuwa inaangushwa, viwanja vikisafishwa, na majengo ya shule kusimamishwa. Chuki katika jamii ambayo shule ilianzishwa, ilivunjwa na kazi ya umisionari wa tiba ambayo tuliifanya. Daktari aliyekuwa karibu aliishi umbali wa maili ishirini. Niliwaambia ndugu kwamba ningemruhusu katibu wangu, muuguzi aliyefunzwa ambaye amekuwa pamoja nami kwa miaka ishirini, kwenda kuwatembelea wagonjwa kila walipomwita. Tulifanya nyumba yetu kuwa hospitali. Muuguzi wangu alitibu kwa mafanikio, na baadhi ya magonjwa magumu ambayo matabibu walikuwa wametamka kuwa hayatibiki. Kazi hii haikuwa bila thawabu yake. Mashaka na chuki viliondolewa. Mioyo ya watu

ilivutiwa, na wengi waliukubali Ukweli. Wakati tulipokwenda pale ilionekana kwamba ilikuwa ni lazima kufungia kila kitu kwa ufunguo, kwa hofu ya wizi. Ni mara moja tu kitu kiliibwa kutoka kwetu, na hiyo ilikuwa muda mfupi baada ya kuwasili kwetu. Sasa jamii inaishi kwa kufuata sheria, na hakuna mtu anayefikiria kuwa ataibiwa. - **{WM 327.4}** *Manuscript* 126, 1902.

Shauku Binafsi kwa Watu. - Tulijaribu kuwa na shauku binafsi kwa watu yaani kuwajali. Ikiwa tulikutana na mtu anayetembea tulipokuwa tukiendesha gari kwenda kwenye kituo kilichokuwa umbali wa maili nne na nusu, tulifurahi kuwaruhusu wapande pamoja nasi katika gari letu. Tulifanya kile tulichoweza kuendeleza ardhi yetu, na tuliwahimiza majirani zetu kuulima

udongo, ili nao wapate matunda na mboga mboga zao wenyewe. Tuliwafundisha jinsi ya kuuandaa udongo, nini cha kupanda, na jinsi ya kutunza mazao yanayokua. Punde walijifunza faida za kujipatia mahitaji yao kwa njia hii. Tulitambua kuwa Kristo alikuwa na shauku binafsi kwa wanaume na wanawake wakati alipokuwa anaishi hapa duniani. Alikuwa mmisionari wa tiba kila mahali alipokwenda. Tunapaswa kwenda kote tukitenda mema, kama vile alivyofanya. Tumeagizwa kuwalisha wenye njaa na kuwavisha walio uchi, kuwaponya wagonjwa na kuwafariji wale wanaoomboleza. - *Manuscript* 126, 1902. **{WM 328.1}**

Kubana Matumizi kwa Ajili ya Kuwasaidia Wengine. - Tunaishi kwa

kubana matumizi kwa kila njia na kufanya utafiti wa jinsi kila senti inapaswa kutumiwa.... Tunakarabati mavazi yetu tena na tena, tukiweka viraka na kupanua mavazi ili yaweze kuvaliwa kwa muda mrefu kidogo, ili tuweze kuwapa nguo wale ambao ni wahitaji zaidi. Mmoja wa ndugu zetu huko Ormondville, ambaye ni seremala mwenye akili, hakuweza kwenda kwenye ubatizo kwa sababu hakuwa na mavazi ya kubadilisha. Alipopata suti ya bei rahisi alikuwa ni mtu mwenye shukurani mno niliyewahi kumwona, kwa sababu hapo ndipo aliweza kusonga mbele katika kulitimiza agizo la ubatizo. - *Letter* 89A, 1894. **{WM 328.2}**

Nguo Mpya ya Kudumu Sana Zimenunuliwa kwa Ajili ya Kazi ya Msaada. - Baadhi ya watu wetu

wananiambia, "Toa nguo zako za zamani, na hiyo itawasaidia maskini." Je, nitoe mavazi yale ambayo nimeyatia viraka na kupanua, watu singewea kuona kuona kitu chochote ambacho wangeweza kukitumia. Ninawanunulia nguo mpya, ngumu, zenye kudumu muda mrefu. Nimetembelea viwanda ambapo wanatengeneza nguo za sufu na kununua kiasi fulani cha mabaki ambayo huenda yana kasoro kidogo lakini zinaweza kununuliwa kwa unafuu, na zingeweza kuwa na manufaa kwa wale ambao tunawapa. Ninaweza kumudu kuvaa mavazi ya zamani hadi yatakaposhindikana kukarabatiwa. Nimemnunulia mjomba wako nguo nzuri suruali na kizibao, na sasa anapewa nguo nzuri za heshima. Kwa njia hii ninaweza kutoa mavazi ya

kudumu kwa familia ya watoto wengi, ambazo wazazi wao wasingefikiria kuyapata kwa ajili yao. – *Kitabu hicho hicho*. (Ibid) **{WM 328.3}**

Ununuzi wa Kuni Kutoka kwa Wakulima Maskini. – Umaskini umeenea sana katika jamii kiasi kwamba njaa imewakazia macho wengi usoni, na sehemu ya kushangaza mno ya jambo hilo ni kwamba wakulima wanaonekana kutokujiweza kabisa kubuni mipango ambayo kwayo wangeweza kugeuza muda wao na pesa kuwa na manufaa.... Tunanunua kuni kutoka kwa ndugu zetu ambao ni wakulima, na tunajaribu kuwapa watoto wao wa kiume na wa kike ajira. Lakini tunahitaji mfuko mkubwa wa hisani ambamo ndani yake tungeweza kutoa fedha za kuziepusha familia na njaa. Wale ambao wanahitaji

msaada wetu si wa daraja la wazururaji au ombaomba, bali ni watu ambao katika nyakati za neema wamepata pesa nyingi kama kufikia dola ishirini na arobaini kwa juma.... Niligawana akiba ya chakula cha nyumbani kwangu na familia za aina hii, wakati mwingine nikienda maili kumi na moja kwa ajili ya kutuliza mahitaji yao. - *Letter* 89a, 1894. **{WM 329.1}**

Kujihusisha kwa Ajili ya Mwanafunzi Mhitaji. – Tafadhali muulize Ndugu —– kuhusiana na mavazi ambayo anahitaji, na kile anachokihitaji tafadhali mpatie, na udai malipo hayo kutoka kwangu. Hajapokea sanduku lake, na nina hofu anaweza kuteseka kwa kukosa nguo muhimu za kubadili. - *Letter* 100, 1893. **{WM 329.2}**

Kumsaidia Mchungaji Anayeteseka kwa Ugonjwa. - Ndugu na Dada A. wamekuwa wakifanya kazi kwa matokeo mazuri huko Ormondville, kama maili mia moja kutoka hapa.... Nilikutana naye huko Napier, na aliniambia kuwa mimi ndiye niliyempeleka kwenye shule ya huko Healdsburg, nikimlipia gharama zake ili apate elimu. Nilishukuru sana kuona matokeo ya uwekezaji huu. **{WM 329.3}**

Tulituma Ndugu A.... katika taasisi ya St. Helena.... Anateseka sana. Nimetenga dola mia tatu kwa ajili ya suala hili, ingawa kuna hali nyingi ambapo kila dola inahitajika, lakini ninajisikia kutokuwa na kizuizi kabisa katika kusaidia katika jambo hili. Ni jambo ambalo wale wanaompenda na

kumcha Mungu ni lazima waoneshe huruma yao kwa namna halisi na kuzingatia kwamba Kristo alitambulisha maslahi Yake na wanadamu wanaoteseka. - *Letters* 79 na 33, 1893. **{WM 330.1}**

Mama White Akabiliana na Matatizo ya Mfadhaiko. – Familia ya ndugu M. ni wafanyakazi wenye bidii iwapo tu wangeweza kupata kazi ya kufanya. Hatutapenda kuwaona wakienda wakiwa na njaa au wakiwa bila nguo au wakiwa wamekata tamaa. Wamenunuliwa, wamenunuliwa kwa damu ya Kristo, na wana thamani kwa Mungu. Wakati tukiwa katika nchi hii tutaendelea kuwasaidia maskini na wenye dhiki kwa kadiri inayowezekana. Ndugu M. ana madeni ya mahali anapoishi; nilikidhi gharama ya riba ya

robo ya mwisho, pauni saba, ambayo sikutarajia chochote, lakini sikupenda, na nisingetaka kuona familia ile ikitupwa barabarani kwa kukosa kodi.... Tunaomba kwa bidii sana kwamba Bwana afanye kazi kwa niaba ya familia hii inayopendwa. **{WM 330.2}**

Tunafadhaishwa sana sisi wenyewe kuelewa wajibu wetu kwa hawa wote wanaoteseka. Familia nyingi sana hazijaajiriwa, na hiyo inamaanisha kuwa ni maskini, wenye njaa, wenye dhiki, na kulemewa. Sioni njia nyingine isipokuwa kusaidia roho hizi maskini katika hitaji lao kubwa, na nitafanya hivi ikiwa Bwana atapendezwa. Naye hupendezwa. Neno Lake ni imara, na haliwezi kushindwa, wala kubadilishwa na hila yoyote ya kibinadamu kulikwepa. **{WM 330.3}**

Lazima tuwasaidie wahitaji na wanyonge Shetani asije akawatoa mikononi mwetu, kutoka katika safu zetu, na kuwaweka, wakiwa chini ya majaribu, katika safu zake. - *Letter* 42, 1894. **{WM 330.4}**

Ununuzi kwa Ajili ya Kukidhi Mahitaji ya Maskini. - Ninakwenda mji wa Sydney leo kwenye mnada wa kila mwaka kwa ajili ya kununua baadhi ya bidhaa. Huko wanakuwa na mauzo ya namna hii ili kuondokana na bidhaa za zamani madukani mwao. Maskini wanaotuzunguka kotekote wanateseka kwa ajili ya chakula na mavazi, na ninaweza kununua kwa unafuu kwa kuyatembelea maduka haya. Tunabana matumizi kadiri iwezekanavyo, na kuna haja ya kutosha kwa ajili ya kufanya hivyo.... Kuna maskini wengi ambao

wanasumbuka kwa kukosa chakula na mavazi ambao ni wa nyumba ya imani. Pochi zetu hazitaweza kutosheleza kukidhi mahitaji ya wale tunaowajua. "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo," Yesu alisema, "mlinitendea Mimi." Ni ya thamani iliyoje Maneno haya ya faraja kwa maskini! ” - *Letter* 39, 1895. **{WM 330.5}**

Chama cha Dorkasi Kinaundwa. - Jumapili imekuwa ni siku yenye shughuli nyingi kwetu, kuandaa kwa ajili ya maskini sana, na kuweka mipango kadhaa ambayo itanipunguzia mimi pamoja na familia yangu kufanya kila kitu ambacho kinatakiwa kufanyika. Dada C., mwanamke anayestahili heshima, amewekwa chini kitandani mwake kwa ugonjwa wa mishipa ya

nyonga (sciatica). Ana mwana mwenye umri wa miaka kumi na tatu, na mama mzee, ambaye hajiwezi na hana namna chochote cha kujikimu. Mama huyu amepata msaada kutoka kwa wanawe wa kulipa kodi ya nyumba, na kadiri ambavyo nyakati zimezidi kuwa ngumu na kubana hiki ndicho kinachoonekana kuwa wana uwezo wa kufanya. Pia tunaye Ndugu. R. na mkewe na watoto wanne wasiojiweza. Yeye anafanya kila awezacho kwa ajili ya kuwasaidia watoto wake wasio na hatia, lakini daima wako katika uhitaji. Anapata kidogo tu kama faida yake. Sasa tunazunguka kwa washiriki wa kanisa ili kuona kama wanaweza kutupatia nguo za zamani kwa ajili ya familia hizi fukara. Nimekuwa nikinunua nguo nzuri mnadani kwa ajili ya kuwafanyia

mambo kuwa rahisi, na pia kuwapa chakula. **{WM 331.1}**

Baadhi ya familia yetu jana walikuwa nje kwa ajili ya safari ya hisani, yaani kusaidia wahitaji, nao walifanya mwanzo mdogo. Baadhi ya vitu vilikusanywa. Kuna familia nane ambazo tumekuwa tukiwasaidia kwa yote ambayo tulidhani ni vyema kuyafanya. **{WM 331.2}**

Chama cha Dorkasi kinafunguliwa juma hili kuzichunguza na kuzirekebisha/kuzikarabati nguo za zamani na mpya kwa ajili ya kuwasaidia wahitaji. Watu wa familia yangu pamoja na mimi tumetoa michango mingi ya pesa na mavazi. Changamoto iliyo juu yetu kuhusu umati huu mkubwa siyo ndogo. Kwani wala hatuwatafuti, bali

wale wenye shida, wenyewe wanatutafuta. Mambo haya yanalazimishwa ung'amuzi au utambuzi kwetu; nasi tunajua fika kwamba hatuwezi kuwa Wakristo na kisha tukawapita hawa kando, na kusema, "Pata joto na uvae," na kuacha kufanya vitu vile ambavyo vingepa joto na kuwavisha. Bwana Yesu anasema, "Maskini mnao siku zote pamoja nanyi." Wao ni urithi wa Mungu kwetu. - *Manuscript* 4, 1895. **{WM 331.3}**

Kutoa Msaada wa Chakula na Mavazi. - Familia yetu imelazimika kuwasaidia maskini kwa chakula na mavazi, na kuwasaidia wajane na yatima kwa zawadi za pesa na pia chakula na mavazi. Hii ni sehemu ya kazi yetu kama Wakristo ambayo haiwezi kupuuzwa. Kristo alisema, "Maskini mnao siku zote

pamoja nanyi," na katika sehemu hii ya shamba la mizabibu la Bwana huo ni Ukweli halisi. Kutenda mema katika namna zake zote kumeamrishwa kwa wamisionari wa Bwana na Maandiko Matakatifu. Soma 2 Wakorintho 9. Unaona, si tu kwamba kazi yetu ni kuhubiri, bali tunapowaona wanadamu wanaoteseka ulimwenguni, tunapaswa kuwasaidia katika shida zao za maisha. Hivyo tutakuwa vyombo mikononi mwa Mungu.... **{WM 332.1}**

Wale ambao wamejitoa kwa Bwana watafungwa nira pamoja na Kristo na watafanya kazi katika mielekeo ya Kristo, daima wakimtazama Yesu kwa ajili ya hekima na uamuzi sahihi juu ya jinsi ya kutenda. Wengi huleta ari, usongo, bidii yao na tabia zao za asili katika ukarimu wao; hawa wanatenda

kwa mihemko ya ghafla: wanawapa wale ambao wanapata wazo la kuwapa; na wengine ambao kwa kila hali wanastahili kama hao, wao, kama kuhani na Mlawi, wanawaangalia lakini hawahisi shauku yoyote juu yao, na hupita upande mwingine, ambao ni upande wa kutokujali na kupuuza. Kutenda mema katika aina zake zote kumeamriwa katika Maandiko Matakatifu, lakini busara na kuzingatia kwa uangalifu kunahitajika ili kujua jinsi ya kuonesha rehema na kuwasaidia wale walio wahitaji kweli. Njia ambayo ni yenye faida kwa pande zote mbili ni kuwasaidia ili waweze kujimudu; kufungua njia mbele yao badala ya kuwapa pesa; kuwatafutia kazi fulani kwa ajili yao kufanya; onesha busara; na hakikisha unayafanya matumizi ya fedha

kwa namna ambayo itatenda mema zaidi kwa maskini wa Bwana kwa wakati wa sasa na ujao. - *Letter* 31b, 1895. **{WM 332.2}**

Kazi Kutolewa kwa Familia Maskini. - Kulikuwa na wengi hapa ambao walikuwa maskini na wenye uhitaji. Wanaume ambao walikuwa wakijaribu kumtumikia Bwana na kushika amri Zake hawakuweza kutoa chakula kwa familia zao, na walituomba tuwape kitu cha kufanya. Tuliwaajiri, na walikula mezani kwetu. Basi tukawalipa ujira wao kwa ukamilifu, mpaka wakaweza kusaidia jamaa zao kwa nguo zao zinazofaa na kuleta furaha. Kisha tukawaacha waende kutafuta kazi mahali pengine. Baadhi yao tulilazimika kuwapa suti za Willie (mwana wake), ili kuwafanya wafae na kufanana na wale

waliokuja kwenye mikutano ya Sabato.- *Letter* 33, 1897. **{WM 332.3}**

Kutoa Kazi, Vitabu, na Nguo. - Wale katika nchi hii ambao hupokea Ukweli wengi wao ni maskini, na wakati wa baridi ni jambo gumu kwao kuhimili/kuzikimu familia zao. Tangu nilipoandika barua iliyotangulia, nililetewa barua kutoka kwa... mtu ambaye alikuwa mjenzi wa mabehewa. Alikuwa katika umaskini mkubwa miaka miwili iliyopita, na tulimpa kazi. Alilazimika kuiacha familia yake, mke na watoto watano, katika viunga vya Sydney, na kuja Cooranbong, karibu maili tisini kutoka huko ili kupata kazi. Kabla ya hapo alikuwa akishirikiana na kaka yake, ambaye pia ni mjenzi. Wa mabehewa. **{WM 333.1}**

Lakini alipoikubali Sabato alipoteza kazi yake, na alifanya kazi kwa mshahara mdogo, na mwishowe hakuweza kupata kazi. Yeye ni mtu mwenye akili, muungwana, mwalimu hodari katika shule ya Sabato, na Mkristo mkweli. Tuliendelea kuwa naye maadam tulikuwa na kazi ambayo angeweza kufanya, na alipoondoka aliuliza kwa upole kama tungeweza kumruhusu kuchukua vitabu vichache juu ya Ukweli wa sasa, kwani hakuwa na chochote. Nilimpa vitabu vyenye thamani ya karibu dola sita. Pia aliuliza kama tulikuwa na mavazi yoyote tusiyoyatumia ambayo tungeweza kumpa, ambayo mke wake angeweza kuyatengeneza kwa ajili ya watoto. Nilimpa sanduku la nguo, ambalo kwa

ajili yake alishukuru mno. - *Letter* 113, 1897. **{WM 333.2}**

Kama Ilivyowekwa Mbele Yake na Bwana. - Kwa nini hamchunguzi mambo ya watu kama Ndugu_____? Yeye ni Mkristo muungwana kwa kila maana ya neno hili. Yeye ni mtu ambaye Mungu anampenda. Watu kama yeye ni wa thamani kubwa machoni pa Bwana. Ninamfahamu vizuri. **{WM 333.3}**

Nilipata shauku katika suala lake.... Nilijitahidi kuyatangulia mahitaji yake na kamwe kutokumweka mahali ambapo angetakiwa kuomba kazi. Nilipokuwa kule Cooranbong nilijaribu kuweka mfano wa jinsi ambavyo wahitaji wanapaswa kusaidiwa. Nilijaribu kufanya kazi kwa namna

iliyowekwa mbele yangu na Bwana. - *Letter* 105, 1902.**{WM 333.4}**

Chama cha Dorkasi Nyumbani kwa E. G. White. - Jana jioni tulikuwa na Wanachama wa Dorkasi nyumbani kwetu, na wafanyikazi wangu ambao hunisaidia katika utayarishaji wa makala zangu kwa ajili ya gazeti na upishi na kushona, watano kati yao, walikaa hadi usiku wa manane, wakikata nguo. Walitengeneza jozi tatu za suruali kwa ajili ya watoto wa familia moja. Mashine mbili za kushona zilifanya kazi hadi usiku wa manane. Nadhani hapajawahi kuwa na wafanyakazi wenye furaha kuliko wasichana hawa jioni ya jana. **{WM 334.1}**

Tulitengeneza kifurushi cha nguo kwa ajili ya familia hii, na tulidhani

ilikuwa ndiyo yote ambayo tungeweza kufanya. Dada C. sasa yuko kwenye safari hii fupi ya rehema kwenda kwa familia hii maskini, akikata mavazi kutoka katika nguo zilizotolewa. Pia kuna familia nyingine zitakazopewa. Na sasa inakuja ombi jingine, na inabidi tuwape vitu vya kuvaa kwa ajili ya majira ya baridi. Hivi ndivyo imekuwa tangu tuingie katika nchi hii. Na bila ya shaka tutaitikia wito wa kutuma sanduku la nguo kwa ajili ya wahitaji hawa. Ninakuambia tu mambo haya ili ujue kwamba tumezungukwa na umaskini. Mke wa mvuvi huyu anapaswa kubatizwa Sabato ijayo. Maskini wanahubiriwa injili. Watu wa eneo hili wana kidogo sana ya mema ya ulimwengu huu. - *Letter* 113, 1897. **{WM 334.2}**

Kuwasaidia Wagonjwa na Mafukara. - Wagonjwa hutuomba msaada, nasi tunakwenda kuwasaidia. Dada McEnterfer, msaidizi wangu na muuguzi, anaitwa kutoka maili nyingi kote kutoa maagizo (prescribe treatment) na kuwapa matibabu. Amekuwa na mafanikio mazuri. Hakuna daktari huko Cooranbong, lakini tutajenga hospitali au Sanitariumu hivi karibuni, ambapo wagonjwa wanaweza kuletwa na kutunzwa. Zamani tuliwaleta nyumbani kwetu na kuwatunza, kwani hatuwezi kuwaacha wanadamu wateseke bila kufanya kitu cha kuwaondolea.... **{WM 334.3}**

Hatuchukui malipo kwa ajili ya chochote tunachokifanya, lakini ni lazima tuwe na hospitali, ambayo itagharimu kidogo kadiri iwezekanavyo,

ambapo tunaweza kuwa na hali zinazofaa na vifaa vya kuwahudumia wagonjwa. **{WM 334.4}**

Hii ni kazi ya Kristo, na hii lazima iwe kazi yetu. Tunataka kufuata kwa karibu nyayo za Mwalimu. Tunawakuta mahali hapa watu wenye akili nyingi, ambao wakati fulani walikuwa katika nafasi za raha, lakini umaskini umewafikia. Tunawapatia hawa kazi, na kuwalipa, na kwa jinsi hiyo kupunguza shida zao. Hii ndio kazi hasa ya kufanywa ili kuponya maradhi ya roho pamoja na ya mwili. Kristo Ndiye Mponyaji hodari wa roho na mwili. **{WM 334.5}**

Kristo alitamka, "Maskini mnao siku zote pamoja nanyi." Lo, ni jinsi gani ninatamani kufanya zaidi ya

ninavyofanya sasa. Bwana na anitie nguvu, ndilo ombi langu, ili niweze kufanya yote ambayo ameniagiza kufanya. Jana sanduku la nguo lilipelekwa kwa familia maskini lakini yenye akili na bidii. Baba ni mchapakazi mzuri, mtengenezaji wa mabehewa. Anafanya kazi pale anapoweza kupata kazi. Hili sasa ni sanduku la tatu la nguo tulilomtumia. Roho zinakuja katika Ukweli kupitia kwa ushawishi wa familia hii, na Ndugu Starr anaenda Sydney kuwabatiza watu kadhaa ambao wameongoka katika Ukweli. **{WM 335.1}**

Ninatamani kuona kazi hii ikiendelea. Tutasonga mbele kufanya kazi kwa uvumilivu, na Bwana atafanya kusadikisha na kuongoa. Hatuwezi kuwapuuza maskini. Kristo alikuwa

maskini. Alijua ufukara na uhitaji. Ninatumia kila dola ya mapato yangu kuendeleza kazi hii.... Tunamaanisha kufanya kazi wakati mchana ungalipo, kwa maana usiku unakuja ambapo mtu hawezi kufanya kazi. - *Letter* 111, 1898. **{WM 335.2}**

Kazi ya Umisionari wa Tiba Pote Katika Cooranbong. - Dada Sara McEnterfer, kwa kushirikiana na Ndugu James, mkulima wangu, wamekwenda kumtembelea Ndugu C., ambaye anaishi porini maili sita kutoka hapa. Ndugu huyu ameukubali Ukweli tangu tulipokuja Cooranbong.... **{WM 335.2}**

Sasa habari zimetufikia kwamba ndugu yetu mpendwa amepatwa na

homa ya matumbo. Bwana Pringle ndiye mtu pekee katika kijiji hicho ambaye anajua chochote juu ya kutoa matibabu bila dawa; lakini wiki sita zilizopita aliitwa kwenda kumhudumia Mheshimiwa B., ambaye pia alikuwa chini kwa homa ya matumbo. Amekaa naye usiku na mchana, na sasa amerejea nyumbani kwake, akiwa amechakaa kwa uchovu. Hivyo hawezi kutegemewa kumuuguza Ndugu C. **{WM 335.4}**

Sara na Ndugu J. Wamekwenda kuona hali ilivyo. Kama Ndugu C. anaweza kuhamishwa, ni lazima aletwe karibu na sisi, hata kama itabidi kubebwa juu ya machela. Hatuwezi kumwacha alale huko na kufa, amwache mkewe na watoto wake kuhurumiwa na kila mtu atakayewahurumia. .....**{WM 335.5}**

Tarehe 21 Machi. Sara ndio tu amerudi na habari njema kwamba Ndugu C. anaendelea vizuri. Alishambuliwa, lakini Bwana Pringle, ambaye aliweza kumtembelea, alimkuta akiwa ni mgonjwa tofauti sana na bwana B. Ndugu C. ni mwanamatengenezo wa afya, na pale ugonjwa wake ulipopewa matibabu ya nguvu homa ile ilitekewa. Yeye ni dhaifu, lakini ameamka na kuvaa, na ni mchangamfu na mwenye furaha katika Bwana. Sara anasema kuwa mahindi anayolima yatasaidia kwa kiasi kikubwa kuihimili familia yake. Wana kinu cha mkono, nao husaga nafaka hii tena na tena mpaka imekuwa laini. Kutokana na huo wanatengeneza mkate wao, kwa maana hawana fedha za kununulia unga laini. Tutawatumia unga

kiasi. Hii ndio kazi ambayo imefanyika katika hali kadhaa. Tumewasaidia watu kuweza kujimudu wenyewe. **{WM 336.1}**

Ndugu C. Ana kitu ndani yake ambacho hakitamruhusu, ikiwa ana afya, kumtegemea mtu yeyote. Lakini yule mtu aliyenunua mashua yake hajamlipa chochote, kwa kuwa asingeweza. W. C. White aliiona shida ya Ndugu C., na kukopa pauni nane kutoka kwa mhunzi wetu na kumkopesha, ili apate namna ya kuanza tena. Na wote wana furaha na kushangazwa sana kuona mwanzo alioufanya. Takribani ya ekari kumi na mbili zimetengenezwa na kupandwa nafaka tamu na nafaka za shambani. Nafaka tamu watakula, na

nafaka za shambani watauza. Mboga mboga ambazo zimekuzwa husaidia sana katika kuilisha familia. Wavulana wadogo wanafanya kazi pamoja na baba yao kama wakulima wadogo. Wana bidii sana na wenye ari kiasi kwamba inafurahisha kuwatazama na kuona jinsi walivyo na furaha katika kazi yao. Hawana jamii nyingi zaidi ya jamaa wa familia yao wenyewe, lakini wako katika shule bora hasa zaidi ya yoyote ambayo wangeweza kuwamo. - *Letter* 48, 1899. **{WM 336.2}**

Usikivu wa Kwanza kwa Washiriki wa Kanisa Walio Wahitaji. - Kuna familia ambazo wamepoteza kazi zao ambazo walikuwa nazo kwa miaka ishirini. Mtu mmoja na

mkewe wana familia kubwa ya watoto ambayo tumekuwa tukiwatunza. Ninalipa gharama za watoto wanne shuleni kutoka kwa familia hii moja. Tunaona hali nyingi ambazo ni lazima tusaidie. Hawa ndio watu bora tuliowasaidia. Wana familia kubwa, lakini ni maskini wa Bwana. Mtu mmoja alikuwa mjenzi wa mabehewa, mtengenezaji wa makabati, na fundi wa magurudumu, na mtu muungwana wa daraja bora machoni pa Mungu, anayesoma mioyo ya watu wote. Familia hii tuliipatia mavazi kutoka katika familia yetu kwa miaka mitatu. Tuliihamisha familia hii kwenda Cooranbong. Tulitarajia kuwasaidia kupata nyumba msimu huu wa baridi. Nimewaruhusu kuishi katika hema yangu, nao wameweka paa ya bati juu

yake na wameishi ndani yake kwa mwaka. Kila mtu anampenda mtu huyu, mke wake, na watoto. Ni lazima tuwasaidie. Wanaye baba na mama ambao ni lazima wawasaidie. Familia tatu za jinsi hii ziko kwenye majengo ya shule, na lo, laiti tungekuwa na pesa za kuwasaidia kujenga nyumba ya bei nafuu ya mbao, wangefurahi kiasi gani! Ninatumia kila senti niliyonayo katika kazi hii ya kusaidia. Lakini inajalisha kwangu mimi kwamba ni nani ambaye nitamsaidia, kama ni maskini wa Mungu wanaoteseka ambao wanatunza amri Zake na kukosa kazi zao kama matokeo yake au kama ni mtu mwenye kukufuru anayezikanyaga amri za Mungu chini ya miguu yake. Na Mungu anaiheshimu tofauti hiyo. Tunapaswa kuwafanya wanaume na wanawake hawa wote kuwa

watenda kazi pamoja na Mungu. - *Letter* 45, 1900. **{WM 336.3}**

“Tuliwasaidia Wote Tulioweza.” - Katika Australia tumejaribu kufanya yote tuwezayo katika mwelekeo huu. Tulikaa katika Cooranbong, na pale, ambapo watu walilazimika kumwagizia daktari kutoka umbali wa maili ishirini na tano, na kumlipa dola ishirini na tano kwa kila ziara, tuliwasaidia wagonjwa na watesekao kwa yote tuliyoweza. Kwa kuona kwamba tulikuwa tunafahamu kitu fulani kuhusu magonjwa, watu walileta wagonjwa wao kwetu, nasi tuliwatunza. Kwa jinsi hiyo tulivunja kabisa chuki mahali hapo…….**{WM 337.1}**

Kazi ya umisionari wa tiba ndiyo kazi ya utangulizi, ni daraja la kufungua milango, kazi ya uanzilishaji (pioneer work). Inapaswa kufungamanishwa na huduma ya injili. Ni injili katika utendaji, upendo kwa vitendo, injili inayotekelezwa kwa matendo. Nimesikitishwa sana kuona kwamba watu wetu hawajaishikilia kazi hii kama ambavyo iliwapasa.... **{WM 337.2}**

Mbingu yote inapendezwa na kazi ya kuwatuliza wanadamu wanaoteseka. Shetani anatumia nguvu zake zote ili apate udhibiti juu ya roho na miili ya wanadamu. Anajaribu kuwafunga kwenye magurudumu ya gari lake. Moyo wangu unasikitishwa ninapoangalia makanisa yet, ambayo yanapaswa kuunganishwa/kushikamana katika moyo na roho na utendaji na kazi ya

umisionari wa tiba. - *The General Conference Bulletin*, Aprili 12, 1901. **{WM 337.3}**

Mama White Alidumu Kuwa na Huruma Pana Katika Maisha Yake Yote

Iliyooneshwa kwa Mjane wa Rais McKinley. - Siwezi kulala zaidi ya saa nane usiku. Mara nyingi ninaamshwa saa saba usiku moyo wangu ukiwa umevutwa kwa huruma kwake mke wa Rais McKinley aliyefiwa. Mmoja anachukuliwa na mwingine anaachwa. Yule mwenye nguvu ambaye mapenzi yake makubwa yangeweza kumwegemea, hayupo. Alipokuwa na afya njema, akitimiza majukumu ya ofisi yake, mkono unaoonekana kuwa ni wa

urafiki ulinyoshwa, ambao Rais McKinley alikuwa tayari kuushika. Mkono ule wa Yuda ulishika bastola na kumpiga risasi Rais. Katikati ya matukio ya maisha mazuri na furaha yalikuja masikitiko na huzuni na mateso na majonzi. Angewezaje kufanya kitendo hiki kibaya sana cha mauaji? **{WM 338.1}**

Moyo wangu una huruma kubwa kwa yule aliyebaki. Nimekuwa nikirudia mara kwa mara, Lo, ni jinsi gani maneno yote ya huruma ya mwanadamu yalivyo mapungufu. Kuna maelfu ambao wangezungumza maneno ya kuufariji moyo unaovunjika kama ingewezekana, lakini hawaelewi jinsi ambavyo maneno ni dhaifu katika kumfariji aliyefiwa, ambaye katika udhaifu wake daima alipata moyo wa kibinadamu ndani ya

mumewe, uliojaa upole na huruma na upendo. Mkono wenye nguvu wa mwanadamu ambao mke dhaifu anayeteseka aliuegemea, haupo sasa.

Sitamani kwamba dada yetu awe na majuto kidogo na upendo kidogo kwa yule mume mwaminifu, lakini kwamba sasa anapaswa kumwangalia Yeye aliye Rafiki yake bora, Yeye ambaye upendo Wake umeoneshwa kwake maisha yake yote. Ningemwambia maneno ya Isaya 61:1-3: "Roho ya Bwana MUNGU i juu Yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa, na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji

wote waliao; kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe taji ya maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito; wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na Bwana.” - *Diary,* 1901. **{WM 338.3}**

Kuwahudumia Wazee waliokuwa mashujaa wa Vita. (War Veterans) - Wakati fulani nilikuwa na mabaki ya vitabu na Masomo ya Sabato kadhaa vilivyohifadhiwa mahali fulani katika Battle Creek. Tafadhali mwombe Ndugu Amadoni atafute kwa bidii vitu hivi vyote, na kunitumia.... **{WM 339.1}**

Tunaweza kutumia vitabu vidogo vya Masomo ya Sabato na maandishi mengine kwa faida nzuri katika nyumba

za mayatima na katika maeneo mengine mengi ambapo vitabu hivi vidogo vitathaminiwa sana. Tunaweza kutumia baadhi yao katika Nyumba ya Maaskari huko Yountville, ambapo mamia ya wanajeshi wa zamani wanasadiwa kimaisha katika majengo makubwa ya serikali. Tunawapa watu hawa kila usikivu unaowezekana. Kila Sabato kundi kutoka katika Sanitariamu na makanisa ya St. Helena linawatembelea, kuimba nyimbo za kidini na kuzungumza nao. Wanapendezwa na mikutano hii, na wanaonekana kufurahishwa na kila kitu ambacho watu wetu hufanya kwa ajili yao. **{WM 339.2}**

Tunatuma magazeti kwa maaskari hawa waliostafu hawa na tumeweka katika maktaba yao nakala za kazi zangu, *Christ's Object Lessons,* na baadhi ya vitabu vyangu vingine vikubwa. Wengi wa watu hawa wana akili nyingi. Ndugu na dada zetu wanafanya kazi katika shamba hili, na tunatarajia kufanya mengi zaidi kwa wanajeshi hawa kuliko ambavyo tumefanya hadi sasa. Wakati mwingine hotuba-yaani hubiri fupi, linalolenga, mada moja maalum ya Biblia-hutolewa, na wanasikiliza kwa shauku kubwa. Nyimbo za injili, sala fupi, na mazungumzo mazuri, yote kwa pamoja, huonekana kuwa ndicho hasa kinachohitajika kuwavutia wazee hawa. Nao husema, "Kamwe hatujawahi

kufanyiwa kazi kama hii hapo kabla!” **{WM 339.3}**

Tunatamani kudumu kueneza vitabu na magazeti miongoni mwa askari hawa. Tafadhali tusaidie kila unachoweza katika mwelekeo huu kwa kukusanya pamoja kitu kwa ajili ya wao kusoma - vitabu na magazeti vilivyojaa Ukweli wa Biblia. - *Letter* 96, 1903. **{WM 339.4}**

Barua kwa Watoto Wasio na Baba

San Jose, California Juni 29, 1905
Wapendwa Watoto:

Ninalazimika kuandika mistari michache kwa ajili yenu. Tunatamani kwamba tungeingia nyumbani kwenu na kulia pamoja nanyi na kupiga magoti pamoja nanyi katika maombi. Je! Kila mmoja wenu atamtafuta Bwana na

kumtumikia? Mnaweza kuwa baraka kubwa kwa mama yenu kwa kutokufanya kitu chochote ambacho kitafanya moyo wake kuwa na huzuni. Bwana Yesu atawapokea ikiwa mtatoa mioyo yenu Kwake. Fanyeni yote yanayowezekana ili kummpunguzia mama yenu masumbufu na mizigo yote. **{WM 340.1}**

Bwana ameahidi kuwa Baba kwa yatima. Kama mtampa mioyo yenu Yeye, Naye atawapa uwezo wa kuwa wana na binti za Mungu. Ikiwa watoto wakubwa watamsaidia mama kwa kubeba mizigo mingi iwezekanavyo, na kwa kuwatendea watoto wadogo kwa wema, kuwafundisha kutenda haki na kutokumsumbua mama, Bwana atawabariki sana. **{WM 340.2}**

Toeni mioyo yenu kwa Mwokozi Mwenye upendo, na mfanye tu mambo yale ambayo ni ya kupendeza machoni Pake. Usifanye chochote cha kumhuzunisha mama yako. Kumbuka kwamba Bwana anawapenda, na kwamba kila mmoja wenu anaweza kuwa mshiriki wa familia ya Mungu. Ikiwa mtakuwa waaminifu hapa duniani, Yeye atakapokuja katika mawingu ya mbinguni, mtakutana na baba yako, na mtakuwa familia iliyoungana pamoja.

Kwa upendo,

Ellen G. White. - *Letter* 165, 1905.**{WM 319.1}**